

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

---

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 1 Juni, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Ledian M. Mng'ong'o) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MHE. GREGORY G. TEU (K. n. y. MHE. MARGARET S. SITTA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII):-**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MHE. GRACE S. KIWELU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 119

**Fedha kwa Ajili ya Kutengeneza Mitaro ya Barabara**

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri za Miji na Wilaya ikiwemo za Mpanda na Sumbawanga ambazo huharibika mara kwa mara kwa sababu ya ukosefu wa mitaro:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutengeneza mitaro hiyo ili kuokoa fedha zinazotumika mara kwa mara kutengeneza barabara zinazosombwa na maji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mitaro katika barabara za mijini. Katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda kuanzia Mwaka wa Fedha 2012/2013 hadi Mwaka wa Fedha 2014/2015, jumla ya Sh. 502,000,000 zimetumika kujenga mitaro ya maji ya mvua. Kwa sasa Mji wa Mpanda una kilometa 20.2 za mitaro ya maji ya mvua. Hata hivyo kwa kuzingatia mtandao wa barabara uliopo katika mji huo wenye jumla ya kilometa 251.5 za mitaro ya maji na mvua zinahitajika kujengwa. Aidha, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 zimeombwa Sh. 150,000,000 za kuendeleza ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua katika barabara za Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ina kilometa 204.55 za mtandao wa barabara za mijini na hivyo kufanya jumla ya kilometa 409.1 ziwe na uhitaji wa kuwekewa mitaro ya maji ya mvua. Kwa sasa Mji wa Sumbawanga una kilometa 13.5 za mitaro ya maji ya mvua ambapo ujenzi hufanyika kila mwaka wa fedha na kwa kutenga Sh. 50,000,000 za kujenga mita 500 za mitaro ya maji ya mvua katika maeneo korofi, barabara za kiwango cha lami na changarawe.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac!

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba niongeze swali ili nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezoeleka sasa kwa Serikali, inapopanga bajeti inaweka fedha kwa wingi kwa maneno, lakini inapoamua kupeleka katika Halmashauri, inapeleka kwa uchache sana, yaani kidogo ambazo haziwezi kumalizia ile miradi na kuleta adha katika mitaa yetu kule, barabara za pale mjini, mvua inapokuja tena inaharibu hata kile kipolwa kidogo kilichokuwa kimetengenezwa. Sasa napenda kuiuliza Serikali, haioni kwamba kazi za kurudia rudia ni uharibifu wa fedha, vile vile ni kuwabebesha mzigo wa lawama Wakurugenzi wa Halmashauri husika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika nyakati kadhaa kunaweza kuwa kuna tatizo la upatikanaji wa fedha na ule mradi uliokusudiwa usitekelezwe kwa wakati halafu tukapata tatizo la mvua labda, halafu ikaharibu pia hata *structure* ile ya awali. Mikakati ya Serikali wakati wote ni kuhakikisha kwamba, mradi unapoanza unakamilika na pale ambapo tunatenga bajeti fedha itolewe ili iweze kukamilika. Kwenye eneo la barabara na maeneo ya miji tunavyo vyanzo viwili ambavyo tunavitumia mara nyingi katika kuboresha huduma zetu za barabara na mitaro yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna fedha ambayo inatengwa kupitia bajeti ya Halmashauri yenyewe lakini mbili tunayo ile miradi ya barabara ambayo tunatengewa fedha kila mwaka ili tuweze kuiimarisha. Kwa sababu ya uhitaji mkubwa wa matengenezo ya barabara, sasa tumeona tuhakikishe kwamba tunatenga fedha kwa mradi mmoja mmoja ambao unatakiwa kuanzwa na kukamilika badala ya utaratibu wa awali wa kuwa tunatenga kidogo barabara hii, kidogo barabara ile, badala yake fedha zinakuwa hazikamiliki, haziletwi kwa wakati kama ambavyo tumeleza na tatizo limeshaelezwa mara nyingi na Wizara ya Fedha ikija hapa itaeleza utaratibu unaotumika katika kuleta fedha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge jambo analolieleza tunalifahamu na tutahakikisha kwamba mradi ule tuliouanza tunaukamilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje, swali la nyongeza!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika gharama ambazo Serikali inatumia kwenye Halmashauri zetu nchi nzima ni kutengeneza barabara ni fedha nyingi sana na hii inatokana na kwamba Halmashauri nyingi hazina *grader* kwa hiyo wanatafuta Wakandarasi kuja kutengeneza barabara za Halmashauri ambazo *in real sense* tunatumia hela nyingi sana. Hii ni kwa Halmashauri zote nchi hii ikiwemo na hata Halmashauri ya Jiji la Mwanza ninakotoka. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa amri kwa Halmashauri zote nchi hii, kila Halmashauri ihakikishe inakuwa na *grader* linalofanya kazi ili kupunguza gharama za kutengeneza barabara kwa kuwapa makandarasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba Halmashauri zinazo kazi nyingi sana za barabara na mara nyingi hutumia wazabuni katika kurekebisha hata yale matengenezo madogo madogo.

Sisi tunaamini kwamba Halmashauri inapoweza kuwa na mipango yake yenyewe, inapona kwamba inatumia gharama nyingi kwenye zabuni mbalimbali na wanaweza kuwa na *alternative* ni suala la Madiwani kuona umuhimu wa ununuzi wa *grader* na kuweza kurekebisha kazi ndogo ndogo au zile muhimu badala ya kutumia wazabuni ambao gharama yake inakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili kwa sababu Halmashauri nyingi tumeona zimeshaanza kununua ma-*caterpillar* yake yenyewe na kufanya kazi za barabara iweze kukamilika. Kwa manufaa ya Wilaya ya Nyamagana ambayo pia Mheshimiwa Mbunge anaweza kushauri pale na tumeshawahi kutoa maelezo haya kwenye Halmashauri, pamoja na zilizotekeleza, sasa Nyamagana ione kupitia mipango yake ya ndani na kuona umuhimu wa kupunguza gharama kwa wazabuni, sasa iweze kununua vyombo vyake yenyewe. Kwa kuwa tuna Wahandisi, wataalam tunaweza kuajiri tu *operator* ili waweze kufanya zile kazi ndogo

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

ndogo wao wenyewe badala ya kutumia wazabuni ambao pia gharama yake ni kubwa kama nilivyosema awali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, nilikuona!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka tu kuuliza swali dogo la nyongeza. Tunajua Serikali inatumia fedha nyingi katika ujenzi wa barabara. Hapa nazungumzia barabara kuu ya kutoka Mwanza kwenda Musoma. Kupitia lile eneo la Bunda kuna maeneo ambayo barabara kabla haijakabidhiwa tayari imeshaharibika. Sasa nataka kujua, hivi ni vigezo gani mnavyotumia kuwapata Wakandarasi ambao wanajenga barabara chini ya kiwango; barabara kabla haijakabidhiwa tayari imeshakatika?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu, Mheshimiwa Mhandisi Lwenge!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba inawezekana kwa yeye jinsi alivyoona kwamba barabara imeharibika kabla haijakabidhiwa, lakini *assessment* siku zote tunaifanya barabara ikishakabidhiwa. Sasa kama bado Mkandarasi anaendelea kufanya kazi pale, unajuaje kama kipande hiki kimekwisha? Mpaka kikabidhiwe ndipo tunasema hiki kimekwisha na kimepokelewa. Barabara yoyote haiwezi kupokelewa kama haijafikia kiwango kinachotakiwa kulingana na mkataba ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili ni jambo la usimamizi, sisi tunaendelea kufuatilia. Kwa hiyo, kama kweli anachokisema ndiyo hivyo basi tutakwenda kuona tuone kama hicho kipande kimekabidhiwa na kimeharibika kabla ya muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunakwenda swali linalofuata, Mheshimiwa Josephine Genzabuke. Samahani, samahani, swali linalofuata ni la Mheshimiwa Deo Filikunjombe. Mheshimiwa Esther Bulaya!

Na. 120

### **Kufikisha Maji Safi na Salama Mji wa Ludewa**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE)** aliuliza:-

Maji safi na salama ni muhimu kwa afya za wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji safi na salama katika Mji wa Ludewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Ludewa unakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 13,000 ambapo kati yake ni asilimia 40 tu ndiyo wanaopata huduma ya maji kutoka kwenye vyanzo vya Ngalawe na Mkondachi.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali ilitenga fedha jumla Sh. 500,000,000 kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji katika mji huo. Aidha, Serikali imetoa jumla ya Sh. 100,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye chanzo cha maji cha Mapetu ambapo taratibu za kumpata Mkandarasi zimekamilika. Kwa sasa Mkataba uliopelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa ajili ya mapitio na kupata idhini unasubiriwa na mradi huu ukikamilika utawezesha asilimia 56 ya wakazi wa Mji wa Ludewa kufikiwa na huduma ya maji kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Serikali imetenga jumla ya Sh. 400,000,000 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya maji katika Mji wa Ludewa, ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kutibu maji. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya maji katika Mji wa Ludewa na Viunga vyake kwa kadiri rasilimali fedha itakavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwanza kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Wananchi wa Ludewa ni miongoni mwa watu ambao wanapata adha kubwa sana kutokana na tatizo la maji. Kwenye jibu lake la msingi amesema mwaka wa fedha uliopita walitenga Sh. 100,000,000 kati ya Sh. 500,000,000, kwamba mwaka huu wametenga Sh. 400,000,000 sasa hizi Sh. 400,000,000 ni mwaka ule au ni mwaka mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona, kutopeleka fedha kama ambavyo Serikali imejipangia imekuwa ikichelewesha miradi ya maji kukamilika. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa watahakikisha wanapeleka fedha kwa wakati ili wananchi wa Ludewa waachane na adha ya kutafuta maji ambayo wanaipata wakiwemo akinamama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kulikuwa na mradi wa maji wenye gharama ya Sh. 450,000,000 katika vijiji viwili; Kijiji cha Mgeta na Kijiji cha Nyangaranga, Jimbo la Bunda. Hivi tunavyozungumza wananchi wanalazimishwa kupokea mradi ambao haujakamilika. Kwa upande wa Nyangaranga ilipaswa wajenge na maeneo ya kunyweshea mifugo, hata moja hawajajenga. Kwa upande wa Mgeta walikubaliana kuwe na DP kumi, wamejenga saba, lakini katika DP moja hakuna mtaro...

**MWENYEKITI:** Swali kwa ufupi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja. Hakuna mtaro wala mabomba. Hivi tunavyozungumza maeneo mengine mabomba hawajayafukia, mitaro hawajayafukia, wanafukia kwa mkono, hivi Mkandarasi kama huyu amebebwa kupitia tu nyadhifa za watu ambao wanambeba, mnamchukulia hatua gani? Wanamtumia Mkuu wa Wilaya kwenda kuwalazimisha wananchi kupokea mradi ambao haukajakamilika, je...

**MWENYEKITI:** Ester swali kwa ufupi, siyo hotuba!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza Serikali mnasemaje kuhusiana na Wakandarasi wasiomaliza mradi na kutumia viongozi kwenda kutisha wananchi kupokea miradi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu!

**NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyaweka. La kwanza, tunatambua tatizo la maji katika Mji wa Ludewa na inatokana na kwamba mradi ule umekuwa wa muda

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

mrefu, mradi ulijengwa mwaka 1970, kwa hiyo kuna uchakavu na uvujaji mkubwa wa maji. Kwa hiyo Serikali kwa kutambua hilo Mwaka wa Fedha uliopita tulitenga Sh. 500,000,000 lakini kutokana na upatikanaji wa fedha tulipeleka Sh. 100,000,000 na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha Halmashauri imetenga Sh. 400,000,000 kwa maana mradi ulivyosanifiwa unagharimu Sh. 500,000,000 ambapo zimepelekwa Sh. 100,000,000 ili kukamilisha mradi huo ambao sasa upatikanaji wa maji utaongezeka kutoka asilimia 38 mpaka asilimia 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe tu na nimeshaongea na Mheshimiwa Deo Filikunjomba, anaelewa tatizo hili na nia nzuri ya Serikali, nimwombe awe na subira, tupitische bajeti yetu ili tuweze kutekeleza na kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu miradi ambayo anaitaja Mheshimiwa Ester Bulaya. Alishanifuata na alishanieleza juu ya miradi hii kutokukamilika, kwa maana kama vituo vilikuwa vimepangwa, kama mradi haujakamilika. Tunaendelea kulifanyia kazi lakini nitoe tu tamko kwamba, wananchi wasiendeleo kupokea miradi ambayo haijakamilika. Kama ambavyo ilikuwa imewekwa katika usanifu, kama kulikuwa na vituo vilikuwa vimeainishwa na kila kitu cha kuweza kufanyika katika mradi huo, basi waupokee ukiwa katika hali ambayo kama ambavyo ilikuwa imeelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutalifanyia kazi suala ambalo Ester Bulaya amelisema kuhusu Vijiji vya Mgeta na tutatuma wataalam wetu kuthibitisha juu ya jambo hilo, naomba tu wananchi wawe na subira, Serikali itafuatilia jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunakwenda swali linalofuata Mheshimiwa Josephine Genzabuke!

Na. 121

### **Mradi wa Maji-Kasulu**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:

Katika Wilaya ya Kasulu ipo miradi ya Maji ambayo ilianzishwa, lakini mpaka sasa haijakamilika:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili miradi hiyo iweze kukamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu inatekeleza Program ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini tangu mwaka wa fedha 2012/2013. Utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Nyumbigwa kwa gharama ya shilingi milioni 890.7 na utekelezaji umetekelezwa kwa 97% ambapo jumla ya shilingi milioni 683.9 zimetumika. Mradi wa Maji wa Kisangezi kwa gharama ya shilingi milioni 882.9 na umetekelezwa kwa 65% ambapo jumla ya shilingi milioni 287.4 zimeshatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ni pamoja na Nyarugusu kwa gharama ya shilingi milioni 423.4 na utekelezaji wake umefikia 70% ambapo jumla ya shilingi milioni 221.6 zimetumika. Aidha, mradi wa maji wa RungweMpya kwa gharama ya shilingi bilioni 1.46

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

umetekelezwa kwa 50% ambapo shilingi milioni 285.2 zimeshatumika. Serikali itaendelea kutekeleza miradi hiyo mpaka itakapokamilika ili wananchi wapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri pia inatekeleza miradi ya ukarabati yenye kutoa matokeo ya haraka kwa Vijiji vya Heru Juu, Karunga, Munyengera na Muhunga na utekelezaji wake uko kwenye taratibu za manunuzi. Gharama za miradi hiyo yote ni shilingi milioni 585.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Halmashauri imetenga jumla ya shilingi milioni 298.4 kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya maji kwa ajili ya kuendeleza kutekeleza miradi ya maji katika Wilaya ya Kasulu. Ukamilishaji wake utaendelea kufanyika kadiri rasilimali fedha zitakavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine, swali la nyongeza!

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa muda mrefu sasa wanawake wa Mkoa wa Kigoma yapo maeneo ambayo wameendelea kuteseka kutokana na tatizo la maji na huku wakishindwa kabisa kufanya shughuli za maendeleo na kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma tumejaaliwa kuwa vyanzo vingi vya maji, mito mikubwa na midogo pamoja na Ziwa Tanganyika. Je, ni lini sasa Serikali itawaondolea wananchi kero hii ambayo imesababisha udhalilishaji wa wanawake, magonjwa na vifo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Mji wa Kasulu maji yanayotoka ni machafu sana, mabomba yanatoa maji machafu, wakati wa masika maji yanayotoka kwenye mabomba yamejaa tope, wekundu na uchafu mbalimbali, lakini kadhalika wakati wa kiangazi maji ni machafu. Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kuweka dawa ya kutibu maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakubaliana naye juu ya vyanzo vya maji katika Mkoa wa Kigoma na Serikali inatambua hilo na ndiyo maana tunaendelea kutekeleza miradi ya maji kutokana na vyanzo alivyovitaja katika ziwa, maji ya mserereko na maji toka chini ya ardhi. Nia ya Serikali ni kuona kwamba tunaendelea kutekeleza miradi ya maji na kuwaondolea adha Watanzania wote wakiwemo wanawake kama kama alivyosema Mheshimiwa Genzabuke. Tutaendelea kutekeleza miradi ya maji kutokana na fedha na naamini kabisa miradi hii ambayo tumeianzisha tutaitekeleza kadiri tutakavyopata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nakubaliana naye kwamba kwa Mji wa Kasulu kumekuwa na matatizo ya maji kuwa machafu na hili nimwombe yeye Mbunge na Wabunge wengine kwamba lipo tatizo kwa pale Kasulu Mjini wananchi kufanya shughuli za kijamii zinazopelekea kuchafua vyanzo vya maji. Tuna taarifa hizo na Halmashauri na Mamlaka ya Maji Kasulu imejipanga, nimwombe yeye kama Mbunge basi tuendeleo kuhamasishana wakati Serikali inatumia fedha nyingi sasa hivi kukarabati na kupanua miundombinu ya maji katika Mji wa Kasulu, basi katika chanzo cha maji wananchi waache kufanya shughuli ambazo zinapelekea kuchafua vyanzo vya maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo, nilikuona!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii....

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan subiri kwani kuna majibu ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Naibu Mawaziri kwa majibu mazuri, lakini napenda niongeze tu kwamba, katika Mji wa Kasulu katika mwaka 2013/2014, Serikali ilituma shilingi milioni 300 kwenye Halmashauri ya Kasulu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji katika Mji wa Kasulu. Kwa sababu zisizojulikana Halmashauri ya Kasulu ilizitumia fedha hizo kwa shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisisitize maagizo ambayo yalitolewa kwa Halmashauri ya Kasulu kwamba, fedha hizo zirudishwe mara moja kutokana na vyanzo vyake vya ndani ili zitumike katika kuboresha miundombinu ya maji ya mji huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, bado tatizo la miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ni mibovu sana na hapa ninavyozungumza hakuna maji katika maeneo mengi ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Pamoja na kwamba mabomba yamewekwa lakini yanapasuka na Wizara au watumishi wa Wizara hawarekebishi miundombinu hiyo na matokeo yake wananchi wanateseka sana. Je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kwamba tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam ambalo lina watu zaidi ya milioni tano linapatiwa ufumbuzi wa haraka ili wananchi hususan akinamama waendeleo kufanya kazi zao badala ya kukaa kusubiri misururu mirefu ya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NABU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jiji la Dar es Salaam lina changamoto kubwa na hasa sasa ambapo tunaendelea na ukarabati na upanuzi wa miradi mikubwa ya maji. Natambua yapo maeneo ambayo yanakosa maji kutokana na ukarabati unaoendelea, lakini pia kutokana na kwamba tunatarajia miradi mikubwa ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini, Serikali hivi sasa inafanya utaratibu wa kumpata Mkandarasi kuondoa miundombinu ya zamani ya maji na hata yale mabomba yanayoitwa ya Mchina sasa yatatoa maji miradi hii itakamilika, lakini na maeneo mengine ambapo maji yataendelea kuvuja kutokana na uchakavu, ndiyo maana sasa hivi tunapanga kumpata Mkandarasi ili kurekebisha kasoro hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama siyo sababu hizo, nikuahidi kwamba, baada ya swali hili, nikitoka nitaongea na Mkurugenzi wa DAWASCO ili kujua ni nini hasa tatizo na lirekebishwe mara moja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali lingine ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda.

Na. 122

### **Mradi wa Maji Unaofadhiliwa na Benki ya Dunia**

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA** aliuliza:

Mradi wa Maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia; *(Phase II World Bank Project)*, umepangwa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utaalim elekezi katika Vijiji vya



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ngoheranga na Tanga; lakini katika programu zote za Wizara, Vijiji vya *Sofi Mission*, Sofi Majiji na Kiswago havikuhusishwa. Katika kukabiliana na changamoto ya tatizo la Maji katika vijiji hivi Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga iliomba kufanyika utafiti, uchimbaji na uwekaji wa pampu katika vijiji hivyo vya Sofi Mission, Sofi Majiji na Kiswago:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa visima hivyo na miundombinu ya usambazaji maji katika Vijiji vya Ngoheranga na Tanga?
- (b) Je, Serikali ina programu gani ya utekelezaji wa kuwapelekea maji wakazi wa Vijiji vilivyosahaulika na Sofi Mission, Sofi Majiji na Kiswago?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Mponda, Mbunge wa Ulanga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Miradi ya Vijiji 10 katika Halmashauri zote nchini. Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga inatekeleza Miradi ya Vijiji 10 katika Vijiji vya Lupilo, Minepa, Igota/Kichangani, Lupunga, Tanga, Malinyi, Makerere, Ngoheranga, Kipingo, Gombe, Mgolo na Nkonko ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Utafiti wa visima virefu umeanza katika Vijiji vya Ngoheranga (visima saba), Tanga (visima sita) na Nkonko (visima saba) na ujenzi wa mradi utanza mwezi Juni, 2015.
- (b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya *Sofi Mission*, Sofi Majiji na Kiswago havijasahaulika kupelekea huduma ya maji. Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2014 kupitia fedha za LGCDC imetenga kiasi cha sh. 56,500,000/= kwa ajili ya kugharamia utafiti, uchimbaji na ujenzi wa kisima kirefu kwa ajili ya vijiji vya Sofi Majiji na Sofi Mission. Aidha, kupitia bajeti ya Mfuko wa Jimbo, Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imekarabati visima viwili na kukamilisha utafiti wa visima vinne katika Vijiji vya Sofi Majiji na Kiswago.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muuliza swali Dkt. Mponda!

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Waziri kwa umakini wake wa ufuatiliaji wa masuala ya maji na hata majibu yake yanaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Hivyo Vijiji tunavyovizungumza vya *Sofi Mission*, Sofi Majiji na Kiswago, jibu la Wizara kwamba wametenga shilingi milioni 56, naomba nimpe kwanza taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba, hizo fedha zilizotengwa mpaka sasa hivi hazijaja na vile vile tayari Halmashauri wamefanyia mabadiliko kupeleka kwenye matumizi mengine. Kwa hiyo, fedha hizo hazipo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulionana na nilimwandikia barua Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa hakuna dhamira ya wazi kabisa kusaidia tatizo la maji katika vijiji hivyo vitatu naomba basi aweke utaratibu maalum na akaahidi kwamba utaingiza kwenye BRN 2015/2016. Swali la kwanza, je, ni lini ataanza kuingiza Vijiji hivyo vya Sofi Majiji, Sofi Mission na Kiswago katika BRN?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kule Ngoheranga kwenye Kitongoji cha Mkanga wamechimba kisima kimepatikana maji ya kutosha, sasa kwa nini wasitumie kisima hicho kutengeneza miundombinu ili kumaliza tatizo la maji Ngoheranga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana naye kwamba nimeshafika katika Jimbo lake, tumekagua miradi ya maji na haya anayoyapongeza ni kutokana na hizo ziara. Nakubaliana naye kwamba tumeshaongea, ameleta barua na vijiji anavyovisema tumeviingiza katika mwaka huu wa bajeti, asubiri tu bajeti itakapowasilishwa, atuunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba, kwa ajili ya kujenga miundombinu katika kijiji ambacho amesema kisima kimechimbwa basi, tutafuatilia ili fedha zipatikane na miundombinu ya maji ijenge, wananchi wanufaika na mradi huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, sina matatizo na Wizara ya Maji au mambo ya maji. Tatizo langu ni ubadhirifu unaofanywa na wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi hasa Idara ya Maji. Nilizungumza katika hotuba ya Waziri Mkuu, pesa zilizotumika ambazo ni hewa Kirando shilingi milioni 200, Matara shilingi milioni 125 na Namanyere shilingi milioni 120, hakuna ongezeko la maji wala hakuna kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Wizara inijibu, je, inataka kuwaona wafanyakazi kweli ni halali na majibu wanayoleta bila kwenda kuhakiki miradi ya maji katika Wilaya ya Nkasi jinsi fedha zinavyoliwa vibaya. Serikali ya CCM inatukwa na wananchi wa Nkasi kwa ajili ya watumishi wa Idara ya Maji, hakuna hatua inayochukuliwa bado wanajisifu kwamba Mbunge hatufanyi lolote. Nataka kujua, Serikali inachukua hatua gani kwa wabadhirifu wa Idara ya Maji katika Wilaya ya Nkasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba alitoa tuhuma hizo wakati akichangia hotuba ya Waziri Mkuu, lakini hakuishia pale, tulikuja tukashauriana, ametueleza mimi na Waziri na Waziri ameahidi kwamba jambo hili analifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haitoshi, Mheshimiwa Keissy tayari ameshaandika na barua na imekwenda mpaka TAKUKURU na nimepata kopi na Waziri amepata kopi. Kwa hiyo, namuahidi kwamba, barua niliyoipata nilimpa Katibu Mkuu. Kwa hiyo, TAKUKURU na Katibu Mkuu na maagizo ya Waziri kwa pamoja, tutapata majibu juu ya suala hilo na ikithibitika watachukuliwa hatua kali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Betty Machangu!

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takribani zaidi ya miaka 10 miradi inayofadhiliwa na *World Bank* ya Vijiji 10 kwenye kila Wilaya sasa hivi haijatekelezwa hata nusu katika nchi nzima. Je, Serikali ina tamko gani katika hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI;** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitofautiane naye kidogo kwa sababu si kweli kusema kwamba toka miradi hii imeanza kutekelezwa haijafikia hata nusu, maana yake hata mradi tu ukianza kutekelezwa ni dhamira tosha kwamba miradi hii imeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kusema labda ambayo haijakamilika, lakini kwa ujumla tumetoa taarifa Bungeni mara kwa mara na tumeona idadi ya watu wakiongezeka kupata maji na nimefanya ziara kwa Mheshimiwa Mrema kuna mafanikio makubwa na kwa Mheshimiwa Dkt. Chami ambapo yeye huko ndiko anakotoka, tumeona mafanikio makubwa. Kwa hiyo, nasema kwamba, aitie moyo Serikali na kwamba tatizo letu ni upatikanaji wa fedha, dhamira iko palepale ya kuhakikisha tunawafikia wananchi kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christowaja!

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Mradi wa Maji wa Mwankoko, Manispaa ya Mkoa wa Singida umekamilika, lakini ninachotaka kujua ni kwamba, ni kwa nini sasa Serikali kupitia SUWASA imeshindwa kuwalipa fidia watu wapatao 239 ambao iliwatoa katika maeneo yao na wanadai jumla ya sh. 1,510,427,654/= mpaka sasa? Wizara inasemaje kuhusu madai ya fidia ya watu hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mwankonko naujua na nimeshafika, lakini nasema kwamba kama kuna watu wanadai fidia jambo hilo tutalifanyia kazi na uzuri ni kwamba Wakurugenzi wote wa Mamlaka ya Maji wanakuwepo hapa kuanzia kesho. Kwa hiyo, hili suala tutakuwa tumelipatia ufumbuzi na nitakupa majibu endapo kweli watu hawa wanadai kwa mujibu wa sheria, basi watapatwa haki yao.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara inayofuata ya Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Salvatory Macheqli.

Na. 123

### **Meli ya MV. Butiama**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. SALVATORY N. MACHEMLI)** aliluliza:-

Meli ya MV Butiama imesimama kufanya kazi kwa muda mrefu sasa:-

- (a) Je, ni tatizo gani lililofanya kusimama kufanya kazi kwa meli hiyo?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuikarabati meli hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machelmi, Mhandisi mahiri na Mbunge na Ukerewe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Meli ya MV Butiama imesimama tangu mwaka 2010 kutokana na matatizo ya *engine, gearbox, viungo vya propeller shaft* na vifaa vingine vidogo vidogo katika meli hiyo. *Engine* na *gearbox* vinatakiwa kubadilishwa na kufungwa vipya.
- (b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kuitengeneza MV Butiama kama Mheshimiwa Rais alivyowaahidi wananchi wa Ukerewe. Mkandarasi wa kuitengeneza meli hiyo amepatikana, gharama ya matengenezo ikiwa ni Dola za Marekani laki saba (700,000.00), sawa na shilingi bilioni 1.33 (kama Dola moja kwa shilingi itakuwa ni sh. 1,900). Gharama hizo zinahusu ununuzi wa *engine* na *gearbox* pamoja na vifaa vyake, bima, usafiri na matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya matengenezo yanayowezesha Meli za Kampuni ya Huduma za Meli ikiwemo MV Butiama kuendelea kutoa huduma zinazokusudiwa kwa usalama. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha, meli hiyo bado haijatangenezwa na Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha za kutengeneza meli zake ikiwemo meli ya MV Butiama na mara fedha zitakapopatikana meli hiyo itatangenezwa.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Dkt. Mbassa!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Meli hii inayozungumziwa ilikuwa ni ya abiria pamoja na mizigo. Imekuwa ikifanya kazi kwa muda mrefu sana kiasi kwamba imezalisha fedha za kutosha. Sasa imesimama kwa takriban miaka mitano. Je, huu siyo uzembe wa Wizara kwa kushindwa kuitengeneza meli hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Ziwa Victoria, Meli ya MV Victoria imesimama vilevile kwa matatizo ya kiufundi ilihali sababu ni ileile.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na matengenezo ya meli hii ambayo ni kiungo muhimu cha usafiri kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, si kweli kwamba kuna uzembe katika kufanya matengenezo ya hizi meli kwa sababu suala linahusu fedha na kama fedha haipatikani, jambo hili haliwezi kuhesabiwa kama ni uzembe. Tumekuwa tukileta hapa maombi ya bajeti kwa ajili ya matengenezo ya hizi meli, lakini kwa bahati mbaya *performance* ya bajeti imekuwa haiwezeshi fedha hizi kupatikana na hivyo matengenezo kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu MV Victoria, ni kweli imesimama kwa matengenezo makubwa. Meli hizi zina umri mkubwa, kwa hiyo, zinaharibika mara kwa mara na sisi kama Serikali hatuwezi tukaacha meli ambazo tuna wasiwasi nazo ziendeleo kutoa huduma ilihali tunajua kwamba, jambo lolote baya linaweza kutokea. Kwa hiyo, tunazisimamisha zifanyiwe matengenezo ili kulinda maisha ya watumiaji wa meli hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, ambalo linaelekezwa Wizara ya Fedha, litaulizwa na Mheshimiwa Mustapha Akunaay.

Na. 124

**Leseni ya Umiliki wa Magari**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY** aliuliza:-

Kwa nini magari au matrekta ambayo yalikuwa mabovu yanadaiwa leseni ya umiliki wa magari (*Motor Vehicle License*) kwa kipindi ambacho magari au matrekta hayo hayakutumika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu! (*Makofi*)

Haya imetoshwa ameelewa. Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea na majibu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA)** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ni vitendo na wakati ni sasa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria inayotoza ada ya leseni ya mwaka kwa vyombo vya moto; vyombo vyote ambavyo haviko barabarani kwa sababu yoyote ile havijasamehewa ada hiyo. Hata hivyo, iwapo chombo husika kitaondolewa kwenye mfumo wa usajili kwa sababu yoyote ile ikiwa ni pamoja na ubovu katika kipindi husika, basi hakitahusika na ada hiyo kwa muda wote ambapo chombo hakitakuwa kwenye mfumo wa usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia sheria hiyo, tunashauri kwamba, wamiliki wa vyombo vyote vya moto ambavyo ni vibovu na havitumiki ikiwa ni pamoja na magari, ni vyema wakafika kwenye Ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania, ili kufuta usajili wa vyombo hivyo kwa muda na hivyo kutoendelea kutozwa ada ya leseni ya kila mwaka kwa kipindi chote ambapo vyombo hivyo havitakuwa vinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo haya, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, matrekta hayalipiwi na yamesamehewa ada ya leseni ya mwaka kutokana na umuhimu wake kwa wakulima.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Akunaay!

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kuiuliza Serikali kwamba, wakati wa kufuatilia ulipaji wa leseni hizo imekuwa ni usumbufu barabarani kwa magari kusimamishwa; je, ni kwa nini TRA isitume *invoice* kwa wahusika ambao hawajalipa badala ya kuwasumbua wasafiri wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, kwa nini Askari wa Usalama Barabarani (*Traffic Polices*) huzuia magari ambayo hayajalipa leseni wakati hii ni kodi ya kawaida na kutaka walipe kwa lazima badala ya kutumia taratibu za sheria za kudai kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza utaratibu wa kuyalipia magari palepale unaunganishwa na ukaguzi kwamba, kama mtu atakuwa hajafuatilia kulipa na ikatokea mpaka yuko barabarani ukaguzi ukafanyika na ikaonekana hakuwa amelipa, hicho ndicho kinasababisha alipishwe palepale. Kwa hiyo, utaratibu mzuri utakuwa ni wa kutimiza wajibu kwamba, hata yule ambaye anatakiwa kulipa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

anatakiwa atimize wajibu kwa kulipia ofisini ili kuondoa bughudha ama huu usumbufu ambao unaweza ukajitokeza kwa kulipia barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la kuwafuata ama kutuma *invoice*, tunakwenda kwenye utaratibu ambako malipo mengine yameshaanza kufanywa kwa kutumia mtandao. Jambo hilo linafanywa na Max-Malipo pamoja na taasisi nyingine kwenye malipo yanayohusiana na hilo. Kwa hiyo, hilo nalo tunakokwenda litaanza kufanyika kwa kupitia mtandao ambapo hakutakuwepo na ulazima wa kuonana kati ya anayelipa na anayetoza hiyo kodi au tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na lenyewe hilo litaondoa huo usumbufu na hakutakuwepo na foleni. Nasema Mheshimiwa Mustapha Akunaay naye anakubali hilo kwamba, mabadiliko ni vitendo na wakati ni sasa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leticia Nyerere!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na kero hizi za *licenses* za kiholela holela, kuna kero nyingi sana kuhusu magari nchini. Angalia mfano mtu ameingiza gari nchini ambayo ameinunua kwa Dola 2000, lakini inakuja inafanyiwa tathmini ya Dola 6000, je, hiyo ni haki kweli? Hii ni sawa na kumlazimisha mtoto wa umri wa miaka 14 awe na miaka 44. Hili halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu kwa Serikali; ni lini sasa Serikali yetu itawapa wananchi unafuu kwa kuzingatia tathmini halisi badala ya kubuni jinsi wanavyotaka? Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Leticia kwamba, hayo anayoyasema anatomia *experience* ya Mataifa mengine kwani ameishi sana na Mataifa ya watu ambao wanazingatia kila mmoja kutimiza wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Watanzania wengi wanatimiza wajibu wao vizuri katika masuala haya yanayohusu kuweka wazi bei za kitu halisi, bado tuna changamoto kwa hapa Tanzania ya mbinu za watu kutaka kukwepa kodi. Kwa hiyo, hilo ndiyo linalosababisha zitumike taarifa rasmi za kwenye mfumo wa mawasiliano wa nchi na nchi kuhusu bidhaa ile inayouzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo linatokea ni lipi! Inatokea kwenye mfumo bei imetajwa nyingine, halafu inatokea yule ambaye anataka kununua gari ile anasema niletee *invoice* yenye bei hii.

Sasa Mamlaka ya Mapato ikitambua kwamba, kwenye mfumo bei ya gari lile ni kiasi fulani, lakini wale wanaouziana wameandika kiasi fulani, hapo ndipo ambapo huwa wanachukua bei ile ambayo iko kwenye mfumo.

Kwa hiyo, ikitokea bidhaa ile bei ya kwenye mfumo na ile iliyoandikwa kwenye *invoice* ni ile ile, hakuna tathmini au makadirio mengine ambayo yanafanywa na Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwa Watanzania kwamba, tujue kodi ndiyo kujitegemea na ndiyo maendeleo, tutumie bei halisi ili tusije tukaleta huu usumbufu wa kuwa na makadirio ya aina tofauti na ile bei ambayo ilikuwa imetolewa kwenye mfumo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala.

Na. 125

**Kuongeza Bajeti ya Afya**

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuongeza Bajeti ya Afya ili ifikie Azimio la Abuja la asilimia 15?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa Azimio la Abuja ambalo linataka Bajeti ya Afya ifikie asilimia 15 ya bajeti yote ili iweze kuboresha huduma katika Sekta ya Afya. Aidha, ni kweli kwamba, bajeti ya afya haijafikia asilimia 15 ya bajeti yote kwa mujibu wa Azimio la Abuja kutokana na ufinyu wa mapato ukilinganisha na mahitaji ya Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2013/2014, Sekta ya Afya ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 1,497.8 ambazo ni sawa na asilimia 10 ya bajeti yote ya Serikali baada ya kutoa *Consolidated Fund Services (CFS)* na mwaka huu wa fedha 2014/2015, Sekta ya Afya imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1,588.2 ambayo vilevile ni sawa na asilimia 10 ya bajeti yote. Bajeti hii ya Sekta ya Afya inajumuisha bajeti ya Afya katika Mikoa na Halmashauri, ambapo bajeti hizo zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, suala la afya ni mtambuka. Kwa kuwa, afya ni suala mtambuka, tunaweza kupunguza mahitaji ya fedha katika sekta hii muhimu kama tutaweza kuimarisha huduma katika sekta zingine mtambuka kama vile maji, lishe, mazingira, makazi na miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Maeneo haya yasipohudumiwa vizuri yanaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa na ajali na hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya bajeti katika sekta hii muhimu, hususan dawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, swali la nyongeza!

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa alichokifanya jana na kukiwakilisha vyema kizazi changu cha viongozi. Kwa lugha ya Kipolisi tungesema alichoshusha jana ni kushusha kitu kizito chenye ncha kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la nyongeza, kwa kuwa, hata hiyo asilimia 10 inayotengwa haiendi, ni nini kitakuwa kipaumbele cha Serikali katika mwaka wa fedha ujao ikizingatiwa kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na mimi hapa ni Marais tarajali? Ni nini yatakuwa hasa mambo ya kipaumbele ya kufanya kwenye Serikali ya mabadiliko ni vitendo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna njia mbadala za kutengeneza fedha kwenye Sekta ya Afya ambazo hazijapewa kipaumbele kwenye nchi yetu. Nini kifanyike ili njia hizo ziweze kutumika kupata fedha kutoka kwenye vyanzo mbadala katika Serikali ijayo?

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nampongeza Dkt. Kigwangala kwa ujasiri wake na kuibeba ajenda ya Watanzania. Tunaungwanishwa na Dkt. Kigwangalla na ajenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kipaumbele katika bajeti inayofuata. Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla imekuwa na jitihada kubwa za kuweka utaratibu wa kuhakikisha makusanyo yanaongezeka (kwa sababu kinachokwamisha kufikia ile asilimia 15 ni makusanyo), ili kuweza kuhakikisha kwamba, Azimio hilo linatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo Serikali na Wizara ya Fedha inajitahidi ni kuhakikisha kwamba, matumizi yanaelekezwa katika mambo muhimu ambapo pia afya ni jambo muhimu kwa Taifa letu kama ambavyo iko kwa Mataifa mengine. Kwa hiyo, kipaumbele cha Serikali katika kuhakikisha tunafikia lengo hilo kama ambavyo bajeti imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, itakuwa ni kuongeza makusanyo na kubana matumizi yasiyo na lazima ili fedha hizo ziweze kwenda katika jambo hili la muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa awamu inayofuata ambayo ameisemea Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, kama awamu iliyopita imeweza kufika asilimia 10, niwahakikishie Watanzania kwamba, awamu inayofuata itafikisha hiyo asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili alilouliza ni kwamba, wapi njia mbadala ya fedha itapatikana? Tumeisemea kwanza, hata katika sekta yenyewe tumepata taarifa na ushuhuda kwamba, maeneo ambayo wameweza kukusanya vizuri maduhuli yanayotokana na sekta yenyewe na wakatumia utaratibu wa kielektroniki, wameweza kuongeza makusanyo. Kwa hiyo, hiyo nayo itaweza kwenda kwenye matumizi hayo ya kuongeza dawa na bajeti kwenye sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo hata jana nililisema ni udhibiti. Mara zote Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya dawa zinazotakiwa kwenda kwa ajili ya wananchi, lakini kumekuwepo na utaratibu na mazoea kwamba, kila mtu anayeugua anaambiwa akanunue dawa katika duka linalotazamana na hospitali anapotibiwa. Kwa hiyo, udhibiti utaongezeka ili kuhakikisha dawa ambazo zimenunuliwa kwa ajili ya wananchi hazipitii madirishani na kwenda kuuzwa katika maduka binafsi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yamekwisha na sasa ni matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba leo tarehe 1 Juni, 2015 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, itakuwa na maonesho ya kazi na majukumu yanayotekelezwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, Wizara hiyo inawaalika Waheshimiwa Wabunge wote, Watumishi wa Serikali na wageni wote kutembelea maonesho hayo kwenye viwanja vya maonesho katika Jengo la Habari.

Naomba niwatambue wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao ni Bi. Consolata Mgimba, Naibu Katibu Mkuu. Ahsante na karibu. (Makofi)



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Wengine ni Profesa Eustella Bhalalusesa, Kamishna wa Elimu. Karibu. Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara hii. Wakuu wa Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na wadau mbalimbali wa elimu. Karibuni wote. *(Makofi)*

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, kutoka Jimboni kwake ambao ni Mheshimiwa Hafsa Juma Kilingo na Mheshimiwa Mwanaharusi Hamis Jarufu, Madiwani kutoka Jimbo la Bagamoyo. Wako wapi hao Waheshimiwa Madiwani, kutoka Jimbo la Bagamoyo? Karibuni sana. Mbunge wenu anachapa kazi na asanteni kwa kumsaidia. *(Makofi)*

Wageni 60 wa Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoka Jimboni kwake, wako wapi kutoka Same Mashariki, karibuni sana Mbunge wenu ana chapa kazi mnamwona. *(Makofi)*

Wageni wengine ni 52 wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ambao ni Waheshimiwa Madiwani 19 wakiongozwa na Mheshimiwa Musa Matoka na Viongozi 33 wa vijana wakiongozwa na Ndugu Kei Mbwambo, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM, Wilaya ya Same wanatoka Jimbo la Same Mashariki wako wapi hao, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Suzan Lyimo, Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao ni wanafunzi 47 wa Kampala *International University* wakiongozwa na Ndugu David Payovera wako wapi hao karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni 52 wa Mheshimiwa Diana Chilolo, ambao ni Wana Kwaya wa Moyo Mtakatifu wa Yesu, Kanisa Katoliki Jimbo la Singida, wageni kutoka Jimbo la Singida karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Rahel Mashishanga, ambao ni Wenyeviti wa Mitaa (CHADEMA) ya Viwandani na Sanungu, Bariadi Mjini ambao ni Lazaro Joseph Singibala na Ndugu Ndilanha Maduhu Igumi, wako wapi? Karibuni sana. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Lusinde ambaye ni Katibu wa Jimbo na Kada wa CCM Ndugu Patrick Nyambuya, yuko wapi Ndungu Patrick Nyambuya. Ahsante kwa kumsaidia Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni ni wanafunzi 89 wa Sekondari ya Maria De Mattias, Dodoma wako wapi hao wanafunzi? Karibuni sana kwa ziara ya mafunzo msome kwa bidii na wengine ni wanafunzi 26 na Walimu saba kutoka shule ya Msingi Mazengo, naomba Walimu saba na wanafunzi wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI  
MHESHIMIWA LAZARO SAMUEL NYALANDU (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA  
2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyochambua na kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kama Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, aliyeteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hivyo kuwa msaidizi wangu mkuu katika kusimamia elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja na Mheshimiwa Innocent Sebba walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kupata fursa ya kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuwakilisha wananchi katika Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Katibu Mkuu, Profesa Sifuni Ernest Mchome; Naibu Katibu Mkuu, Bibi Consolata Phillipo Mgimba; Kamishna wa Elimu, Profesa Eustella Peter Bhalalusesa; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi za elimu zilizo chini ya Wizara yangu kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru Wahadhiri, Wakufunzi, Walimu na Watumishi wote kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Napenda pia kuwashukuru, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Washirika wa Maendeleo na Taasisi Zisizo za Serikali, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Wanataaluma, Wanafunzi na Wazazi au Walezi kwa ushirikiano wao katika kuiendeleza Sekta ya Elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu kwa kifo cha Mbunge mwenzetu mpendwa, Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote waliofiwa na ndugu na wapendwa wao kutokana na maradhi, ajali, majanga na matukio mbalimbali yaliyotokea katika nchi yetu. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi pamoja na kuwapa faraja wote walioondokewa na wapendwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; kwa mujibu wa Hati Idhini iliyounda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina majukumu kama yalivyoainishwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa nne hadi tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2014/2015; naomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kuanzia tarehe 1 Julai, 2014 hadi tarehe 30 Aprili, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Maduhuli Mwaka 2014/2015; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu ilikadiria kukusanya jumla ya sh. 213,447,418,474.00

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

ambapo sh. 9,108,383,900.00 zilipangwa kukusanywa na Idara na sh. 204,339,034,574.00 zilipangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 30 April, 2015 kiasi cha maduhuli yaliyokusanywa ni Sh. 162,811,384,265.97 sawa na asilimia 76.3 ya makadirio. Kati ya makusanyo hayo, Sh. 5,136,353,002.60 zilikusanywa na Idara na sh. 157,675,031,263.37 zilikusanywa na Taasisi. Kiasi kikubwa cha maduhuli kilitokana na malipo ya ada na huduma mbalimbali za elimu zilizotolewa na Idara na Taasisi za Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2014/2015, bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu, ilikuwa sh. 344,207,056,000.00. Kutokana na marekebisho ya bajeti kwa Wizara zote, kiasi cha sh. 2,423,036,000.00 kilipunguzwa kutoka kwenye bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika robo ya pili, bajeti ya Wizara iliongezwa kwa sh. 4,490,000,000.00 kwa ajili ya kulipia deni la *Inter University Council for East Africa* na kufikia sh. 346,274,020,000.00. Kati ya fedha hizo, mishahara ilikuwa sh. 268,756,248,000.00 ambapo Mishahara ya Idara ilikuwa sh. 52,976,832,000.00 na mishahara ya Taasisi ilikuwa sh. 215,779,416,000.00. Matumizi Mengineyo yalikuwa sh. 77,517,772,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015, kiasi cha sh. 286,043,459,577.02 sawa na asilimia 83.1 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida kimepokelewa na kutumiwa na Wizara yangu. Kati ya fedha hizo, sh. 238,592,738,417.67 ni za mishahara. Matumizi Mengineyo yalikuwa ni sh. 47,450,721,159.35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za Matumizi Mengineyo zilizopokelewa, sh. 17,556,516,175.35 zilitumika kulipa madeni ya baadhi ya Taasisi na ya Wizara ambayo yalikuwa tayari yamehakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali ambapo sh. 8,956,743,006.65 ni madeni ya Taasisi na sh. 8,599,773,168 ni madeni ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015; mwaka wa fedha 2014/2015, jumla ya sh. 454,813,333,000.00 ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara yangu. Hata hivyo, kiasi cha sh. 1,200,000,000 kilipunguzwa na kufikia sh. 453,613,333,000.00, ambapo fedha za ndani zilikuwa sh. 383,734,000,000.00 na fedha za nje zilikuwa sh. 69,879,333,000.00. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015, jumla ya sh. 335,003,135,231.66 sawa na asilimia 73.9 zilikuwa zimepokelewa ambapo sh. 305,822,570,000.00 ni fedha za ndani na sh. 29,180,565,281.66 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015; Wizara yangu ni moja ya wadau wakubwa wa Sekta ya elimu ambayo ilijiwekea vipaumbele vikuu viwili katika mwaka wa fedha 2014/2015. Vipaumbele hivyo ni:

- (a) kuinua ubora wa elimu na kujenga Stadi stahiki katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo; na
- (b) Kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa usawa katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa vipaumbele vya Sekta, Wizara yangu ilifanya kazi kwa kushirikiana na Wizara, Taasisi zenye shule na vyuo, Taasisi Zisizo za Serikali ambazo zinamiliki na kuendesha shule na vyuo mbalimbali nchini pamoja na wadau wengine.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii sasa kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu kulingana na Hati Idhini ya Wizara yangu katika kutekeleza vipaumbele vya Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utungaji wa Sera za Elimu; moja ya majukumu ya Wizara yangu ni kubuni na kutunga Sera mbalimbali kuhusu Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Juu. Lengo la Sera hizi ni kutoa mwelekeo katika kutekeleza majukumu ya uendeshaji wa Elimu na Mafunzo katika ngazi mbalimbali. Katika eneo hili, mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu imefanya yafuatayo:-

- (a) Ilikamilisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 13 Februari, 2015.
- (b) Rasimu ya andiko la uanzishwaji wa Bodi ya Kitaalam ya Walimu imekamilika. Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuanzisha Bodi ya Kitaalam ya Walimu umeandaliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Kitaalam ya Makatibu Wakuu wa Wizara (IMTC);
- (c) Mtaala wa darasa la kwanza na la pili umeandaliwa kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mtaala wa mwaka 2005.
- (d) Waraka wa Elimu Namba (4) wa mwaka 2014 unaoipa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) jukumu la kuandika Vitabu vya Kiada na kuratibu utayarishaji na utoaji wa Ithibati kwa vitabu vya ziada na vifaa vingine vya kujifunzia kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu umetolewa.
- (e) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera za Elimu na Mafunzo umeimarishwa kwa kuandaa na kutoa nyaraka kama zilivyoainishwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 12:
- (f) Mkakati wa kuhuisha na kuoanisha programu za Elimu na Mafunzo kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira umeendelea kutekelezwa kwa kufanya yafuatayo:-
  - (i) Chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ilishiriki kuandaa na kukamilisha miundo ya Mitaala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu pamoja na muundo wa viwango vya Elimu ya Juu.
  - (ii) Vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika fani za Biashara na TEHAMA vilivyoandaliwa chini ya uratibu wa IUCEA vimekamilika. Vyuo na Taasisi za Ithibati (NACTE na TCU) vimeanza kutumia vigezo hivyo katika kupitia Mitaala ya Biashara na TEHAMA;
  - (iii) Mitaala 10 ya Kitaifa ngazi ya Astashahada, Stashahada na Stashahada ya Juu na Mitaala 60 ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi inayozingatia umahiri na mahitaji halisi ya soko la ajira na maendeleo ya Taifa imetayarishwa na kuidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usajili wa Shule; katika kuimarisha mfumo wa usajili wa shule, Kitengo cha Usajili wa Shule kimepandishwa hadhi kuwa Idara ya Ithibati ya shule yenye vitengo vitatu ambavyo ni Ithibati ya Shule za Serikali, Ithibati ya Shule zisizo za Serikali na Uwekaji Viwango vya Miundombinu ya Shule chini ya Ofisi ya Maendeleo ya Elimu Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kusajili shule kwa lengo la kuzipatia Ithibati na Idhini ya kufundisha masomo husika. Mwaka wa fedha 2014/2015, Shule za Awali na

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Msingi 60 zilisajiliwa. Kati ya hizo, shule 57 ni za Binafsi na tatu ni za Serikali ambapo shule binafsi za Awali pekee ni mbili na Shule za Msingi pekee ni mbili. Aidha, Shule 45 za Sekondari zilisajiliwa kati ya hizo shule 12 ni za Serikali na 33 ni za Binafsi. Shule 32 ni za kidato cha kwanza hadi cha nne na 13 za kidato cha tano hadi cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi; hili ni jambo muhimu sana katika kuimarisha ubora wa Elimu na Mafunzo yanayotolewa katika ngazi hiyo. Hadi kufikia Aprili, 2015, yafuatayo yametokeleza:-

- (a) Asasi 11,531 kati ya 17,021 zilizolengwa sawa na asilimia 67.7 zilifanyiwa tathmini ya Uthibiti Ubora. Asasi hizo zilijumuisha shule za Awali na Msingi 8,197, Sekondari 3,222 na Vyuo vya Ualimu 112;
- (b) Mfumo wa Uthibiti Ubora wa kielektroniki unatengenezwa kwa kufanya majaribio katika Wilaya saba za Magu, Mtwara Vijijini, Bagamoyo, Makete, Temeke, Siha na Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi, Ofisi za Uthibiti Ubora zimefunguliwa katika Halmashauri nane za Wilaya mpya za Kaliua, Njombe Mjini, Wanging'ombe, Makambako, Nyang'wale, Busega, Geita Mjini na Nyasa. Ofisi katika wilaya nyingine zitaendelea kufunguliwa kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Walimu 217 wameteuliwa kuwa Wathibiti Ubora wa Elimu Msingi na kupangwa katika ofisi za Ukaguzi wa Shule za Kanda na Wilaya. Magari mawili yamenunuliwa na 45 yapo katika hatua za mwisho za ununuzi kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi katika ofisi za Kanda na Wilaya. Utekelezaji wake utanza tarehe 1 Julai, 2015. Aidha, katika kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, Idara ya Ukaguzi wa Shule imepandishwa hadhi kuwa Idara ya Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi ambapo itakuwa na watendaji hadi ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya Ualimu yaliendelea kutolewa katika Vyuo vya Serikali na vya binafsi na kuwezesha upatikanaji wa Walimu wenye sifa na weledi na kukabiliana na upungufu wa Wwalimu, hususan wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Katika mwaka 2014/2015 yafuatayo yametokeleza:-

- (a) Programu ya mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati ya miaka mitatu kwa wahitimu wa Kidato cha nne wenye ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu imeanzishwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Wanachuo 2,142 wamedahiliwa katika mwaka wa masomo 2014/2015. Kati yao 1,964 ni Stashahada ya Elimu ya Sekondari na 178 ni Stashahada ya Sayansi Shule za Msingi);
- (b) Stashahada ya Juu ya Masomo ya Sayansi na Hisabati kwa ajili ya shule za Sekondari imeanzishwa katika Vyuo vya Ualimu vya Korogwe, Monduli na Kleruu ambapo jumla ya wanachuo 365 wamedahiliwa;
- (c) Wawezeshaji wa Kitaifa 24 wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wakufunzi wa Walimu wa darasa la kwanza na la pili kumudu Stadi za KKK. Aidha, Wakufunzi 480 wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo Walimu wa darasa la kwanza na la pili kufundisha Stadi za KKK;
- (d) Vyuo vya Ualimu vimepandishwa hadhi ambapo sasa vitapewa lthibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi badala ya kusajiliwa na ofisi ya Kamishna wa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Elimu. Mambo mengine yaliyotekelezwa yameelezwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 19 hadi 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uratibu wa Taasisi na Wakala; Wizara yangu ina jumla ya Taasisi na Wakala 89 za Elimu na Mafunzo. Kati ya hizo, tatu ni za Ithibati na Uthibiti Ubora wa Elimu ya Ufundi Stadi, Elimu ya Ufundi na Eimu ya Juu; mbili ni za Mitaala na Mitihani; mbili za Mikopo na Ruzuku mbalimbali; moja ni Bodi ya huduma za Maktaba; moja ni Tume ya Taifa ya UNESCO na kituo kimoja cha 'Hazina Data' kilichopo Kituo cha Maendeleo Dakawa. Aidha, zipo Taasisi za mafunzo 79 zikiwemo 28 zinazoendeshwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara zimeainishwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 21 hadi 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi na Utekelezaji wa Programu na Miradi; katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilitekeleza miradi mbalimbali kama ifuatayo:

- (a) Iliendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Kujifunza na Kufundisha katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo kupitia mafunzo kazini ya Walimu na miradi mbalimbali kama vile, Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kama maelezo yalivyotolewa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 56 hadi 57.
- (b) Iliimarisha mfumo wa upatikanaji na utoaji wa taarifa za elimu (*Education Sector Management Information System - ESMIS*) katika ngazi zote na kuhifadhi taarifa na takwimu katika ofisi za Wakala wa Serikali Mtandao (e- GA).
- (c) Iliendelea kutegemeza utoaji wa elimu ya msingi nchini kupitia Mpango wa Kitaifa wa kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LANES).
- (d) Iliendelea kutegemeza utoaji wa elimu ya sekondari kama maelezo yalivyotolewa katika kifungu cha kidogo cha (i – iv) katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 58 hadi 59.
- (e) Ilingia makubaliano na Serikali ya Canada kupitia Umoja wa Vyuo vya Ufundi na Taasisi nchini Canada (*CICan*) katika kutekeleza Mpango wa Kuongeza Ujuzi wa Kuweza Kuajiriwa/Kujajiri ulioanza mwaka 2014 - 2019 kwa Watanzania 1,200 katika Sekta za Utalii, Gesi Asilia, Mafuta na Madini.
- (f) Iliendelea kufanya tafiti ili kukamilisha mradi wa '*Education and Skills for Productive Jobs*' ambao utakuwa ni mwendelezo wa mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ambao unakwisha ifikapo Januari 2016;
- (g) Iliunda Kamati ya kuandaa utekelezaji wa mradi wa *Partnership for Applied Science, Engineering and Technology (PASET)* katika ngazi ya taifa; na
- (h) Ilianzisha taratibu za kujiunga na mradi wa *African Centres of Excellence* unaolenga kuwa na vituo mahiri vya utafiti vya kikanda katika baadhi ya Vyuo Vikuu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa; Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ilitekeleza mikakati ya Matokeo Makubwa Sasa. Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka mmoja (2013/2014) Sekta ya Elimu imefanikiwa kwa asilimia 81 na kushika nafasi ya kwanza katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya mikakati hiyo.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mafanikio ambayo tayari yamehakikiwa na 'Presidential Delivery Bureau' ni kama yalivyoorodheshwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 60 hadi 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utekelezaji wa mikakati hii ni kupanda kwa ufaulu wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi kutoka asilimia 50.6 mwaka 2013, hadi kufikia asilimia 56.99 mwaka 2014 na kupanda kwa ufaulu wa mtihani wa kumaliza Kidato cha Nne kutoka asilimia 57.09 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 69.76 mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto; katika utekelezaji wa majukumu na bajeti ya mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilipata changamoto katika maeneo mbalimbali inayoyasimamia kama ifuatavyo:-

- (i) Kuimarisha mifumo ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Sera za Elimu, hususan, katika maeneo yaliyoguswa na ugatujaji;
- (j) Upatikanaji wa rasilimali fedha za kutosha na kwa wakati na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara yakiwemo yafuatayo:-
  - (i) Kulipa madeni ya wazabuni na huduma nyingine ambayo sasa yanafikia sh. 45,855,370,632.70 ambapo sh. 25,195,672,974.20 ni deni la wazabuni wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi na sh. 5,148,207,930.00 ni deni la posho za Wahadhiri;
  - (ii) Kuwezesha upanuzi wa miundombinu ya Elimu ya Ufundi ili kukabiliana na mahitaji ya Taifa katika fani za ufundi;
- (k) Changamoto ya kupata Walimu mahiri wa kufundisha Stadi za KKK kwa kiwango cha kutosha kwa wanafunzi wa madarasa ya chini (Darasa la I na II);
- (l) Namna ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ili ikaribiane au kupita ile ya nchi jirani ambazo zina kiwango cha wastani wa asilimia tano ya rika lengwa ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.7 kwa Tanzania;
- (m) Upatikanaji wa wataalam wa Kitanzania katika mnyororo wa thamani katika fani za gesi, mafuta, chuma, urani, makaa ya mawe na madini mengine; na
- (n) Upatikanaji wa rasilimaliwatu na rasilimali nyingine za kutosha ili kuwezesha Uthibiti Uboru wa Elimu na Mafunzo kufanyika kwa ufanisi kulingana na miongozo ya Uthibiti Uboru katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kama zilivyoainishwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 65 hadi 66.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi na nyingine hazina budi zipewe ufumbuzi wa haraka kabla hazijaendelea kuwa kero kubwa katika azma yetu ya kupata Taifa lenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vipambebe na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2015/16: Vipambebe vya Sekta ya elimu vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka 2015/16 ni vifuatavyo:-

- (a) Kuongeza upatikanaji wa fursa ya elimu kwa usawa katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo;

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

- (b) Kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi stahiki katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo, na;
- (c) Kuimarisha taasisi za usimamizi wa ubora wa elimu pamoja na Ufuatiliaji na Tathmini ili zitekeleze majukumu ya kuhakikisha elimu bora inatolewa katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Hati Idhini iliyotolewa mwaka 2010 na urekebishaji wa muundo wa Wizara uliofanyika 2015, Wizara yangu inalenga kutekeleza vipaumbele vya Sekta katika maeneo yafuatayo:-

- (a) Utungaji na utekelezaji wa Sera za Elimu;
- (b) Ithibati ya Shule;
- (c) Uthibiti ubora wa elimu;
- (d) Mafunzo ya Ualimu, hususan Ualimu wa Sayansi, Hisabati, Ufundi, Lugha na KKK;
- (e) Uratibu wa shughuli za Taasisi na Wakala; na
- (f) Usimamizi wa utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la utungaji na utekelezaji wa Sera za Elimu, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuanza utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kulingana na Mkakati wa Utekelezaji;
- (b) Kupitia na kurekebisha sheria na miongozo mbalimbali ya elimu ili kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014;
- (c) Kukamilisha uundwaji wa Mamlaka ya Ithibati na Uthibiti Ubora Elimu Msingi na Sekondari ili kuhakikisha kuwa utoaji wa elimu unazingatia Sera, Miongozo na Mitaala ya elimu yenye kukidhi mahitaji ya soko na jamii;
- (d) Kuimarisha Taasisi ya Elimu Tanzania katika kushughulikia Ithibati na Uthibiti wa vitabu, zana na vifaa mbalimbali vya Elimu Msingi na Sekondari;
- (e) Kuhuisha mitaala na kuimarisha mfumo wa utoaji wa Elimu ya Juu, Ufundi na mafunzo ya Ufundi Stadi ili kutoa elimu kulingana na mahitaji halisi ya soko la ajira na maendeleo ya Taifa;
- (f) Kuoanisha programu za Elimu ya Juu pamoja na Ufundi ili utoaji wa elimu hiyo uzingatie mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi kwa maendeleo ya Taifa letu;
- (g) Kuandaa mfumo, miundo na taratibu nyumbufu za kumwezesha Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali katika mikondo ya kitaaluma na kitaalam;
- (h) Kuandaa mfumo, muundo mpya wa Taifa wa Tuzo na Tathmini pamoja na kuhuisha taratibu za kujiunga na ngazi mbalimbali za elimu ili kuendana na muundo mpya wa Taifa wa Tuzo na Tathmini;



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tupunguze kelele. Endelea Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti:

- (i) Kuandaa mwongozo wa miundombinu na vifaa vya maabara na mwongozo wa kusimamia utekelezaji wa mitaala kwa kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi wenye mahitaji maalum;
- (j) Kuandaa mwongozo wa matumizi ya Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni katika kujifunza na kufundishia;
- (k) Kuandaa mikakati ya kutekeleza makubaliano, mikataba, maamuzi ya Kikanda na Kimataifa ikiwemo kupima kiwango cha utekelezaji wa mpango wa Afrika wa Elimu, Malengo ya Milenia na maendeleo yanayoishia 2015; na
- (l) Kuendelea kuoaisha mifumo na Mitaala ya ngazi zote za elimu na ile ya Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Ithibati ya Shule, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Itasajili shule za Msingi na Sekondari kwa kutilia mkazo zaidi shule za Ufundi na Sayansi pamoja na vituo vya Elimu ya Watu Wazima na Vituo vinavyotoa Elimu ya Sekondari nje ya Mfumo Rasmi;
- (b) Itaimarisha mfumo na taratibu za usajili wa shule ili kuendana na mahitaji halisi ya soko na maendeleo ya Taifa;
- (c) Itaendelea kuelimisha umma kuhusu taratibu za usajili wa shule; na
- (d) Kusajili Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ili kuendelea Kuthibiti Ubora wa Elimu Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Itafuatilia ubora wa elimu katika asasi 17,242 zikiwemo 8,225 za Elimu ya Msingi na 313 za Sekondari zilizokuwa katika utepe mwekundu, Asasi 6,672 za Elimu ya Msingi na 1,722 za Sekondari zilizokuwa katika utepe wa njano.
- (b) Itaimarisha mfumo na taratibu za Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi ili kuwa na ufanisi zaidi;
- (c) Itaimarisha ofisi za Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi kwa kuongeza idadi ya Wathibiti Ubora 570, kutoa mafunzo kwa Wathibiti Ubora 517, kununua magari 35, kompyuta 782, samani na vifaa vya ofisi kwa ajili ya Wilaya mpya zilizoanzishwa; na
- (d) Itakamilisha ujenzi wa ofisi za Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi za Wilaya za Hai, Urambo, Sumbawanga Mjini, Masasi, Mtwara Mjini na Namtumbo.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia utoaji wa mafunzo ya Ualimu, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Itaendelea kuimarisha ufundishaji wa Walimu wa Stadi za KKK ikiwemo kuanzisha maabara saba za lugha katika vyuo vya Ualimu chini ya mpango wa 'LANES';
- (b) Itaendelea kutekeleza mikakati ya kupunguza uhaba wa Walimu wa Sayansi na Hisabati; na
- (c) Itahuisha Mkakati wa Menejimenti na Maendeleo ya Walimu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia Taasisi na Wakala, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Itajenga uwezo wa taasisi za usimamizi wa ubora wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Juu, Ufundi na Ufundi Stadi ili kuhakikisha kuna elimu bora katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo;
- (b) Itainua ubora wa Elimu ya Juu na Ufundi ili kuendana na maendeleo ya kizazi cha tatu na kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 kupitia tafiti na mafunzo yanayokidhi mahitaji ya jamii na stadi za mafunzo;
- (c) Itaimarisha Ufundishaji na Kujifunza kwa kuweka mifumo ya kidigiti (TEHAMA) itakayoweza Walimu na wanafunzi kupata maandiko muhimu kwa maendeleo ya elimu na Taifa kwa ujumla; na
- (d) Itakamilisha miradi ya *African Centres of Excellence, Skills for Productive Jobs na Partnership for Applied Science, Engineering and Tachnology – PASET* ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya mwaka 2015/2016 ya Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara yameoneshwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kutoka ukurasa wa 73 hadi 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Usimamizi na Utekelezaji wa Programu na Miradi, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu: Itafanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Mwalimu; na kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa programu za Elimu.
- (b) Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa:
  - (i) Kupanga shule kulingana na madaraja ya ufaulu;
  - (ii) Kutoa mafunzo ya Kujenga Uwezo wa Walimu na Wanafunzi kwa shule za Msingi;
  - (iii) Kutoa mafunzo ya Kujenga Uwezo wa Walimu na Wanafunzi kwa shule za Sekondari;
  - (iv) Kuwezesha utoaji wa motisha kwa shule na Halmashauri zilizoonyesha mafanikio katika matokeo ya mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne;

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (v) Kuwezesha ujenzi wa nyumba 40 za Walimu katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi; na
  - (vi) Kuwezesha uratibu, ufuatiliaji na uendeshaji wa shughuli za Miradi ya Elimu, ikiwemo miradi ya BRN.
- (c) Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu:
- (i) Kukamilisha maandalizi na kuanza ukarabati wa Vyuo sita vya Ualimu, ujenzi wa Vyuo vya Mkoa vinne vya Ufundi Stadi na ujenzi wa hosteli Morogoro V TTC pamoja na jengo la maabara katika Chuo cha Ufundi Arusha;
  - (ii) Kujenga uwezo wa Vyuo vya Ualimu nchini katika kuandaa Walimu wa Sekondari katika fani za Sayansi na Teknolojia;
  - (iii) Kujenga uwezo wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika kuandaa na kufundisha Mitaala inayozingatia umahiri; na
  - (iv) Kununua mitambo, zana na vifaa vya kufundishia, vitabu, vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya Chuo cha Ufundi Arusha, Vyuo vya Ualimu na Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro;
- (d) Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi:
- (i) Kuandaa zana za kufanyia tathmini endelevu ya upimaji Stadi za KKK na kuingiza katika mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ubora wa shule, kukamilisha kiunzi cha udhibiti wa ubora pamoja na kujenga uwezo wa matumizi ya kiunzi hicho;
  - (ii) Kukamilisha Mwongozo wa Mwalimu wa Stadi za Maisha na kuchapisha vitabu vya Stadi za maisha kwa madarasa ya kwanza na la pili; darasa la tatu na la nne na darasa la tano mpaka la saba;
  - (iii) Kuendesha mafunzo kuhusu KKK kwa Maafisa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Walimu wa Darasa la kwanza, la pili, la tatu na la nne, Wakufunzi wa Uwezeshaji, Walimu na Wanafunzi kuhusu TEHAMA, Maafisa 100 kuhusu Utafiti wa KKK na Uwekaji wa Mikakati ya Mazingira rafiki shuleni; na
  - (iv) Kujenga uwezo wa Watendaji katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri juu ya matumizi sahihi ya mwongozo wa Huduma ya Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni.
- (e) Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, kutekeleza ni pamoja na:
- (i) Kufuatilia ujenzi na upanuzi wa miundombinu katika shule 528 na tathmini ya matokeo ya shule 264 katika Halmashauri 132;
  - (ii) Kuimarisha 'Hazina Data' na Mfumo wa kukusanya, kuchakata na kuhifadhi takwimu, kufanya mapitio ya zana za kukusanya takwimu

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

pamoja na kuwezesha utoaji mafunzo kwa watumishi wa kitengo cha takwimu;

- (iii) Kutoa mafunzo kazini kwa Walimu 10,000 wa shule za sekondari nchini;
  - (iv) Kuzijengea uwezo Taasisi za Ithibati ya Elimu Msingi, ADEM, TIE na NECTA; na
  - (v) Kufanya ufuatiliaji wa ruzuku za uendeshaji wa shule katika Halmashauri na ukaguzi wa mahesabu ya Mradi.
- (f) Mradi wa Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA: Kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na kujifunza.
- (g) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Mpango wa Elimu kwa Waliokosa (Ndiyo Ninaweza); (i) Kuwajengea uwezo wawezeshaji 100 wa vituo vipya 20 vilivyoko katika Halmashauri zenye watu wengi wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu; na (ii) Kuwezesha Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya vituo vya kisomo cha Ndiyo Ninaweza katika Halmashauri 20.
- (h) Mpango wa Kuongeza Ujuzi wa Kuweza Kuajiriwa au Kujiajiri (*Improving Skills Training for Employment Program-ISTEP 2014-2019*): (i) Kuanza kutoa mafunzo katika Sekta za Utalii, Gesi Asilia, Mafuta na Madini kwenye vyuo sita vya Tanzania vya Awamu ya Kwanza kwa kushirikiana na vyuo sita vya Canada ambavyo tayari wameshaingia navyo ubia; na (ii) Kufanya mchakato wa vyuo vitano vya Tanzania ili viingie ubia na vyuo vitano vya Canada katika Sekta za Utalii, Gesi Asilia, Mafuta na Madini na kuanza kutoa mafunzo Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yake kulingana na vipaumbele vya mwaka 2015/2016, Wizara inatarajia kutumia jumla ya Sh. 989,552,542,000/=. Kati ya fedha hizo sh. 510,877,383,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 478,675,159,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani na hitimisho; kwa namna ya pekee naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniadini na kunipa dhamana ya kuongoza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kipindi cha miaka mitano tangu mwaka 2010 hadi mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Watumishi wa Wizara, Wahadhiri, Wakufunzi, Walimu, Wanafunzi, Wazazi na Watanzania wote kwa ujumla kwa ushirikiano wenu mliionipa katika kipindi chote cha uongozi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani za pekee ziende kwa wananchi wangu wa Jimbo la Bagamoyo kwa kuendelea kuniadini na kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Elimu, wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Asasi za Kiraia, viongozi mbalimbali na wananchi ambao wamechangia katika kufanikisha utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia kufanikisha Mipango ya Elimu na Mafunzo ni pamoja na Serikali zifuatazo:-

Algeria, Australia, Canada, China, Cuba, Denmark, India, Japan, Marekani, Misri, Msumbiji, Norway, Pakistan, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi na Uturuki. Aidha, mashirika yaliyochangia katika kufanikisha programu za Elimu na Mafunzo ni pamoja na *Aga Khan Education Services, Airtel, Barclays Bank, Benki Kuu, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Taifa ya Biashara, Book Aid International, British Council, CAMFED, Care International, Children International, Children's Book Project, DFATD, COL, Commonwealth Secretariat, CRDB, DAAD, DANIDA, DfID, EDC, FEMINA, Ford Foundation, GIZ, ILO, International Reading Association, Irish Aid, JICA, JOVC, KOICA, Mwananchi Communications, NMB, NORAD, NUFFIC, OPEC, Oxfam, Peace Corps, Plan International, Rockefeller, Shirika la Volkswagen, SIDA, Sight Savers International, TENMET, Tigo, Umoja wa Nchi za Ulaya, UNAIDS, UNDP, UNESCO, UNESCO Institute for Life Long Learning, UNFPA, UNICEF, USAID, VODAC, VSO. KUHN International GmbH, CIGan* na Taasisi mbalimbali duniani zinazoshirikiana nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2015/2016; kwa taarifa hii, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ya jumla ya Sh. 989,552,542,000/= kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) Sh. 109,022,940,370/= zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara na Vitengo ambapo Sh. 70,993,671,000/= ni kwa ajili ya Mishahara na Sh. 38,029,269,370/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

(b) Sh. 401,854,442,630/= zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo, Sh. 325,024,671,000/= ni kwa ajili ya Mishahara na Sh. 76,829,771,630/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh. 478,675,159,000/= zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, Sh. 446,578,000,000/= ni Fedha za Ndani ambapo Sh. 348,300,000,000/= ni kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu sawa na asilimia 78 ya Fedha za Ndani na Sh. 32,097,159,000.00 ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara yangu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani <http://www.moe.go.tz>

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Hoja imeungwa mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu! Hoja haijaungwa mkono!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimwite Mwenyekiti...

Waheshimiwa utulivu!

Naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. MARGARET S. SITTA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Tabora wote na wananchi wa Urambo, kwa jinsi ambavyo tumekuwa tukishirikiana nao kwa muda mrefu na naomba ushirikiano huo uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Kamati ya Huduma za Jamii, kutoa pole za dhati kwa ndugu, marafiki na wapiga kura katika Jimbo la Mbinga Mgharibi kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wao, ndugu yao, marehemu Kapteni Komba. Wakati huo huo nitoe pole kwa Wabunge wote waliofiwa na ndugu zao, marafiki zao, wapiga kura wao, akiwemo Mjumbe wa Kamati hii ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Zabein Mhita, ambaye alifiwa na mumewe Dkt. Mohamed Mhita; tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya kikanuni ambayo ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kuangalia utekelezaji wa malengo ya kibajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015, Kamati ilikutana na Wizara na pia kufanya ziara katika baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka huu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi zilizotembelewa na Kamati ni pamoja na, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Taasisi ya Elimu Tanzania na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi zote za Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma kuanzia tarehe 9 hdi 13 Machi, mwaka huu na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ambayo ilitengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Pwani Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba Kampasi ya Mloganzila ambao unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Korea Kusini. Vile vile mradi huu unahusisha

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

ujenzi wa Hospitali kubwa ya kufundishia ambayo pia itatoa huduma za tiba kwa Watanzania. Mkoani Morogoro, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya ukarabati na upanuzi katika Vyuo Vikuu vya Sokoine na Mzumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Dodoma, Kamati ilikagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hosteli katika *School of Health Sciences, Natural Sciences and Mathematics* katika Chuo Kikuu cha Dodoma, pamoja na ukarabati wa Chuo cha Ualimu cha Bustani, kilichopo Wilayani Kondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ziara hizo, Kamati imeandaa maoni ambayo ni sehemu ya taarifa hii kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa shughuli za Wizara pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 hadi 7 mwezi Mei mwaka huu, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilikutana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dkt. Shukuru J. Kawambwa, Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015; baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa maoni na mapendekezo iliyoyatoa kwa Wizara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, imebaini kwamba, Serikali imezingatia na kufanyia kazi baadhi ya ushauri ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Elimu na Mafunzo ambayo ilizinduliwa mwezi Februari, mwaka huu na kuanza kwa mchakato wa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers Service Commission*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna maeneo ambayo Kamati inaishauri Serikali iendelee kuyafanyia kazi yakiwemo haya yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (*Teachers Service Commission*) kwa kutunga sheria ili ianze kazi katika mwaka ujao wa fedha 2015/16. Kamati inaishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha chombo hiki.
- (ii) Kuimarisha shughuli za Ukaguzi kwa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa Wakala ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi zaidi.
- (iii) Kuhakikisha wanafunzi wanaosomea Ualimu wanapata mafunzo ipasavyo. Aidha, wawezeshwe kuhudhuria Mafunzo ya Vitendo (*Block Teaching Practice – BTP*) kwa muda usiopungua wiki nane kwa Vyuo vya Serikali na Binafsi. (*Makofi*)
- (iv) Pia, Utoaji posho maalumu kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu hasa yale ya pembezoni ikiwa ni sehemu ya *Retention Scheme*.
- (v) Pia, Kuendelea kuwezesha Wanafunzi wa Elimu ya Juu kupata mikopo kwa kuzingatia uwezo wa familia wanazotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 578.7 hii ikiwa ni asilimia 69 ya kiwango chote kilichoidhinishwa ambacho ni shilingi bilioni 799.9. Mgawanyo wa fedha iliyopokelewa uko kama ifuatavyo:-

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa na Idara pamoja na Vitengo vya Wizara ilikuwa ni shilingi bilioni 63.2 kati ya shilingi bilioni 106.6 hii ikiwa ni asilimia 59.4 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Taasisi, kiasi cha shilingi bilioni 195.7, kati ya bilioni 239.8 kilipokelewa. Hii ikiwa ni sawa na asilimia 81.7 ya kiwango hicho kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shilingi bilioni 319.9 zilipokelewa kati ya bilioni 453.7 zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hii ni sawa na asilimia 70.5 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa mwenendo wa utoaji wa fedha unaweza ukaonekana kuwa ni mzuri hasa kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, hiyo ni kwa sababu fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu sasa ziko katika fungu la maendeleo la Wizara hii. Aidha, bado upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ni tatizo kwani hadi mwezi Machi kuna taasisi zilikuwa hazijapokea hata senti moja kwa ajili ya maendeleo, licha ya bajeti kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mfano, ni Chuo Kikuu cha Mzumbe ambacho licha ya kuidhinishwa shilingi milioni 850 kilikuwa hakijapokea hata senti moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imeathiri sana utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa taasisi hizo. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali izingatie kupeleka fedha zinazotengwa kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto Zinazoikabili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Katika kutekeleza majukumu yake Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

- (a) Utendaji kazi usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kutokana na ufinyu wa bajeti.
- (b) Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kutotolewa kabisa, kutolewa kwa kiwango kidogo au kucheleweshwa.
- (c) Ukosefu wa mpango ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi unaolenga kutekeleza vipaumbele walivyojiweka.
- (d) Kuongeza makusanyo ya ndani ya Wizara kwa kubuni vyanzo vipya vya makusanyo.
- (e) Mfumo dhaifu wa kuhudumia Walimu unaohusisha vyombo zaidi ya kimoja na hivyo kusababisha urasimu katika upatikanaji wa haki za Walimu.
- (f) Ukosefu wa posho ya mazingira magumu kwa Walimu hasa walioko pembezoni.
- (g) Upungufu katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) inayolenga kudhibiti utoaji holela wa mafunzo ya elimu ya ufundi stadi nchini.
- (h) Mchango wa *Skill Development Levy* katika utekelezaji wa majukumu ya VETA kutotosha.
- (i) Utoaji huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kutotengewa fedha za kutosha.



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

- (j) Kukosekana kwa utaratibu mzuri wa Serikali kuwatumia wahitimu wanaokopeshwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- (k) Ongezeko kubwa la wanafunzi wa elimu ya juu wanaohitaji mikopo bila kuwa na mikakati ya kuongeza vyanzo vya mapato kwa Bodi ya Mikopo.
- (l) Taasisi za Elimu ya Juu kutopewa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na shughuli za maendeleo.
- (m) Elimu ya Watu Wazima kutowekewa mkakati maalum wa kukabiliana na tatizo la kutojua kusoma na kuandika.
- (n) Pia, Hatua ya kuiweka Elimu ya Juu pamoja na Elimu ya Msingi na Sekondari, chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kunaifanya ikose usimamizi unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Katika mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekusudia kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 286 ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 9.3 zitakusanywa na Wizara na bilioni 276.9 zitakusanywa na taasisi. Aidha, Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 989.6 ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Hili ni ongezeko la asilimia 23.7 ikilinganishwa na bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina juu ya mgawanyo wa fedha katika Bajeti ya Wizara hii na kubaini uhitaji wa fedha kwa baadhi ya vifungu vyenye mahitaji ya lazima, kikiwemo Kifungu 2002 cha Ukaguzi wa Elimu nchini (*School Quality Assurance*). Kamati ilishauri uhamisho wa fedha kutoka baadhi ya vifungu na kuzipeleka katika kifungu hiki ili kukiongeza uwezo wa kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 mwezi Mei, mwaka huu Kamati ilikutana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dodoma na kupewa mrejesho kuhusu ushauri wa Kamati wa kufanya marekebisho ya kibajeti katika vifungu vya Wizara. Jumla ya fedha zilizoongezwa katika kifungu hicho cha 2002 ni shilingi milioni 40.5 na kukifanya Kifungu hicho sasa kiwe na jumla ya shilingi bilioni 25.8 kama tengeo jipya. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia ushauri huo wa kufanya mabadiliko ya ndani ya vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kwa kuwa Wizara hii inatekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*) ili kufikia lengo la mpango huo Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Utendaji usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu. Ili kusimamia viwango vya ubora wa elimu nchini hasa kwa kuzingatia kasi ya ongezeko la taasisi za elimu nchini kuanzia ngazi ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, ukaguzi ni jambo muhimu sana. Pia Ukaguzi ni muhimu katika maandalizi ya Walimu vyuoni, wanavyoendelezwa, wanavyofanya kazi na hata wanavyohudumiwa ili kufikia lengo la kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya umuhimu huo, bado jambo la Ukaguzi limekuwa halipewi uzito unaostahili kwani bado linasimamiwa na Idara tu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi huku ikitengewa bajeti finyu. Kwa mfano; katika kipindi cha miaka miwili ya fedha iliyopita (2013/2014 na 2014/2015) wastani wa bajeti ya ukaguzi ilikuwa shilingi bilioni 18.5 kiasi ambacho ni kidogo sana ikilinganishwa na ukubwa wa jukumu la utekelezaji.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati itaendelea kusesitiza suala la Ukaguzi hadi Kamati itakaporidhika kwamba, limepewa hadhi stahili. Ni kutokana na msisitizo huo Kamati inashauri yafuatayo:-

- (i) Serikali iruhusu Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa Wakala unaojitegemea ili uweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi zaidi.
- (ii) Wakati mchakato wa kuifanya Idara hii kuwa Wakala, Serikali iwezeshe kwa raslimali fedha, watu na vifaa. Aidha, bajeti inayotengwa kwa ajili ya Ukaguzi wa Elimu itumike kwa kusudi hilo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*). Kamati inaendelea kupongeza hatua ya Serikali kuingiza Sekta ya Elimu katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*). Iwapo mpango huu utatekelezwa kikamilifu utasaidia kuweka na kuimarisha misingi thabiti katika Elimu ya Msingi kupitia Mradi wa *Literacy and Numeracy Education Support (LANES)* na Elimu ya Sekondari kupitia Mpango Maalum wa Elimu ya Sekondari (*MMES II*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu ambapo katika mwaka uliopita jumla ya shilingi bilioni 28.9 zilitengwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya *BRN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali ihakikishe kunakuwa na utaratibu wa kupima matokeo ya miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu wa *BRN* ili jamii iweze kutathmini mafanikio yanayopatikana na kutofautisha na miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara na taasisi zake, kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na taasisi zake inakusudia kukusanya shilingi bilioni 286 lakini imepanga kutumia jumla ya shilingi 989.6. Kwa kuzingatia utofauti uliopo baina ya makusanyo na matumizi, Kamati inaona upo umuhimu mkubwa wa Wizara kuongeza makusanyo na inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Wizara iimarishe ukusanyaji wa maduhuli kwa zile taasisi ambazo zimeonesha udhaifu mkubwa katika eneo la ukusanyaji. Miongoni mwa taasisi hizo ni Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, zimekusanya kwa asilimia 50 tu ya malengo. Kwa mfano; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, inapaswa kubuni namna bora ya kuwatambua wanufaika wa mikopo na kisha kuwafikia kwa lengo la kukusanya mapato.

(ii) Wizara iangalie namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato kwa taasisi zake kwani mfumo huo umeonesha mafanikio makubwa katika maeneo mengine.

(iii) Taasisi ambazo hazikufanya vizuri katika makusanyo ni vyema zikajifunza kutoka kwenye taasisi zilizofikia au kuvuka malengo.

(iv) Wizara ibuni vyanzo vipya vya makusanyo ili kuongeza mapato.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kujadili malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilibaini kwamba Wizara imejiwekea vipaumbele vya kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba Wizara izingatie vigezo vya SMART wakati kitekeleza vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara umekwama au unasukasua kutokana na ukosefu wa fedha zinazotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara ilikuwa imepokea asilimia shilingi bilioni 70.5 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ambazo zilikuwa ni shilingi bilioni 453.7. Sehemu kubwa ya fedha hizo ilikuwa ni kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambayo ni sawa na takribani asilimia 78 ya fedha zote za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa fedha za Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, katika fedha za Maendeleo ili kutoa picha halisi ya bajeti ya maendeleo na mwenendo wa utoaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya taarifa kuonesha kuwa hadi Machi 31, 2015 asilimia 70.5 ya fedha za maendeleo ilikuwa imetolewa, miradi mingi ya maendeleo iliyotengewa fedha ilikuwa haijapokea hata senti moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inahoji kama mwenendo wa fedha za miradi ya maendeleo ni huu, ni vipi Wizara hii ambayo ni miongoni mwa Wizara zilizo katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) itaweza kufikia malengo yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi ya maendeleo ambayo inahitaji hatua za haraka na makusudi ili kunusuru utekelezaji wake. Kwa mfano, ukarabati wa upanuzi wa Chuo Kikuu mradi huu haujapewa fedha yoyote. Kwa mfano mwaka 2014/2015, Bunge lako Tukufu lilipitisha jumla ya shilingi milioni 850 lakini hadi Machi mwaka huu hakuna fedha zilizotolewa. Kamati inashauri Serikali ihakikishe inatoa fedha ya mradi huu ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Chuo Kikuu cha Sokoine, kutokana na Fedha za Maendeleo kutopelekwa, Chuo kinadaiwa na Mkandarasi kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa mradi wa ujenzi wa mabweni uliokamilika mwaka 2009. Hali hii inasababisha Chuo kutishiwa kupelekwa Mahakamani. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha hizo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma; mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo umekuwa ukiathiri ukamilishaji wa miradi ya maendeleo katika chuo hiki. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha kwa chuo hiki ili kiweze kukamilisha ujenzi wa majengo ya hosteli kwa ajili ya shule ya *Health Sciences, Natural Sciences and Mathematic*.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo; kwa mujibu wa Mitaala ya taaluma ya Ualimu nchini, Wanafunzi wa Ualimu wanapaswa kuhudhuria mafunzo ya *BTP* kwa siku 56 yaani Wiki nane). Kamati inashauri Serikali kuipa umuhimu taaluma kwani kwa kuwa na Walimu ambao hawakuandaliwa vya kutosha kutakuwa na athari kwa watoto wetu na kuweza kuzalisha matabaka kielimu. (*Makofi*)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Mwanamapinduzi na Mtetea Haki wa Afrika, Mzee Nelson Mandela alisema na nanukuu: “*Education is the most powerful Weapon that we can use to change the World.*” Mwisho wa kunukuu. Tafsiri yake ni kwamba: “Elimu ndiyo silaha yenye nguvu zaidi ambayo tunaweza kuitumia kubadilisha dunia.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzito huo huo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Wataalam ambao tunawaandaa ili wawapatie watoto wetu silaha hii muhimu ya elimu, wanaandaliwa vya kutosha ili waweze kutimiza jukumu hilo kikamilifu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukosefu wa ufanisi katika Mfumo wa kuhudumia Walimu; miongoni mwa changamoto zinazowakabili Walimu ni kukosekana kwa ufanisi katika mfumo unaotumika kuwahudumia Walimu yaani (*Teachers Service Delivery System*). Mfumo huo umekosa ufanisi kutokana na Walimu kuhudumiwa na vyombo zaidi ya kimoja. Hali hiyo imesababisha usumbufu kwa Walimu ikiwa ni pamoja na kuchelewesha katika upandaji wa yeye, malipo mbalimbali ikiwemo mishahara na fursa za masomo. Kamati inashauri:-

(i) Serikali iangalie upya mfumo wa kuhudumia Walimu ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu. Kamati inashauri kwamba, chombo hiki kianze kazi kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016.

(ii) Serikali iangalie namna ambavyo eneo la huduma za Walimu linaweza kuwa sehemu ya Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa, yaani BRN.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu na mazingira yao magumu ya kazi; Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, Serikali itekeleze ahadi ambazo imekuwa ikizitoa mara kwa mara kuhusu kuboresha na kutoa posho ya mazingira magumu kwa Watumishi wa maeneo hayo wakiwemo Walimu, ili kuwapa motisha ya kutekeleza majukumu yao na kutochukia taaluma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inashauri Serikali ihakikishe Walimu walio katika mazingira hayo wanapewa fursa ya kujitendeleza na kupata mafunzo wakiwa kazini kwa lengo la kuendelea kuwajengea uwezo katika taaluma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri, Serikali iangalie namna ya kuiongezea VETA uwezo zaidi ikiwa ni pamoja na kuangalia upya asilimia inayotengwa katika *skills development levy* ili iweze kutimiza wajibu wake kikamilifu na kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutokana na ongezeko la taasisi za elimu ya ufundi nchini, Kamati inaishauri Serikali ikamilishe mchakato wa mabadiliko ya sheria ili kuboresha utendaji wa NACTE na kuipa mamlaka zaidi ya kusimamia kikamilifu ubora wa mafunzo ya elimu na ufundi stadi nchini. Aidha, Baraza liongezewe rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali, ihakikishe watoto wanaotoka familia duni wanapata mikopo licha ya utaratibu masomo ya vipaumbele. Aidha, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, iongezewe uwezo wake wa kifedha na kupanua wigo wa kutoa mikopo, vile vile itafute namna ya kuwatambua wanufaika wa Bodi ili warejeshe mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhuisha mafunzo ya kuwajengea uwezo Walimu katika mafunzo ya Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK). Hata hivyo, inaishauri Serikali kuhakikisha inaufanya mpango huo kuwa endelevu kwa kuangalia namna ya kutenga fedha za ndani ili kuugharamia badala ya kutegemea vyanzo vya nje tu.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum; kwa kuwa makundi ya watoto wenye mahitaji maalum nayo yanahitaji fursa sawa katika kupata elimu bora, Kamati inapendekeza kuwe na Idara kamili katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambayo itasimamia kikamilifu masuala ya watu wenye mahitaji maalum. Aidha, Idara hiyo itengewe fedha za kutosha ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Juu kutenganishwa na Elimu ya Msingi, hatua ya kuchanganya Elimu ya Juu pamoja na Elimu za Msingi na Sekondari, kumeiongezea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mzigo mkubwa katika usimamiaji wa Sekta ya Elimu nchini. Kamati inashauri Serikali usimamizi wa elimu ya juu uondolewe katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Watu Wazima; tatizo la kutojua kusoma na kuandika limeendelea kuongeza nchini na hakuna mkakati wowote unaolenga kulikabili. Kamati inashauri Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), kuandaa mkakati maalum ambao utasaidia kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhimisho ya Wiki ya Elimu; Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuendelea na utaratibu huu kwani unatoa fursa kwa wadau wa elimu kukutana, kutafakari, kutathmini na kubuni mikakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwako wewe mwenyewe binafsi kwa ushauri na maelekezo ambayo yameiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, nawashukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa; Naibu Waziri wa Elimu ya Mafunzo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge; Katibu Mkuu, Profesa Sifuni Mchome pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani kwa kushirikiana nami katika kuiongoza vyema Kamati. Pia nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge wa Huduma za Jamii, kwa namna walivyoonesha weledi, busara na umakini katika kujadili Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, huu ni mwaka wa uchaguzi, nitumie nafasi hii kuwatakiwa Wajumbe wote wa Kamati hii pamoja na Wabunge wengine kila la kheri katika Uchaguzi Mkuu ujao na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatumia kukutana tena katika Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuwa na nafasi ningewatambua Wajumbe wa Kamati hii, lakini nadhani kwa muda ulivyo haiwezekani, lakini nawashukuru sana wajumbe wa Kamati hii, wote mrudi tena tukutane humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa kuwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati, Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Happiness Ndalu, Msaidizi wa Kamati Jane Ndulesi na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Charles Mloka, chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashiillah kwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti, Mwalimu Margaret Simwanza Sitta.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa mwaka wa Fedha 2014/15, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya kikanuni ambayo ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na kuangalia utekelezaji wa malengo ya kibajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/15, Kamati ilikutana na Wizara na pia kufanya ziara katika baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka huu wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi zilizotembelewa na Kamati ni pamoja na, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) zote za Jijini Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, pia Kamati ilifanya ziara katika Mkoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma kuanzia tarehe 09 – 13 Machi, 2015 na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ambayo ilitengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2014/15.

Katika Mkoa wa Pwani Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba (MUHAS) Kampasi ya Mloganzila ambao unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Korea Kusini. Vilevile mradi huu unahusisha ujenzi wa Hospitali kubwa ya kufundishia ambayo pia itatoa huduma za tiba kwa Watanzania.

Mkoani Morogoro, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya ukarabati na upanuzi katika Vyuo Vikuu vya Sokoine (SUA) na Mzumbe (MU).

Katika Mkoa wa Dodoma, Kamati ilikagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hosteli katika **School of Earth Sciences, Natural Sciences and Mathematics** katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), pamoja na ukarabati wa Chuo cha Ualimu cha Bustani, kilichopo Wilayani Kondo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara hizo, Kamati imeandaa maoni ambayo ni sehemu ya taarifa hii kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa shughuli za Wizara pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 05 hadi 07 Mei, 2015, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilikutana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dkt. Shukuru J. Kawambwa (Mb) Dar

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

es Salaam kwa lengo la kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika**, uwasilishaji wa Waziri ulijikita katika maeno yafuatayo;

- Utekelezaji wa Maoni ya Kamati kwa Wizara ambayo yaliyotolewa katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2014/15;
- Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2014/15, na
- Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwakawa Fedha 2015/16

### 2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa maoni na mapendekezo iliyoyatoa kwa Wizara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 imebaini kwamba, Serikali imezingatia na kufanyia kazi baadhi ya ushauri ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Elimu na Mafunzo ambayo ilizinduliwa mwezi Februari, mwaka huu na kuanza kwa mchakato wa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers Service Commission*).

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna maeneo ambayo Kamati inaishauri Serikali iendelee kuyafanyia kazi yakiwemo haya yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (*Teachers Service Commission*) kwa kutunga sheria ili ianze kazi katika mwaka ujao wa fedha 2015/16. Kamati inaishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha chombo hiki.
- (ii) Kuimarisha shughuli za Ukaguzi kwa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa Wakala ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi zaidi.
- (iii) Kuhakikisha Wanafunzi wanaosomea Ualimu wanapata mafunzo ipasavyo. Aidha, wawezeshwe kuhudhuria Mafunzo ya Vitendo (*Block Teaching Practice - BTP*) kwa muda usiopungua wiki 8 kwa Vyuo vya Serikali na Binafsi;
- (iv) Utoaji posho maalumu kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu hasa yale ya pembezoni (*Retention Scheme*)
- (v) Kuendelea kuwezesha Wanafunzi wa Elimu ya Juu kupata mikopo kwa kuzingatia uwezo wa familia wanazotoka.

### 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi **213, 447, 418,474/=**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 kiasi cha shilingi **147,151,613,150/=** kilikuwa kimekusanywa, ikiwa ni sawa na asilimia **69** ya makisio. Makusanyo haya ni pungufu ikilinganishwa na yale yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kamati ina matumaini kwamba, Wizara itaendelea na juhudi za kukamilisha ukusanyaji wa makusanyo ya maduhuli yaliyosalia katika kipindi kilichobakia kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha. Aidha, Wizara ibuni mbinu mpya za kuondokana na ukusanyaji duni wa maduhuli.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni **799,020,389,000/=** kwa ajili ya Wizara ambapokati ya fedha hizo shilingi **344,207,056,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **454,813,333,000** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kutokana na marekebisha ya bajeti (cut off budget) yaliyofanywa kwa Wizara zote, bajeti ya Wizara ilipungua kwa asilimia 0.45 na kufikia shilingi **795,397,353,000/=**

Hata hivyo, katika robo ya pili bajeti ya Wizara iliongezeka hadi shilingi **799,887,353,000/=** kutokana na nyongeza ya shilingi **4,490,000,000/=** iliyotolewa kwa ajili ya kulipia deni la Baraza la Vyuu Vikuu vya Afrika Mashariki (*Inter University Council of East Africa -IUCEA*). Kutokana na mabadiliko hayo, shilingi **346,274, 020, 000/=** zilielekezwa kwenye matumizi ya kawaida na shilingi **453,613,333,000/=** katika matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni **578,672,226,078.68** hii ikiwa ni asilimia **69** ya kiwango chote kilichoidhinishwa ambacho ni shilingi **799,887,353,000/=**. Mgawanyo wa fedha iliyopokelewa uko kama ifuatavyo:

Fedha ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa na Idara pamoja na Vitengo vya Wizara ilikuwa ni shilingi **63, 248, 696, 725/=** kati ya shilingi **106,563,814,000/=** hii ikiwa ni asilimia 59.4 ya fedha zilizoidhinishwa.

Kwa upande wa Taasisi, kiasi cha shilingi **195,607,394,122/=** kati ya shilingi **239,710,206,000/=** kilipokelewa, hii ikiwa ni sawa na asilimia **81.7** ya kiwango hicho kilichoidhinishwa.

Aidha, shilingi **319,816,135,231.66** zilipokelewa kati ya shilingi **453,613,333,000/=** zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hii ni sawa na asilimia 70.5 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ingawa mwenendo wa utoaji wa fedha unaweza ukaonekana kuwa ni mzuri hasa kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, hiyo ni kwa sababu fedha za mikopo ya Wanafunzi wa elimu ya juu sasa ziko katika fungu la maendeleo la Wizara hii.

Aidha, bado upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ni tatizo kwani hadi mwezi Machi kuna taasisi zilikuwa hazijapokea hata senti moja kwa ajili ya maendeleo, licha ya bajeti kuidhinishwa na Bunge lako tukufu. Mfano ni Chuo Kikuu cha Mzumbe ambacho licha ya kuidhinishwa shilingi milioni 850 kilikuwa hakijapokea hata senti moja.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeathiri sana utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa taasisi hizo. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali izingatie kupeleka fedha zinazotengwa kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kikamilifu.

### **3. CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YAUFUNDI**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

- (i) Utendaji kazi usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kutokana na ufinyu wa bajeti;



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (ii) Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kutotolewa kabisa, kutolewa kwa kiwango kidogo, au kucheleweshwa;
- (iii) Ukosefu wa mpango ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi unaolenga kutekeleza vipaumbele walivyojiwekea;
- (iv) Kuongeza makusanyo ya ndani ya Wizara kwa kubuni vyanzo vipya vya makusanyo.
- (v) Mfumo dhaifu wa kuhudumia Walimu unaohusisha vyombo zaidi ya kimoja na hivyo kusababisha urasimu katika upatikanaji wa haki za walimu;
- (vi) Ukosefu wa posho ya mazingira magumu kwa Walimu;
- (vii) Upungufu katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) inayolenga kudhibiti utoaji holela wa mafunzo ya elimu ya ufundi stadi nchini;
- (viii) Mchango wa *Skill Development Levy* katika utekelezaji wa majukumu ya VETA kutotosha;
- (ix) Utoaji huduma kwa Wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutotengewa fedha za kutosha;
- (x) Kukosekana kwa utaratibu mzuri wa Serikali kuwatumia wahitimu wanaokopeshwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;na
- (xi) Ongezeko kubwa la Wanafunzi wa elimu ya juu wanaohitaji mikopo bila kuwa na mikakati ya kuongeza vyanzo vya mapato kwa Bodi ya Mikopo.
- (xii) Taasisi za Elimu ya Juu kutopewa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na shughuli za maendeleo.
- (xiii) Elimu ya Watu Wazima kutowekewa mkakati maalum wa kukabiliana na tatizo la kutojua kusoma na kuandika.
- (xiv) Hatua ya kuiweka Elimu ya Juu pamoja na Elimu ya Msingi na Sekondari, chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kunaifanya ikose usimamizi unaostahili.

### 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

**Mheshimiwa Spika**,katika mwaka wa Fedha 2015/16 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekusudia kukusanya maduhuli ya shilingi **286,074,568,684.47** ambapo kati ya hizo shilingi **9,286,463,100/=** zitakusanywa na idara na shilingi **276,806,105,584.47** zitakusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Aidha, Wizara imeomba kuidhinishwa jumla ya shilingi **989,552,542,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Fedha hizi ni ongezeko la asilimia **23.7** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15 ambayo ilikuwa ni shilingi **799,887,353,000/=**.

**Mheshimiwa Spika**, katika fedha hiyo inayoombwa shilingi **510,877,383,000/=** zitatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*recurrent expenditure*) na sh. **478,675,159,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (*development expenditure*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina juu ya mgawanyo wa fedha katika Bajeti ya Wizara hii na kubaini uhitaji wa fedha kwa baadhi ya vifungu vyenye mahitaji ya lazima, kikiwemo Kifungu 2002 cha Ukaguzi wa Elimu nchini (*School Quality Assurance*). Kamati ilishauri uhamishowa fedha kutoka katika baadhi ya vifungu na kuzipeleka katika kifungu hiki ili kukiongezea uwezo wa kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 14 Mei, 2014 Kamati ilikutana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dodoma na kupewa mrejesho kuhusu ushauri wa Kamati na kufanya marekebisho ya kibajeti katika vifungu vya Wizara. Jumla ya fedha zilizoongezwa katika kifungu hicho ni sh. **40,500,000/=**

**Mheshimiwa Spika**, katika tengeo la awali kifungu hicho cha 2002 "*School Quality Assurance*" kilikuwa shilingi **25,782,807,000/=** Fedha iliyoongezewa ni sh. **40,500,000/=** na sasa tengeo jipya ni shilingi **25,823,307,000/=**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia ushauri huo na kufanya mabadiliko ya ndani ya vifungu vya Wizara kwa lengo la kuiwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

#### **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii inatekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ili kufikia lengo la mpango huo kamati inatoa ushauri ufuatao:-

#### **5.1 Utendaji usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu**

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia viwango vya ubora wa elimu nchini hasa kwa kuzingatia kasi ya ongezeko la taasisi za elimu nchini kuanzia ngazi ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, ukaguzi ni jambo muhimu sana. Pia Ukaguzi ni muhimu katika maandalizi ya Walimu vyuoni, wanavyoendelezwa, wanavyofanya kazi na hata wanavyohudumiwa ili kufikia lengo la ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, licha ya umuhimu huo, bado jambo la Ukaguzi limekuwa halipewi uzito unaostahili kwani bado linasimamiwa na Idara tu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi huku ikitengewa bajeti finyu.

Kwa mfano; katika kipindi cha miaka miwili ya fedha iliyopita (2013/14, na 2014/15) wastani wa bajeti ya ukaguzi ilikuwa shilingi bilioni **18.5** kiasi ambachoni ni kidogo sana ikilinganishwa na ukubwa wa jukumu la utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati itaendelea kusisitizasuala la Ukaguzi hadi itakaporidhika kwamba, limepewa hadhi stahili. Ni kutokana na msisitizo huo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iruhusu Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa Wakala unaojitegemea ili uweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi zaidi;

(ii) Wakati mchakato wa kuifanya Idara hii kuwa Wakala, Serikali iwezeshe kwa raslimali fedha, watu na vifaa. Aidha, bajeti inayotengwa kwa ajili ya Ukaguzi wa Elimu itumike kwa kusudi hilo tu.

## **5.2 Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Sekta ya Elimu.**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kupongeza hatua ya Serikali kuingiza Sekta ya Elimu katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Iwapo mpango huu utatekelezwa kikamilifu utasaidia kuweka na kuimarisha misingi thabiti katika Elimu ya Msingikupitia Mradi wa *Literacy and Numeracy Education Support* (LANES) na Elimu ya Sekondari kupitia Mpango Maalum wa Elimu ya Sekondari (MMES II).

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu ambapo katika mwaka uliopita jumla ya shilingi **bilioni 28.9** zilitengwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya BRN.

Kamati inashauri Serikali ihakikishe kunakuwa na utaratibu wa kupima matokeo ya miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu wa BRN ili jamii iweze kutathmini mafanikio yanayopatikana na kutofautisha na miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa kawaida.

## **5.3 Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara na taasisi zake**

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na taasisi zake inakusudia kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi **286,074,568,684.47** lakini imepanga kutumia jumla ya shilingi **989,552,542,000**. Kwa kuzingatia utofauti uliopo baina ya makusanyo na matumizi, Kamati inaona upo umuhimu mkubwa wa Wizara kuongeza kiwango cha makusanyo yanayotokana na vyanzo vya ndani.

Aidha, ili kuongeza wigo wa mapato kutokana na vyanzo vya ndani, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Wizara iimarishe ukusanyaji wa maduhuli kwa zile taasisi ambazo zimeonesha udhaifu mkubwa katika eneo la ukusanyaji. Miongoni mwa taasisi hizo ni Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, zimekusanya kwa asilimia 50 tu ya malengo. Kwa mfano; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, inapaswa kubuni namna bora ya kuwatambua Wanufaika wa mikopo na kisha kuwafikia kwa lengo la kukusanya mapato.

(ii) Wizara iangalie namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji na uhibiti wa mapato kwa taasisi zake kwani mfumo huo umeonesha mafanikio makubwa katika maeneo mengine.

(iii) Taasisi ambazo hazikufanya vizuri katika makusanyo ni vyema zikajifunza kutoka kwenye taasisi zilizofikia au kuvuka malengo.

(iv) Wizara ibuni vyanzo vipya vya makusanyo ili kuongeza mapato.

## **5.4 Mkakati wa Wizara kutekeleza Vipaumbele**

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kujadili malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilibaini kwamba Wizara imejiwekea vipaumbele vya kutekeleza majukumu yake. Vipaumbele hivyo ni:-

- i. Kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi stahiki katika ngazi zote za elimu;

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

ii. Kuimarisha taasisi za usimamizi wa ubora wa elimu pamoja na ufuatiliaji na tathmini; na

iii. Kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa usawa katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kamati kwamba Wizara izingatie vigezo vya SMART wakati ikitekeleza vipaumbele hivyo ili kuhakikisha inafikia malengo yaliyokusudiwa kwa ufanisi zaidi.

### **5.5 Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo**

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara umekwama au unasuasua kutokana na ukosefu wa fedha zinazotengwa.

Mheshimiwa Spika, ingawa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara ilikuwa imepokea asilimia **70.5** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ambazo zilikuwa ni shilingi **453,613,333,000/=** sehemu kubwa ya fedha hizo ilikuwa ni kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambayo ni sawa na takribani asilimia **78** ya fedha zote za maendeleo.

Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa fedha za Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, katika fedha za Maendeleo ili kutoa picha halisi ya bajeti ya maendeleo na mwenendo wa utokaji wa fedha hizo kwa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati ni kwamba, licha ya taarifa kuonesha kuwa hadi Machi 31, 2015 asilimia **70.5** ya fedha za maendeleo ilikuwa imetolewa, miradi mingi ya maendeleo iliyotengewa fedha ilikuwa haijapokea hata senti moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inahoji kama mwenendo wa fedha za miradi ya maendeleo ni huu ni vipi Wizara hii ambayo ni miongoni mwa Wizara zilizo katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) itaweza kufikia malengo yake?

### **5.6 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2014/15**

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Fungu 46, Kamati imebaini changamoto kadhaa na kushauri yafuatayo:-

#### **(i) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe**

Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa chuo hiki kimekuwa kikiomba bajeti ya maendeleo ili kiweze kukarabati mabweni, kumbi za mihadhara, madarasa, nyumba za wafanyakazi na miundombinu ya maji, kutokana na uchakavu wake. Hata hivyo, kwa miaka miwili mfululizo (2013/14 na (2014/15) chuo hiki hakijapata fedha yoyote ya maendeleo. Kwa mfano; katika mwaka wa fedha 2014/15 Bunge lako Tukufu lilipitisha jumla ya shilingi milioni **850** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini hadi Machi, mwaka huu hakuna fedha yoyote iliyotolewa.

Hali hii inakatisha tamaa taasisi husika, na pia inaliingiza taifa katika gharama zaidi kwani miradi ya maendeleo inashindwa kukamilika kwa wakati na hivyo kusababisha ongezeko za gharama ikilinganishwa na zile za awali.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za miradi kwa wakati na kiwango cha kutosha, la sivyo ni bora isiruhusu kuanza kwa miradi kama haina uhakika wa fedha. Pia, Serikali isianzishe miradi mipya kabla ya kukamilisha ya zamani.

**(ii) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine**

Mheshimiwa Spika, kutokana na fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo kutopelekwa kama ilivyotarajiwa, Wakandarasi wa baadhi ya miradi wametishia kuupeleka uongozi wa chuo Mahakamani wakishinikiza kulipwa fedha zao. Mfano ni Mkandarasi aliyetekeleza mradi wa ujenzi wa Mabweni ya Wanafunzi ambao ulikamilika toka mwaka 2009 na anakidai chuo shilingi bilioni 1.2

Hiini fedheha kwani viongozi wa chuo sasa wanalazimika kufanya kazi zao kwa wasiwasi wakihofia mkondo wa sheria kuwaangukia na hivyo, Kamati inashauri Serikali kutoa fedha hizo ili kuondoa kadhia hii.

**(iii) Mradi wa Ujenzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma**

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma ndiyo chuo kikuu chenye umri mdogo ikilinganishwa na vyuo vingine nchini na ambacho kinatarajiwa kuwa kikubwa kuliko vyote baada ya kukamilika kwake, hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo umekuwa ni changamoto inayoathiri ukamilishaji wa miradi ya maendeleo.

Kamati inashauri Serikali kutoa fedha kwa chuo hiki ili kiweze kukamilisha ujenzi wa majengo ya hosteli kwa ajili ya shule ya *Earth Sciences, Natural Sciences and Mathematics* ili kuwawezesha Wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

**5.7 Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo (BTP)**

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na Walimu waliobobea katika taaluma hiyo ni lazima Wanafunzi wa Ualimu wapate fursa ya kuhudhuria mafunzo ya vitendo (*Block Teaching Practice - BTP*). Huo ni utaratibu wa taaluma ya Ualimu duniani kote. Hata hivyo, taaluma hiyo inaanza kuingia mashakani kutokana na muda wa mafunzo hayo kupungua kwa kasi katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha iliyopita kutokana na ufinyu wa bajeti

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mitaala ya taaluma ya Ualimu nchini, Wanafunzi wa Ualimu wanapaswa kuhudhuria mafunzo hayo kwa siku 56 (Wiki 8), lakini muda huo umepungua hadi siku 21 (2014) na sasa umefikia siku 14 (2015). Sababu ya kupungua mwa muda huo ni ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilipokea shilingi bilioni 7.6 kati ya shilingi bilioni 9.7 zilizoidhinishwa hii ikiwa ni sawa na asilimia 78.9 ya fedha zilitakiwa kutolewa. Katika mwaka fedha uliofuata 2014/15 licha ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya BTP kupungua hadi shilingi bilioni 7.8 bado kiasi kilichotolewa kilishuka sana kwani Wizara ilipokea shilingi bilioni 2.8 tu hii ikiwa ni sawa na asilimia 35.5 ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapata wasiwasi wa kuibuka kwa matabaka ya Walimu katika jamii yetu kwani Walimu kutohudhuria mafunzo ya BTP kwa siku 56 (Wiki 8) kutaathiri ubora wao wa kitaaluma.

Kamati inaishauri Serikali kuipa umuhimu taaluma hii kwani, kuwa na Walimu ambao hawakuandaliwa vya kutosha kutakuwa na athari kwa Watoto wetu na kunaweza kuzalisha matabaka ya kielimu.

Mheshimiwa Spika, Mwanamapinduzi na Mtetea Haki wa Afrika, Mzee Nelson Mandela aliithamini sana elimu kiasi cha kusema maneno haya na ninanukuu **“Education is the most powerful Weapon that we can use to change the World.”** Tafsiri ya Kiswahili maneno haya ni kwamba, **“Elimu ndiyo silaha yenye nguvu zaidi ambayo tunaweza kuitumia kubadilisha Dunia.”**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uzito huo huo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Wataalam ambao tunawaandaa ili wawapatie Watoto wetu silaha hii muhimu ya elimu, wanaandaliwa vya kutosha ili waweze kutimiza jukumu hilo kikamilifu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

#### **5.8 Ukosefu wa ufanisi katika Mfumo wa kuhudumia Walimu (Teachers Service Delivery System).**

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changanoto zinazowakabili Walimu ni kukosekana kwa ufanisi katika mfumo unaotumika kuwahudumia (Teachers Service Delivery System). Mfumo huo umekosa ufanisi kutokana na Walimu kuhudumiwa na vyombo zaidi ya kimoja. Hali hiyo imesababisha usumbufu kwa Walimu ikiwa ni pamoja na kuchelewesha katika, upandaji wa vyeo, malipo mbalimbali ikiwemo mishahara na fursa za masomo. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iangalie upya mfumo wa kuhudumia Walimu ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu ambayo pia itasaidia kutatua kero nyingine zinazowakabili Walimu nchini. Kamati inashauri kwamba, ni vyema chombo hiki kikanza kazi katika mwaka huu wa fedha 2015/16.

(ii) Serikali iangalie namna ambavyo eneo la huduma za Walimu linaweza kuwa sehemu ya Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa, katika Wizara ya Elimu ili kupunguza usumbufu uliopo na kuwapa Walimu ari zaidi ya kazi.

#### **5.9 Walimu na mazingira magumu ya kazi**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, upungufu wa Walimu katika maeneo ya vijijini nayale ya pembezoni mwa nchi unachangiwa kwa kiasi kikubwa na mazingira magumu ya kazi wanayokumbana nayo.

Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, Serikali itekeleze ahadi ambazo imekuwa ikizitoa mara kwa mara kuhusu kuboresha na kutoa posho ya mazingira magumu kwa Watumishi wa maeneo hayo wakiwemo Walimu, ili kuwapamotisha ya kutekeleza majukumu yao na kutochukua taaluma zao.

Kamati pia inashauri Serikali ihakikishe Walimu walio katika mazingira hayo wanapewa fursa ya kujiendeleza na kupata mafunzo wakiwa kazini kwa lengo la kuendelea kuwajengea uwezo katika taaluma yao.

#### **5.10 Utekelezaji wa Majukumu ya VETA**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuunga mkono uamuzi wa Serikali kuhakikisha inajenga Chuo cha Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) katika kila Wilaya. Hatua hii ni muhimu hasa katika kipindi hiki ambacho Wahitimu wa shule za Msingi na Sekondari wameongezeka. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba ada ya ujuzi “Skills Development Levy ya asilimia 2 ambayo inapelekwa kuhudumia utoaji wa mafunzo hayo haitoshi kuiwezesha VETA kutimiza majukumu yake kikamilifu.

Kamati inashauri, Serikali iangalie namna ya kuiongezea VETA uwezo zaidi ili iweze kutimiza wajibu wake kikamilifu ambao ni pamoja na kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, ili navyo viweze kutoa mafunzo hayo.

#### **5.11 Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la taasisi zinazotoa elimu, changamoto zinaongezeka hasa katika eneo la udhibiti wa utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi stadi nchini.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ambalo lina dhamana ya kusimamia udhibiti wa utoaji wa mafunzo hayo, linakabiliwa na changamoto inayosababishwa na mapungufu katika sheria yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kushauri Serikali ikamilishe mchakato wa mabadiliko ya sheria, ili kuboresha utendaji wa NACTE na kuipa mamlaka zaidi ya kusimamia kikamilifu ubora wa mafunzo ya elimu na ufundi stadi nchini.

Pia Kamati inashauri Baraza hilo kupata raslimali watu hasa katika maeneo ambayo ni muhimu kwani zipo baadhi ya idara muhimu zina mtumishi mmoja mmoja, jambo ambalo ni hatari sana kwani baadhi ya shughuli zinaweza kukwama pale wafanyakazi hao wanapopata dharura.

#### **5.12 Idadi ya Wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya Juu**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuunga mkono juhudi kubwa ya Serikali ya kuendelea kuongeza kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ili kutoa fursa zaidi kwa Watanzania kupata elimu ya juu nchini. Juhudi hizo ni pamoja na kuwezesha Wanafunzi wa Shule ya Sheria (*Law School of Tanzania*) na Walimu wanaosomea Stashahada ya Ualimu kwa masomo ya Sayansi na Hisabati, kupatiwa mikopo. Hata hivyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iangalie namna ya kubuni utaratibu utakaowawezesha wahitimu wa baadhi ya taaluma, kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni kwa miaka kadhaa kabla ya kuhamia mijini. Utaratibu huu unaweza kuhusisha Watumishi hao kupatiwa posho maalum na kusaini mikataba ya kufanya kazi katika maeneo hayo kwa kipindi maalum kabla ya kuhamia mijini.

(ii) Serikali ihakikishe Watoto wanaotoka familia duni wanapata mikopo licha ya utaratibu masomo ya vipaumbele.

(iii) Ili kuhakikisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSB) inaongeza uwezo wake wa kifedha na kupanua wigo wa kutoa mikopo, kuwe na mkakati wa makusudi ambao utawezesha wanufaika wa bodi hiyo kutambulikana na kuanza kurejesha mikopo yao.

#### **5.13. Mpango wa Mafunzo ya Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK)**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhuisha mafunzo ya kuwajengea uwezo Walimu katika mafunzo ya Kuandika, Kusoma na Kuhesabu – KKK. Hata hivyo, inaishauri Serikali kuhakikisha inaufanya mpango huo kuwa endelevu kwa kuangalia namna ya kutenga fedha za ndani ili kuugharamia badala ya kutegemea vyanzo vya nje tu.

#### **5.14 Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa makundi ya watoto wenye mahitaji maalum nayo yanahitaji fursa sawa katika kupata elimu bora, Kamati inapendekeza kuwe na Idara kamili katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambayo itasimamia kikamilifu masuala ya watu wenye mahitaji maalum. Aidha, idara hiyo itengewe fedha za kutosha ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

#### **5.15 Elimu ya Juu kutenganishwa na Elimu ya Msingi na Sekondari**

Mheshimiwa Spika, hatua ya kuchanganya Elimu ya Juu pamoja na Elimu za Msingi na Sekondari, kumeiongezea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mzigo mkubwa katika usimamijwa sekta ya elimu nchini. Kamati inashauri usimamizi wa elimu ya juu uondolewe katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

#### **5.16 Elimu ya Watu Wazima kukosa mkakati wa kupunguza tatizo la kutojua kusoma nakuandika**

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutojua kusoma na kuandika limeendelea kuongeza nchini na hakuna mkakati wowote unaolenga kulikabili. Kamati inashauri Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), kuandaa mkakati maalum ambao utasaidia kukabiliana na hali hii.

#### **5.17 Maazimisho ya Wiki ya Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilipata fursa ya kuhudhuria Maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini yaliyofanyika kwa mara nyingine tena Mkoani Dodoma. Kamati imeipongeza sana Serikali kwa kuendelea na utaratibu huu kwani maadhimisho haya yatatoa fursa kwa wadau wa elimu kukutana, kutafakari, kutathmini na kubuni mikakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha elimu nchini. Ni maoni ya Kamati kwamba, jambo hili liendeleo kuboreshwa ili liwe chachu ya kuinua kiwango cha elimu nchini.

### **6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, ninatoa shukrani za dhati kwako binafsi kwa ushauri na maelekezo ambayo yameiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, ninawashukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb), Naibu Waziri wa Elimu ya Mafunzo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb), Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani (Mb) kwa kushirikiana nami katika kuiongoza vyema Kamati. Pia ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge wa Huduma za Jamii, kwa namna walivyoonesha weledi, busara na umakini katika kujadili Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Kwa kuwa, huu ni mwaka wa uchaguzi, nitumie fursa hii kuwatakiwa Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Wabunge wengine kila lakheri katika Uchaguzi Mkuu ujao na Inshallah Mwenyezi Mungu atajalia tutakutana tena katika Bunge lijalo.

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-



1. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb – Mwenyekiti,
2. Mhe. Stephen Hillary Ngonyani, Mb –M/ Mwenyekiti,
3. Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Agripina Zaituni Buyogera, Mb - “
5. Mhe. Faki Haji Makame, Mb - “
6. Mhe. Christowaja Gerson Mtinda, Mb - “
7. Mhe. Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mb -”
8. Mhe. Riziki Omar Juma, Mb - “
9. Mhe. Dkt. Antony Gervas Mbassa, Mb - “
10. Mhe. Ezekia Dibogo Wenje, Mb - “
11. Mhe. Ali Juma Haji, Mb - “
12. Mhe. Juma Sururu Juma, Mb - “
13. Mhe. Gregory George Teu, Mb - “
14. Mhe. Abia Muhama Nyabakari, Mb - “
15. Mhe. Salome Daudi Mwambu, Mb - “
16. Mhe. Zabein Muhaji Mhita, Mb - “
17. Mhe. Mohamed Gulam Dewji, Mb - “
18. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - “
19. Mhe. Hasnain Mohamed Murji, Mb - “
20. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - “
21. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb- “

**Mheshimiwa Spika**, nihitimisha kwa kuwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati, Ndugu Chacha T. Nyakega, Ndugu Happiness Ndalu, Msaidizi wa Kamati Jane Ndulesi na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Charleschini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah, kwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
HUDUMA ZA JAMII  
01 Juni, 2014**

**MWENYEKITI:** Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na Wizara hii, Mheshimiwa Susan Lyimo!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama hapa kusoma hotuba hii. Kipekee namshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kuendelea kuniamini katika kusimamia Wizara hii nyeti kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza kwa dhati wenyeviti wenza wa UKAWA; Mheshimiwa Dkt. Emanuel Makaidi wa NLD, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba wa CUF na Mheshimiwa James Mbatia wa NCCR-Mageuzi kwa kazi kubwa sana na nzuri wanayofanya ya kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na UKAWA kwa kuwa ndio tumaini pekee

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

lilobaki la kuwakomboa na ndio njia pekee ya kuiondoa Serikali ya CCM madarakani ifikapo 25/10/2015. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba wananchi wote wanaokerwa na kuporomoka kwa shilingi yetu, ufisadi, rushwa na hali mbaya ya maisha yetu, watumie fursa hii ya maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kujitokeza kwa wingi na kuwahi kujiandikisha mapema daftari litakapopita katika maeneo yao kwani ndiyo njia pekee ya kuiondoa CCM madarakani *democratically*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanawake wa Mkoa wa Kinondoni kichama kwa ushirikiano wao, kipekee nawashukuru viongozi wa CHADEMA na wanachama wa Jimbo hilo kwa ushirikiano mnaonipatia katika kutimiza nia na ndoto zangu. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maisha ya Bunge hili la Kumi yatafikia ukomo wake hivi karibuni, hii itakuwa ni hotuba yangu ya mwisho kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii ya Elimu. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakumbukwa kwa kwa jitihada zake za kuikosoa na kuishauri Serikali juu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa lengo la kuboresha elimu hapa nchini.

Ni imani yangu kwamba niliitumikia nafasi hii ya Waziri Kivuli wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa uaminifu na weledi mkubwa na ni furaha yangu vile vile kwamba wananchi na wadau wote wa elimu waliridhika na mchango wa kazi hii ya upinzani, ndiyo maana tunashuhudia wengi wakija katika Bunge hili ili kusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM ilivyoshindwa Kutekeleza Ilani yake Kuhusu Elimu; Serikali hii ya Awamu ya Nne ya CCM imeshindwa kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi kuhusu Elimu kwa mihula yote miwili ya utawala wake. Ibara ya 85 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 inasema kwamba:

"Serikali itachukua hatua za kuboresha, kuimarisha elimu ya awali hadi ya Chuo Kikuu na kuhakikisha kwamba elimu ya ngazi zote itakayotolewa nchini tangu sasa iwe na ubora utakaowawezesha vijana wetu kuchukua nafasi zao stahiki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla". Hiki ni kituko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Awali; Chama cha Mapinduzi kiliwaahidi watanzania kupitia Ilani yake ya uchaguzi kufanya yafuatayo katika Elimu ya Awali

- (a) Kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi ina darasa la Elimu ya Awali lenye madawati yanayolingana na hali ya watoto wa elimu hiyo.
- (b) Kujenga vyoo kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali ili wasiingiliane na wale wa shule ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwaambia wananchi wote kwamba, walitapeliwa na CCM kwani Serikali ya CCM haikutekeleza ahadi hiyo hata japo kwa asilimia 50. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge wananchi kama imetekeleza ujenzi wa madarasa ya elimu ya awali katika kila shule ya msingi nchini na

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

kuweka madawati yanayolingana na watoto hao, hasa tukizingatia kwamba muda wa ilani hiyo unakwisha mwezi wa Kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya elimu ya awali bado ni ya duni sana ambapo asilimia kubwa ya watoto bado wanakaa chini. Aidha, uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi bado umeendelea kukua ambapo mwaka 2010 ilikuwa Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 73; mwaka 2012, Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 124 na mwaka 2013, Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 199. Hii ni kwa mujibu wa kitabu cha *BEST* ambacho ni cha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu ya msingi, Chama cha Mapinduzi kimeendelea kuwachidi wananchi na kusema kwamba; kitaendelea kuyaboresha maslahi ya Walimu ili kuhakikisha mishahara itolewayo inazingatia hali halisi ya maisha na soko. La pili, kuendelea kuimarisha ukaguzi wa shule na kuhakikisha kuwa shule inakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na taarifa ya ukaguzi kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waliamini, wakaichagua CCM kwa kishindo, lakini baada ya kushika dola wamesahau haya yote waliyoahidi. Wote tunajua madhila yanayowapata Walimu wetu, kilio chao cha malimbikizo ya mishahara na stahili zao nyingine ni cha muda mrefu sana. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba baadhi ya Walimu walioajiriwa tarehe 1 Mei, 2015 hadi leo hawajalipwa fedha yao ya kujikimu (*settling in allowance*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema walimu ndio nyenzo kuu katika elimu lakini cha ajabu Walimu wa Tanzania wamekuwa wakionewa na kudhalilishwa kila leo. Mfano, Serikali imetoa muundo mpya wa madaraja ya mishahara ya Walimu Julai, 2014 unaojulikana kama *TGTS* ambapo zaidi ya Walimu laki moja (100,000) wanapaswa kutoka *E* kwenda *F*. Walimu hawa kwa makisio ya chini wanahitaji zaidi ya bilioni mia moja (100,000,000,000/=) kwa maana ya kwamba wastani ya nyongeza ya sh. 100,000/= kwa mwezi. Kwa mahesabu rahisi kama ni Walimu 100,000 x 100,000/= kwa miezi 12 kuanzia mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, bado inaonesha wazi kwamba, lile limbikizo la mishahara ya Walimu na marupurupu yao linaendelea kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu ni kwamba hivi karibuni Serikali imeendelea kutumia kero za Walimu kisiasa. Kwa mfano, Mheshimiwa Dkt. Kikwete akizungumza na Chama cha Walimu hivi karibuni alisema kabla hajaondoka madarakani atahakikisha Walimu wamelipwa madeni yao kana kwamba hakuyaona madeni hayo toka alipoingia madarakani mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi; ni wazi kuwa bila ukaguzi ubora wa elimu hauwezi kupatikana. Licha ya majigambo na ahadi hewa ya Serikali hii kupitia Ilani ya CCM, kwamba kila shule itakuwa inakaguliwa mara moja kwa mwaka, takwimu za Wizara zinaonesha kwamba, ukaguzi wa shule umefikia asilimia 37 tu. Hii ina maana kwamba zaidi ya asilimia 63 ya shule za msingi na sekondari hazikukaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya CCM ni ya ajabu sana kwa kuwa imechoka, inajichanganya na imefikia hatua haina kumbukumbu ya mambo iliyowahi kuahidi. Nasema hivi kwa sababu, tarehe 29 Aprili, 2013, Rais Dkt. Jakaya Kikwete aliwaahidi wananchi kupitia mazungumzo yake na Wakuu na Wamiliki wa Shule za Sekondari binafsi huko Mbeya kwamba, Serikali ingeanzisha Wakala wa Ukaguzi anayejitegemea na kwamba Serikali ingemwezesha Wakala huyo kwa rasilimali fedha /watu na vitendea kazi ili kimarisha utendaji kazi ya ukaguzi na matokeo yake yataonekana kwa muda mfupi.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo halijafanyika, lakini kibaya zaidi ni Ofisi ya Waziri Mkuu kuandika barua ya kumbukumbu No: CBC/10/348/05/10...

**MWENYEKITI:** Utulivu, Waheshimiwa naomba utulivu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ya tarehe 13 Oktoba, 2014 inayositisha agizo la Rais la kuanzisha Wakala wa Ukaguzi wa Shule. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutoa maelezo juu ya mkanganyiko huu ndani ya Serikali kuhusu uanzishwaji wa Wakala wa Ukaguzi wa Shule. Swali la kujuliza, hivi tuna Serikali ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumaliza sehemu hii kwa kuwaambia wananchi kwamba, elimu haijawahi kuwa kipaumbele katika sera za CCM kwa Awamu zote Nne za utawala wake, ndiyo maana haiitekelezi hata ilani yake yenyewe. Sera ambayo CCM imepigia upatu kwa miaka yote 53 ya Uhuru na ambayo pia imeshindwa kutekeleza ni Kilimo, ndiyo maana toka enzi za uongozi wa Hayati Baba wa Taifa kumekuwa na sera zinazosikika kwamba Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kuponu, Kilimo ni Uhai, Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa na sasa Kilimo Kwanza. Hatujawahi kusikia Elimu Kwanza, wala Elimu ni Uhai, katika utawala wa CCM kwa miaka yote 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu Kwanza, ni Sera ya Upinzani. Ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA ya 2005 na 2010 na imepewa kipaumbele cha kwanza, cha pili na cha tatu. Kwa kuwa sasa hivi tupo katika ushirikiano wa UKAWA, sera hii imekuwa ni sera ya UKAWA. Hivyo Kambi ya Upinzani inawaonya wanaotangaza nia ya kugombea Urais wa Tanzania kupitia CCM kuacha kuwawadanganya wananchi kwamba elimu itakuwa kipaumbele namba moja ikiwa watachaguliwa, kwa kuwa walikuwa Serikalini tena wakishika nyadhifa za juu kwa miaka yote tangu uhuru wakashindwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba CHADEMA iliposema elimu itakuwa bure kama ingechaguliwa kuunda Serikali mwaka 2005 na 2010, CCM iliendesha propaganda chafu na kuwapotosha wananchi kwamba haiwezekani kutoa elimu bure. Hata hivyo, ili kuthibitisha ile methali isemayo kwamba njia ya mwongo ni fupi na ukiwa muongo uwe na kumbukumbu, CCM sasa hivi imekubali kula matapishi yake yenyewe na kusema katika kipengele chake cha 3.1.5 cha Sera Mpya ya Elimu ya mwaka 2014 kwamba elimu ya msingi itakuwa bure kwa maana ya kutoka shule ya awali mpaka kidato cha nne. Huu ni uthibitisho kwamba, CCM imeboba katika wizi hadi kufikia hatua ya kuiba sera za upinzani waziwazi bila aibu. Hii inathibitisha kwamba Sera za Upinzani zinatekelezeka na kwa maana hiyo, UKAWA ukitwaa madaraka ya dola katika uchaguzi wa Oktoba, 2015, elimu ya msingi mpaka chuo kikuu itakuwa bure na bure kweli kweli, kwa kuwa rasilimali tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera Mpya ya Elimu...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kelele. Nitaanza kuwataja mmoja mmoja ninyi mnaopiga kelele.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaah!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WAZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ilizinduliwa kwa mbwembwe nyingi lakini ukiisoma sera ile ni vituko vitupu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilidhani kwamba, baada ya Sera ya Elimu ya 1995 kuwa na upungufu mwingi uliophelekea mambo mengi kuharibika basi ingekuwa somo tosha kwa maboresho ya sera hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunashindwa kutekeleza sera zetu kwa kuwa zimekuwa ni sera bainishi yaani *substantive policies* na hivyo kubainisha upungufu tu na kuacha sehemu ya pili ya utekelezaji. Hivyo kilichobainishwa kinashindikana kutekelezwa kwa kuwa nyenzo za utekelezaji haziwekewi mkazo. Kimsingi, ili sera itekelezake, ni lazima iwe na ngazi hizi mbili yaani sera bainishi na sera namna. Sera nyingi hapa nchini zimekuwa dhafu na kutokutekelezwa kwa kukosa ngazi ya pili yaani *procedural policies*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Sera ya Elimu iweze kutekelezeka, inahitaji kupatiwa ufumbuzi wa mambo matatu la sivyo hakutakuwa na jipya. Mambo hayo ni pamoja na walimu bora, zana bora za kufundishia na walimu wenye motisha.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetenga kiasi gani katika bajeti hii kwa ajili ya zana bora za kufundishia na motisha kwa walimu ili kurahisisha utekelezaji wa Sera Mpya? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu inasema Serikali itahakikisha kuwa elimu ya msingi katika mfumo wa umma inatolewa bila ada. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulithibitishia Bunge hili kama elimu bila ada itanza kutolewa katika mwaka wa fedha 2015/2016 au tamko tu la kisera na kisiasa kwa ajili ya kuendelea kuwahadaa Watanzania ili wapatiwe kura katika uchaguzi unaokuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule binafsi. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu gharama za shule za binafsi kuwa kubwa mno kiasi kwamba ni wananchi wachache wanaweza kuwalipia watoto wao ada hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imefanya jitihada gani katika kuwianisha gharama za elimu katika shule binafsi na za Serikali ili kuondoa matabaka ya utoaji wa elimu. Kwa kuwa wenye shule binafsi wanadai gharama zao ziko chini kama tutaangalia *student unit cost*, je, pamoja na malalamiko haya watu wenye shule binafsi, Serikali imefanya utafiti gani kujua kama ni kweli ili wananchi wajue gharama halisi za wanafunzi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha na la aibu kwa Serikali ya CCM kujigamba kuwa imeleta maendeleo kushindwa kuwapatia wanafunzi madawati licha ya utajiri wa rasilimali za misitu tulizo nazo na licha ya ujuzi na nguvu kazi iliyopo katika magereza yetu ambapo wafungwa na mahabusi wangeweza kutumika kutengeneza madawati hayo. Ni aibu kubwa kwa Serikali hii ya CCM kujigamba kwamba Sera Mpya ya Elimu na Waziri Mkuu kujibu swali hapa Bungeni na kukazia kwamba wanafunzi wa shule za msingi watapatiwa kompyuta mpakato (*laptops*) ilhali sehemu kubwa ya watoto wetu bado wanakaa chini na wengine wanakalia mawe kama nyani kwa miaka 54 sasa ya uhuru. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapata tabu sana kuelewa kama Serikali hii imechanganyikiwa au iko *serious* kwamba itawapa watoto kompyuta ambao hawana pa kukaa na wala shule hizo hazina umeme. Je, bajeti yao iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Kenya na Rwanda wameweza kuwapa watoto wao kompyuta mpakato kwa maana ya *laptops*. Sasa tunataka Waziri atakapojumuisha atuambie hiyo bajeti iko wapi? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, hivi Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi iliyokaaa zaidi ya mara 212 kwa maana ya mara nne kila mwaka ukiacha vile vikao vya dharura kwa miaka yote 53 na nusu ya uhuru, huwa wanajadili nini ikiwa

hali ya upatikanaji wa madawati ni tete huku magogo yetu yakiuzwa China na kwingineko? Kambi Rasmi ya Upinzani imeshawishika kuamini kwamba, Serikali hii ya CCM si kwamba tu imechoka...

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti wafanye adabu hawa!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WAZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Bali pia imefikia ukomo wa kufikiri na kwa maana hiyo kuiruhusu kuendelea kutawala ni kuruhusu anguko la nchi kama Waswahili wanavyosema ni janga la taifa na ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni mwalimu, kwani unaweza kuwa na madarasa mazuri sana, maabara ya viwango vya juu lakini bila mwalimu mwenye motisha na aliyepewa mafunzo vizuri hakuna chochote kitakachofanyika. Elimu ni sawa na kiwanda ambapo mwanafunzi ni malighafi, walimu na vitabu ndiyo mashine za uchakataji na usindikaji. Hivyo kama ilivyo kwa malighafi inapopita kwenye mashine tunachopata ni kitu kipya kama pamba kuwa nguo, ngano kuwa bia, zabibu kuwa wine na kadhalika. Hivyo mtoto anaingia hajui chochote lakini anategemewa atoke amebadilika kwa kujua kusoma, kuandika na kubwa zaidi kujitambua na kujua kuchambua mambo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, kama elimu ya ualimu inayotolewa ina ubora wa kutosha kwa kuwa mwalimu bora ndiye anayegemewa katika kuwafundisha watoto wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na mtaala wa mafunzo ya ualimu, mafunzo kwa vitendo kwa walimu yaani *block teaching* yanapaswa kutolewa kwa wiki nane na nashukuru Mwenyekiti wa Kamati amezungumzia suala hili. Cha ajabu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi wameendelea kuwapatia walimu mafunzo kwa muda wa wiki mbili tu. Bunge lako Tukufu kwa kutambua umuhimu wa ubora wa walimu ilipitisha bajeti ya shilingi bilioni 7.2 mwaka jana. Serikali kwa kutothamini fani hii ilipunguza kiasi hicho au imepelekea shilingi bilioni mbili tu mpaka tarehe 30 Aprili, kwa maaana ya asilimia 28 na ndiyo maana walimu wetu wameenda *block teaching* kwa muda wa wiki mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha na inatia hasira kusikia kwamba Serikali inasema mkakati iliyo nao ili kuhakikisha walimu hawa waliokosa mafunzo kwa vitendo, watakuwa chini ya uangalizi wa ukaguzi wa shule kwa kipindi cha mwaka mmoja pindi watakapojiriwa ili kupata muda wa kutosha kwa mazoezi ya ufundishaji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaihoji Serikali itatekeleza vipi mpango huo wa ukaguzi na kwa bajeti ipi ikiwa ukaguzi uliofanyika ni asilimia 30 tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu. Elimu ya juu ndiyo inayomfunza kijana jinsi ya kuchambua mambo na kujenga weledi katika fani mbalimbali. Mwalimu Nyerere, katika kitabu chake cha Uhuru na Maendeleo, alisema:-

*"Intellectuals have a special contribution to make to the development of our nation, and their knowledge and greater understanding that they should poses, should be used for the benefit of the society of which we are all members".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume na maneno ya Hayati Baba wa Taifa, mchango wa wasomi wetu katika maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla umewekewa vikwazo na mfumo wa utawala wa Serikali hii ya CCM. Wasomi wenye elimu ya juu kokosa ajira limekuwa ni jambo la kawaida na wasomi pia kukosa fursa katika mazingira bora ya kujijajiri nayo ni changamoto. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kueleza Bunge imewasaidiaje

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

wahitimu wa elimu ya juu kama vile wahandisi, wale wanaochukua fani za kilimo na wanasheria katika kuanzisha kampuni zao za uhandisi ili waweze kujiajiri? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, nchi hii inafuata falsafa gani ya elimu kwa sasa? Yaani *What is our current education philosophy?* Wote tunajua wakati wa Baba wa Taifa, tulikuwa na falsafa ya elimu ya kujitegemea yaani *education for self reliance*. Kwa hiyo, tunamtaka Waziri atueleze sasa hivi tunafuata falsafa ya namna gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya elimu ya juu. Elimu katika ngazi zote nchini imepanuka kwa kasi isiyozingatia ubora. Hii inadhihirishwa na utafiti uliofanywa na *The Global Competitiveness Index (GCI)* ya mwaka 2013/2014 kuangalia ubora wa vyuo vikuu kwa nchini katika nchi 148 duniani. Matokeo yanaonesha Kenya ikishika nafasi ya 44, Uganda ya 82, huku Tanzania ikishika nafasi ya 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tafiti kuonyesha Tanzania tulivyo nyuma katika ubora wa elimu, sasa hivi kumezuka tatizo kubwa la utofauti wa mitaala ya vyuo vikuu hususan vile vya binafsi hali inayopelekea migomo na sintofahamu miongoni mwa wanafunzi. Mfano mzuri ni vyuo vya *IMTU, St. Joseph* na *Kampala International University*. Kwa muda mrefu tatizo hili limefikishwa kwa wahusika na bado ufumbuji wa kina haujajulikana. Tunaitaka Serikali itueleze uswahiba uliopo kati yake na vyuo hivi na ni kwa nini wanafunzi wa Kitanzania wateseke kwa manufaa ya wamiliki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, kumekuwa na tofauti kubwa ya mitaala ya elimu ya juu kati ya vyuo vya elimu vya Serikali na vyuo binafsi. Hali hii ya elimu ya juu kwa sasa hasa vya binafsi katika mikakati wa kufanya biashara zaidi kuliko kutoa huduma ya elimu, imesababisha baadhi ya vyuo kuongeza muda wa programu zake kutoka miaka minne hadi sita. Miaka minne hadi miaka minne na nusu na miaka mitano hadi mitano na nusu. Tunataka Serikali itueleze hili ongezeko la miezi sita litagharamiwa na nani huku wataalamu wa Bodi ya Mikopo wakidai kutotambua nyongeza hiyo. Hali hii imesababisha pia baadhi ya vyuo kujitengenezea mitaala yake kwa lengo la kuwavutia wanafunzi kwa kile kinachoitwa *bridging courses* na hivyo kutanua wigo wa kujipatia faida zaidi bila kuzingatia ubora wa elimu. Mfano ni wahitimu wa Astashahada ya Famasi ya *Kampala International University*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na utofauti mkubwa wa mitaala katika vyuo vya elimu ya juu jambo linalosababisha kukosekana kwa ubora linganifu wa elimu ya juu katika ngazi mbalimbali; na kwa kuwa udhaifu wa mitaala katika elimu ya juu umesababisha mara kadhaa migogoro kati ya wanafunzi na watawala wa vyuo husika na hivyo kusababisha baadhi ya wanafunzi kusimamishwa masomo na kufukuzwa kabisa; na kwa kuwa Tume mbalimbali zilizoundwa kuchunguza ubora wa elimu hapa nchini zilibaini kuwa kuporomoka kwa elimu ni kukosekana kwa mitaala thabiti inayoeleweka na isiyozingatia ubora wa elimu katika mazingira mahalia; na kwa kuwa Tume ya Elimu ya Juu (*TCU*) ina mamlaka ya kuratibu na kusimamia mitaala ya vyuo vya Elimu ya Juu; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuiagiza Tume ya Vyuo Vikuu kutoa ndani ya kipindi cha siku sitini, mwongozo mpya kwa vyuo vya elimu juu nchini kuhusu ya vigezo vya kuzingatia wakati wa kuandaa mitaala ya elimu ya juu.

(ii) Kuvifungia mara moja vyuo vyote vya elimu ya juu vinavyoendeshwa kwa maslahi ya kibiashara zaidi bila kuzingatia mitaala na ubora wa elimu mpaka hapo vitakapojirekebisha. (Makofi)

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

(iii) Kuiagiza Tume ya Vyuo Vikuu nchini kusitisha mara moja kutoa ithibati kwa vyuo vya elimu ya juu ambavyo vitakuwa havina mitaala iliyozingatia vigezo vitakavyowekwa na Tume hiyo ya Elimu ya Juu.

(iv) Kuwa na mfumo mmoja tu wa udahili yaani *central admission system* ambayo utasaidia sana kuondoa kinachoendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza ni kwa nini Tume ya Vyuo Vikuu nchini ilitoa ithibati kwa Chuo Kikuu cha *Kampala International University* huku wakijua baadhi ya programu hazijasajiliwa na Bodi mbalimbali kama ile ya *Pharmacy* hivyo kusababisha hasara kwa chuo na wanafunzi? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kutoa majibu kwa maswali yafuatayo: -

(i) Ni kwa nini baadhi ya programu zinazofanana mfano *Medical Laboratory* na *Pharmacy* kwa chuo kikuu cha Kampala zitofautiane kwa kiasi kikubwa na vyuo vikuu vingine kama Muhimbili, KCMC na kadhalika?

(ii) Ni kwa nini TCU na Wizara wanapopata taarifa za matatizo haya hawajali na kuacha jambo hilo liote mizizi na kuleta athari kubwa kama ilivyotokea *KIU, St. Joseph* na *IMTU*?

(iii) Ni kwa nini inapotokea tatizo na kuonyesha wazi Serikali ndiyo yenye makosa, wanafunzi ndiyo wanakuwa wahanga badala ya Serikali kuwajibika? (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WAZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Tangu Sheria ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuanzishwa, kumekuwa na changamoto nyingi kuhusu mikopo ya elimu ya juu hadi Rais alipoteua Tume iliyoongozwa na Profesa Maboko Makenya kushughulikia matatizo ya mikopo ya elimu ya juu. Kinachotushangaza ni kwamba, ripoti ya Tume hiyo haijawekwa hadharani na bado matatizo ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu yako palepale. Wanafunzi hawapati fedha kwa wakati hali inayoleta adha kubwa kwa wanafunzi kwani wengi wao wanatoka kwenye familia duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumeshauri mara kadhaa kuhusu matatizo ya mfumo ya mikopo ya elimu ya juu na kuupuzwa, Serikali mpya ya UKAWA italipa kipaumbele suala hili la mikopo ya elimu ya juu kwa kutambua kwamba, mikopo ni haki ya mwanafunzi na bila mikopo hiyo hawatasoma kwa utulivu na kuzifikia ndoto zao kama ilivyo kwenye Sera ya CHADEMA ya 2005/2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haitaki ushauri wa UKAWA basi walau ijifunze kutoka nchi jirani ya Rwanda inavyofanya kuhusu mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza yafuatayo:-

(i) Ni kwa nini haitoi fedha ya mikopo hadi wanafunzi wagome na kuandamana?

(ii) Ni wapi fedha hizo zinakwenda hasa ukizingatia 100% ni za ndani?

(iii) Ni kwa nini ndani ya masaa 12 tu ya mgomo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tarehe 19/5/2015, fedha hizo zilitoka? Au ni Sera ya CCM kuwajengea wanafunzi tabia ya



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

kupata haki zao kwa migomo na baadaye kusema ni UKAWA wanachochea migomo vyuoni?  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa elimu na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Takwimu za ripoti ya utekelezaji wa BRN ya *Presidential Delivery Bureau* na Jarida la HakiElimu la Hali ya Utekelezaji wa BRN zinaonesha kuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa BRN ulikuwa na changamoto nyingi za kiutendaji na mambo mengi yanayohusiana na fedha hayakutekelezwa. BRN ya Elimu ilibaninisha wazi kutoa ruzuku ya asilimia 100 yaani shilingi 10,000/= kwa kila mwanafunzi shule za msingi na shilingi 25,000/= kwa mwanafunzi shule za sekondari, lakini utekelezaji umekuwa kwa asilimia 42 tu kwa msingi na asilimia 48 tu kwa sekondari. Ujenzi wa miundombinu haukitekelezeka pia ambapo kati ya shule 792 zilizopangwa kufanyiwa ukarabati hadi ilipofika Machi, 2014, ni shule 56 tu zimekarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya BRN kutatua mgogoro wa walimu na kufanya walimu wafundishe ipasavyo. Wakati BRN inaanza asilimia 53 ya walimu walikuwa hawapo darasani yaani hawafundishi. Utafiti wa Shirika la Twaweza kwenye kijarida namba 13 cha mwaka 2014, unaonesha kuwa, hivi sasa ni asilimia 34 tu ya walimu ndiyo wanaingia na kufundisha muda wote wa kipindi na idadi iliyobaki ama wanaingia kwa muda mfupi tu au hawaingii kabisa. Kwa takwimu hizi za utekelezaji, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza, ni mambo gani au ni miujiza gani iliyofanywa na sekta ya elimu hadi kuipatia sekta hiyo asilimia 81 katika utekelezaji ilihali katika malengo yoke yote ya BRN ya elimu hakuna hata lengo moja lililofikia asilimia 50? Ni wazi Serikali haijawekeza vya kutosha katika elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalochekesha ni pale Serikali hii ya CCM inaposema kwamba katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa imefikia asilimia 81. Kwa mtu yeyote mwenye akili timamu atajiuliza, ni uwekezaji gani umefanyika hadi tukapata matokeo haya? Je walimu ambao ndiyo watendaji wakuu wamefanyiwa nini? Ni jambo la kusikitisha kuona uwekezaji ukipungua lakini matokeo yakiwa mazuri zaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, kuna miujiza gani kama si mbinu chafu na za ujanja ujanja kama tuliovyosema mwaka juzi? Ukweli kilichofanyika ni kubadili alama na madaraja jambo ambalo kimsingi ni mbinu chafu na hauoneshi uhalisia wa uwezo wa watoto wetu na hivyo hawataweza kujajiri wala kuajiriwa nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuelewe kila mtoto wa kitanzania anahitaji elimu bora kwani elimu ni kwa ajili ya kujikomboa na kujibadili. Mwalimu Nyerere alisema mwaka mmoja kabla ya kifo chake akiwa *Open University*:-

*"Not all of us will have the same concept of community, but all of us have a need to belong, nobody is asking us to love others more than we love ourselves but those of us who have been lucky enough to receive a good education have a duty also to help to improve the well being of the community to which we belong, is part of loving ourselves"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa kiasi gani wasomi wa nchi hii na wenye madaraka mnapenda watoto wa Tanzania wapate elimu bora? Au sisi wenyewe watoto wetu wako nje ya nchi? Je, tunaboreshaje elimu yetu kwa kuwa kufanya hivyo ni sehemu ya kupendana? Tumeshindwa na tunashuhudia wasomi wetu waliopata elimu bora wamekuwa chanzo cha kuharibu elimu yetu, kwa kuruhusu akili ndogo kutawala akili kubwa. Haiwezekani Profesa aliyepewa kuongoza sekta ya elimu ashindwe kutoa ushauri kuhusu uboreshwaji wa elimu. Inawezekanaje Maprofesa wetu hawa wasajili na watoe ithibati kwa vyo vikiu vyenye maabara yenye kiwango cha shule za kata halafu mnategemea wahitimu wa vyo hivi waajiriwe, waajiriwe wapi? (Makofi)

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua, Wizara ya Elimu imegatua madaraka lakini ukiangalia katika fedha zilizopangwa katika Wizara ya Elimu kati ya shilingi bilioni 478 ni shilingi bilioni 126 tu ndiyo zimepangwa kwenye Serikali za Mitaa ambazo ndiyo zinatekeleza shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Hakuna nchi yoyote iliyoendelea hapa duniani bila kuwekeza kwenye elimu. Malaysia inajivunia maendeleo yake kwa kuwa iliwekeza kwa vitendo katika elimu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaarifu wananchi wake kwamba, kwa kuwa Serikali ya CCM haina nia ya dhati ya kuboresha elimu yetu kutokana na kushindwa hata kutekeleza ilani yake yenyewe kuhusu elimu, Serikali mpya ya UKAWA itakayoingia madarakani baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2015 itayashughulikia matatizo yafuatayo katika sekta ya elimu:-

- (i) Uhafifu na uduni wa elimu inayotolewa katika ngazi mbalimbali;
- (ii) Kuongezeka kwa idadi ya watu wasiojua 3Ks;
- (iii) Uduni wa shule za sekondari;
- (iv) Uduni wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (v) Mkanganyiko wa lugha ya elimu ya kufundishia na kujifunzia;
- (vi) Kutokuwa na mfumo thabiti kuhusu ugharamiaji wa elimu na hasa elimu ya juu;
- (vii) Usimamizi dhafu wa elimu inayotolewa na taasisi zinazomilikiwa na watu na mashirika yasiyo ya kiserikali;
- (viii) Kutokuwa na uwiano kati ya wanachojifunza wahitimu na kinachoendelea katika ulimwengu wa kazi, kutokana na udhafu wa mitaala na ufundishaji. Matokeo yake, wahitimu wetu walio wengi hawajiriki wala hawawezi kujijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nawatakia Wabunge wote kila la kheri wanapoelekea uraiani baada ya Bunge hili kuvunjwa, lakini pia nawatakia ushindi wa kishindo wagombea wote wa Udiwani, Ubunge na Urais watakaopendekezwa na UKAWA kugombea nafasi hizo, ili Serikali ya Awamu ya Tano itokane na UKAWA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Watanzania wote wanaopenda kuona taifa letu likisonga mbele kwa kasi ya kumuondoa adu ujinga, jambo lililoshindwa kutekelezwa na Serikali ya CCM, ni UKAWA tu wanaweza kubadili hali hii kwa kuboresha mfumo wa elimu na kuwekeza kwa vitendo katika elimu. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki UKAWA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI MHE. SUSAN ANSELM JEROME LYIMO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013*

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa spika**, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuweza nkusimama hapa kusoma hotuba hii. Kipekee namshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Mhe. Freeman Mbowe kwa kuendelea kuniamini katika kusimamia Wizara hii nyeti kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, nawapongeza kwa dhati wenyeviti wenza wa UKAWA; Mhe. Dkt. Emanuel Makaidi wa NLD, Mhe. Prof. Ibrahim Lipumba wa CUF na Mhe. James Mbatia wa NCCR Mageuzi kwa kazi kubwa sana na nzuri wanayofanya ya kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na UKAWA kwa kuwa ndio tumaini pekee lilobaki la kuwakomboa na ndio njia pekee ya kuiondoa serikali ya CCM madarakani ifikapo 25/10/2015. Hivyo naomba wananchi wote wanaokerwa na kuporomoka kwa shilingi yetu, ufisadi, rushwa na hali mbaya ya maisha watumie fursa hii ya maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kujitokeza kwa wingi na kuwahi kujiandikisha mapema daftari litakapopita katika maeneo yao kwani ndio njia pekee ya kuiondoa CCM madarakani kidemokrasia.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanawake wa Mkoa wa Kinondoni kichama kwa ushirikiano wao, kipekee nawashukuru viongozi wa CHADEMA na wanachama wa Jimbo hilo kwa ushirikiano mnaonipatia katika kutimiza nia na ndoto zangu. Mungu awabariki sana.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa maisha ya Bunge hili la kumi yatafikia ukomo wake hivi karibuni, hii itakuwa ni hotuba yangu ya mwisho kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakumbukwa kwa kwa jitihada zake za kuikosoa na kuishauri Serikali juu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa lengo na nia nzuri ya kuboresha elimu hapa nchini. Ni imani yangu kwamba nilitumikimia nafasi hii ya Waziri Kivuli wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa uaminifu na weledi mkubwa. Na ni furaha yangu vilevile kwamba wananchi na wadau wote wa elimu waliridhika na mchango wa kazi za upinzani katika wizara hii.

## 2. SERIKALI YA CCM ILIVYOSHINDWA KUTEKELEZA ILANI YAKE KUHUSU ELIMU

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hii ya awamu ya nne ya CCM imeshindwa kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi kuhusu Elimu kwa mihula yote miwili ya utawala wake. Ibara ya 85 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 inasema kwamba: **“Serikali itachukua hatua za *kuboresha, kuimarisha elimu ya awali hadi ya Chuo Kikuu na kuhakikisha kwamba elimu ya ngazi zote itakayotolewa nchini tangu sasa iwe na ubora utakaowawezesha vijana wetu kuchukua nafasi zao stahiki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla*”**.

### (a) Elimu ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Chama cha Mapinduzi (CCM) kiliwahidi watanzania kupitia Ilani yake ya uchaguzi kufanya yafuatayo katika Elimu ya Awali endapo kitapewa ridhaa ya kuongoza Serikali.

i. Kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi ina darasa la Elimu ya Awali lenye madawati yanayolingana na hali ya watoto wa elimu hiyo.

ii. Kujenga vyoo kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali ili wasiingiliane na wale wa shule ya msingi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwaambia wananchi wote kwamba walitapeliwa na CCM kwani Serikali ya CCM haikutekeleza ahadi hiyo hata japo kwa asilimia 50. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge wananchi kama

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

imetekeleza ujenzi wa madarasa ya elimu ya awali katika kila shule ya msingi nchini na kuweka madawati yanayolingana na watoto hao, sambamba na ujenzi wa vyoo vya watoto wa elimu ya awali katika kila shule ya msingi ili wasiingiliane na wale wa shule ya msingi kama ilivyoahidi.

**Mheshimiwa Spika**, mazingira ya elimu ya awali bado yako duni sana ambapo asilimia kubwa ya watoto bado wanakaa chini. Aidha kumekuwa na ongezeko la matatizo ya kukosa matundu ya vyoo, kukosa chakula jambo linalowafanya watoto kukosa hamasa ya kujifunza kutokana na njaa, na vifaa duni vya kufundishia na kujifunzia.

**Mheshimiwa Spika**, Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi kwa elimu ya awali nao umekuwa ni tatizo. Japo lengo la kitaifa ni mwalimu 1 afundishe wanafunzi 25, hali ya uwiano wa kitaifa ni mbaya sana ambapo takwimu za BEST za mwaka 2013 zinaonesha uwiano hivi sasa ni mwalimu 1 anafundisha wanafunzi 199 na kila mwaka unaongezeka ambapo mwaka 2010 ulikuwa 1:73 ukaendelea kukua na kufikia 1:124 mwaka 2012, na sasa umefika 1:199

### **(b) Elimu ya Msingi**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha elimu ya msingi, Chama cha Mapinduzi pia kiliwaahidi wananchi kufanya yafuatayo endapo kinegopewa ridhaa na wananchi kuongoza Serikali:

i. Kuendelea kuyaboresha maslahi ya walimu ili kuhakikisha mishahara itolewayo inazingatia hali halisi ya maisha na soko.

ii. Kuendelea kuimarisha ukaguzi wa shule na kuhakikisha kila shule inakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na taarifa ya ukaguzi kufanyiwa kazi.

**Mheshimiwa Spika**, wananchi waliamini, wakaichagua CCM kuongoza dola. Lakini baada ya kushika dola wamesahau kabisa yote waliyoahidi. Wote tunajua madhila yanayowapata walimu wetu. Kilio chao cha malimbikizo ya mishahara na stahili zao nyingine ni cha muda mrefu sana. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba hata mishahara ya walimu imekuwa haifiki kwa wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kwamba baadhi ya walimu walioajiriwa tarehe 1 Mei, 2015 hawajalipwa fedha yao ya kujikimu (settling in allowance) hadi leo.

**Mheshimiwa Spika**, kama tulivyosema walimu ndio nyenzo kuu katika elimu lakini cha ajabu walimu wa Tanzania wamekuwa wakionewa na kudhalilishwa kila leo. Mfano Serikali imetoa muundo mpya wa mishahara ya walimu Julai, 2014 unaojulikana kama TGTS ambapo zaidi ya walimu laki moja (100,000) walipaswa kutoka E kwenda F. Walimu hawa kwa makisio ya chini wanahitaji zaidi ya bilioni mia moja (100,000,000,000/=) kwa wastani wa nyongeza ya shilingi 100,000/= kwa mwezi. Kwa mahesabu rahisi kama ni walimu 100,000 x 100,000/= kwa miezi 12 kwani muundo huu umeanza toka Julai, 2014.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuonyesha fedha zilizotengwa kwa ajili ya nyongeza ya mishahara ya walimu katika bajeti hii. Msingi wa hoja hii ni kuepuka mwendelezo wa malimbikizo ya madeni ya walimu ambayo licha ya kuwa kero kwa walimu sasa pia yameanza kutumiwa kama kete ya kisiasa nyakati za chaguzi. Nathubutu kusema hivyo kwa sababu Rais Kikwete akizungumza na chama cha walimu hivi karibuni alisema kabla hajaondoka madarakani atahakikisha walimu wamelipwa madeni yao kana kwamba hakuyaona madeni hayo tangu 2005 alipoingia madarakani. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali pia kulieleza Bunge hili kama lile deni ambalo Serikali ilisema inalihakiki na kwamba sasa ni bilioni 10 lipwa lini na tengeo lake katika bajeti hii liko wapi? Aidha Kambi Rasmi

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

ya Upinzani Bungeni inataka kujua wale walimu zaidi ya 37,000/= waliopandishwa madaraja lakini hawajarekebishiwa mishahara yao watalipwa lini?

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ukaguzi; ni wazi kuwa bila ukaguzi ubora wa elimu hauwezi kupatikana. Licha ya majigambo na ahadi hewa ya Serikali hii kupitia Ilani ya CCM; kwamba kila shule itakuwa inakaguliwa mara moja kwa mwaka, takwimu za wizara zinaonesha kwamba, ukaguzi wa shule umefikia asilimia 37 tu. Hii ina maana kwamba zaidi ya asilimia 63 ya shule za Msingi na sekondari hazikukaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hii ya CCM ni ya ajabu sana kwa kuwa imechoka, inajichanganya na imefikia hatua ambayo hata haina kumbukumbu ya mambo iliyowahi kuahidi. Nasema hivi kwa sababu tarehe 29 Aprili, 2013, Rais Jakaya Kikwete aliwahidi wananchi kupitia mazungumzo yake na Wakuu na Wamiliki wa Shule za Sekondari binafsi huko Mbeya kwamba "Serikali ingeanzisha Wakala wa Ukaguzi anayejitegemea na kwamba Serikali ingemwezesha Wakala huyo kwa rasilimali fedha /watu na vitendea kazi ili kimarisha utendaji kazi ya ukaguzi na matokeo yake yataonekana kwa muda mfupi",

**Mheshimiwa Spika**, jambo hilo halijafanyika, lakini mbaya zaidi ni kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani imesikitishwa sana na utendaji wa serikali hii baada ya ofisi ya Waziri Mkuu kuandika barua ya kumbukumbu No: CBC/10/348/05/10 ya tarehe 13 Oktoba, 2014 inayositisha agizo la Rais la kuanzisha wakala wa ukaguzi wa shule. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutoa maelezo juu ya mkanganyiko (confusion) huu ndani ya Serikali kuhusu uanzishwaji wa wakala wa ukaguzi wa shule. Swali la kujiuliza tuna serikali ngapi??

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumaliza sehemu hii kwa kuwaambia wananchi kwamba, Elimu haijawahi kuwa kipaumbele katika sera za CCM kwa awamu zote nne za utawala wake ndio maana haitekezi hata ilani yake yenyewe. Sera ambayo CCM imepigia upatu kwa miaka yote 53 ya uhuru na ambayo pia imeshindwa kutekeleza ni Kilimo. Ndio maana tangu enzi za uongozi wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere sera zilizosikika ni **Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona, Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa, na sasa Kilimo Kwanza**. Hatujawahi kusikia Elimu Kwanza kwa utawala wa CCM kwa miaka yote 53 ya uhuru.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Elimu Kwanza ni Sera ya Upinzani. Ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA ya 2005, na 2010 na imepewa kipaumbele cha kwanza, cha pili na cha tatu. Na kwa kuwa sasa hivi tupo katika ushirikiano wa UKAWA, sera hii imekuwa ni Sera ya UKAWA. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaonya wanaotangaza nia ya kugombea Urais wa Tanzania kupitia CCM kuacha kuwawadanganya wananchi kwamba Elimu itakuwa kipaumbele namba moja ikiwa watachaguliwa, kwa kuwa walikuwa Serikalini kwa miaka yote tangu uhuru na wakashindwa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Itakumbukwa kwamba CHADEMA iliposema elimu itakuwa bure kama ingechaguliwa kuunda Serikali mwaka 2005 na 2010, CCM iliendesha propaganda chafu na kuwapotosha wananchi kwamba haiwezekani kutoa elimu bure. Lakini ili kuthibitisha ile methali isemayo kwamba *njia ya mwongo ni fupi*, CCM sasa hivi imekubali kula matapishi yake na kusema katika kipengele cha 3.1.5 cha Sera Mpya ya elimu ya mwaka 2014 kwamba Elimu ya Msingi itakuwa bure. Huu ni uthibitisho kwamba CCM imebobeza katika wizi hadi kufikia hatua ya kuiba sera za upinzani waziwazi bila aibu!!! Lakini inathibitisha kwamba Sera za Upinzani zinatekelezeka, na kwa maana hiyo, UKAWA ukitwaa madaraka ya dola katika uchaguzi wa Oktoba, 2015 Elimu ya Msingi mpaka Chuo Kikuu itakuwa BURE KWELI KWELI.

## **2. SERA MPYA YA ELIMU 2014**

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Elimu ilizinduliwa kwa mbwembwe nyingi lakini ukiisoma vizuri sera ile ni vituko vitupu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilidhani kwamba, baada ya Sera ya Elimu ya 1995 kuwa na mapungufu mengi yaliyopelekea mambo mengi kuharibika basi ingekuwa somo tosha kwa maboresho ya sera hii, lakini kwa masikitiko makubwa sera hii imekuwa ni ya matamko tu.

**Mheshimiwa Spika**, tumekuwa tunashindwa kutekeleza sera zetu kwa kuwa zimekuwa ni sera bainishi (substantive policies) na hivyo kubainisha mapungufu tu na kuacha sehemu ya pili ya utekelezaji. Hivyo kilichobainishwa kinashindikana kutekelza kwa kuwa nyenzo za utekelezaji haziwekewi mkazo. Kimsingi, ili sera hii itekelezake ni lazima iwe na ngazi hizi mbili yaani sera bainishi na sera namna. Sera nyingi hapa nchini zimekuwa dhaifu na kutokutekelezwa kwa kukosa ngazi ya pili yaani sera namna.

**Mheshimiwa Spika**, Ili sera hii ya elimu iweze kutekelezeka inahitaji kutafutiwa ufumbuzi wa mambo matatu la sivyo hakutakuwa na jipya. Mambo hayo ni pamoja na walimu bora, zana bora za kufundishia, na walimu wenye motisha. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetenga fedha kiasi gani katika bajeti hii kwa ajili ya zana bora za kufundishia na motisha kwa walimu ili kurahisisha utekelezaji wa Sera Mpya ya Elimu?

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania imekuwa inasifika sana kwa kuandika vizuri sera zake lakini utekelezaji wake ni **Shidaa!!!** Mfano sera hii haienzi ni kwa kiasi gani itaondoa ubaguzi au matabaka ya elimu hasa viwango vya elimu. Aidha, haienzi nini maana ya kufuta ada ikiwa kuna michango ni mingi kuliko ada yenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Elimu inasema serikali itahakikisha kuwa elimu ya msingi katika mfumo wa umma inatolewa bila ada. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulithibitisha Bunge hili kama elimu bila ada itaanza kutolewa kwa mwaka wa fedha 2015/16, au tamko hili la sera lilikuwa ni la kisiasa kwa ajili ya kuendelea kuwahadaa watanzania?

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu kwa swali hili kwa sababu asa hivi wazazi wengi wana mkanganyiko wa suala hili kwa kuwa wanafahamu kuwa kwa kuwa sera hii imezinduliwa mwezi Februari 2015 na matarajio yao ni kwamba utekelezaji wa elimu bure utanza mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kujibu hoja hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ikumbuke kuwa changamoto kubwa za mazingira ya kufundishia na kujifunzia zinatokana na ufinyu wa bajeti na pia serikali kutotoa fedha za kutosha shuleni. Mathalani katika utekelezaji wa MEM I na MEM II ni wastani wa shilingi 5,000 hadi shilingi 6,000 kati ya shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi ndio zilitolewa na serikali na hata katika MEM III bado serikali imeshindwa kutoa fedha hizi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015 serikali imetoa wastani Shilingi 860 tu, kwa kila mwanafunzi badala ya shilingi 10,000. Kambi Raasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kwa kiwango gani changamoto hizi zinapatiwa ufumbuzi katika bajeti ya 2015/2016 au ndio kusema Business **as Usual**.

### **3. SHULE BINAFSI**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu gharama za shule za binafsi kuwa kubwa mno kiasi kwamba ni wananchi wachache wanaweza kuwalipia watoto wao ada na gharama nyingine katika shule hizo. Na kwa kuwa shule hizo zinatoza ada kubwa zinakuwa na uwezo wa kuwapa motisha walimu na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza hivyo kuonekana kwamba zinatoa elimu bora kuliko zile za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili limeleta matabaka katika utoaji wa elimu kwani sasa inaonekana kwamba shule za Serikali ni kwa ajili ya watu masikini na shule binafsi ni kwa ajili ya watoto wa matajiri. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imefanya jitihada gani katika kuwianisha gharama za elimu kati ya shule binafsi na shule za Serikali ili kuondoa matabaka katika utoaji wa elimu? Kwa kuwa wenye shule binafsi wanadai gharama zao ziko chini kama tutaangalia **Student's Unit Costs**. Je pamoja na malalamiko hayo ni kwa nini serikali haijafanya utafiti kujua kama hili ni kweli ili wananchi wajue gharama halisi za elimu?

#### **4. SERIKALI YA CCM ILIVYOSHINDWA KUWAPATIA WANAFUNZI MADAWATI MASHULENI TANGU UHURU**

**Mheshimiwa Spika**, ni jambo la kusikitisha na ni aibu kwa Serikali hii ya CCM inayojigamba kuwa imeleta maendeleo kushindwa kuwapatia wanafunzi madawati licha ya utajiri wa rasilimali za misitu tulizo nazo, na licha ya ujuzi na nguvu kazi iliyopo katika magereza yetu ambapo wafungwa na mahabusi wangeweza kutumika kutengeneza madawati hayo.

**Mheshimiwa Spika**, ni aibu kubwa kwa Serikali hii ya CCM kujigamba katika Sera Mpya ya Elimu na Waziri Mkuu kujibu swali hapa Bungeni na kukazia kwamba wanafunzi wa shule za msingi watapatiwa Kompyuta Mpakato (Laptops) ilhali sehemu kubwa ya watoto wetu bado wanakaa chini na wengine wanakalia mawe kama nyani kwa miaka 54 sasa ya uhuru. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapata tabu kuelewa kama Serikali hii imechanganyikiwa au iko *serious* kwamba itawapa kompyuta wanafunzi wambao hawana pa kukaa shuleni na shule hizo hazina umeme.

**Mheshimiwa Spika**, wenzetu wa Kenya na Rwanda wameweza kuwapa watoto wao kompyuta mpakato (Laptops). Katika bajeti ya elimu - Kenya toka 2013 walitoa laptops kwa wanafunzi wote wa shule za msingi lakini hapa kwetu ni porojo tu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuonesha bajeti ya kununua laptops kwa wanafunzi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera Mpya ya Elimu na ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Waziri Mkuu akijibu swali hapa Bungeni kwamba wanafunzi wote wa shule za Msingi watapatiwa kompyuta mpakato.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, hivi Kamati Kuu ya CCM iliyokaa zaidi ya mara 212 (x4 kila mwaka) ukiacha vile vikao vya dharura kwa miaka yote 53 na nusu ya uhuru huwa inajadili nini ikiwa hali ya upatikanaji wa madawati ni tete kiasi hiki huku magogo yetu yakiuzwa China na kwingineko? Kambi Rasmi ya Upinzani imeshawishika kuamini kwamba Serikali hii ya CCM si kwamba imechoka tu bali pia imefikia ukomo wa kufikiri na kwa maana hiyo kuiruhusu kuendelea kutawala ni kuruhusu anguko kuu la nchi au waswahili wanasema ni janga la Taifa na ni **shiiida**.

#### **5. ELIMU YA UALIMU**

**Mheshimiwa Spika**, Elimu ni mwalimu, kwani unaweza kuwa na madarasa mazuri sana, maabara ya viwango vya juu lakini bila mwalimu mwenye motisha na aliyepewa mafunzo vizuri hakuna chochote tutakachofanikiwa. Elimu ni sawa na kiwanda ambapo mwanafunzi ni malighafi, walimu na vitabu ndio mashine za uchakataji na usindikaji. Hivyo kama ilivyo kwa malighafi inapopita kwenye mashine tunachopata ni kitu kipya kama pamba kuwa nguo. n.k. Hivyo mtoto anaingia hajui chochote lakini anategemewa atoke amebadilika kwa kujua kusoma, kuandika na kubwa zaidi kujitambua na kujua kuchambua mambo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kama Elimu ya Ualimu inayotolewa ina ubora wa kutosha kwa kuwa mwalimu bora ndiye anayegemewa katika kuwafundisha watoto wetu

**Mheshimiwa Spika.** Kulingana na mtaala wa mafunzo ya ualimu, mafunzo kwa vitendo kwa walimu (Block Teaching Practice) yanapaswa kutolewa kwa wiki 8 kila mwaka wa masomo. Kwa miaka miwili 2013/14 na 2014/15 mafunzo yametolewa kwa wiki 2 tu yaani wiki 4 badala ya wiki 16. Kupunguza muda wa mafunzo kwa vitendo kunapunguza pia weledi na uwezo wa mwalimu husika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili sababu za kupunguza muda wa mafunzo kwa vitendo na athari zitakazotokana na muda huo kupunguzwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia inahoji, Serikali inategemea kuwapata walimu wa kiwango gani cha weledi ikiwa inapunguza muda wao wa mafunzo?

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako Tukufu kwa kutambua umuhimu na ubora wa waalimu lilipitisha bajeti ya shilingi **7,210,370,000/= (2014/2015)**. Serikali kwa kutothamini fani hii ilipunguza kiasi hicho kwa shilingi **5,165 006, 020, sawa na 72%**, hii ina maana kwamba fani ya Elimu ya Ualimu wamepata shilingi **bilioni 2 tu** sawa na asilimia 28% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huo hadi April 2015.

**Mheshimiwa Spika,** inasikitisha na inatia hasira kusikia kwamba Serikali inasema mkakati iliyo nao ili kuhakikisha walimu hawa waliokosa mafunzo kwa vitendo, “watakuwa chini ya uangalizi wa wakaguzi wa shule kwa kipindi cha mwaka mmoja pindi watakapoajiriwa ili kupata muda wa kutosha wa mazoezi ya ufundishaji” Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji Serikali itatekeleza vipi mpango huo wa ukaguzi na kwa bajeti ipi ikiwa ukaguzi uliofanyika ni asilimia 30 tu?

## 6. ELIMU YA JUU

**Mheshimiwa Spika,** elimu ya juu ndio inayomfunza kijana jinsi ya kuchambua mambo na kujenga weledi katika fani mbalimbali. Mwl. Nyerere, katika kitabu chake cha Uhuru na Maendeleo, alisema: **“Intellectuals have a special contribution to make to the development of our nation, and their knowledge and greater understanding that they should possess, should be used for the benefit of the society of which we are all members”**

**Mheshimiwa Spika,** Kinyume na maneno ya Hayati Baba wa Taifa, mchango wa wasomi wetu katika maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla umewekewa vikwazo na mfumo wa utawala wa Serikali hii ya CCM. Wasomi wenye elimu ya juu kokosa ajira limekuwa ni jambo la kawaida, na wasomi pia kukosa fursa na mazingira bora ya kujiajiri nayo ni changamoto kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kueleza imewasaidiaje wahitimu wa elimu ya juu kama vile wahandisi, kilimo, wanasheria, katika kuanzisha Kampuni zao za uhandisi, Kampuni za huduma za kisheria (Law firms), Kampuni za ushauri nasaha kwa waliohitimu fani za Saikolojia nk. Nauliza hivi kwa sababu kodi za wananchi zimetumika kuwasomesha wahitimu hao lakini mwisho wa siku wanabaki mitaani bila tija yoyote. Hii inamaana kwamba Taifa limeingia hasara kuwasomesha watu ambao hatimaye hawana mchango wowote katika uchumi wa nchi na badala yake wanakuwa tegemezi na kuongeza kiwango cha umasikini nchini. Na haya yote yamesababishwa na mitaala mibovu ya elimu ambayo imeshindwa kuwajengea uwezo wa kujiajiri pale wanapokosa ajira za moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, nchi hii inafuata falsafa gani ya elimu kwa sasa? *What is our current education philosophy?* Nauliza hivi, Mhe. Spika, kwa sababu wakati wa utawala wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, nchi hii ilikuwa ikifuata falsafa ya “Elimu ya Kujitegemea” yani *Education for Self Reliance*, ambapo msingi wa elimu ulikuwa ni kumwezesha aliyenufaika na elimu kujiajiri katika sekta mbalimbali za uzalishaji mali. Lakini kwa hali ilivyo sasa, elimu yetu haionekani kuwa na msingi wa kumsaidia mhitimu kujiajiri. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka



kujua kama ile falsafa ya elimu ya kujitemea imefutwa, na kama imefutwa sasa hivi taifa lina falsafa gani ya elimu au tupo tupo tu?

## **7. MATATIZO YA ELIMU YA JUU**

**Mheshimiwa Spika**, elimu katika ngazi zote nchini imepanuka kwa kasi isiyozingatia ubora. Hii inadhihirishwa na utafiti uliofanywa na The Global competitiveness Index (GCI) mwaka 2013/14 kuangalia ubora wa vyuo vikuu kwa nchi 148 duniani. Matokeo yanaonesha Kenya ikishika nafasi ya 44, Uganda ya 82, huku Tanzania ikishika nafasi ya 100.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na tafiti kuonyesha Tanzania tulivyo nyuma katika ubora wa elimu ya Juu, sasa hivi kumezuka tatizo kubwa la utofauti wa mitaala ya Vyuo Vikuu hususan vile vya binafsi hali inayopelekea migomo na sintofahamu miongoni mwa wanafunzi. Mfano mzuri ni vyuo vya St. Joseph na Kampala International University (KIU). Kwa muda mrefu tatizo hili limefikishwa kwa wahusika na bado ufumbuzi wa kina haujulikana. Tunaitaka serikali itueleze uswahiba uliopo kati yake na Vyuo hivi. Na ni kwa nini wanafunzi wakitanzania wateseke kwa manufaa ya wamiliki?

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema hapo awali, kumekuwa na tofauti kubwa ya mitaala ya Elimu ya juu kati ya vyuo vya elimu ya juu vya Serikali na vyuo binafsi. Tofauti hii kubwa kwa upande mmoja imesababishwa na kuongezeka kwa kasi kwa vyuo vya Elimu ya juu nchini kutokana na ongezeko la watu wanaohitaji elimu lakini kwa upande mwingine tofauti hii imesababishwa na ukweli kwamba elimu hasa kwa vyuo binafsi inatolewa kibiashara zaidi kuliko huduma. Kutokana na hali hii ya vyuo vya elimu ya juu (hasa vya binafsi) kuwa katika mkakati wa kufanya biashara zaidi kuliko kutoa huduma ya elimu, imesababisha baadhi ya vyuo kuongeza muda wa programu zake kutoka miaka minne hadi minne na miezi sita, na miaka hadi mitano na miezi sita bila kuzingatia utaratibu wa bodi ya mikopo. Tunataka serikali itueleze hili ongezeko la miezi sita litagharamiwa na nani huku wataalamu wa bodi wakidai kutotambua muda huo wa nyongeza?

**Mheshimiwa Spika**, hali hii imesababisha pia baadhi ya vyuo kujitengenezea mitaala yake kwa lengo la kuwavutia wanafunzi kwa kile kinachoitwa "bridging courses" na hivyo kutanua wigo wa kujipatia faida zaidi bila kuzingatia ubora wa elimu inayotolewa na bila kujali namna elimu iliyotolewa inavyoendana na mazingira ya nchi yetu. Kutokana na hali hii, vijana wengi wanaohitimu ngazi mbalimbali katika elimu ya juu wamekuwa wakishindwa kuingia katika soko la ajira kwa kuwa masomo waliyofundishwa hayaendani na mahitaji halisi ya soko la ajira; Mfano ni wahitimu wa Astashahada ya famasi ya Kampala International University.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kumekuwa na utofauti mkubwa wa mitaala katika vyuo vya elimu ya juu jambo linalosababisha kukosekana kwa ubora linganifu wa elimu ya juu katika ngazi mbalimbali; na kwa kuwa kukosekana kwa ubora linganifu wa elimu ya juu unaozingatia mazingira ya nchi yetu kumesababisha vijana wengi wanaohitimu elimu ya juu katika ngazi mbalimbali kukosa sifa za ushindani katika katika soko la ajira na hivyo kukosa fursa mbalimbali za ajira; na kwa kuwa udhaifu wa mitaala katika elimu ya juu umesababisha mara kadhaa migogoro kati ya wanafunzi na watawala wa vyuo husika na hivyo kusababisha baadhi ya wanafunzi kusimamishwa masomo na kufukuzwa kabisa; na kwa kuwa Tume mbalimbali zilizoundwa kuchunguza ubora wa elimu hapa nchini zilibaini kuwa elimu ya Tanzania imekuwa ikiporomoka mwaka hadi mwaka; na kwa kuwa kati ya sababu zilizotajwa za kuporomoka kwa elimu ni kukosekana kwa mitaala thabiti inayoeleweka na inayozingatia ubora wa elimu katika mazingira mahalia; na kwa kuwa Tume ya Elimu ya Juu (TCU) ina mamlaka ya kuratibu na kusimamia mitaala ya vyuo vya Elimu ya Juu;

**HIVYO BASI**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya yafuatayo:

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

- i. Kuiagiza Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kutoa ndani ya kipindi cha siku sitini, mwongozo mpya kwa vyuo vya elimu juu nchini kuhusu ya vigezo vya kuzingatia wakati wa kuandaa mitaala ya elimu ya juu.
- ii. Kuvifungia mara moja vyuo vyote vya Elimu ya Juu vinavyoendeshwa kwa maslahi ya kibiashara zaidi bila kuzingatia mitaala na ubora wa elimu mpaka hapo vitakapojirekebisha;
- iii. Kuiagiza Tume ya Vyuo vikuu nchini (TCU) kusitisha mara moja kutoa ithibati kwa vyuo vya Elimu ya Juu ambavyo vitakuwa havina mitaala iliyozingatia vigezo vitakavyowekwa na Tume ya Elimu ya Juu.
- iv. Kuhakikisha muda wa Provisional Accreditation ni wa kipindi cha mwaka mmoja tu ili kuondoa athari kwa wanafunzi wetu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleza ni kwa nini Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) ilitoa ithibati kwa Chuo Kikuu cha Kampala International University huku wakijua baadhi ya program hazijasajiliwa na Board mbalimbali kama ile ya Pharmacy hivyo kusababisha hasara kwa Chuo na wanafunzi? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu kwa maswali yafuatayo:

- i. Ni kwa nini baadhi ya program zinazofanana mfano Medical Laboratory na Pharmacy kwa Chuo Kikuu cha Kampala International University (KIU) zitofautiane kwa kiasi kikubwa hivyo na Vyuo Vikuu vingine kama Muhimbili, KCMC nk? Mfano wakati KIU wana kozi 14 wenzao wana 7 – 8 tu?
- ii. Ni kwanini TCU na Wizara wanapopata taarifa za matatizo haya hawajali na kuacha jambo hilo liote mizizi na kuleta athari kubwa kama ilivyotokea KIU, St. Joseph na IMTU?
- iii. Ni kwa nini inapotokea tatizo na kuonyesha wazi Serikali ndio yenye makosa wanafunzi ndio wanakuwa wahanga badala ya Serikali kuwajibika?

### **8. BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU**

**Mheshimiwa Spika**, tangu sheria ya Bodi ya Mikopo kuanzishwa, bado kumekuwa na changamoto nyingi kuhusu mikopo ya elimu ya juu hadi Rais alipoteua Tume chini ya Prof. Maboko Makenya kushughulikia matatizo ya mikopo ya Elimu ya Juu. Kinachotushangaza ni kwamba ripoti ya Tume hiyo haijawekwa hadharani na bado matatizo ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu yako pale pale. Wanafunzi wengi hawapati fedha kwa wakati hali inayoleta adha kubwa kwa wanafunzi kwani wengi wao wanatoka kwenye familia duni. Kwa mfano wanafunzi wanaosoma kozi ya ualimu katika Chuo Kikuu cha St. Joseph, hawajalipwa fedha zao za mikopo tangu mwezi Machi 2015 jambo linalowafanya waishi maisha ya dhiki na hivyo kushindwa kusoma. Kinachoshangaza ni kwamba wenzao wa Uhandisi wamelipwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza ni kwa nini inatoa mikopo kwa ubaguzi? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa nini Chuo cha St. Joseph kiliwafukuza wanafunzi hao waliokosa mikopo na kuvumilia zaidi ya siku 50, na ni nini hatima ya wanafunzi hao?

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu urejeshwaji wa mikopo ya elimu ya juu, imebainika kwamba urejeshaji ni mdogo sana kwa kuwa hakuna mfumo mzuri unaoratibu zoezi la ukopeshaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu. Kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa

ikishauri kazi hiyo kufanywa na mabenki yetu lakini mpaka sasa ushauri huo haujatekelezwa. Tunaitaka Serikali kulieleza bunge hili kama Bodi ya Mikopo ina wataalamu wa mikopo kwa ajili ya kazi hiyo. Ili kuyapatia ufumbuzi matatizo ya mikopo ya elimu ya juu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka vilevile Serikali kutoa ripoti ya tume ya Profesa Maboko ambayo ilipewa jukumu la kutafuta vyanzo vya matatizo na kupendekeza namna ya kukabiliana na matatizo ya mikopo ya elimu ya juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuwa tumeshauri mara kadhaa kuhusu matatizo ya mfumo wa mikopo ya elimu ya Juu na kupuuzwa. Serikali Mpya ya UKAWA italipa kipaumbele suala la mikopo ya elimu ya juu kwa kutambua kwamba mikopo ni haki ya wanafunzi na bila mikopo hiyo hawataweza i kusoma kwa utulivu na kuzifikia ndoto zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kama Serikali haitaki ushauri wa UKAWA basi basi walau ijifunze kutoka nchi jirani ya Rwanda inavyofanya kuhusu mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya juu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza yafuatayo:

- i. Ni kwanini haitoi fedha ya mikopo hadi wanafunzi wagome na kuandamana?
- ii. Ni wapi fedha hizo zinakwenda hasa ukizingatia 100% ni za ndani?
- iii. Ni kwa nini ndani ya masaa 12 tu ya mgomo wa UDSM 19/5/2015 fedha zikatoka?

Au ni sera ya CCM kuwajengea wanafunzi tabia ya kupata haki zao kwa migomo na baadaye kusema ni UKAWA wanachochea migomo vyuoni?

**9. UWEKEZAJI KATIKA ELIMU NA MPANGO MATOKEO MAKUBWA SASA (BRN).**

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu mbalimbali za ripoti ya utekelezaji wa BRN ya Presidential Delivery Bureau na Jarida la HakiElimu la hali ya utekelezaji wa BRN zinaonesha kuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa BRN ulikuwa na changamoto nyingi za kiutekelezaji na mambo mengi yanayohusiana na fedha hayakutekelezwa. BRN ya Elimu ilibaninisha wazi kutoa ruzuku ya asilimia 100 yaani shilingi 10,000/= kwa kila mwanafunzi shule za msingi na shilingi 25,000/= kwa shule za sekondari lakini utekelezaji umekuwa kwa asilimia 42 tu kwa msingi na asilimia 48 tu kwa sekondari.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa miundombinu haukutekelezeka pia ambapo kati ya shule 792 zilizopangwa kufanyiwa ukarabati hadi ifikapo mwezi March 2014, ni shule 56 tu zimekarabatiwa. Lengo la utoaji mafunzo ya usimamizi kwa walimu wakuu halikutekelezwa ipasavyo ambapo kati ya walimu 19,035 waliotarajiwa kupata mafunzo ifikapo September 2013, ni walimu 3,469 tu sawa na asilimia 18 ndio wameshapatiwa mafunzo.

**Mheshimiwa Spika,** dhamira ya BRN kutatua mgogoro wa walimu na kufanya walimu wafundishe ipasanyo ilikuwa ni nzuri hasa kwa kutoa motisha kwa walimu na kulipa madeni ya walimu. Wakati BRN inaanza asilimia 53 ya walimu walikuwa hawapo darasani yaani hawafundishi. Utafiti wa Shirika la Twaweza kwenye kijarida namba 13 cha mwaka 2014 unaonesha kuwa hivi sasa ni asilimia 34 tu ya walimu ndio wanaingia na kufundisha muda wote wa kipindi na idadi iliyobaki ama wanaingia kwa muda mfupi tu au hawaingii kabisa. Kwa takwimu hizi za utekelezaji, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inauliza: ni mambo gani yaliyofanya sekta ya elimu hadi kuipatia sekta hiyo alama 81 katika utekelezaji ilihali katika malengo yote ya BRN ya elimu hakuna hata lengo moja ambalo limetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 20?

**Mheshimiwa Spika,** ni wazi Serikali haijawekeza vya kutosha katika elimu. Hii inadhahirishwa na bajeti zetu. Kwa mfano mwaka 2014/15 Kenya ilitenga sh Bilioni 294.6 sawa na

asilimia 27.3% ya bajeti yake kwenye elimu huku Tanzania ikitenga shilingi 3.46 bilioni sawa na asilimia 17 ya bajeti kuu kwenye elimu. Lakini ieleweke hata hizo zilizotengwa ni asilimia kidogo zilizokwenda kwa wastani wa 50 au chini hadi Machi 2015. Lakini takwimu zinaonesha kuwa katika nchi za Afrika Mashariki Kenya imetumia 7.8% ya GDP katika elimu huku Tanzania ikitoa 1.49 % ya GDP, Uganda 5.8% na Rwanda 4.8%. Haiwezekani usiwekeze halafu utegeme mavuno mazuri. Ni sawa na mimea inahitaji kuwekwa mbolea na kupaliliwa na hata kumwagiliwa. Ni jambo linalosikitisha kuona watoto wakikaa darasani kwa miaka saba na kutoka bila chochote. Watoto hawapati chakula shuleni jambo linalowafanya watoroke shule Jirani zetu Kenya toka 2013 walianza program ya kula shuleni ambayo kimsingi ni motisha hasa kwa watoto wa familia maskini.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo linalochekesha ni pale Serikali hii ya CCM inapotamba kuwa elimu imefanikiwa kwa 81% katika mpango wa matokeo makubwa sasa. Kwa mtu yeyote mwenye akili timamu atajuliza ni uwekezaji gani umefanyika hadi tukapata matokeo haya. Je walimu ambao ndio watendaji wakuu wamefanyika nini? Je maslahi yao, motisha na mazingira yao yameboreshwa? Ni jambo la kusikitisha kuona uwekezaji ukipungua lakini matokeo yakiwa mazuri zaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji; "kuna miujiza gani kama si mbinu chafu na za ujanja ujanja kama tulivyosema mwaka juzi? Ukweli kilichofanyika ni kubadili alama na madaraja jambo ambalo kimsingi ni mbinu chafu na hauoneshi uhalisia wa uwezo wa mtoto. Ieleweke kuwa Tanzania sio kisiwa na kwamba ukosefu wa ajira unachangiwa na ubovu wa wahitimu wetu kutokana na mfumo wetu wa elimu na hasa mfumo mpya wa madaraja na alama.

**Mheshimiwa Spika** Ni lazima tuelewe kila mtoto wa kitanzania anahitaji elimu bora kwani elimu ni kwa ajili ya kujikomboa na kujibadili (liberation and transformation). Ni vibaya sana kuwajaza watoto wa maskini kwenye shule za viwango vya chini. Kama Mwalimu Nyerere alivyosema mwaka mmoja kabla ya kifo chake (5/3 1998) akiwa Open University "*Not all of us will have the same concept of community, but all of us have a need to belong ..... nobody is asking us to love others more than we love ourselves but those of us who have been lucky enough to receive a good education have a duty also to help to improve the well being of the community to which we belong, is part of loving ourselves*"

**Mheshimiwa Spika**, ni kwa kiasi gani wasomi wa nchi hii na wenye madaraka mnapenda watoto wa watanzania kupata elimu bora? Au sisi wenyewe watoto wetu wako nje ya nchi? Je tunaboreshaje jamii/elimu yetu kwa kuwa kufanya hivyo ni sehemu ya kupendana? Tumeshindwa kwa kuwa tunashuhudia wasomi wetu waliopata elimu bora wamekuwa chanzo cha kuharibu elimu yetu kwa kuruhusu akili ndogo kutawala akili kubwa. Haiwezekani Profesa aliyepewa kuongoza sekta ya elimu ashindwe kutoa ushauri kuhusu uboreshwaji wa elimu. Inawezekanaje maprofesa wasajili/ watoe ithibati kwa vyuo vikuu vyenye maabara yenye kiwango cha shule za kata? Mnategemea wahitimu wa vyuo hivi waajiriwe wapi?

## **10. UCHAMBUZI WA BAJETI**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na bajeti ya sekta nzima kuendelea kuongezeka kutoka Trilioni 3.46 mwaka 2014/15 hadi trilioni 3.88, sawa na takribani asilimia 10 tu ya fedha iliyopangwa mwaka jana, si ongezeko linaloweza kuleta mabadiliko yanayoonekana katika sekta ya elimu. Tunasema hivi kwa kuzingatia kuwa thamani ya shilingi imeshuka na mfumuko wa bei umeongezeka. Inawezekana ongezeko hili ni matokeo ya urekebishaji mfumuko wa bei badala ya ongezeko halisi katika matumizi.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo uchambuzi unaonesha kuwa bado kiwango cha fedha za bajeti ya sekta kinachopangwa ni asilimia kati ya 15 – 17 cha bajeti nzima ya serikali.

Tanzania hatujaweza hata kufikia kiwango kilichokubaliwa cha azimio la Darkar Senegal chini ya EFA, cha kuwekeza hadi walau asilimia 20 ya bajeti ya taifa katika elimu. Wakati tunaamini kuwa kiwango cha asilimia 17 si kibaya, lakini ni muhimu kujua kuwa bado Tanzania inawekeza asilimia kati ya 10-11 tu ya bajeti ya sekta ya elimu kwenye miradi ya maendeleo ukilinganisha na majirani zetu Kenya, Rwanda, na Uganda ambao wamefikia walau asilimia 20 -25.

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi sekta ya elimu imeendelea kupewa kipaumbele kwa maana ya kuwa sekta inayopokea fungu kubwa zaidi la bajeti ya serikali. Wakati ikipangiwa trilion 3.46 mwaka jana sekta ya miundombinu ambayo ilifuatia ilipokea takribani trilion 2.3 wakati mwaka huu sekta ya elimu imepangiwa trillion 3.88 wizara inayofuatia ambayo ni miundombinu imeshuka zaidi hadi takribani Trilion 1.9. Hata hivyo bado kuna mapungufu makubwa ambayo inabidi yafanyiwe kazi;

- Kiwango cha fedha zinazokwenda kwenye matumizi ya kawaida bado ni kubwa sana kuliko kinachokwenda kwenye matumizi ya maendeleo ambayo ni muhimu zaidi. Mathalani katika makadirio ya Trilioni 3.88 yanayopendekezwa mwaka huu wa fedha kwenye sekta ya elimu, 84% zimeelekezwa katika matumizi ya kawaida huku asilimia 16 pekee (bilioni 604) ndizo zinaombwa kwa ajili ya maendeleo. Pia kati ya Tsh bil 604 zilizopangwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo asilimia 50 ya fedha hizi zimepangwa kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na hivyo fedha zinazobaki kwa ajili ya miradi halisi ya maendeleo ni ndogo sana kulingana na changamoto zinazokabili sekta ya elimu hasa elimu ya msingi na sekondari. Tunatoa rai kwa Wizara kuongeza fedha zaidi kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali za mitaa.
- Tunatambua, Wizara ya Elimu imegatua madaraka na sasa hivi shughuli nyingi za elimu ya msingi na sekondari zinatekelezwa na serikali za mitaa na Wizara ya Elimu imebaki na jukumu la ushauri, utengenezaji wa sera na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera. Cha kushangaza katika makadirio ya bajeti ya maendeleo ya sekta ya Elimu, kati ya Sh billion 604 zilizopangwa, sh bilioni 478.7(asilimia 79) zimepangwa wizara ya ya Elimu na Tsh bilioni 126 tu ndio zimepangwa serikali za mitaa. Swali la kuuliza inakuwaje tunapanga fedha nyingi kwenye kazi za ushauri, utungaji wa sera na ufuatiliaji na kupanga fedha kiasi kidogo kwenye serikali za mitaa ambazo ndio zinatekeleza shughuli nyingi za maendeleo? Unawezaje kutatua changamoto za miundombinu elimu ya msingi na sekondari kwa kupanga shilingi bilioni 126 tu.
- Changamoto nyingine ambayo imekuwapo na imeendelea kujitokeza katika bajeti ya mwaka huu, ni utegemezi wa bajeti ya maendeleo kwa wahisani. Uchambuzi unaonesha bado takribani asilimia 50% ya bajeti ya maendeleo sekta ya elimu inatarajiwa kutoka kwa wahisani.
- Changamoto ya mwisho ambayo ni lazima tuiseme, ni kutokuwepo kwa uwiano kati ya bajeti inayopangwa, fedha ambazo hutolewa na hazina au wahisani na kiwango ambacho hasa kinatumika katika utekelezaji wa mipango na bajeti. Kwa miaka mingi wizara, halmashauri na taasisi zimekuwa zikitekeleza bajeti pungufu kutokana na kutopatiwa kiwango sahihi kilichopangwa katika bajeti, na hata kinachotolewa hakitolewi kwa wakati. Hivyo wakati mijadala ikiendelea juu ya elimu ni muhimu serikali ifikirie upya suala hili na ikiwezekana kupunguza kiwango cha bajeti kama utekelezaji utaonekana kuwa na shida. Uchambuzi wa shirika la HakiElimu unaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, matumizi halisi ya bajeti ya maendeleo ya wizara imekuwa asilimia kati ya 50-65 tu ya bajeti iliyopangwa. Na hii ndio imekuwa sababu kuu kwa miradi mingi kudorora na kusababisha sekta ya elimu kubaki na changamoto nyingi na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

## **11. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, hakuna nchi yoyote iliyoendelea hapa duniani bila kuwekeza kwenye elimu. Malaysia inajivunia maendeleo yake kwa kuwa iliwekeza kwa vitendo katika elimu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaarifu wananchi wote kwamba, kwa kuwa Serikali hii ya CCM haina nia ya dharti ya kuboresha elimu yetu kutokana na kushindwa hata kutekeleza ilani yake kuhusu elimu, Serikali ya Mpya ya UKAWA itakayoingia madarakni baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2015 itayashughulikia matatizo yafuatayo katika sekta ya elimu na kuyatafutia ufumbuzi wa kudumu:

- i. Kutokuwa na malengo yakinishi ya kielimu ya jumla na katika ngazi mbalimbali.
- ii. Uhafifu na uduni wa elimu inayotolewa katika ngazi mbalimbali, na hasa katika ngazi ya msingi na sekondari yanayodhihirishwa
- iii. Kuongezeka kwa idadi ya watu wasiojua 3K (kusoma, kuandika na kuhesabu)
- iv. Uduni wa shule za sekondari: ni asilimia nne tu ya shule za sekondari nchini ndizo zinazokidhi vigezo vya chini kabisa vya hadhi ya sekondari-hizi takribani shule 160 tu kati ya shule za sekondari zaidi ya 4000 zilizopo nchini.
- v. Uduni wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi mbalimbali za elimu.
- vi. Walimu wasio na motisha na kada ya ualimu kutelekezwa kwa ujumla.
- vii. Kutokuwa na uwiano kati ya walichojifunza wahitimu na kinachoendelea katika ulimwengu wa kazi, kutokana na udhaifu wa mitaala na ufundishaji. Matokeo yake: Wahitimu wetu walio wengi hawaajiriki wala hawawezi kujijiri.
- viii. Kutokuwa na mfumo thabiti kuhusu ugharamiaji wa elimu, na hasa elimu ya juu
- ix. Usimamizi dhaifu wa elimu inayotolewa na taasisi zinazomilikiwa na watu na mashirika yasiyo ya kiserikali au ya umma. Matokeo yake: tuna mifumo zaidi ya mmoja katika nchi moja
- x. Kutokupewa kipau umbele kwa elimu ya awali (miaka 3-6) ambayo ndiyo msingi wa kujifunza katika ngazi za baadaye
- xi. Mkanganyiko wa lugha ya elimu (kufundishia na kujifunzia).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, na wataanzania wote wanaopenda kuona taifa letu likisonga mbele kwa kasi ya kumwondoa adui ujinga jambo lililoshindwa kutekelezwa na Serikali ya CCM, ni UKAWA tu wanaoweza kubadili hali hii kwa kuboresha mfumo wa elimu na kuwekeza kwa vitendo katika elimu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa nawatakiwa wabunge wote kila la heri wanapoelekea uraiani baada ya bunge hili kuvunjwa, lakini pia nawatakiwa ushindi wa kishindo wagombea wote wa udiwani, ubunge na urais watakaopendekezwa na UKAWA kugombea nafasi hizo, ili Serikali ya awamu ya tano itokane na UKAWA.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Susan Anselm Jerome Lyimo (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI NA WAZIRI KIVULI WA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI**

Tarehe 1 Juni, 2015

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo. Namuita mchangiaji wetu wa kwanza Mheshimiwa Abia Nyabakari-, atafuatiwa na Dokta Grace Puja na Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema ajiandae. Uchangiaji ni dakika kumi kumi. -

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nataka niseme kitu kimoja, wengine wametangaza nia zao kwenye viwanja vikubwa, wengine kwenye kumbi kubwa, wengine kwenye mikutano mikubwa wakiangaliwa na watu, kushangiliwa na kusikilizwa lakini na mimi pia leo natangaza nia kwamba nakwenda katika Wilaya ya Buhigwe. Kabla sijaendelea, lazima leo nianze na utetezi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tusikilizane!

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Buhigwe, ni watu ambao hatuna ardhi ya kutosha na maeneo yetu yamekaa kibiashara. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kitu cha kwanza itulettee VETA katika Wilaya ya Buhigwe. Katika mikakati yote ya Serikali mwaka ujao tunataka kusikiliza mkijenga chuo cha VETA katika Wilaya ya Buhigwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, ndugu zangu ni naomba niwaambie, kila siku ni kulaumiwa ndani ya Bunge hili Tukufu, lakini wanaolaumu, hawatuonyeshi kwamba wamefanya kitu gani kinachoweza kuwapeleka mbele. Kila siku ni kusema, umaskini uliokithiri kwa Watanzania wengi umesababishwa na kuwa na viongozi wabovu ndani ya CCM. Vilevile wanasema, CCM imefanya Watanzania wakose fursa za ajira na kuendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Niwaambie ndugu zangu Watanzania, kazi ya shetani ni kuchochea mioyo ya watu ili waweze kuwa na hasira. Ni kuharibu, ni kubomoa na kisha kuangamiza. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie majini hao.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Leo wao hawawezi kujifanya ni Watakatifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie Watanzania, sisi wote tulioko ndani ya Bunge hili tulipewa fedha na Serikali kwa ajili ya kuwalipa madereva, tunapewa posho za madereva. Sasa nataka niulize upande wa pili, ni nani anayeweza kusema kwamba sisi tutatenda haki mkiwa Serikalini, madereva wenu mmewapa posho zote sawasawa, mnataka nizataje, sitaki. Mseme kwamba mnawapa posho nje ya mshahara. Watu wanaendesha magari wenyewe kutoka Moshi, Rukwa, Kigoma. *(Kicheko)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WABUNGE FULANI:** Hakuna taarifa, kaa chini wewe.

**MWENYEKITI:** Tuendeleo, hakuna taarifa.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Muda wangu ulindwe.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni elimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa, naomba ukae chini.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja siyo madereva, ni elimu.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini. Msikilize amalize hoja yake, mbona unanyanyuka harakaharaka, ya nini? Endelea Mheshimiwa Nyabakari.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taifa letu ni changa kiuchumi...

**MBUNGE FULANI:** Miaka 50 ni changa?

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Tumeingiza mambo mengi ya tegemezi, wote tunafahamu.

**MBUNGE FULANI:** Miaka 50 ni changa?

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Badala ya kutafakari juu ya Watanzania ambao hawajawa na fikra halisi za kujitambua katika kujitegemea na kuinua uchumi wetu wa nchi, matokeo yake yamekuwa ni kuandamanisha watu usiku na mchana kwa ajili ya fikira zetu za kuwa na dhamira ya kuingia Ikulu. Ikulu haiwezi kuingiwa bila kuweka mikakati madhubuti, haiwezekaniki. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hawaendi hao.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Kila siku ni uchokozi, yaani tuwaunge mkono tu ninyi muingie Ikulu, ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaeleze, katika karne nyingi, kulikuwa na watawala, akina *Napoleon, Churchill, Kennedy* pamoja na viongozi wengine, hata akina *Hitler*. Hawa watu walipoingia madarakani walitamani kuitawala dunia nzima, wakaona kama wao wanaweza kuleta mabadiliko katika nchi. Ndugu zangu naombeni niwambie...

**MBUNGE FULANI:** Waambie.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Hata wao wenyewe walishindwa kutawala magonjwa, vifo, njaa, vita na migogoro na matokeo yake walijiua. Ninyi pia nawaambia...

**MBUNGE FULANI:** Watajiua.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mnayoyasema kama mnavyowadanganya Watanzania, watawanyofoa macho na kuwala mishikaki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye mada nyingine, naomba sasa niweze kuchangia katika Wizara hii. Naipongeza Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika ujenzi wa chuo chetu cha *UDOM*. Wamefanya kazi nzuri lakini tunaomba wazidi kubarikiwa, wasituchoke, waendeleo kutusaidia ili chuo chetu kiweze kumalizika. *(Makofi)*



**MBUNGE FULANI:** Mtanyofolewa macho.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawaelewi, bajeti ya Serikali yetu ni finyu, nini kinasababisha bajeti yetu iwe finyu? Tangu vyama hivi vilipoanza, vijana wanazidi kuzorota, hawataki kufanya kazi, matokeo yake uchumi wake unazorota, sasa ndiyo wanaanza kusema Serikali itenge Mfuko wa Vijana, vijana waweze kujitegemea. Haiwezekani watu wenye nguvu, watu vijijini wakalime, waumie, wafanyabiashara wafanye, eti watengewe watu wenye nguvu Mfuko wa kuendesha biashara zao! Huu ni unyonyaji ndugu zangu na hawa ni watu wasiowatakia Watanzania mema, haiwezekani! *(Makofi)*

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kitu kimoja, bajeti ya Serikali yetu...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Hamna taarifa.

**MWENYEKITI:** Hamna taarifa, kaa kwanza, subiri kwanza, endelea Mheshimiwa Nyabakari.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo, chuo cha UDOM walitengewe shilingi bilioni 27 kwa ajili ya maendeleo lakini cha ajabu bajeti hiyo imeshuka mpaka shilingi bilioni mbili, kulikoni? Chuo hiki wanachosema kwamba kitakuwa mfano katika Afrika Mashariki na Afrika ya Kati kisimalizike kwa kutengewa fedha hiyo, kitaisha baada ya miaka 50, hiki kitu hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni fedha za uendeshaji wa chuo hicho, mwaka 2007 na 2008 walitenga shilingi bilioni 1.07 lakini cha ajabu wamepewa shilingi milioni 62.99, chuo hiki kitaendeshwaje? Maji tu wanalipia shilingi milioni 100, umeme wanalipia shilingi milioni 62, kwa nini Serikali isianganilie hili jicho ambalo ni mboni ya nchi yetu, wakaongeza fedha ili hiki chuo kimalizike. Ndugu zangu huku ni kuchezea akili ya Watanzania na kuchezea fedha za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima wataalam na Serikali ikae chini iweze kutumaliza chuo hiki, hakiwezi kutuletea mambo ya *maintenance* mara hii, ni kitu ambacho hakiwezekani. Nendeni mkimalizie hii ndiyo heshima ya nchi yetu, wasomi watoke pale, shilingi bilioni 2 kutoka shilingi bilioni 27, hiki kitu haikiwezekani! Chuo hiki hakiwezi kuendesha kwa utaratibu huu, haki kwa wakati ndiyo jambo la kweli. Mnasubiri yawe magofu ndiyo muanze kukarabati eti mnamaliza chuo, muwajibike kuipa Serikali yetu heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie ndugu zangu, kama hamuwezi kumaliza chuo hiki, huku ni kuchezea akili ya Watanzania na kuharibu fedha za zao. Fikirieni malengo yaliyotarajiwa mkamalize chuo hicho kwa wakati. Mnajua kabisa, vijana wengi nchi hii hawafanyi kazi na watu wanazidi kuwahimiza kwenye maandamano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba ndugu zangu, hata kama mnataka kuchukua dola, semeni yale mtakayokwenda kuyafanya, siyo kuchochea hasira. Mungu hapendezwi na jambo hilo. Kila jambo lina wakati wake, msilazimishe kwenda Ikulu, Watanzania ipeni CCM kura kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyabakari, sasa namuita Dokta Grace Puja.

**MHE. DKT. GRACE K. PUJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa hii kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na hotuba zingine ambazo zinafuatana na hotuba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii na kunipa afya na uhai kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kutoa elimu kwa ufanisi mkubwa kwa miaka 51 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine ambao tulisoma kati ya elimu ya mkoloni na ya Serikali ya uhuru tunajua tofauti lakini wale wengine ambao hawajui elimu ya mkoloni ilikuwaje wanasema hakuna maendeleo. Bila shaka mnajua takwimu, sina haja ya kuzitoa, lakini sisi wenye ndiyo takwimu, takwimu iko hapa, sisi wenyewe. Sidhani kama Bunge la kwanza la Tanganyika lilikuwa na Wabunge wasomi kama sisi tulioko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia mambo machache na la kwanza ni kuhusu elimu ya awali. Katika Sera ya Elimu, elimu ya awali imewekwa kwamba ni sehemu ya elimu ya msingi kwa watoto wa Kitanzania. Hata hivyo, kunahitajika nguvu ya ziada kuhakikisha kwamba elimu hii inatolewa kwa ufanisi badala ya kuachia badhi ya taasisi kwa mfano, vijiji, shule zilizoko vijijini unakuta elimu ya awali haitolewi kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba Serikali iweke mkakati maalum kuhakikisha kwamba elimu ya awali inatolewa kama ilivyoainishwa katika Sera ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kugusia suala ambalo tayari limezungumziwa juu ya mafunzo ya ualimu lakini nadhani Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii amelizungumzia sana, kwamba walimu wanatakiwa wapate elimu ya vitendo kwa muda gani. Kwa hiyo, sina haja ya kurudia nadhani limeshaleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia juu ya utambuzi wa wataalamu wa VETA. Najua kwamba katika elimu ya VETA, wanafunzi wale wanaohitimu wanapata vyeti lakini kufuatia mazungumzo yangu na wataalam wa eneo hilo wanasema kwamba ukiwa na cheti unapewa mshahara mdogo kwa sababu inaonekana ile elimu haithaminiwi kama ukipata degree au shahada. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, pengine kuna haja ya kutayarisha utaratibu maalumu kutambua vile vyeti vya VETA na pengine kuweka utaratibu ambao ni endelevu ili mtu akishapata cheti au *certificate* aweze pia kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani inawezekana pia kuwa na *advance certificate* katika mfumo uleule ili kwamba asiwe na ulazima wa kwenda kupata degree kwanza ndiyo aweze kupata mshahara mzuri au aweze kutambuliwa. Kwa sababu wale watu wenye vyeti ni wataalam ambao wana kitu kinaitwa *hands on experience*, wale ni watu ambao wanafanya kazi za mikono, kama ni bomba, anajua namna ya kulishughulikia, amefundishwa namna ya kufanya kazi ile, siyo amesoma tu vitabu kwamba huwa wanafanyaje ukitaka kufanya jambo fulani. Kwa hiyo, kuna haja ya kutambua utalam huu na kuuwekea mkakati ambao unawatia ari wale wanaojiendeleza katika fani hiyo nao waweze kutambuliwa na maslahi yao yaweze kushughulikiwa.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine unahusu gharama za elimu ya juu. Kwa hapa Tanzania tumezoea sana suala la mikopo, mimi nimesoma hapa Tanzania na nje na nimeona jinsi ambavyo wanafunzi wa nchi zingine kama Marekani na Canada, wanakwepa sana mikopo. Mtu anaogopa kwenda kupata mkopo kwa sababu akikopa, kwa maisha yake yote yeye atakuwa analipa mkopo tu lakini sisi kwa sababu hatuna namna nyingine, tunaona kwamba ndiyo mkombozi wetu, lakini tunajenga taifa ambalo litakuwa na wasomi ambao watalipa mikopo kwa maisha yao yote. Kwa hiyo, napenda hilo jambo litambuliwe kwa sababu kutoa mikopo siyo jambo pekee la kugharamia elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wanaotaka elimu ya bure, napenda kusema kwamba hakuna elimu ya bure. Elimu inapokuwa hailipiwi, wewe usipolipa, kuna mtu mwingine analipa. Sisi tuliosoma katika Serikali ya Nyerere, ni kwamba tunaposamehewa ada Serikali inalipa badala yetu lakini hakuna kusema kwamba elimu ya bure ipo, hamna elimu ya bure. (Makofi)

Kwa hiyo, kuhusiana na mikopo, badala ya mikopo kuna namna nyingine ya kufadhili elimu. Kuna kitu kinaitwa *work study* kwa Kiswahili maana yake ni kwamba, wanafunzi wanakuwa wanashindana, mwanafunzi anapopata *work study* maana yake anaruhusiwa kufanya kazi halafu ule mshahara anaopata unalipia baadhi ya malipo yake kwa mfano anaweza kulipia ada, kununua vitabu lakini ni mpango ambao unashughulikiwa na Serikali. Kwa hiyo, wanafunzi kama hao, wanaruhusiwa kupata msaada huu kutokana na kwamba wanasomea *courses* ambazo zinahitajika katika fani fulani, zinahitajiwa na Serikali au mashirika fulani, kwa hiyo, kuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna nyingine inaitwa *bursaries*. Wenzetu waliosoma kabla yetu walipata kitu kinaitwa *bursaries*, siyo mikopo, walipewa msaada yaani walifadhiliwa moja kwa moja. Mtindo huu unatumika katika nchi nyingi duniani kwa maana kwamba, wale ambao wanasoma katika fani ambazo ni nyeti au zinahitajika, wanapewa *bursaries* lakini kwa kushindana, wale wanaofaulu ndiyo wanapata hizo *bursaries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtindo mwingine ni kwamba mzazi anaweka akiba, tangu mtoto anapozaliwa unaweka akiba, *education fund* kwa ajili ya *family*, duniani wapo wazazi wanaweka akiba hiyo. Kwa mfano, Botswana nasikia wanatumia sana mtindo huu, kila mtoto anapozaliwa, mzazi wake anahamasika kuweka akiba kwa ajili ya elimu ya mtoto huyo. Badala ya kutegemea tu kwamba Serikali italipia kila kitu, wazazi tuna wajibu wa kuwasomesha watoto wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo itolewe na mabanki. Serikali inasema haishughuliki na biashara lakini naona inajihusisha na biashara ya mikopo. Hiyo mikopo inatakiwa itolewe na mabanki kwa sababu ukikopa lazima ulipe, mkopo siyo zawadi, mkopo siyo msaada ukikopa unatakiwa ulipe tena kwa *interest* yaani kwa faida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kupendekeza kitu ambacho kinahusiana na kazi ya muda. Sisi hapa Tanzania kuna wengine wamesema tunafanya kazi kwa mazoea kwa maana kwamba ukishaajiriwa unapata mshahara kila mwisho wa mwezi, lakini ni nani anahakikisha kwamba kweli umefanya hiyo kazi uliyotakiwa kufanya? Nimeona nchi nyingine wanavyofanya, kunakuwa na *supervision*, sisi kwetu hapa kitu ambacho hakipo ni *supervision*. Tuki-*introduce* au tukileta mtindo wa kufanya kazi *full time*, kazi ya kudumu na kazi ya muda tutakuwa na nafasi ya wanafunzi wetu, kwa mfano, wanaosoma vyo vikiu kupata kazi ya muda.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nashangaa kwamba sisi Tanzania unakaa miaka yote tangu umezaliwa unamaliza chuo kikuu hujawahi kufanya kazi, utakapomaliza chuo kikuu ndipo unaanza kutafuta kazi sasa. Wenzetu wa nchi zilizoendelea, ukishafika miaka 16 unaruhusiwa kufanya kazi ya muda, labda masaa mawili, masaa manne kwa wiki ili uanze kuzoea kupata hela yako na kuitunza na kujua namna ya kuthamini hela. Hapa wanafunzi wetu wakipata mikopo unashtukia wengine wanamaliza baada ya wiki mbili kwa sababu hawajazoea kushika hela. Kwa hiyo, naomba Serikali ifikirie uwezekano wa kuleta mfumo wa kufanya kazi kwa muda na kufanya kazi kwa muda wa kudumu kwa sababu kazi nyingine siyo lazima uajiri mtu kwa saa nane, mtu anaweza akafanya kazi kwa saa mbili au saa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwalimu Dokta Grace Puja kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo wajiandae.

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siridhiki kabisa jinsi ambavyo walimu wa Halmashauri ya Moshi wanavyohudumiwa. Niliwahi kuuliza swali hapa kuhusu mgogoro uliokuwepo kati ya walimu wa Halmashauri ya Moshi na Maafisa Elimu. Maafisa Elimu hawa wanawatesa walimu, wanawanyima haki zao, mishahara, hela za likizo, hela za uhamisho, matibabu, gharama za mazishi na masomo zote hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati ule Serikali ikanijibu kwamba huo mgogoro uliokuwepo kati ya Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Moshi na walimu ulidumu kati ya mwaka 2012 na ulimalizika Februari, 2015. Unaweza ukaona hiki kipindi ni kikubwa sana. Majibu niliyopata ni kwamba kuhusu malimbikizo ya mishahara, yaani watu wananyimwa mishahara yao, wanahangaishwa, stahiki ambazo zilipaswa zilipwe katika kipindi hicho, ni shilingi milioni 676.7; unaweza ukaona ni fedha nyingi sana na zilihusu walimu 579.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najjuliza Serikali iko wapi? Walimu wanateseka, walimu hawalipwi mishahara yao wakati mwafaka mpaka wanakuwa na malimbikizo. Kama kufikia Februari, 2015 ndiyo mlilipa hizi shilingi milioni 676.7, je, nina hakika gani kwamba kuanzia Machi, Aprili, Mei mpaka Juni tatizo hilo halipo tena? Kwa hiyo, nitaomba wakati Waziri anajumuisha anihakikishie kwamba walimu wangu wa Halmashauri ya Moshi shida hiyo ya mishahara haipo tena, malimbikizo hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi hela za uhamisho. Kuanzia 2012 mpaka Februari 2015 walimu hao walikuwa wanadai shilingi milioni 646.8. Mtu anahamishwa fedha zake halipwi, mtu anakwenda likizo fedha halipwi, ni mgonjwa anahitaji matibabu fedha halipwi, gharama za mazishi na masomo hazitolewi. Sasa naomba anihakikishie kwamba kuanzia Machi, Aprili, Mei mpaka Juni, ugonjwa huu uliopo kwenye Halmashauri ya Moshi unaendelea au umemalizika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili ambalo tumeshasema hapa na Wabunge wengi wamechangia, kuhusu kuanzisha *Teachers Service Commission*. Nadhani wote tumekubaliana kwamba lazima tuwe na chombo kimoja kitakachounganisha walimu kuhusu mishahara na mambo yao mengine yote yaani wawe na dawati moja. Nakumbuka na Muswada ulishapitishwa, sasa tulitegemea ikifika Julai hiki chombo cha *Teachers Service Commission* kiwe kimeanza ili walimu wasiendeleo kuteseka na kuhangaika. Kama hatutakipitisha sasa hivi kikaanza Julai, Bunge lijalo kila mtu anajua Novemba kuna mambo

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

fulani ambayo yatazuia hiki kitu kisizungumzwe. Kwa hiyo, naomba Waziri atuhakikishie kwamba Muswada wa *Teachers Service Commission* utasomwa ili iweze kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulizungumza kuhusu wale watu waliowatesa wale walimu wa Halmashauri ya Moshi. Walikuwa wanawahangaisha, walimu wanahangaika huko, wanafanya kazi kwa bidii, nikadai kufahamishwa ni akina nani, Serikali mkasema mliwahamisha; kuhamisha siyo *issue*, nataka kujua ni akina nani tena kwa majina. Leo nitatoa shilingi kama hutataja hao maafisa waliotesa walimu kwa miaka mitatu kule Halmashauri ya Moshi. Kwa hiyo, namwomba Waziri tusije tukaelewana vibaya wakati yeye ni rafiki yangu. Tuwataje, hao ni maharamia sawasawa na maharamia wengine. Mtu anapewa kazi ya kuwahudumia watu halafu hatoi huduma inayotakiwa hasa kwa walimu wetu. Kwa hiyo, majina nayataka, wajulikane ni akina nani hao watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kinatokana na hizi shule zinapopata matatizo. Mimi katika Jimbo la Vunjo shule yangu iliungua, Shule ya Muungano lakini ilibidi nitoe kwenye Mfuko wangu wa Mbunge shilingi milioni 21 na Ndugu Mengi akasaidia, mbona sioni Wizara imetenda shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho akaja Katibu Mkuu wa CCM na ninyi CCM mnaanza kushiriki katika uwongo, sikilizeni maneno aliyoyasema. Katibu Mkuu kwenye Jimbo langu, badala ya kwenda hata kwenye shule kuwapa pole wanafunzi na walimu, anakwenda kufanya mkutano wa hadharani anasema kila Jimbo lina Mfuko wa Mbunge ambapo hupewa shilingi milioni 25 kwa miezi mitatu, kwa mwaka shilingi milioni 100, kwa miaka minne ni shilingi milioni 400, hamuwezi kuwa na kiongozi ambaye yeye ni Mbunge na wakati huohuo ndiye Mwenyekiti wa Mfuko huo, je, si atajipendelea?

Mimi naomba niulize Serikali na Waziri ajibu, ni kweli Jimbo la Vunjo tumepata shilingi milioni 400 kama alivyosema Kinana au mlikuwa mnanipakazia ili walimu wanichukie nionekane mimi ni mwizi, ninakula fedha za walimu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaendelea kusema, fedha hizo ni kwa ajili ya kusaidia vikundi vya akina mama, vijana, maabara mashuleni na vifaa vya mahospitalini. Je, kuna ambaye amewahi kumuuliza Mbunge wenu kuwa fedha hizo zinakwenda wapi? Huo Mfuko una kamati na CCM iko ndani ya Mfuko huo, Mkuu wa Mkoa alikuwepo, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi, mbona hawakumpa taarifa sawasawa? Au ndiyo njama za kutaka kunitoa Vunjo kwa ujanja, mnafikiri walimu watakubali na mimi nahangaikia shida zao? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaendelea kusema, Mbunge hawezi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Fedha za Jimbo. Sasa kama mimi siwezi kuwa Mwenyekiti na hao Wabunge wa CCM nani anakuwa Mwenyekiti wa hizo Kamati? Kwa nini mnakuja kwangu mnasema maneno ya uwongo ninyi CCM? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema, ukishakuwa na Mbunge ambaye yeye ndiye Mwenyekiti wa Chama, anajilimbikizia madaraka yote na hakuna mtu wa kumhoji halafu ndiyo anakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha za Mfuko wa Jimbo, atajinufaisha yeye mwenyewe, Mbunge huyo hawezi kuleta maendeleo katika Jimbo lake zaidi ya kujinufaisha yeye mwenyewe na kuwaacha wananchi wakiwa kwenye hali ya kukosa huduma za kijamii. Kwa nini CCM mnanichangia kama mpira wa kona kule Vunjo? Kwa nini mnajiunga na wapinzani wenzangu kwa kusema maneno ya uwongo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge na Serikali ijue fedha ambazo wameshanipa ni shilingi milioni 150. Mwaka 2010 - 2011 nilipata shilingi milioni 42,

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

mwaka 2012 shilingi milioni 21, mwaka 2013 - 2014 shilingi milioni 42.5, mwaka 2014 - 2015 shilingi milioni 48, jumla shilingi milioni 150, lakini mnakwenda kule kijijini kule Vunjo mnawaambia watu nimechukua shilingi milioni 400! Sasa naomba katika hizo shilingi milioni 400 mtoe hizo shilingi milioni 150 mnipe hiyo chenji, tena leo hii. Au Wabunge wa CCM ndiyo mnawapa hizi shilingi milioni 400 sisi wa upinzani mnatupunja? Kwa nini mnanifanyia hivyo? Kwa nini CCM jamani mnakwenda kusema uwongo? Mna ajenda gani na mimi? Narudia, kwa nini mnanichangia kama mpira wa kona kwa kusema uwongo? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka kusema uwongo huu umenisononesha na wananchi wangu wa Vunjo. Ndiyo sababu kama utasikiliza ile sauti niliyowapelekeeni baadhi yenu, wananchi walimwambia sema yaliyokuleta, kwa sababu alifika mahali akasema Mrema msimpe kura, sikiliza ile sauti, wanamwambia sema yaliyokuleta, habadilishwi mtu hapa. Nami nataka kuwaambia CCM habidilishwi mtu kule Vunjo. Nabadilishwa kwa sababu gani wakati kazi za wananchi nafanya (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachosema, hizi mbinu zinazotumika za kunidhoofisha, za kuninyong'onyeza, kwenda kusema uwongo katika Jimbo langu siyo nzuri. Badala ya kuchangia ile Shule ya Muungano; mimi nimetoa shilingi milioni 21 mbona Katibu Mkuu wa CCM hakusema Moshi Vijijini maana Mheshimiwa Dkt. Chami naye ana Mfuko wa Mbunge na ile shule ni ya watoto wa vipaji maalum, ni wa Vunjo na Moshi Vijijini, hajatoa hata shilingi 100 mbona Katibu Mkuu hakusema? Mbona na yeye anapewa hela kama mimi kwa nini mnasema za kwangu tena mnasema uwongo? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka kusema hapa ni kwamba nataka chenji yangu. Kama ni kweli mmechukua shilingi milioni 400, mimi najua sijachukua, kama ndizo hizo mnatupa, lakini fedha zilizoko kwenye mahesabu ambazo DC anajua na kila mtu anajua pale ni shilingi milioni 150. Kwa hiyo, chenji naomba mnipe nikafanye nayo kampeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, siwezi kuunga mkono hoja mpaka mniambie kinachoendelea. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Lyatonga, nilifikiri unaomba chenji kuendeleza maendeleo kumbe ya kwenda kufanyia kampeni? Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Diana Chilolo atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo na Mheshimiwa James Mbatia ajiandae. (Kicheko)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii nikushukuru kipekee sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu. Kwanza kabisa, nikupongeze wewe binafsi, nafasi hiyo umeenea, umetosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kaka yangu Dokta Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya. Kwa kweli nina kila sababu ya kusema kwamba wanatosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa sina tabia ya kubishana na wapinzani lakini leo nadiriki kufanya hivyo. Msemaji wa Kambi ya Upinzani sijamfurahia sana kwa sababu amepotosha umma kwa kiasi kikubwa. Amesema kwamba Serikali ya CCM imeshindwa, imechoka, wanataka wapinzani wachukue Dola, hivi kweli, mpinzani huyu wa CHADEMA ndiye anayeweza akachukua Dola ambaye hata ofisi yake ya Makao Makuu ya Taifa ni afadhali nyumba anayoishi Diana Chilolo? Chama hicho kufika barabara kuu ni mita mia moja wameshindwa kuweka hata lami kwa ruzuku wanazopata, hao ndiyo wa kupewa Dola? (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Kodi zetu zinafanyaje?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Unatakiwa uoneshe uthubutu wako hata kwa jambo dogo ili watu waweze kukupima.

**MBUNGE FULANI:** Aha, aha!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Hakuna taarifa Mheshimiwa Halima Mdee kaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimsaidie uelewa tu inawezekana mama yangu yupo mwepesi kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee naomba ukae chini, hakuna taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana hajitambui nataka nimsaidie uelewa tu wa bure.

**MWENYEKITI:** Naomba usimalize muda wa Watanzania naomba ukae chini.

**MBUNGE FULANI:** Hajitambui.

**MWENYEKITI:** Endelea tu Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Wewe umekaa hapo kuvunja Kanuni siyo?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Taarifa iko kwenye Kanuni.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa iko kwenye Kanuni unazuia kwa mamlaka gani?

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Diana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Muwapige *brush* vichwa basi wanaonekana wepesi sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi hapa wanafanya kazi za maendeleo hata kwa fedha zao wanazozipata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima nakuomba ukae chini, Mheshimiwa Halima naomba ukae.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Taarifa iko kwenye Kanuni.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa iko kwenye Kanuni kwa nini unakataa?

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu kuzunguza naomba ukae chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iko kwenye Kanuni.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Kaa chini Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Kanuni mmezibadilisha?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ni hivi, maana ya Kanuni kuruhusu taarifa ni kuzuia watu ambao wanaongea vitu vya uongo vipite bila kusahihishwa. Kwa hiyo, natakiwa nitoe taarifa yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae, nitakupa muda wa kutoa taarifa naomba ukae chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sasa itakuwa siyo taarifa tena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima naomba ukae chini, nitakupa muda sijatoa muda mimi, Mheshimiwa Mkosamali kaa.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iko kwenye Kanuni.

**MWENYEKITI:** Ninasema ukae chini, kaa chini nasema, Mheshimiwa Diana Chilolo tuendeleo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea kwa chini)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amediriki kutamka kwamba walimu wanaofanya kazi Tanzania ni asilimia 30 tu wengine wote hawafanyi kazi. Naomba Serikali itakaposimama itoe uthibitisho wa kauli ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa sababu lugha hiyo ni ya kuwakatisha tamaa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kada inayofanya kazi Tanzania ni walimu, ni walimu pekee wako mpaka vijijini. Leo unaponiambia walimu wanaofanya kazi ni asilimia 30 tu, mimi sikuelewi. Nitashukuru sana endapo Serikali itatoa ufafanuzi katika hili, je kauli hii ni kweli na kama ni kweli ni kwa misingi ipi? *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuacha kumsimamisha kwa sababu anatoa taarifa ambazo si sahihi. Naomba unipe nafasi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Chilolo kwamba taarifa tulizoziandika ni utafiti umefanywa na yeye siyo Serikali, aache Waziri aje ajibu, yeye asijibie Serikali. Sisi tumefanya utafiti na tumesema kwamba walimu asilimia 34 ndiyo wanaofanya kazi *full time* wengine wanaenda na kuondoka, sasa yeye atuambie ni utafiti gani ameufanya.

**MJUMBE FULANI:** Huyu anachangia bwana.



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *no research, no data, no right to speak.* (Makofi)

**MJUMBE FULANI:** Hiyo siyo juu yako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Diana Chilolo taarifa hiyo umepewa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo siitambui wala haisaidii Watanzania, Watanzania wamechanganyikiwa na lugha yake, anatakiwa afike mahali awaombe radhi walimu wanachapa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu ni watu wa kuombewa mishahara mikubwa, waombewe posho ya mazingira magumu, waombewe nyumba nzuri za kuishi, waombewe vitendea kazi vya kufanyia kazi, siyo kuwaambia hawafanyi kazi. Hatujawatendea haki walimu, mimi mwenyewe ni mwalimu nimeumia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze sana dada yangu Anne Kilango Malechela, kwa muda mfupi ameshafika Manyoni, ameona majengo tunayotegemea kufungua Chuo cha VETA Manyoni. Nataka kauli ya Serikali, chuo hicho mmekitengea fedha kwenye bajeti hii? Kwa sababu tayari majengo mlishayaona na mmeona yanafaa, tunachosubiri ni fedha ili tuweze kuweka samani katika majengo hayo. Nitashukuru sana mtakaposimama jioni wakati wa ku-*wind up* mueleze chuo hiki kinaanza ama vipi na lini kinaanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivi ni kweli vinatoa elimu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi lakini pia sasa hivi vinatoa elimu ya ufundi. Kwa lugha nyingine naweza nikasema kwamba vyuo hivi sasa ni vyuo mtambuka. Nataka nijue Serikali itakuwa tayari Wizara hii ya Elimu kuchangia fedha kwenye uendeshaji wa Vyuo hivi vya Wananchi ili viweze kuwa na tija ya utoaji wa taaluma. Natambua wazi kwamba vyuo hivi viko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii lakini Wizara ya Maendeleo ya Jamii ina fedha ndogo sana. Kwa kuwa sasa vyuo hivi ni mtambuka, ni vizuri na Wizara hii iwe inatenga fedha kwa ajili ya kuendeleza vyuo hivi ambavyo sasa hivi vinatoa elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu elimu ya watu wazima. Elimu ya Watu Wazima kwa kweli haitengewi pesa kabisa, kama inapata fedha ni kidogo mno. Nataka nijue Serikali, hivi elimu ya watu wazima kitengo hiki bado mnakihitaji ama hamkitaki? Kama hamkitaki, mtakaposimama ni bora msemi kitengo hiki kifutwe ama kama mnakihitaji basi mtuambie mmetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kuendeleza elimu ya watu wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kuhusu Idara ya Ukaguzi. Idara ya Ukaguzi mimi naishukuru Serikali imeweza kuipandisha daraja sasa hivi na imetamka wazi kwamba sasa hivi inapeleka wataalam mpaka ngazi ya kata. Nachotaka kuomba Serikalini suala hili la kupandisha daraja Idara ya Ukaguzi liende sambamba na vitendea kazi. Wakaguzi wetu hawana vitendea kazi hasa usafiri. Wilaya hazina usafiri, je, huko kwenye kata kutakuwa na usafiri? Naiomba Serikali itakaposimama ieleze, imejikita kiasi gani kwa kupandisha daraja Idara ya Ukaguzi katika suala zima la usafiri na utoaji taaluma kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu madeni ya walimu. Naipongeze Serikali kwa sababu imetamka kwamba mpaka sasa hivi kutokea shilingi bilioni 50 imeshalipa madeni imebaki shilingi bilioni tatu tu. Naiomba Serikali yangu, walimu wanachapa kazi na wanahitaji kulipwa madeni yao. Serikali itamke bayana ni lini hizi shilingi bilioni tatu zitamalizika ili

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

waachane na Serikali kuhusu habari ya madeni kwa sababu wanatambua kazi zao, wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanafanya kazi kwa bidii zote na wanahakikisha kabisa inayotolewa inaenda sambamba na *syllabus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba nizungumzie kuhusu KKK. Naipongeza sana Serikali kwa kurudi kwenye mfumo wa zamani, huo ndiyo mfumo utaomkomboa mtoto, utakaotoa taaluma ya mtoto vizuri na ambao utajenga msingi mzuri wa utoaji wa taaluma kuliko mfumo waliokuwa wanautoa. Mtoto mdogo wa darasa la kwanza unamlimbikizia masomo saba, huyo mtoto kuweza hayo masomo saba siyo rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali, Serikali sikivu imesikiliza kilio cha Watanzania na cha Wabunge na hatimaye imekubali kurudi kwenye mfumo huo. Nawaomba walimu wote wanaofundisha madarasa hayo ya kwanza na pili tayari mmeshaanza kutoa semina lakini semina hiyo itolewe kwa walimu wote ili tutakaponza rasmi tuanze walimu wote wakiwa waelewa. Naishukuru sana Serikali na naamini walimu na Watanzania wamefurahi kwani suala hili litanyanyua kiwango cha utoaji wa elimu nchini, wanafunzi watakuwa na uelewa mkubwa kuliko ambavyo tulikuwa tunafanya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu posho za mazingira magumu. Nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, amelieleza hili vizuri sana.

Kwa kweli, kama ni kada inayofanya kazi katika mazingira magumu ni walimu. Walimu wako mpaka vijijini, maeneo ambayo wameshindwa kwenda kuishi kada zingine lakini walimu wamekubali. Kama walimu wamekubali hebu tuwafikirie, wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Maeneo mengine hata barabara hakuna, nyumba zenyewe za kuishi hakuna, hata nyumba za kupanga hakuna, wanaishi kwenye matembe. Hebu fanyeni kila liwezekanalo ili kuhakikisha kwamba posho ya mazingira magumu kwa walimu hasa wa vijijini inatolewa tena ianze rasmi kwenye bajeti hii tunayojadili. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumewakomboa walimu na tutakuwa tumewatia moyo. Walimu wanafanya kazi kwa bidii zote na kwa uaminifu mkubwa lakini Serikali haijawatazama kwa ijicho la huruma. Hii posho ni muhimu Mwenyekiti wa Kamati amesema na mimi nakazia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Rachel Mashishanga na Mheshimiwa Mbatia ajiandae.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii lakini naanza kwa kusema kwamba jukumu la ujenzi wa barabara hata kilomita moja ni jukumu la Serikali. Mbunge hata akusanyiwe mishahara ya miaka mitano pamoja na kiinua mgongo chake hata nusu kilomita hana uwezo wa kuijenga, hilo ni jukumu la Serikali. Kwa hiyo, wale wanaopotosha Watanzania kwa kusema kwamba Mbunge ana haki ya kujenga barabara huo ni upotoshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, watu wamesema kwamba Serikali ya CCM ni Serikali sikivu, mimi nathubutu kusema kwamba Serikali ya CCM ni Serikali ambayo si sikivu, haisikii na imeziba masikio. Vilevile, inajidai kwamba inaona lakini haioni na imepofua macho.

Pia inasema kwamba inasonga mbele, Serikali ya CCM imewarejesha Watanzania nyuma kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya si yangu, naunga mkono hotuba ya Upinzani na ya ya Mwenyekiti wa Kamati. Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati imesema kwamba katika bajeti ya mwaka 2014 kuhusiana na pesa zilizopangwa kwa ajili ya maendeleo kwa Wizara hii, mpaka mwezi Machi, 2015 tunaingia kwenye bajeti mpya hakuajapelekwa hata senti tano, hivi kweli CCM ni Serikali sikivu na inaona makosa yake?

Nasema kwamba tutamtaka Waziri au Serikali itueleze, kwa nini kwa nini pesa hizi ambazo zilipangwa kwa ajili ya maendeleo katika Wizara hii mpaka leo haijafikishwa hata senti tano kwenye taasisi, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kuhusiana na posho za wanafunzi. Serikali hii inasabisha watoto wetu kuingia katika matendo ya ngono zembe kwa sababu haiwapi malipo yao kwa wakati. Kwa hiyo, vijana ambao wana uwezo wanawatumia watoto wetu kuwaingiza katika ngono zembe. Ni Serikali hii inayojiita sikivu ambayo haitaki kuwapatia wanafunzi posho zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi maneno yangu ndiyo nawapa na unayasikia. Jambo lingine ni suala la Chuo Kikuu cha Sokoine. Hapa tunaambiwa kwamba kuna shilingi bilioni 1.2 ambayo Serikali inadaiwa na tunaambiwa kwamba chuo hiki kitapalekwa Mahakamani. Hivi jamani Serikali ya CCM kweli mko makini? Haya maelezo siyatoi mimi, kayazungumza Mwenyekiti wa Kamati. Kweli Watanzania wafike mahali waone kwamba CCM imewarejesha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine tunadai kwamba kila mwanafunzi atakuwa na *computer* lakini kitu cha kusikitisha ni kwamba wanafunzi hao wanaodaiwa kuwa watakuwa na *computer* ni kweli kwamba hawana hata madarasa ya kusomea, wanasomea kwenye miembe. Hivi tutawadanganya vipi wananchi wa Tanzania kwamba watoto wao watasoma kwa kutumia *computer* wakati wanasoma chini ya miembe? *Computer* inatumia umeme, umeme vijijini hakuna, hizo *computer* wanakwenda kuzisomea wapi, wanakwenda kuzitumia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kauli ambayo ni kweli kwamba ilitolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuhusiana na walimu kulipwa malimbikizo yao kabla ya uchaguzi. Hivyo, miaka tisa na zaidi ya awamu mbili ambazo kazifanyia kazi, walimu hawa wameshindwa kulipwa malimbikizo yao na leo wanaambiwa kwamba watalipwa kabla ya uchaguzi. Pesa hizo za kuwalipa malimbikizo ya walimu zitatoka wapi? Bajeti yake iko wapi? Hakuna katika bajeti aliyoisoma Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba malimbikizo hayo yatalipwa kabla ya uchaguzi. Nawapa rai Watanzania kwamba umefika wakati sasa wa kufanya mabadiliko na lazima mabadiliko yao wajandikishe kwa wingi ili wapigie kura UKAWA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba kuna suala zima la ukaguzi wa shule. Tumeambiwa hapa kwamba kutokana na takwimu sahihi iliyopatikana ni kwamba ukaguzi umefanywa kwa 37% lakini 63% haijafanywa ukaguzi. Hivi ubora wa kiwango cha elimu kutokana na tathmini hii umepatikana wapi? Ikiwa ukaguzi haupo, huo ubora wa kiwango cha elimu umepatikana wapi? Mmefanya tathmini gani, mmetumia wataalam gani, mmetumia kiini macho gani mpaka mkatoa takwimu kama elimu imepanda? Ikiwa ukaguzi umeshindwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

kufanyika mtajuaje kama elimu hii imepanda katika kiwango hicho ambacho mmekisema?  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusiwadanganye Watanzania, tusiwalaghai Watanzania na Serikali ya CCM mnapaswa kuwaomba radhi Watanzania kutokana na mnayowafanyia kwa miaka yote 50. Nawaomba na ninyi kwa kipindi hiki jielekezeni kwenye UKAWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita kwanza Mheshimiwa James Mbatia atafuatiwa na Mheshimiwa Rachel Mashishanga na Mheshimiwa Bura ajiandae.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kwa kusema naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani na naunga mkono pia hotuba ya Kamati ya Mama Sitta. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Septemba, 2015, Wakuu wa nchi zote watakutana New York ili kuzungumzia Malengo 17 Endelevu ya Dunia (*Sustainable Development Goals*). Lengo la nne linasema; *to ensure inclusive and equitable quality education and promote lifelong learning opportunities for all*. Tafsiri yangu ni, usawa wa elimu bora shirikishi kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16/8/2013, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki-moon alisema; *a life of dignity to all* yaani maisha yenye kuzingatia mifumo yenye utu kwa wote. Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu wamejifanyia tathmini wamesema, *human dignity is at the heart of human identity* yaani utambulisho wa mwanadamu ni utu wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na haya ili tuzungumzie elimu ya Tanzania, Sera ya Elimu. Baada ya kuisoma n nikajiuliza maswali yafuatayo:-

- (i) Je, BAKITA au Taasisi ya Kiswahili iliipitia sera hii kwa ajili ya kuhakiki lugha.
- (ii) Je, ni fedha kiasi gani zilitumika katika kutengeneza sera hii?
- (iii) Je, kuna tofauti gani kati ya elimu na mafunzo na elimu ya ufundi na mafunzo? Sera ya Elimu ya mwaka 1995 inasema elimu na mafunzo, mwaka 1996 inasema elimu na mafunzo ya ufundi, mwaka 2014 inasema elimu na mafunzo lakini Wizara yenyewe inaitwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.
- (iv) Je, sera hii inajua tofauti kati ya kitu kinachoitwa mitaala na mihutasari? Neno mihutasari humu ndani limeandikwa mara moja lakini neno mitaala limeandikwa mara 46. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa sera hii iliyozinduliwa na Rais tarehe 13/2/2015 siku ya Ijumaa kwa mbwembwe nyingi na Serikali hii kukiri kwamba ni Serikali ya kulalamika, Serikali ya changamoto, utasema labda sera hii imeandikwa na Upinzani lakini Upinzani hawawezi kuandika sera mbovu kiasi hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mmoja ali-*challenge* hotuba ya upinzani, ukisoma ukurasa wa tatu kwenye changamoto zipo karibu 12 mpaka ukifika ukurasa wa nne lakini nimeainisha hapa kuna moja inasema wanafunzi kutomudu lugha ya kufundishia na kujifunzia

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

katika ngazi za elimu. Wanafunzi kutokumudu, kwa nini wanaajiri walimu ambao hawawezi kumudu lugha? Utafiti uliofanywa na wataalamu wetu ambao wanaonyesha walimu wanafundisha kwa kiasi gani maana yake ni nini? Sera hii ni malalamiko na changamoto, humu ndani kuna malalamiko zaidi ya 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sera ndiyo tunapoanzia sasa mfumo wenyewe wa elimu, ukisoma ukurasa wa 22, lengo la elimu ni kuwa na mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo wenye tija na ufanisi na hivyo kuongeza idadi ya wananchi walioelimika na kuwa na maarifa kwenye fani mbalimbali. Sentensi ni moja, ina maneno 26, kiunganishi 'na' kimetumika mara sita. Hii ndiyo sera ya kutupeleka kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema suala, umri wa elimu msingi na muda wa elimu na mafunzo yaani elimu msingi ni kitu kingine, elimu ni kitu kingine na mafunzo ni kitu kingine. Ukurasa wa 22 imeeleza vizuri tu inasema, mtaala wa elimu ya awali umeandaliwa kwa maana ambayo unatakiwa ufundishwe kwa miaka miwili. Ukurasa wa 22 unasema, mtaala unafundishwa kwa miaka miwili, ukurasa wa 27 unasema mtaala ni mwongozo mpana, hata *definition* ya neno mtaala humu ndani ni tatizo, huku wanasema ni mwongozo mpana, nakubaliana nao, lakini huku wanasema mtaala unafundishwa na unafanyiwa mitihani, ukurasa wa 22. Ndiyo maana nimeona ni kwa nini mikataba inayosainiwa ya kifisadi ndani ya nchi hii inakuwa ni mikubwa sana na mibovu kwa sababu hata sera hii imesainiwa wala haijahiririwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia ukurasa wa 42 hata uwiano wa wanafunzi inapofika wavulana kwa wasichana, shule ya msingi 1:1, shule ya sekondari 1:0.9, chuo kikuu 1:2 yaani huku wasichana wamepungua lakini wakifika chuo kiku wanakuwa wao ni wengi kuliko wavulana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi mlikuwa mnabisha tu hapa, soma sera hii katika ukurasa wa 48 wanasema kuna nakisi kubwa ya wataalamu walioelimika. Yaani miaka 50 ya uhuru tunazalisha wataalamu ambao hawajaelimika, iko hapa kwenye ukurasa wa 48, kuna nakisi kubwa ya wataalamu walioelimika kwa kiwango cha juu wanahitajika Tanzania yaani tuna wataalamu ambao hawajaelimika Serikali inakiri yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 55 kwa haraka, changamoto hizi ni pamoja na fedha kutopatikana kwa wakati, zinapohitajika na kutolewa pungufu katika kiasi kilicho dhinishwa hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake yaliyopangwa katika kipindi, inaendelea mpaka inafikia mahali anasema, aidha, uandaliwe utaratibu madhubuti wa kuhakikisha fedha zinafika shuleni na vyuoni yaani fedha zinazopitishwa hazifiki vyuoni. Serikali inayojilalamikia yenyewe ndani ya sera yake yenyewe. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Hii imeandikwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naungana kabisa na wale waliosema Serikali kwa kuwa imekubali na imekiri yenyewe imeshindwa, kwa hiyo, Serikali iliyoshindwa haifai kuendelea kuwepo madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, kwa dunia ye leo tunahitaji elimu inayozingatia mifumo ya elimu inayojali utu wa Mwanadamu. Utu ndiyo msingi mkuu wa haki za binadamu. Mwenyekiti wewe umetuhamasisha watoto wa Kitanzania asilimia 42 wamedumaa. Sasa kama

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

wamedumaa wataelewaje hawa? Wameandaliwaje shule maalum hao waliodumaa ili wasichanganywe na wale wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa la taifa. Katika kila wanafunzi 100 wanafunzi 42 hawawezi wakaendana na wenzao kwa sababu wamedumaa. Kama wamedumaa, maendeleo yote ya mwanadamu yanazingatia mifumo ya elimu inayojali utu, ni tunda la mifumo ya elimu inayojali utu. Sasa hii inaonekana sera yote hii ambayo ndiyo chanzo imeshindwa kutupa mwelekeo sahihi wa elimu inayojali utu wa mwanadamu hata imetufikisha kutokujua tofauti ya mitaala ni nini, mihutasari ni nini, mambo ya ithibati na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect* ni kwamba, kwa kuwa Serikali hii imekiri yenyewe kwenye sera yake hii kwamba imeshindwa, naona elimu yetu iko hoi bin taaban, taifa lische ni hoi bin taaban, hili ni janga, elimu ya taifa letu iko *ICU*, ni janga la kutisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii kwa sera hii ambayo wametumia zaidi ya miaka saba kuiandaa, haina mpango mkakati wa utekelezaji wa sera hii, haina *implementation plan* ya sera hii, Serikali itashirikiana, Serikali itaweka utaratibu, Serikali itabuni, Serikali itashirikisha, Serikali itaita wadau, shirikishi, utaratibu, tutaweka hivi, tutapanda, tutashuka, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukianza kwenye sera mbovu, mitaala itakuwa ni hoi bin taaban, mihutasari hakuna na mpaka leo hii watupe mitaala ambayo inaendana na sera hii, kama wanayo waiweke mezani. Waiweke mezani mitaala inayoendana na sera hii. Hiyo mitaala iko wapi? Sasa hawa wataalam wametengeneza kitu gani na hii imesainiwaje? Imedhalilishwa kiasi gani kwa mbwembwe na jeuri na jazba nyingi nyingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekiri ndani ya sera hii, imelalamika, imetoa changamoto nyingi, tuiombe tu Serikali hii ipumzike, waje watu wengine wenye fikra tofauti, wenye nia njema, wenye dhamira dhamiri yaani wenye nia. Tukiunganisha dhamira zetu vizuri ninaamini madeni ya walimu yatalipwa kwa sababu walimu ndiyo wazalishaji wakubwa lakini wako hoi bin taaban. Tuwekeze kwenye vichwa vya walimu wetu, wanafunzi wetu, madeni ya walimu yalipwe ili tupate maendeleo endelevu ya taifa letu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nipate majibu sahihi kuhusu sera hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa amuita Mheshimiwa Rachel Mashishanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale ajiandae.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache kwa hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, naomba nimpongeze Waziri Kivuli wa Elimu kwa hotuba yake nzuri. Pia niipongeze Kamati kwa maoni yao mazuri kabisa, nafikiri Serikali itayachukua na itayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, naomba nizungumze kitu kimoja. Serikali yako ina zaidi ya miaka 50 sitegemei tukiwapa miaka mingine wanaweza wakafanya miujiza. Kwa hiyo, nawaomba sana Watanzania tunakwenda kwenye uchaguzi, wahakikishe hawa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

mabwana wanapumzika na UKAWA tuna-take place kuhakikisha tunabadilisha kila kitu katika elimu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto zimetolewa hapa na Wizara yenyewe kwenye kitabu chake inalalamika. Naomba nianze na suala la uhaba wa walimu wa sayansi. Wakati nachangia Ofisi ya Waziri Mkuu, nililizungumzia hili kwamba, walimu wa sayansi na hisabati ni wachache sana. Kumekuwa na *tendency* Mawaziri hawajajibu mambo tuliyokuwa tunachangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Sijaona na sijajua ni kwa nini kwa sababu miaka ya nyuma walikuwa wanajibu hoja ambazo zimechangiwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu lakini sasa hivi tunamaliza Wizara sioni wakijibu zile hoja zetu. Matokeo yake sasa tukipata nafasi inabidi turudie ili tuweze kupata majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi ni kubwa sana, sijajua Serikali imejipanga vipi. Naomba Waziri atakapokuja, yeye analalamika uhaba wa walimu wa sayansi na hisabati, atuambie yeye kama Wizara ana mkakati gani na amepanga kitu gani kuhakikisha walimu wanapatikana na wanakuwa wengi ili wanafunzi wetu waweze kufundishwa hayo masomo ambayo ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi kujenga maabara nyingi sana tena za kumwaga, lakini tunazijenga halafu hazina kitu. Mnasema tuwe tunasimama hapa tunawapongeza, hivi tunawapongezaje wakati mmejenga maabara nyingi hazina walimu, hapo tunakupongeza vipi? Haya mmejenga shule nyingi, wanafunzi wanakaa chini, wanafunzi hawana vitabu, hakuna walimu wa kuwafundisha wanafunzi, sasa tutawapongezaje? Hivi utakuwa na *guts* gani za kusimama na kuipongeza Serikali? Tutawapongeza kama kweli mmejenga shule, walimu wapo wa kutosha, vitabu vipo vya kutosha, maabara zina vifaa vyake lakini na walimu wa sayansi wawepo. Sasa siwezi nikasimama hapa nikaipongeza Serikali wakati mtoto anaenda shuleni anakaa chini, naipongeza ili nipate faida gani? Kwa hiyo, tunawaambia mkafanye hivyo ili wanafunzi wetu wapate elimu bora na waweze kufanikiwa katika maisha yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye hii Sera ya Elimu. Nashukuru Mheshimiwa Mbatia amezungumzia vizuri, lakini naomba nijikite kwenye kipaumbele namba mbili cha ubora wa elimu. Wizara ndiyo msimamizi wa hizi sera na kuhakikisha zinatekelezwa. Hivi huu ubora wa elimu utapatikanaje wakati ukienda shuleni hakuna madawati, vitabu, walimu hawalipwi posho za kufundishia, mishahara ni midogo, madarasa hakuna, maabara hakuna na ukienda shule zingine hata vyoo hakuna. Hivi sasa mnategemea kuna muujiza utatoka sehemu uje uwawekee mazingira mazuri ya walimu kufundisha au watoto wasome vizuri? Kwa hiyo, naomba vitu vingine mkiwa mnavitengeneza muwe mnaangalia kama kweli mnaweza kuvisimamia au hamuwezi. Siyo mnakurupuka tu mnaleta vitu hapa halafu mnashindwa kuvifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa katika elimu na mafunzo, hiki ni kipaumbele namba tatu kama sikosei. Shule za awali mpaka sekondari ada zimefutwa lakini mbona michango ni mingi, hivi mmefuta kiini macho au nini? Kwa sababu haiwezekani mnasema mnatoa fursa kwenye elimu na mafunzo halafu watoto wakienda shule wanalipa fedha nyingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mtoto namsomesha shule ya sekondari ya kata, mbali ni 20,000/= ya ada nimelipa zaidi ya Sh.100,000/= sasa mnaposema elimu bure maana yake nini? Kuna wazazi wengine wana watoto wa kike, anaweza asimpeleke mtoto wa kike shule halafu akabaki nyumbani akaolewa, mtoto wa kiume ndiye akapata fursa ya kusoma. Hamuoni kama mnawabagua watoto? Kwa sababu obvious mtoto wa kike atabaki nyumbani kama kuna mtoto wa kiume anasoma. Matokeo yake sasa watoto wa kike hawatatoma. Suala hili naomba mliangalie kama Serikali.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna madai ya wazabuni. Haya madai ya wazabuni Mheshimiwa Waziri ameyazungumza kwenye hotuba yake. Naomba hawa wazabuni walipwe kwa sababu mpaka familia zao sasa hivi zinaishi vibaya. Watu walikuwa wanaishi maisha mazuri lakini sasa hali ni mbaya. Wengine wamefariki kwa kudaiwa na benki? Sasa mnapowakwamisha hawa Watanzania mnategemea watafanya nini au waende wapi? Mimi nafikiri Serikali iangalie tupunguze matumizi mengine yasiyo ya lazima. Nilishazungumza hata kwenye Wizara zingine ambazo nimeweza kuchangia kwamba, matumizi yamekuwa mengi. Wazabuni hawa Watanzania ni wazawa, msipowasaidia watasaidiwa na nani? Naombeni sana mhakikishe hawa Wazabuni wanalipwa madeni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi na mikopo. Hapa ndiyo kuna songombingo. Mikopo wanapewa watu ambao wana uwezo, watoto wa maskini hawapewi tena wanahangaika. Urasimu katika mikopo, jamani naombeni sana Serikali iangalie hii Bodi kwa sababu mimi naweza nikatumia *influence* mtoto wangu akapata mkopo, lakini si sawa. Kuna watoto wa maskini wanatakiwa wapate mkopo asilimia mia, hawapati, wanahangaika na mikopo na wakati mwingine wanaishia katikati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ifuatilie kwa umakini, wale watoto ambao wanatoka kwenye familia duni wapewe mikopo na urasimu usiwepo. Ikishajulikana kweli ametoka kwenye familia maskini apewe mkopo asilimia 100 kwa sababu wanapata shida sana. Hawapati mikopo halafu matokeo yake wanaishia katikati kwenye masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye miradi ya maendeleo. Kamati imezungumza hapa kuna miradi ya maendeleo ambayo utekelezaji wake haujafanikiwa. Mfano, mradi wa ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe. Zilitengwa shilingi milioni 850 lakini mpaka Machi, hakuna hata fedha iliyotoka. Matatizo ya Serikali kusubiri kuomba fedha kwa wahisani ndiyo matokeo yake haya mnakosa fedha. Hivi wewe kweli unataka kujenga nyumba unasubiri mchango kutoka jirani? Yaani hapo inabidi uchukue tu kiti ukae maana miguu itaingia tumboni, huwezi kusubiri upate fedha kutoka kwa jirani.

Naiomba Serikali mambo ya miradi ya maendeleo ambayo ni muhimu ijitahidi kutoa fedha kutoka mafungu yake ya ndani na isitegemee kutoka kwa wahisani kwa sababu mara mkataliwe, mara mpewe masharti na matokeo yake miradi ya maendeleo inasimama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu kufundisha katika mazingira magumu. Hawa walimu jamani tunawaonea, wanafanya kazi katika mazingira magumu na ambayo si rafiki. Mwalimu anasafiri umbali mrefu, anapangiwa shule vijijini huko hamna nyumba, inabidi akakae kwa wanakijiji lakini hamuwapi posho za kufundishia. Nalizungumza tena, hivi kuna shida gani ya kuwapa posho za kufundishia? Kuna shida gani kuwapa posho walimu ambao wanaenda kufundisha maeneo ya pembezoni? Matokeo yake ukienda mikoa ya pembezoni wanafunzi hawafanyi vizuri kwa sababu tu walimu hawafundishi vizuri. Sasa hivi ni mwisho wa mwezi wanakimbilia mjini kufuata mishahara lakini ni mbali. Naomba Serikali kwanza ifanye utaratibu wa kuhakikisha walimu wanajiunga na *NMB Mobile* ili wapunguze zile routes za kuja mjini na matokeo yake wanaacha vipindi kufuatilia fedha muda wa siku tatu au nne, shule inakuwa imesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna walimu ambao wanadai. Kwa mfano, Shinyanga kuna walimu 10 wamestaafu wana karibu mwaka mzima hawajapewa stahili zao. Yaani umemstaafisha mwalimu lakini humpi fedha za kuondoka, sasa unategemea nini? Si unamuongezea maisha magumu? Kama mnaona hamuwezi kuwalipa basi waacheni waendeleo na kazi na muda wa kustaafu uongezeke kwa sababu hamna fedha. Ni bora basi



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

muwe mnawalipa hata hizo za kila mwezi kuliko unamstaafisha halafu unashindwa kumlipa anakaa kwenye eneo lingine anashindwa kwenda nyumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba nizungumzie hiki chuo ambacho Mheshimiwa Waziri amesema kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Hiyo kengele ya ngapi?

**MBUNGE FULANI:** Ya pili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kuweza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na Kamati ya Mama Sitta, kwa taarifa yao nzuri ambayo wameleta mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia msemaji aliyekaa kwa jinsi alivyoona kazi iliyofanywa vizuri na Chama cha Mapinduzi katika kujenga maabara na shule. Nimhakikishie tu kwamba, huwezi kuanza na walimu kama majengo hayapo. Kwa hiyo, tumejenga maabara na walimu wapo wanasomeshwa hapo UDOM na watakwenda kuwafundisha wanafunzi masomo hayo ya sayansi ambayo hatuna walimu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaendelea, niwaombe Watanzania wajiandikishe kwa wingi kwenye Daftari la Wapiga Kura na uzi uleule uliowaonyoa watu mwaka 2010 uendelee kunyoa. Wenye tamaa na wivu, vikaishie barabarani kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ualimu ni kubwa na ngumu, tunawakabidhi watoto wetu tangu asubuhi saa moja, wengine wanalala huko katika shule zetu na wengine wanarudi nyumbani wakiwa wameshinda na walimu tangu asubuhi, kwa hiyo, tusidharau kazi wanazofanya walimu. Hata mwezi uliopita Rais alipowatunuku watoto waliofanya vizuri katika masomo yao tulikuwa na watoto wengi tu waliotoka katika shule za kata ambazo tunaambiwa kwamba, walimu wanafanya kazi kwa asilimia 30. Walimu wangepanya kazi kwa asilimia 30 tulikuwa hatuna haja ya kujenga shule za sekondari na vyyo vikuu lakini tumevijenga tukijua kwamba walimu wanafanya kazi yao vizuri, wanatimiza wajibu wao vizuri pamoja na changamoto walizonazo hawajawahi kukata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi tuwakumbuke walimu. Tume ile iliyokuwa inawahudumia Walimu (Tume ya Huduma kwa Walimu) irudishwe. Tume ile ilikuwa inawasaidia sana walimu katika mambo ya mishahara, uhamisho, posho zao, likizo na kila kitu. Sasa mwalimu yuko TAMISEMI, yuko kwa Mkurugenzi wa Halmashauri (DED), wakati Mkurugenzi wa Halmashauri hana jukumu kubwa na mwalimu kwa sababu yeye kazi yake ni kupendekeza tu kwamba, mwalimu huyu anafaa apandishwe cheo au mishahara. Kwa hiyo, ninaisihi Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi jamani muwafikirie walimu na kurudisha ile Tume ili Walimu sasa hata madeni yao yakaratibiwe na ile Tume ambayo ilikuwa inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu tunawatumia katika mambo mengi, katika uchaguzi tunawatumia walimu. Kwa hiyo, mwalimu siyo wa kumdharau hata kwa dakika moja. Tunataka kura za walimu halafu tunasema wanafanya kazi kwa asilimia 30, hapana, huko ni kuwaonea. *(Makofi)*

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tena Serikali kwa sababu mlituambia kwamba, vyuo vya VETA vitajengwa katika kila wilaya. Katika mkoa wangu ziko wilaya ambazo hazina vyuo vya VETA na wako wanafunzi ambao wanamaliza kidato cha nne na sita, lakini wapo pia waliomaliza darasa la saba ambao wanatamani kuwa na ufundi. Tunawaambia wajitegemee, wanajitegemeaje kama hawana ufundi? Hata masuala ya kilimo, VETA wanafundisha namna ya kufungasha vyakula na matunda na kuwa na viwanda vidogo vidogo lakini bila VETA haiwezekani. Kwa hiyo, kama Serikali ilivyoahidi kwamba, vyuo vya VETA vitajengwa katika wilaya zetu basi tuone sasa juhudi za Serikali kuanzisha vyuo vya VETA katika maeneo yetu ili wale wanafunzi ambao tunasema hawana kazi na wamemaliza elimu ya sekondari, basi waende huko katika vyuo vya VETA ili waweze kujifunza elimu ya ufundi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitishwa na hili linaloendelea katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwamba, mkandarasi alijenga hosteli tangu mwaka 2009 lakini mpaka leo shilingi bilioni 1.2 hazijalipwa. Hatumtendei haki Mkuu wa Chuo cha Sokoine. Niombe kupitia bajeti hii hizo fedha zilipwe jamani. Sasa hivi tumekazania sana shule za sekondari na za msingi inaelekea tunataka kusahau vyuo vikuu. Hebu turudi kwenye vyuo vikuu pia kwa sababu hata hao wanafunzi tunaowaandaa katika shule za msingi na sekondari wanatakiwa kwenda vyuo vikuu. Watakwendaje kama vyuo vikuu masuala ya maendeleo yamesahaulika? Niwasihi hebu tuangalie maendeleo ya vyuo vikuu vyetu, vitengewe fedha za kutosha na fedha zipatikane kwa sababu wanafunzi ni wengi, wana mahitaji mengi kama vitendea kazi na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunazungumza habari ya Idara ya Ukaguzi. Idara ya Ukaguzi ina nini? Mimi Idara yangu ya Ukaguzi hapa Dodoma haina hata baiskeli au pikipiki. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, Idara ya Ukaguzi kama inawezekana kuwa Wakala wawe Wakala ili wapate mahitaji muhimu kama vitendea kazi, ofisi, wa kwangu hapa Dodoma hawana hata ofisi, hawana hata gari unategemea watakagua shule hizo walizopangiwa kuzikagua? Niwaombe sana, wafanyakazi wa Idara ya Ukaguzi wanafanya kazi katika hali ngumu kwa hiyo tuone namna ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya posho, likizo na nyumba za kuishi walimu, najua Serikali hii itashughulikia. Hata hivyo, nashauri yasiwepo tena malalamiko kwamba walimu wanaidai Serikali kwa sababu wanafanya kazi kubwa katika Serikali yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Waziri na nikaona changamoto na pia nimesoma taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii nakaona changamoto zinazoikabili Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kitu ambacho sikukifurahia ni ukosefu wa mipango ya Wizara hii unaolenga kutekeleza vipaumbele, imeandikwa kwenye taarifa ya Kamati. Wizara hii ni Wizara ya Elimu na tunaitegemea sana katika maendeleo ya elimu lakini Wizara inapokosa mpango unaolenga kutekeleza vipaumbele siyo haki na hatuitendei haki kama ndivyo ilivyo. Mimi naamini kwamba kuna wasomi wazuri sana katika Wizara hii ambao wanaweza wakafanya mipango mizuri na wanaweza wakatekeleza mipango hiyo kwa kufuata vipaumbele. Tuna mpango wa BRN sasa kama hatuna mpango unaolenga kutekeleza vipaumbele, BRN haitatekelezeka kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kama Serikali hii imeweka mhibiti wa shule binafsi na hasa suala la ada kwa sababu shule hizi kila mtu anajipangia ada kadri anavyodhani au anavyojisikia. Wako watoto wa maskini kule ambapo wazazi wameamua kwamba hata kama anadunduliza kidogo kidogo lakini mtoto wake asome katika shule hizo. Sasa niombe kama huyu mhibiti hayupo au kama Wizara inadhibiti hebu tuambiwe ukomo wa kiasi ambacho mwanafunzi anatakiwa kulipa kwa sababu ziko shule ambazo zina-charge ada kwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

mwaka shilingi milioni nane, wengine shilingi milioni kumi Tanzania hiihii. Watanzania wanatakiwa kujua, je, kuna mdhibiti wa ada katika shule hizi zisizo za umma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia kuna ukosefu wa fedha kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hapa kwangu Dodoma maeneo ya Mvumi kuna mtoto anayeandikia kidole cha mguu na ameshindwa kwenda sekondari kwa sababu kwanza hatembe, ni mlemavu wa miguu lakini kungekuwa na shule ambayo angeweza kwenda angekwenda. Pamoja na kwamba ufaulu wake ulikuwa chini kidogo yaani alikosa *marks* sita aingie sekondari lakini nilidhani kutokana na ulemavu wake wa kuandika kwa miguu Serikali ingemuangalia kwa jicho la huruma. Yule msichana anaonyeshwa kwenye televisheni kila leo akiandika kwa mguu wake na inaonekana yuko vizuri kiakili. Watoto kama wale naomba Serikali iwatizame kwa jicho la huruma. Kwanza, kuandika kwa mguu siyo kazi rahisi na anajielewa, alihojiwa na mtangazaji nikaona alivyojieleza vizuri. Watoto wenye mahitaji maalumu watizamwe kwa jicho la huruma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita alikuja mama mmoja ambaye mtoto wake ni albino, mtoto wake anatakiwa kwenda sekondari na mwingine anatakiwa kwenda JKT. Akaniambia mama Bura mtoto wangu sitampeleka JKT sijui maisha yake yatakuwaje. Hebu tuwahakikishie wazazi na mimi najua kwamba Serikali inawatizama hao wenye mahitaji maalumu kwa jicho la huruma. Kwa hiyo, inapotokea watoto wenye mahitaji kama hayo, nilimwambia mzazi wake kuwa muache huyu mtoto aende shule na mwenye kwenda JKT muache aende, atatunzwa vizuri kama watoto wengine wanavyosoma na kama watoto wengine wanavyotunzwa vizuri. Naomba Serikali yetu iwahakikishie wazazi kwamba watoto hao, wale wenye *albinism* na wale ambao wana mahitaji maalumu watengewe fedha za kutosha kuwasadia katika shule ambazo watapangiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini suala la walimu litizamwe upya kabisa, suala la ukaguzi litizamwe upya kabisa kwa sababu shule zetu hazikaguliwi siyo kwamba wakaguzi hawataki waende kilomita 200 kwa miguu? Idara ya Ukaguzi ifanywe kuwa Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bura. Sasa namuita Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale atafuatiwa na Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir na Mheshimiwa Ntukamazina ajiandae.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichuke nafasi hii kumshukuru Mungu lakini pamoja na hayo kukupongeza kukalia Kiti hicho kwa sababu wewe ni Mwenyekiti wangu na mimi kwa mara ya kwanza leo ndiyo unanipa mkono nakushukuru sana lakini kazi yako ni nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Elimu, Waziri, Naibu wake pamoja na Watendaji wote kwa kazi na jitihada zao nzuri ambazo wanafanya kuhakikisha kwamba elimu katika nchi hii inaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la mikopo kwa wanafunzi. Suala hili limekuwa ni kubwa na limetikisa nchi, kila mahali migomo imekuwa ni mingi. Nakumbuka tukiwa ndani ya Bunge hili kuna mtu aliyetoa hoja kuhusu kuanzishwa kwa *Education Trust Fund* lakini katika hotuba ya Waziri sijaona mahali popote panazungumzia suala hilo. Nilifikiri ndiyo ingekuwa wakati muafaka sasa kuzungumzia hiyo *Education Trust Fund* ambayo ingesaidia sana kuhakikisha kwamba vijana wetu hawaleti migomo tena katika vyuo.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *Trust Fund* ikianzishwa ingesaidia na nafikiri wataalamu wangejaribu kufanya utafiti ni namna gani inaweza kuanza na kusaidia watoto wetu. Naomba Mheshimiwa Waziri baadaye atakapokuwa anajibu hoja hii labda atueleze hii hoja ambayo ilikuja hapa Bungeni iliishia wapi? Migomo hii inayotokea mara kwa mara ni kwa sababu ya mikopo hii tu. Nafikiria Wizara pia ingekuwa na nafasi ya kujifunza kwa watu wengine hii mikopo inaendeshwa vipi maana ni miaka mingi sasa na kila mwaka matatizo ni hayahaya. Sasa ni vizuri Wizara wangetueleza kwamba watu wengine wamefanya hivi na sehemu nyingine wamefanya hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu miundombinu katika shule zetu. Pamoja na sera na mipango mikakati ya kuboresha elimu nchini na walioathirika sana ni watu wanaoishi vijijini huko, ukienda vijijini huko mazingira ya shule wanayosomea watoto ni mabaya sana labda kwa wale walioko mijini lakini hata shule zingine za mjini zina matatizo hayohayo. Mazingira ya shule ya watoto walioko huko vijijini ni mabaya kabisa. Nafikiria Serikali ingekuwa na mpango sasa angalau hizi shule nazo sasa ziboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tumejenga shule za kata na wananchi wamejitolea wanajenga zahanati, shule sasa wakati mwingine inafikia mahali ambapo kwa kweli wanachoka, maana tumewakamua vya kutosha. Serikali na yenyewe kidogo ingekuwa inasaidia kuhakikisha shule hizi zinaboreshwa kwani mazingira ni mabaya mno. Labda tu kwa sababu Idara hii ya Ukaguzi haina uwezo lakini wangekagua na mazingira. Idara ya Ukaguzi kama itaimarishwa na kupewa hela ya kutosha ingesaidia sana kuboresha mazingira ya shule zetu. Pengine tungekuwa tunapata taarifa au habari lakini kwa sisi ambao tunakaa huku vijijini tunashangaa kwa jinsi shule zile zilivyo zingine zimebomoka, madirisha yameharibika hakuna mpango wowote ambao unafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya Wizara ya Elimu imegatua madaraka kwa Halmashauri lakini Halmashauri hela inayopata kwa ajili ya maendeleo ni ndogo sana. Wanapata 30%, utaboresha shule kweli? Naomba suala hili liangaliwe sana kwa sababu ni muhimu kabisa watoto wetu wasome katika mazingira mazuri. Mtoto anasoma shule imebomoka na tofali zinataka kuanguka! Nafikiria hiyo ingekuwa ni kazi moja ambayo pamoja na kuboresha elimu lakini mazingira pia ya shule zenyewe yaboreke. Watu wapande maua, miti ili kuwe na mazingira mazuri, shule nzuri na madawati ya kutosha. Nchi hii siyo kwamba hatuna hela, zipo nyingi sana. Ukiangalia katika randama utaona matumizi ya hela zinatamika tu hovyoy hovyoy kwa safari na kadhalika, ni nyingi mno. Kama wakati mwingine tungeweza kujiminywa tukachukua hizi hela kutoka katika kila eneo tungeweza kusaidia kuweka madawati shule zote nchi nzima kwa sababu miti na mbao tunazo, ni kitu gani kinakwamisha? Mimi nilikuwa nafikiria hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui hiyo kengele ni ya ngapi?

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya kwanza hiyo endelea.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala haijafika. (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Endelea hiyo ni ya kwanza.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna tatizo la walimu ambao wamestaafu na wanasema kwamba hawalipwi fedha zao na hata kule kwangu

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

wako wengi. Nilijaribu kuongea na Waziri wa TAMISEMI lakini akasema labda kila Halmashauri wakipata OC waweze kukata hela hizo lakini wakati mwingine OC wanayopata ni kidogo sana, kwa hiyo, yale mahitaji ya walimu kwamba waweze kulipwa wote inakuwa ni vigumu sana. Naomba suala hili liangaliwe vizuri, hawa walimu wanaostaafu wapate malipo yao palepale wasicheleweshwe kwa sababu mwingine anafundisha Mbeya anataka kwenda Mwanza ameshindwa kulipwa fedha za safari na nauli kwa hiyo anashindwa kuondoka na huku amestaafu. Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri sana suala hili liangaliwe kwa sababu tukitegemea tu kwamba Halmashauri zitasaidia kuwalipa ni vigumu sana kuweza kuwakamilishia suala hilo kwa sababu hawana fedha ya kutosha, OC ni kidogo sana, naomba suala hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumzie suala la elimu ya watu wazima. Zamani tulikuwa tunapewa *percentages* ya watu wanaojua kusoma na wasiojua kusoma lakini miaka michache hii iliyopita suala hili limesahaulika. Nafikiri ni jukumu la Wizara kutuambia kwa sasa hivi watu wasiojua kusoma na kuandika ni wangapi na kama idadi hiyo inaongezeka ijulikane ili kuwe na mikakati ambayo itasaidia kuwapatia elimu. Inaelekea suala hili halizungumzwi kabisa ni kama limeachwa labda ni kwa sababu ya wingi wa shule tulizonazo lakini kuna watu wengi wasiojua kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani kulikuwa na mikakati na mipango mizuri ya kuwatayarishia mahali maana naona mpaka watu wanaenda kupiga kura mpaka aandikiwe na mtu mwingine hii ni ishara kwamba kuna watu wengi wasiojua kusoma na kuandika. Naomba Serikali iweke mikakati mizuri ili watu wote wapate elimu ambayo itasaidia kuhakikisha kuwa watu wote wanajua kusoma na kuandika. Tunapokwenda kwenye mambo ya uchaguzi, ndiyo maana kura zingine zinaibiwa, mtu mwingine anasema andika hapa yeye anaandika kwingine. Kwa hiyo, naomba sana suala hili liangaliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hizi posho, jamani miaka michache nyuma huko kulikuwa na *allowance* maalumu, watu wanaosoma masomo ya sayansi ukimaliza ulikuwa unalipwa hela zaidi na masomo ya *arts* unalipwa kiasi. Hivi kuna shida gani kuwapatia walimu posho maalum? Anatoka kijijini anaka mbali anatembea kilomita 60 – 70 kwa mguu kwenda kufuata mshahara na kwa bahati mbaya mabenzi huko hayapo. Tungekuwa na benki huko vijijini tugesema sawa lakini kwenda benki unakwenda kilomita 70, halafu unategemea mwalimu aende huko kufuata mshahara wake halafu bado unashindwa kumpatia posho maalumu jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa waganga wa vijijini, walimu wa vijijini wangepaswa kupata posho hiyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri atueleze hapa huu mkakati upo au haupo? Kama upo ni lini mtaanza kuutekeleza? Muanze kuwalipa hawa watu wanapata shida kwani mishahara inaishia kwenye nauli tu. Ndiyo maana hata wakati mwingini upinzani wanasema wanafundisha 30% ni kwa sababu ukweli hawa watu wanasafiri mbali, mtu anaka siku mbili, tatu anafuata mshahara. Hatuwezi kufika kwa namna hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuje na mpango na mkakati ambao kwa kweli unaeleweka tujue kwamba tunawasaidia walimu wetu ambao wanatoka vijijini. Wala siyo gumu hili, ni suala la kuamua tu, tuwapatie posho zaidi. Walimu hawa wanafundisha katika mazingira magumu, nyumba ya kulala hakuna, wanajibanza kwenye nyumba za wenyeji. Naomba Serikali ije na mpango ambao utasaidia kuboresha maisha ya walimu na siyo kama tulivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nasema ahsante sana. (Makofi)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Al- shaymaa.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa afya na pumzi hadi muda huu na sote kukutana tena katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na nitajikita sana kwenye masuala ya watu wenye ulemavu kama kawaida yangu. Naipongeza Serikali kwa masuala fulani ambayo tumepata, Waswahili wanasema hakuna kupata kidogo, ukipata japo kidogo unashukuru. Kwa hiyo, tunashukuru kwa kidogo tulichokipata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa nalopenda kulizungumzia ni masuala ya elimu uumuishi (*inclusive education*). Masuala ya watu wenye ulemavu kuwekwa shule za peke yao, kutokuchanganywa, naipongeza Serikali kuna baadhi ya shule wamechanganya lakini bado. Wanafunzi viziwi wanakaa peke yao, mabubu wanakaa peke yao, watu wenye *albinism* wanakaa peke yao, kweli watapata kuelewa bila kujichanganya na wenzao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakichanganywa wana-cope na wenzao na wao wanapata kidogo changamoto au *challenges* kutoka kwa wenzao lakini wakiwekwa peke yao ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba ile kidogo tuliyopata Serikali iongeze zaidi kwa ajili ya watu wenye ulemavu kuchanganywa na wenzao madarasani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotoa mfano, viziwi wanahitaji lugha ya alama wakichanganywa na wenzao darasani kama vile vifaa vinakuwa hakuna inakuwa rahisi kwa Serikali kuwapatia vile vifaa kwa ajili ya *deafs* ambao wanahitaji *braille*. *Braille* bei yake sasa hivi ni Sh.1,300,000 – Sh.1,500,000 itapatikana wapi, hakuna hivi vifaa. Kwa hiyo, wakijichanganya inakuwa rahisi Serikali kuvitaa vile vifaa wanakuwa na wenzao darasani na wao wanakuwa wanapata yale mahitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali walikuwa na *Action Plan* ya 2010-2017, uandikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu bado ni mdogo. Sijui Halmashauri uhamasishaji wao ukoje lakini mimi nasema iwepo elimu maalumu ya uhamasishaji watu wawapeleke watoto wenye ulemavu mashuleni. Bado kuna huu mtindo wa kuwaficha, eti anaona aibu kumpeleka mtoto shuleni kisa ana *albinism*, anaona aibu akimpeleka ataonekana ana mtoto *albino*. Uone aibu wakati Mwenyezi Mungu ndiye aliyekupa? Unaona aibu una mtoto ana ulemavu wa viungo huwezi kumpeleka shuleni. Kwa hiyo, nasema bado elimu ile ya kuhamasisha kuwapeleka watoto hawa shule bado iko chini. Naomba hii elimu iendelee kuwepo na nafikiri ni Halmashauri wanaohusika kwa suala hili la kuhimiza na kuhamasisha uandikishwaji, kwa sababu asilimia ya uandikishaji ya watoto wenye ulemavu ni chini ya asilimia kumi yaani wanaoandikishwa kwenda shuleni ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa ziara Mkoa wa Mwanza na Balozi wa UNESCO, Mheshimiwa Zulmira Rodrigues, tulienda Sengerema, tumeenda mpaka kwenye shule ya Mitindo. Ile shule ya Mitindo kuna watoto wenye *albinism*, hali niliyoikuta ni ngumu, nimepata maumivu sana. Naomba Serikali iniambie, ile shule ya Mitindo ni nani anaisimamia? Watoto 202, Matrioni wanne (4), wataweza kweli kusimamia watoto kundi kubwa namna hiyo?

Watoto wale wenye *albinism* nimekuta wameungua na jua, wameumia. Kwa sababu yale maumivu mimi nayajua, nimepata maumivu makubwa sana. Wameumia wale watoto kwa kweli. Mimi naomba niambiwe kwamba ni nani anasimamia ile shule ili nipate kuelewa kwa sababu huduma yake kwa kweli imeniumiza mno.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni bajeti. Kamati wamezungumzia kuhusu bajeti kwa ajili ya mambo ya elimu maalum, bajeti ni kiduchu, ni ndogo. Kwa hiyo, pia naomba Serikali waniambie ni kiasi gani walichokitenga safari hii tukisikie kwamba kumetengwa hela kadhaa kwa ajili ya kusaidia masuala ya watu wenye ulemavu na masuala yenyewe ndiyo nimeshasema yasiwe *special* yawe *inclusive* ndiyo tunaitaka. *Special* hapana! Wakiwa peke yao, elimu inadorora, hawa-cope, hawapati *challenges* kabisa. Hiyo ni muhimu, Serikali watanieleza ni pesa kiasi gani imetengwa kwa ajili ya kuhamasisha masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kengele ya kwanza au ya pili?

**MWENYEKITI:** Ni ya kwanza endelea.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni vifaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu bado ni tatizo. Nimetoa mfano wa *braille machine* ambazo *cost* yake ni Sh.1,500,000. Naomba Serikali pia wanieleze kuhusu hili suala la vifaa nini tatizo. Inakuwa ni changamoto pia kwa wale walimu wa elimu maalum wanapata shida katika ufundishaji, wanafundisha katika mazingira magumu kutokana na kwamba hawana vifaa. Ufundishaji wao unakuwa mgumu sana. Nimeshawahi kuongea na walimu wa elimu maalum wanasema wanapata shida sana katika ufundishaji, kazi yao inakuwa ngumu kutokana na kukosekana kwa vifaa vya ufundishaji na kujifunzia wanavyosema watalaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni miundombinu. Suala la miundombinu siyo rafiki kwa watu wenye ulemavu. Bado ni *challenge*, mashule mengi ni *challenge* kwa ajili yao. Nimefika Mitindo wanafunzi wanapewa chakula wamepanga foleni, wale wenye *albinism* wapo juani wanapanga foleni kusubiri chakula, wanaungua na jua. Ie miundombinu ingekuwa rafiki kwa wao kwa maana kwamba wanapata chakula wako kwenye kivuli. Sasa wanapanga foleni yule adui yao jua ndiyo anawachoma! Sasa kuna faida gani kwani baada ya miaka mitatu, minne wanapata kansa tumewakosa na hiyo ndiyo *challenge* kubwa kwa watu wenye *albinism*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nahimiza zaidi Serikali inipe jibu kuhusiana na bajeti ambayo ni kiduchu, haitoshi. Naomba Mheshimiwa Waziri anapojibu na mimi aniweke kwenye kipaumbele cha watu wa mwanzo, kwa sababu masuala ya *disability* mpaka sasa hivi najisikia mimi ndiyo nimezungumza, sijamsikia mwingine ameyataja...

**MBUNGE FULANI:** Na Kamati.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Na Kamati imetaja. Naomba mnapojibu na mimi niwe wa mwanzo na mimi nitajwe mwanzo kuhusu masuala hayo, tuna-*challenges* kubwa. Hatukuacha kushukuru kwa mlilotupa lakini bado tunalia, tupo miguuni kwenu tunawalilieni tunaomba mtusaidie, bado tuna changamoto tunafichwa ndani tusiende shule. Tutoeni ndani twende tukasome na sisi tuweze kujishika kimaisha hapo baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, yangu yalikuwa hayo, naomba sana Serikali initazame kwa macho mawili mimi na kundi kubwa la watu wenye ulemavu waliopo nyuma yangu wanaosikiliza hivi sasa kuhusiana na hizi changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa namuita Mheshimiwa Ntukamazina atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kahigi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu tatu. Moja ni pongezi, pili ni maombi na tatu ni ushauri na ushauri huwa nautoa kama mwalim, mimi ni mwalimu *by profession*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameifanya ya kusimamia ujenzi ya Kampansi ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha MUHAS (Muhimbili University). Nasema hivyo kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Chuo Kikuu cha Muhimbili, nampongeza kwa niaba ya Wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza Katibu Mkuu pamoja na Watendaji kwa kusimamia na kutoa Sera ya Elimu. Hata kama Sera ya Elimu ina upungufu utasahihishwa lakini chonde chonde hata mara moja msije mkasahau umuhimu wa Kiingereza kama *medium of instruction* kwenye *secondary schools* na *universities*. Mheshimiwa Nyangwine huwa *ana-promote* Kiswahili, mimi *na-promote* Kiingereza na Kiswahili. Nakushukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, niwapongeze dada zangu wawili, *Chief Education Officer* - Profesa Bhalalusesa na *Chief Inspector of Schools* - Mama Wasena, kwa kuisaidia Ngara kupata *high school* ya tatu, *Muyenzi High School*. Bado nawaomba tupate *high school* ya nne ya Murusabanga kwa sababu sera ya Serikali inasema tuwe na *high school* kwa kila tarafa na Ngara tunazo tarafa nne, bado moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa nije kwenye maombi. Ombi la kwanza na hili ombi ni la zamani sana, namuomba Mheshimiwa Waziri, kwamba tujengewe chuo cha ufundi katika Wilaya ya Ngara ili watoto wetu wanaomaliza darasa la saba na darasa la kumi na mbili waweze kujipatia ujuzi na kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili ni ukaguzi. Ukaguzi ni *core function* ya Wizara ya Elimu lakini ukaguzi ina bajeti ndogo sana. Ngara ni shule chache zimekaguliwa kwa sababu Ngara wana gari lakini hawana mafuta. Ukaguzi kazi yake ni *quality assurance* ya elimu inayotolewa katika shule. Kwa hiyo, naomba wapewe bajeti nzuri zaidi. Pia mwaka jana nilishauri kwamba tununue pikipiki, pikipiki gharama ni ndogo na zinaweza kusaidia sana katika Wilaya mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la tatu ni ruzuku kwa ajili ya *research*. Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani awamu ya pili aliahidi kwamba Serikali ingetenga fedha asilimia moja ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya *research* ya vyuo vikuu na vyuo vya utafiti. Hatuwezi kuwa na maendeleo bila *RND (Research and Development)*. Kwa mfano, Wahadhiri wa MUHAS na vyuo mbalimbali ni lazima wafanye utafiti kuongeza *knowledge* na mawazo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la nne, naomba Waziri aende Hazina atusaidie vyuo vikuu viwe vinapata ruzuku moja kwa moja kutoka Hazina kwenda kwenye vyuo hivyo badala ya kupitia Bodi ya Mikopo. Kwa sababu ruzuku siyo mikopo, itoke moja kwa moja Hazina kwenda vyuo vikuu, kama itashindikana basi ruzuku ipitie Wizara ya Elimu halafu iende vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye ushauri. Ushauri wangu ni kwamba, mwaka jana nilisema mbele ya Waziri Mkuu kwamba hatuna Wizara ya Elimu na sasa hivi bado nasema hatuna Wizara ya Elimu. Hatuna Wizara ya Elimu kwa sababu idara zote zimehamishiwa TAMISEMI. Wakati huo ilikuwa ni Idara ya Elimu ya Msingi pamoja na Idara ya Sekondari, sasa hivi Idara zote zimehamishiwa TAMISEMI.



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Wizarani kuna vitengo tu, kuna vitengo vitano chini ya Kamishna ambavyo ni Kitengo cha Elimu ya Msingi, Kitengo cha Sekondari, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima, Kitengo cha Mipango na Kitengo cha Ualimu. Ndiyo maana Dada yangu sasa hivi Kamishna kama yule ya Magereza badala ya kuwa *Chief Education Officer* kwa sababu anaongoza vitengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nailaumu Menejimenti ya Utumishi. Menejimenti ya Utumishi kazi yake ni kuhakikisha kwamba inachambua miundo ya Wizara na kuidhinisha miundo ambayo inaongeza ufanisi. Sasa miundo wa Wizara ya Elimu hauongezi ufanisi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nije kwenye diploma. Kulikuwa na diploma zinaitwa *half combination*, diploma hizo zilikuwa zinatolewa katika vyyo vya Mkwawa, Korogwe na Monduli, sasa nasikia zimehamishiwa Chuo Kikuu cha *UDOM*. Mimi kama mwalimu, nimueleze Mheshimiwa Waziri kwamba Chuo Kikuu cha *UDOM* kina *Lecturer* wanaotoa *lecturers*, hakina *professional teachers* wa kuwa-*train* walimu na wakatoka kama walimu. Hilo ni kosa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ilikuwa ni kosa kuhamisha shule za mazoezi (*demonstration schools*) ambazo zinakuwa karibu na vyyo vya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile shule ni *demonstration* zilikuwa zinasaidia vyyo, kwa mfano mimi nimefundisha *Butimba Teachers Collage* mwaka 1971 - 1973, tulikuwa tunapeleka wanachuo wetu kwenye shule ya *demonstration* kwa kuwa kwenye shule hiyo kuna walimu wazuri ili wale wanachuo waone jinsi walimu wazuri wanavyofundisha, sasa shule hizo zimehamishiwa TAMISEMI. Kwa kweli, hilo ni kosa kubwa sana, huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nimesema kwamba mimi ni Yohana Mbatizaji, ninayelia nyikani, lakini naamini kwamba itakuja Serikali ambayo itathamini elimu na Wizara ya Elimu itarudishwa katika hali iliyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namuita Profesa Kahigi na Mheshimiwa Margaret Sitta ajiandae.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akushukuru kwa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu. Nianze tu kwa kusema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa hiyo nilishiriki kutoa mchango katika hotuba yetu ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Margaret Sitta. Kwa hiyo, ninaiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naunga mkono hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa niaba ya Upinzani. Haya yote mawili yakiunganishwa yanaelezea hali halisi ya elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu niseme hali ya elimu nchini siyo nzuri na hapo nimetumia tasifida. Kwa hiyo, mtu unaweza kusema kwamba iko hoi au nini lakini ni namna nyingine ya kuelezea hali hiyo. Ukienda katika shule zetu za msingi nyingi hazina vyyo, hakuna nyumba za walimu, wanafunzi wanashinda kule shuleni bila kupata chakula hata kidogo. Katika hali hii utategemea mafunzo yatawezekana? Kwa hiyo, kuna matatizo mengi yakiwemo madai yao ambayo hayajakamilishwa. *(Makofi)*

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme ukweli walimu wanakabiliwa na mazingira magumu, hapa ni lazima tuliseme. Kwanza chombo cha kuwahudumia hakipo, ni kweli kwamba sasa hivi kuna maandalizi ya kukileta chombo hicho, lakini kwa sasa hivi na kwa muda mrefu chombo hicho hakikuwepo na mazingira yameendelea kuwa magumu, hiyo posho ya mazingira magumu hawapati. Baadhi yao siyo wote badala ya kufundisha darasani wengine wanalazimika kwa sababu ya mazingira hayo magumu kufanya shughuli nyingine. Hilo lazima tuliseme kwa sababu tunawafahamu baadhi yao ni rafiki zetu, hilo lazima tulilisisitize. Kwa hiyo, mazingira magumu ya walimu bado yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye vyuo vikuu vipo taabani, miundombinu imechoka. Tulitembelea Mzumbe tukakuta kwamba mabweni 20 baadhi yaliyojengwa miaka ya 50 yapo hoi, yaani hayafai kabisa kwa binadamu kuishi katika mabweni hayo ya wanafunzi lakini fedha za maendeleo katika vyuo vikuu haiendi huko. Shilingi milioni 850 ya maendeleo mpaka sasa haijapelekwa huko Mzumbe, shilingi bilioni 1.2 toka mwaka 2009 hazijapelekwa SUA na hilo ni deni. Naibu Waziri wa Fedha yupo hapa ayasikie haya ni matatizo makubwa. Kwa hiyo, ni lazima tuyaseme haya kwamba kuna matatizo, haya yanaathiri ujifunzaji na ufundishaji katika shule zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu Sera ya Elimu. Ni kweli inawezekana sera hii ina upungufu na kweli ina upungufu na baadhi yake yameshazungumziwa sitayazungumzia mimi. Mimi nataka kuzungumzia kipengele cha mkakati.

Katika hotuba yake Waziri amesema wanaandaa mkakati na upo katika hatua fulani ya maandalizi. Huo mkakati wa utekelezaji wa sera hii utakamilika lini? Kwa sababu sera yenyewe ni kama Sera ya Maoteo kwa sababu haielezei hali halisi. Kwa sababu kwa mujibu wa sera hii italazimika kila shule ya msingi igeuzwe kuwa shule ya sekondari, sasa ni fedha nyingi ambazo zitatumika katika kubadilisha hali hiyo, ni kama sera ya maoteo tu, siyo kwamba sera hii itatekelezeka leo au kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie lugha ya kufundishia. Lugha ya kufundishia katika sera ni mbili Kiswahili na Kiingereza, sawa, ingawa kwa kawaida nchi huwa inatoa lugha moja ya kufundishia ile nyingine inakuwa ni kigairi (*exception*). Napenda kutoa rai kwa wale ambao bado mpaka leo wanadai kwamba lugha ya kufundishia iendelee kuwa Kiingereza kwa ngazi zote hiyo rai imeshapitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine kuhusiana na ufundishaji wa lugha za kigeni hasa Kiingereza. Mbinu za kufundisha Kiingereza hapa nchini kwa kweli zimepitwa na wakati, ndiyo maana mwanafunzi anaweza kuingia darasani toka darasa la tatu mpaka darasa la kumi na mbili akiwa bado hajaweza kuongea na kuandika Kiingereza vizuri, kwa sababu mbinu zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Wizara kwamba iandae jopo la watalaam wa kufundisha lugha itupatie mbinu bora ambazo zitatumfundishia wanafunzi wetu lugha zote mbili Kiswahili na Kiingereza ili waweze kuwa mahiri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee huduma za maktaba. Huduma za maktaba katika nchi yetu kwa kweli zimerudi nyuma, zamani kulikuwa hata na *mobile library*, maktaba ilikuwa inafanya kazi, kulikuwa na utamaduni wa kusoma, sasa hivi utamaduni wa kusoma haupo.

Napendekeza kwamba Wizara ione namna ya kuanzisha maktaba katika shule zote nchini. Licha ya maabara kunahitajika maktaba ili tuanze kujenga utamaduni wa kusoma katika shule zetu.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi isiyokuwa na utamaduni wa kusoma huwa haina utamaduni wa kuandika, ndiyo maana katika nchi hii kwa kweli wanaoandika vitabu siyo wengi, ni wachache sana lakini ukienda Kenya waandishi ni wengi, ukienda Uganda waandishi ni wengi. Hii dosari tuangalie na tuifanyie marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongelee kuhusu ahadi ya Serikali kupeleka Chuo cha Ufundi Bukombe. Bukombe ilikuwa ni miongoni mwa wilaya 28 ambazo ziliahidiwa kwamba zitajengewa Chuo cha Ufundi mwaka 2010 lakini mpaka leo tumefuatilia jambo hili lakini hadi leo hatujafanikiwa, tunaambiwa kwamba sijui mpango huo umefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuambie kabisa kwamba ile ahadi ya Vyuo vya Ufundi katika wilaya 28 ikiwemo na Bukombe basi ilikuwa ni ahadi isiyotekelezeka, mtuambie hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naomba nimuite Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARETH S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii iliyoko Mezani.

Namshukuru Mungu, nawashukuru Wanawake wa Mkoa wa Tabora, nawashukuru Wananchi wa Urambo, lakini pia nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, ambao tumeshirikiana nao mpaka tukapata hii Taarifa ambayo tumeiwasilisha leo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti, lakini niliona pia nizungumze kukazia yale ambayo Kamati imeona ni ya muhimu sana. Niwatake tu wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kitu kikubwa kinachozungumziwa, ukiangalia mengi ambayo wamezungumzia hata Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni suala la ubora wa elimu. Kwa hiyo, ukizungumzia suala la ubora wa elimu, wa kwanza unayemwangalia ni Mwalimu, jinsi anavyofundishwa mafunzo yake, anavyoendelezwa na anavyohudumiwa na ndiyo maana tunazungumzia suala la chombo cha huduma kwa Walimu (*Teachers' Service Commission*), ili tumwangelie kwa mapana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Teachers' Service Commission* ikiundwa itamsajili Mwalimu kwa kuangalia sifa zake, *whether* anakwenda Shule ya Binafsi au anakwenda Shule ya Serikali; kwa hiyo, itasajili Walimu, itawapanga kwenye shule, itaangalia jinsi wanavyopandishwa madaraja, itawachukulia hatua za kinidhamu, itaangalia jinsi wanavyopata posho zao. Ndiyo maana tundiambia Wizara ya Elimu kwamba, chombo hiki kianze mwaka wa fedha mpya 2015/2016, ili Mwalimu aangaliwe kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siku ya leo namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, atuhakikishie kwamba, mwezi Julai chombo cha kuhudumia Walimu kitakachowapunguzia shida walizonazo kitaanza. Nashukuru Mwenyezi Mungu, tulikuwa na Mheshimiwa Waziri wote kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu, tarehe 26 Mei 2015 na Mheshimiwa Rais akatamka pale; sasa tunataka yeye atutajie hapa, yeye ndiyo mtekelezaji atutajie hapa!

Mheshimiwa Rais alisema wiki mbili za mwisho katika Bunge hili, zitajikita katika Miswada Muhimu, mmojawapo ukiwa ni huu wa kuanzisha chombo cha kuhudumia Walimu, kwa sababu bila Sheria haiwezekani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akiwa anajumuisha athibitise, kwa sababu yeye ndiyo mtekelezaji kwamba, kweli Chombo cha Huduma kwa Walimu kitaanza mwaka mpya wa fedha huu. (Makofi)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, huwezi kuzungumzia ubora wa elimu kama huna Wakaguzi; nani atakupa taarifa za kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina takwimu hizi ambazo zimetoka kwenye Kitabu cha TAMISEMI kinasema, kwa takwimu zao za mwaka 2013, kuna Shule za Msingi za Serikali 15,578, Shule Binafsi za Msingi 767, Shule za Serikali za Sekondari 3,528, Shule Binafsi za Sekondari 1,048 na Taasisi zingine. Vyuo vya kufundishia Walimu vya Serikali vinapata kama 32, wakati Vyuo Binafsi vinavyofundisha Walimu ni vingi vya binafsi kuliko vya Serikali, viko karibu 52. Sasa utaona kutokana na wingi wa taasisi zinazotoa elimu, pamoja na kufundisha Walimu, ni nyingi kiasi ambacho tunahitaji ukaguzi wa makini, ili tujue ubora wa elimu inayotokea huko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa kitu kimoja; mimi nilikuwa Afisa Elimu Wilaya ya Kinondoni katika miaka ya 1994, ninajua kulikuwa hakuna shule za sekondari. Kwa hiyo, Shule kama za Kumbukumbu na nyingine nyingi tu, kuna mwaka hawakutoa hata mwanafunzi mmoja kutokana na uhaba wa Shule za Sekondari. Kwa hiyo, tuipongeze Serikali kwa kuongeza Shule za Sekondari, lakini tunachozungumzia sisi hapa ni ubora sasa hivi; ndiyo maana tunasema ukaguzi uimarishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilitaka nimsaidie Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla; Waziri Mkuu alipokuwa anahitimisha hoja yake ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mei 16, 2015, ukurasa wa 64, nilienda kwenye Hansard, naomba ninukuu kwa ruhusa yako: "Mheshimiwa Spika, ninamalizia na mambo mawili; nilimsikiliza Mama Sitta wakati akizungumza hapa, alikuwa anazungumzia sana juu ya uwezekano wa kuwa na chombo mahususi kwa ajili ya ukaguzi wa elimu. Kimsingi, nilimwambia bahati nzuri Serikalini jambo hili limeshatazamwa, tumeliangalia tunaona ni jambo zuri, kwa sababu ukitaka kuimarisha elimu lazima Idara ya Ukaguzi nayo iimarishwe sana. Sasa dhana pengine ni kuwa na chombo mahususi kisimamie eneo hili asilimia 100, wao waweze kusimamia ukaguzi kwa upana na kwa karibu zaidi, nataka nimhakikishie kwamba, tutaliangalia kwa macho ya karibu sana tuone how best we can do that ili tuweze kulfanya jambo hili vizuri na kwa nia njema."

Anaendelea: "Mheshimiwa Spika, tayari tumeshakubali kuwa na chombo ambacho kitasimamia ajira, nidhamu na kadhalika, lakini hiyo peke yake haitoshi, iko haja ya kutazama hili eneo la ukaguzi tuone kwa kiasi gani tunaweza tukafanya vizuri." Akapigiwa na makofi, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unakamilisha hapa, naomba uhakikishe haya maneno aliyoyasema Waziri Mkuu mbele ya Bunge hili tarehe 16 Mei 2015 kwamba, yote ni mazuri. Kwanza, chombo cha Walimu kitakuwepo. Pili, ukaguzi utapewa na chombo chake. Mheshimiwa Waziri wakati wa kuwasilisha useme hivyo na nitashukuru ukiwasilisha vizuri ili huko baadaye tusiulizane maswali mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la usajili wa shule. Tumeshakuwa na shule nyingi za msingi na sekondari kwa idadi niliyoisema hapa. Kwa hiyo, sasa hivi ni suala la kuimarisha ubora. Tumekuomba kama Kamati na tunarudia leo, Kamishna anaposajili shule sasa haina haja ya kuchukua kiholela, aangalie vigezo vyote vinavyostahili kuwa na shule bora, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa maji kwa visima au kujenga matenki ya kukusanya maji ya mvua. Vilevile upatikanaji wa vyoo na miundombinu ya kusaidia wenzetu wenye mahitaji maalum.

Tumemwomba Kamishna, leo tunarudia kwamba, sasa usajili wa shule ufanywe kwa umakini zaidi kwa sababu shule zimetosha ni nyingi mno, sasa tunaangalia ubora. Kwa hiyo,

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

isiwe mtu kusajili tu kwa sababu amekuja kuleta *pressure*, lakini tufuate miundombinu vikiwemo vyoo na miundombinu mingine ambayo inaweza kuwasaidia wenzetu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nilitaka nimuunge mkono Mheshimiwa Al-Shaymaa, alipozungumzia kuhusu Idara inayoangalia mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ni kweli Mheshimiwa Waziri, sijaona suala hili likitiliwa umuhimu! Kuwe na Idara inayoangalia mahitaji ya watoto wenye mahitaji maalum na kupewa fedha, itasaidia sana jengo hili au Bunge hili, kama wakati wa kuhitimisha Mheshimiwa Waziri utatuambia ni kiasi gani kimetengwa katika Idara gani ambayo kweli inalenga kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nashukuru sana. Namalizia kwa kuishukuru sana Kamati; Kamati nitawakumbukeni, mlinipa heshima kwa miaka mitano, tena mara ya mwisho nikapita bila kupingwa, basi naomba tuombeane. Ninyi Kamati na mimi mwenyewe tuombeane, wale waliotupa kura watupe tena turudi hapa, ili tuone kweli haya tunayowaambia Wizara ya Elimu wameyatekeleza au bado. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Hotuba ya Wizara ya Elimu. Mimi naomba nianze na hoja ya ujenzi wa Vyuo vya VETA katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012/2013, Wizara ya Elimu ilitupa sisi Wabunge wote Majedwali ambayo yalikuwa yanaonesha kwamba, Wizara ya Elimu itatujengea Vyuo vya VETA. Katika majwedwali yale, Wizara ya Elimu ilionyesha kwamba, kila Wilaya itajengewa hicho Chuo cha VETA mwaka gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale kwa mujibu wa Majedwali yale yalikuwa yanaonesha kwamba, tungejengewa Chuo cha VETA kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Sasa tunamaliza Bunge na tunaondoka, sijajua vyuo hivyo vimeyeyukia wapi?

Ningependa kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Vyuo hivi vimekwenda wapi na mpango mpaka sasa hivi uko namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, ukurasa wa 21. Kamati ya Huduma za Jamii katika ukurasa huu imezungumzia kutenganisha ama kutenganishwa kwa elimu za msingi, elimu za sekondari na elimu ya juu. Mimi naomba kuunga mkono hoja hii na napenda niongeze kwamba, hata hapo kwenye Idara ya Sekondari peke yake, ninakumbuka mwaka 2013 niliishauri Serikali, niliomba sana na nilisema labda kwa kukumbusha tu kwamba, tuna shule zile tunazifahamu ambazo ni *giant schools*, zinafahamika. Kuna Shule za Sekondari za Kilakala, Mzumbe, Ilboru, Tabora Girls, Tabora Boys, Msalato na kadhalika, zinafahamika tukiitaja *giant schools*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi ukizitembelea sasa siyo shule zile ambazo tunazifahamu. Nakumbushia tena, shule ziko kwenye hali mbaya mno! Niliomba Serikali mwaka 2013 hebu itengeneze utaratibu wa kuziondoa shule hizi kutoka TAMISEMI kwa maana ya kuhudumiwa na Halmashauri zetu za Wilaya. Unaichukua shule kama *Mzumbe Secondary* inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, shule ambayo ina wanafunzi karibu 900, shule ambayo inachukua wanafunzi wenye vipaji maalum, halafu bajeti za Halmashauri zetu zinaeleweka! Matokeo yake unakuta shule hizi zina madeni makubwa.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara ya Elimu kuziwekea *limit* kwamba, hamruhusiwi kukopa, hamruhusiwi kutumia ama kununua kitu chochote kile nje ya bajeti, lakini inafikia mahali wanashindwa. Madeni makubwa ya vyakula yako kwenye shule hizi! Walimu sasa wanaonekana kama hizi shule ndiyo zao, mnawapa mizigo mikubwa mno, wanafunzi wanapokosa chakula wanahangaika kwenda kwa wazabuni ambao hamjawalipa, Walimu Wakuu wanachukulia shule hizi kama za kwao wanakwenda kuhangaika kutafuta chakula kwa ajili ya wanafunzi. Kwa nini sasa hizi *giant schools* na hata zile ambazo siyo *giant schools*, lakini ni za *boarding* msifikirie kuzipatia bajeti zinazotosha ama muangalie utaratibu mwingine mzuri unaofaa badala ya kuziacha zihudumiwe na Halmashauri zetu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Wilayani kwangu pale, kuna shule moja tu ya A-Level, lakini ni kubwa, ina wanafunzi karibu 1,000. Halmashauri yangu haiwezi kuhudumia wanafunzi hawa wote kufuatana na kipato cha Halmashauri. Hebu angalieni utaratibu wa kuziondoa hizi shule zote ambazo tunazifikiria kwamba, ni *giant schools*, mnazifahamu ninyi wenyewe, tengenezeni utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia madeni ya Vyuu Vikuu na Vyuu vya VETA, lakini kuna wazabuni wa ndani wa kawaida sana ambao wametumia *millions* na *millions* za fedha kuwalisha wanafunzi na kuwapelekea wanafunzi vitabu na vifaa vya maabara. Madeni yako kule, shule moja unakuta ina madeni milioni 600, milioni 400; hivi Wizara ya Elimu mmeshapitia kwenye hizo shule mkajaribu kuangalia kama hayo madeni yako sawa na mkataya-clear namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnawaumiza wazabuni wadogo walioko kule, wana hali mbaya sana. Wengine wana mikopo ya benki, wengine hali zao ni mbaya kwa kifupi. Ninaomba hebu tengenezeni utaratibu, pitieni kila shule; kaangalieni shule hii inadaiwa kiasi gani madeni ya chakula, vifaa vya maabara na vitabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie masuala ya maabara. Tumejenga maabara za kutosha, lakini nina uhakika bado hatuna Walimu wa kutosha na hata tukiwa na Walimu wa kutosha bado tunahitaji *technicians*. Mwalimu hawezi kuwa *technician* na huyohuyo akawa Mwalimu. Tuwe na Walimu, baada ya Mwalimu kufundisha akimaliza amefundisha *chemistry* yake, basi na maabara kule awepo *technician* ambaye sasa atasaidiana kuwafundisha wale wanafunzi kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba niunge mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nina dakika tano; kuna mchangiaji, Mheshimiwa Susan Lyimo, dakika tano zinaweza kukutosha kwa sababu mchana umesema haupo?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini leo katika hoja hii tunachangia dakika kumi, kwa hiyo, dakika tano haziwezi kunitosha, *unless* nachangia dakika tano sasa hivi halafu dakika tano nitakaporudi!

**MWENYEKITI:** Basi acha nimpe mchangiaji mwingine.

Hakuna anayekubali dakika tano za Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nitishe shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 7.55 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

### HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Umbulla, atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza!

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niwe mchangiaji jioni ya leo kwenye Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji Wakuu wa Wizara ya Elimu, kwa kazi kubwa wanayoifanyia elimu ya nchi yetu ili hatimaye Tanzania iwe na elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeze Kamati ya Huduma za Jamii, ambapo mimi ni Mjumbe vilevile, kwa kazi kubwa ya kuishauri Serikali chini ya Mwenyekiti wetu mahiri, Mama Margreth Sitta. Hakika kwa mikakati yote ambayo imetolewa na Wizara na ile ambayo tumeishauri kama Kamati, naamini elimu itaboreka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nitoe angalizo kwenye Hotuba ya Waziri Kivuli. Nimesikitika sana kuona Waziri Kivuli ameibezwa slogan ya KILIMO KWANZA! Mimi nadhani sote tunajua kwamba, binadamu anaweza akaishi hata miaka mia moja bila kuwa na elimu ya darasani, lakini kamwe hawezi kuishi hata kwa muda mfupi bila kupata chakula. Kwa hiyo, nadhani ni wazi kwamba, Serikali ya CCM inapanga mikakati yake ama vipaumbele vyake kulingana na jinsi ambavyo wanaiona wananchi wake wanaweza wakanufaika kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa kwamba, KILIMO KWANZA kilipambana na mabadiliko ya tabia ya nchi; kwa mfano, mwaka juzi tulikuwa na mvua ya kutosha, maghala yetu yalifurika kwa chakula, lakini mwaka jana tumeona upungufu wa mvua isipokuwa hafi Mtanzania kutokana na tatizo la njaa. Kwa hiyo, Rais wetu aliona mbali kuona kwamba, ni lazima ahakikishe suala la njaa linakuwa historia katika nchi yetu, ndipo sasa na mikakati mingine kwa awamu zinazofuata za Chama cha Mapinduzi kutawala na nina hakika itatawala, itaamua sasa iendeleo na kipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kuhusu changamoto zinazowakabili Walimu wanapopangwa maeneo ya vijijini.

Naipongeze Kamati hasa ilipoona haja ya kuweka posho maalum kwa ajili ya Walimu wanaopangwa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu ambazo inafanya elimu iwe duni sana katika mazingira ya vijijini ni pale ambapo Walimu wanakuwa katika mazingira magumu. Fikiria Mwalimu kijana mdogo anapangwa vijijini, mahali ambapo hakuna umeme, hakuna mtandao wala mawasiliano, hakuna huduma muhimu, unategemea akae pale na aweze kuwafundisha wanafunzi na elimu ile iboreke, siyo jambo ambalo linawezekana kwa urahisi.

Naiomba Serikali, kwa jinsi ambavyo Kamati yetu imeshauri iweze kuhakikisha inatoa posho maalum na si posho tu bali vilevile iweze kufikiria jinsi ambavyo itawapa *refresher courses* Walimu hao wanaopelekwa maeneo ya vijijini. Hii itawasaidia sana pia kujiona wamethaminiwa na pia itawapunguzia maisha magumu ya mazingira yale ambayo wanaishi vijijini. Vilevile wataboresha taaluma zao kwa jinsi ambavyo watakuwa wamepelekwa katika *courses* hizo na

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

hatimaye itakuwa manufaa pia kwa watoto wetu waweze kusoma kwa amani na waweze kufanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la VETA, Kamati imetoa ushauri kwamba, iboreshe VETA kadiri inavyoona. Nami naunga nayo, lakini si VETA peke yake, tunalo tatizo la ajira katika nchi yetu. Njia pekee ya kukabiliana na tatizo la ajira ambalo ni janga la Dunia siyo janga la Taifa, ni jinsi ambavyo tutaweza kuwatoa wahitimu wetu kutoka VETA, lakini vilevile kutoka Vyuo Vikuu vyote, wale ambao watakuwa wanahitimu, waweze kutayarishwa kwa namna ya kujijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo pekee ya kuweza kukabiliana na tatizo la ajira. Nichukue fursa hii kukipongeza Chuo Kikuu Mzumbe, ambacho nadhani kama nakumbuka, walishaendesha kongamano la kujaribu kushawishi, Vyuo Vikuu katika nchi yetu viweze kuwatoa wahitimu ambao watakapohitimu siyo tu wawe wametayarishwa kwa ajili ya elimu ya kwenda kujijiriwa maafisini, bali kwa namna ambayo wataweza kujijiri pale ambapo watakwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utoaji wa fedha za Miradi; nitoe masikitiko yangu na hasa nikizingatia mimi nawakilisha Bunge letu kwenye Baraza la Chuo Kikuu Mzumbe. Inasikitisha kuona fedha zinazotolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Vyuo Vikuu vyetu hususan Chuo Kikuu cha Mzumbe, milioni 850, haikutolewa hata senti moja ilipofikia Machi 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasikitisha kwa sababu tunatarajia kuboresha Vyuo Vikuu, lakini vilevile Vyuo hivi vionekane bora kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kama mtakumbuka, tumekuwa na matatizo na changamoto nyingi zilizotokana na Vyuo Vikuu vyetu kugoma na mambo kama hayo, lakini Chuo Kikuu Mzumbe katika historia ya nchi yetu, haikuweza kugoma hata siku moja. Hii haina maana kuwa, haikuwa na changamoto, bali ni kutokana na utawala bora na pia kukabiliana na matatizo yanayojitokeza ili kuweza kuhakikisha chuo hicho kinakuwa *stable* na kinaweza kuhimili matatizo. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweze kuona ni namna gani kiasi kile kilichopangwa kwa ajili ya vyuo vyetu hususan Chuo Kikuu Mzumbe, kiweze kufikishwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu ukaguzi wa elimu. Mimi nafikiri ukaguzi ni jambo moja, lakini kufanyia kazi ama kutekeleza yale yanayotokana na ukaguzi wa elimu ni jambo la pili. Kwa hiyo, nashauri kwamba, ukaguzi unapofanyika na jinsi Kamati ilivyoshauri kwamba kuwe na chombo mahususi kuhakikisha ukaguzi unaboreshwa kulingana na jinsi ambavyo sasa hivi haijawa kamilifu vizuri; naamini kutokana na tafiti za ukaguzi, ndipo tutaweza kuboresha elimu yetu. Katika tafiti za ukaguzi tutaona upungufu uliopo, matatizo yaliyopo, mafanikio yaliyopo na kutokana na hayo yatakuwa yameonekana ndipo tutaweza kuona ni namna gani kutokana na ukaguzi wetu huo tuweze kuboresha elimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu kukosekana kwa Vyuo vya VETA Mkoani kwetu Manyara. Mkoa wa Manyara umegawanywa kutoka Mkoa wa Arusha na kama tunavyoelwa, unapogawa Mkoa mpya kutoka Mkoa mwingine, kuna tabia ya kusahau maendeleo ya Mkoa ule mpya ambao unaanzishwa. Ninasikitika kuona kwamba, sisi tumesahauliwa katika vipaumbele vyote hasa kuanzisha Vyuo vya VETA ambavyo vitaweza kusukuma ajira ya vijana wetu na hasa kuboresha mazingira ya vijana wetu kujijiri. Ninaishauri Serikali iutazame Mkoa wetu wa Manyara, kuona ni namna gani inaweza ikatuanzishia Vyuo vya VETA vya kutosheleza, kwa sababu tunaamini hii ndiyo njia pekee ya kuendeleza ajira ya vijana na kuondokana na ajira pungufu hapa nchini mwetu.



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, mimi nilikuwa na haya machache kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Mabumba ajiandae!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hatimaye kwa kunipa nafasi nami nianze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka rekodi sawa, napingana na mchangiaji aliyechangia asubuhi kusema vijana hawafanya kazi. Leo hii vijana waliomaliza Vyuho Vikuu hawapendi kutembea na vyeti mpaka vinachakaa, ni kwa sababu mazingira yetu hayajawawezesha vijana kujijiri kutokana na taaluma waliyosomea. Leo hii vijana vijijini hawana mashamba ya kulima, wana eka chache ambazo ni za kubangaiza tu kula wao na familia zao, tena mashamba ya mjomba, shangazi, baba au mama. Kwa hiyo, tunapotoa michango yetu tufikirie kwa kina sana suala la vijana, matatizo ya vijana ni suala la kidunia, suala la kiasia, ndiyo maana nchi za Waafrika wanakutana ni namna gani ya kutatua matatizo ya vijana ikiwepo elimu na ajira. Kwa hiyo, nasikitika nikiona michango kama hiyo halafu mwakilishi wao niko humu ndani nanyamaza kimya siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ubora wa elimu, hatuzungumzii kwamba Serikali hakuna walichokifanya, wamejenga shule za kata, tunakubali ni hatua nzuri. Naungana na Hotuba ya Kamati ya Mama Sitta, amezungumzia vizuri sana. Ukiacha mambo ya siasa, mbwembwe, nini, Hotuba pia ya Kambi ya Upinzani kuna mambo ambayo wamezungumza ya msingi tuyachukue tuyafanyie kazi. Nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Ndassa juzi alipokuwa akisema, kuna mambo mengine ya msingi wanayotoa wenzetu tuyachukue, zile mbwembwe za kisiasa tunaachana nazo ya msingi tunayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ubora wa elimu, hatusemi Serikali haijajenga shule za kata, kuna mambo ya msingi mengine tumepitisha humu ndani hayatekelezwi. Wabunge waliokuwepo tangu 2001 mnajua, kuna Sheria walipitisha humu mwaka 2001, tazameni Sura ya 412, kuhusiana na fedha kupeleka kwenye Mfuko wa Elimu (TEA). Ninavyozungumza, miaka kumi hawajawahi kupeleka hata asilimia moja; je, tuna dhamira ya dhati kwamba elimu ni kipaumbele?

Kama haitoshi, tumefanya *amendment* baada ya hoja ya Mheshimiwa Mwigulu hapa 2013, Sheria Na. 3, ambayo imetoa mchanganuo mpana na kusema, Serikali itenge asilimia isiyopongua mbili kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida ukitoa maendeleo na Deni la Taifa, hawajawahi kutimiza. Je, bado tunasema tuna dhamira kwamba elimu ni kipaumbele?

Hesabu ile miaka kumi, mwaka mmoja tu ndiyo wamepeleka 0.05; hivi kwenye ile miaka kumi fedha zingekuwa zinatoka tungekuwa tunazungumza hapa?

Tunapozungumza tuna uchungu na Taifa letu, tuko kwenye Dunia ya ushindani wa kitaaluma, tunataka vijana wetu waende wakashindane kwenye soko la ajira la kidunia kwenye msingi huu wa elimu ambao fedha hazitolewi halafu tuje tunyamaze tusifie!

Mwaka jana walipaswa TEA wapewe bilioni 185 hazijatoka hata shilingi moja, ndiyo maana vijana wanagoma vyuoni fedha haziendi kwa wakati. Hivi tunavyozungumza ndiyo maana tunawachangisha kule wananchi michango ya maabara ni kazi ya TEA, tuwape pesa hatuwapi. *(Makofi)*

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sasa tukisema tunafanya kazi kwa mazoea, hatutaki kufanya kazi kwa mazoea ndiyo maana tunasema mabadiliko kwa vitendo wakati ni sasa. Hatuwezi kufanya kazi kwa mazoea miaka kumi 0.05, tumefanya *amendment* tena hamjatenga! Hivi ninavyoongea, mwaka huu TEA mnatakiwa muwape bilioni 346 hamjawapa! Unapozungumzia TEA ndiyo *engine* kwenye Wizara ya Elimu, kama ambavyo tunazungumzia REA Nishati na Madini. Tutakuja kuwakaba tu hapa akina Mheshimiwa Kawambwa, mama yangu hapo Anna Kilango, hamuwapi hela. Kuna watu tu Wizara ya Fedha wanaweza wakapeleka milioni 900 kwenye anasa nyingine, TEA hawawapi fedha kwenye jambo la msingi. Milioni 300, milioni mia moja themanini na kwenye hiki kipindi tu hamjatenga, miaka kumi halafu tuiseme.

Unapozungumzia kuondoa tatizo la watoto wetu kukaa chini, jukumu hilo TEA wangepanya. Tunapozungumzia ujenzi wa maabara, TEA wangepanya. Tunapozungumzia leo hii kuhusiana na migomo ya wanafunzi, mngewapeleka fedha TEA wangepanya. Kuna mchanganuo hapa Bodi ya Mikopo asilimia 64, TEA asilimia 30, TCU asilimia 3, NACTE asilimia 3, haziendi. (Makofi)

Tutatengenezaje mazingira ya elimu yetu kuwa bora? Sisi Wabunge kazi yetu kuisimamia Serikali, haya ndiyo tunayosema hatuwezi Bunge likawa kama *rubber stamp* tu kuendelea kufanya kazi kwa mazoea, hatuwezi, lazima tubadilike. Mabadiliko ni vitendo, tuanze. Nashukuru kauli hii ilitolewa na mgombea anatoka Wizara ya Fedha, tuisubiri Awamu ya Tano tuanze sasa hivi. Hamuwapi fedha na mimi nitashika mshahara nipate majibu sahihi, tunatunga sheria, wasimamizi wa sheria hamtimizi, hamfuati zile sheria. Leo hii tuna matatizo watoto wanakaa chini, leo hii nyumba za Walimu hakuna, Walimu wako kwenye mazingira magumu, kwa sababu chombo ambacho kipo kisheria hatukipelekei fedha. Tunamsifia hapa Mheshimiwa Magufuli anajenga barabara, anapewa fedha. Sasa leo hii elimu hatuipi kipaumbele! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye Mkutano wa Viongozi wa Vijana Duniani, moja ya mambo ya msingi ni jinsi gani ambavyo vijana wanatengenezewa mazingira mazuri ya elimu ya ushindani. Hivi tunavyozungumza, Duniani, ni asilimia 25 ya vijana wenye ajira *permanent*, asilimia 13 ndiyo wenye ajira za mkataba, 65 ni hizi za kawaida. Sasa leo tujiulize; mfumo wetu wa elimu unaweza ukatoa mwanasheria akaenda kushindana katika ile asilimia 25? Mfumo wetu wa elimu tunaweza kutoa mwanataaluma mwingine akaenda ku-*penetrate* kwenye ile asilimia 13?

Lazima tutengeneze mazingira hayo sasa. Tanzania hatupo kwenye kisiwa, tupo kwenye ushindani, wote tutajisikia raha hapa tukiambiwa tuna ma-*lawyer* wako Marekani, wako wapi, ni bahati tu watu kama akina Mheshimiwa Mwigulu pale wali-*penetrate* wakafika hapa. Kwa misingi hii tunayoiweka ya vyombo ambavyo vinatakiwa vionyeshe ubora wa elimu yetu hatuvipi pesa tutaweza vipi? *Ten years* imepita tukabadilisha Sheria kama kawaida yetu, tumebadilisha hata senti tano hatujapeleka halafu mnasema watu wafanye kazi, wanafanya kazi vipi wakati hamuwapi pesa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa masikitiko makubwa, tunahitaji maendeleo, maendeleo hayawezi kupatikana kama hatuwezi ku-*invest* kwenye elimu vya kutosha, elimu yetu ikawa bora. Vile mnavyovifanya tunawapongeza, lakini tusicheze na elimu, tutarudisha ukoloni mamboleo. Kwa sababu wenzetu wataandaa wataalam kila siku watakuwa wanakuja hapa wageni kushika nyadhifa mbalimbali, hiyo siyo sawa, hatutolitendea haki Taifa hili, hatutowatendea haki Vijana wa Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia hilo kwa kirefu na nitahitaji majibu na nitashika shilingi. Hakuna kijana wa Chuo Kikuu anayependa kugoma, wote wanapenda kuandaa

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

maisha yao. Hivi ninavyozungumza, Mzumbe bado hawajapata fedha. St, Joseph wanafukuzwa kwa kudai haki yao! Wako mtaani watu wametoka vijijini, siyo *fair*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kuzungumzia hii dhana ya vipaumbele. Leo hii dhana ya Bodi ya Mikopo ni kumsaidia mtoto maskini. Kuna watu wametoka *dream* zao kuwa wanasheria, leo anaambiwa ukitaka upate mkopo kwa asilimia mia moja, nenda kasomee ualimu, nenda kasomee udaktari. Dhana hii inaondoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Ya kwanza ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Ya pili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Bulaya. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Suzan Lyimo, akifuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Mabumba na Mheshimiwa Maria Hewa ajiandae!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Nilitaka nianze na suala zima ambalo limepotoshwa sana ndani ya Ukumbi huu na Wabunge wa CCM, suala la Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia kusema, kama huna utafiti huna sababu ya kuongea ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza na bahati nzuri sana iko kwenye Kitabu cha BRN cha Wizara kwamba, walipoanza asilimia 53 ya Walimu ndiyo walionekana wanafundisha na leo imeonekana kama ambavyo nimesema na huu utafiti umefanywa na Twaweza. Kama mtu anaupinga aje na utafiti wake, kwa sababu utafiti unapingwa na utafiti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, hawa walimu ambao tumekuwa tunawalea humu Bungeni kwa muda mrefu, ni Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi imewafanya wawe wanauza vitumbua, imewafanya wawe wanatembea bila kuingia madarasani na ndiyo sababu utafiti unasema hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme ni kweli Walimu wanapata aza nyingi sana na katika hotuba zangu kama Waziri Kivuli toka 2006, nimekuwa nikingelea masuala ya Walimu. Kwa hiyo, tusianze kubabaishana humu ndani kwa kufikiri kwamba, Walimu hawa ambao mnawatetea leo hii watawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka niliweke vizuri ni suala ambalo Mheshimiwa Chilolo amelizungumza kwamba, CHADEMA hatuna hata Ofisi, kwa hiyo, hatuwezi kuchukua madaraka. Nataka nimwambie hivi, hata Ofisi hizo za CCM zote ni mali ya Serikali wakati wa Chama kimoja mlizipora kama ambavyo mmepora viwanja vya michezo. Kwa hiyo, msitambe na jambo ambalo siyo lenu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mambo mengi yamezungumzwa na ni wazi kwamba, mengi ambayo wengi wamechangia hayako wala kwenye Wizara ya Elimu, kwa sababu tunajua kumekuwa na ugatuaji. Kwa hiyo, nitaenda *specific* kwenye masuala ya Wizara ya Elimu na ninaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu mnisikilize kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumzie suala la matatizo ya Vyuo Vikuu hapa nchini. Nimesoma kidogo kwenye risala lakini naomba niongee ili niweke uzito na Waziri aje atupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Vyuo vya Elimu ya Juu hasa Vyuo Binafsi na nitazungumzia *specific* vyuo vitatu; Chuo cha IMTU, Chuo cha *Kampala International University* na Chuo cha St. Joseph cha Arusha na cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya vyuo hivi yanajulikana kwa muda mrefu sana na mimi binafsi nimelifuatilia suala hili, nimeenda TCU nimedanganywa sana na watu wa TCU kwamba, tutaenda lakini hatukwenda. Baada ya kuona yote haya, nikaona mimi kama Waziri Kivuli na Naibu wangu, Mheshimiwa Nassari, pamoja na kwamba hatuna rasilimali kama Serikali ilizonazo za magari, tulitumia magari yetu kwenda mpaka Chuo cha St. Joseph. Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba, nilimpa taarifa, lakini vilevile Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi amempa taarifa za matatizo ya St. Joseph.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo hii tunapongea, bado matatizo hayajatatuliwa. Tukaambiwa Tume itaundwa, tulikuwa kwenye Kamati ya Huduma za Jamii *two weeks ago*, wameenda Maprofesa Chuo Kikuu cha St. Joseph; na nieleze tu kwa masikitiko makubwa, bahati nzuri *Report* ninayo hapa, hakuna chochote kilichofanyika, hawakuwaona wanafunzi, wamekula hela bure. Jambo la ajabu, Chuo kile kwa taarifa za Waheshimiwa Wabunge, kinatoa *courses* za ualimu wa sayansi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukudhihirishia kwamba, hawakufanya kazi wanatuletea matokeo kwamba pale mwanafunzi anasoma somo moja tu la kufundishia. Kwa utaratibu, mimi ni Mwalimu na Walimu wataniunga mkono, haiwezekani mwanafunzi asome somo moja la kufundishia, ni lazima asome masomo mawili; lakini maprofesa hawa ambao ni wasomi wanatuambia wanafanya hivi ili kupunguza tatizo la walimu! Hivi mwalimu mmoja anayesoma masomo mawili ya kufundishia na mwanafunzi mmoja anayesoma somo moja la kufundishia, yupi ambaye atasaidia zaidi kupunguza tatizo la Walimu wa Sayansi? Kwa hiyo, hayo ni matatizo makubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tatizo la *Kampala University*, tulizungumza mwaka juzi kwamba, Tanzania inaweza kuwekwa kwenye Kitabu cha Maajabu ya Dunia na leo narudia, tunapeleka huko huko nchi hii. Nitaomba Waziri atuambie, inawezekanaje mwanafunzi anayesoma *PCM*, anayesoma *GHL*, aje asomee *pharmacy*? Haya ndiyo mambo yanayotokea katika Chuo cha Kampala. Inawezekanaje mtu wa *arts* aende akasome kozi inayoitwa *briging course* kwa muda wa miezi mitatu halafu aje awe Mfamasia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu Bodi ya *Pharmacy*, ambayo barua yake ninayo hapa, wamegundua kwamba, kuna wanafunzi ambao hawana viwango vya kusoma katika fani ya famasia. Ndiyo sababu mpaka leo hawajapata leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka TCU ituambie; ilikuwaje ikawapa *admission* wanafunzi ambao hawana viwango vya kwenda pale? Watuambie pia ni kwa nini kumekuwa na hiyo *system* ya *central admission* lakini vilevile Chuo cha Kampala kinaingiza watu bila kufuata

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

system hiyo na ndiyo sababu inachukua wanafunzi wa *form four* waliopata *division zero* na wa *form six* waliopata *division zero* kwa kozi inayoitwa *bridging course*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kina *capacity* ya wanafunzi 30,000, tunavyoongea sasa hivi kina wanafunzi 20,000. Kwa nini tunapeleka wanafunzi kwenye vyuo hivi binafsi ambavyo havina viwango tunaacha kuwapeleka kwenye Vyuo vya Serikali kwa sababu kama wamekuwa *admitted* maana yake wamefikia *minimum qualification*? Kwa nini tunaanacha nafasi hizo tunaenda kupeleka wanafunzi ambao hawastahili? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka majibu ni kwa nini Serikali kama *Kampala University* inafuata mitaala ya Uganda, ni kwa nini Kodi za wananchi ziwaliapie wanafunzi ambao kimsingi hawawezi kuja kufanya kazi Tanzania? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa St. Joseph, Prof. Kitila Mkumbo, alitumwa ameenda kufanya kazi pale, ameangalia na amekuja na changamoto na Ripoti iko Wizarani. Nimeomba kwa nini Ripoti hii hailetwi kwa sababu na wao wanafuata Mtaala wa Kihindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mwanafunzi atoke St. Joseph aende akafundishe somo moja! Kwa hiyo, tunaomba, kama Bodi ya Mikopo inawapa mikopo watu wa namna hii, maana yake ni nini? Kama siyo, tunataka kujua uswahiba wa Serikali na hivi vyuo, kwa sababu Vyuo vyetu vya Serikali viko *empty*; kwa nini hatuwapeleki kule tunawapeleka kwenye vyuo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa wale waliopita Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanajua, tunaposema *VD* siyo *veneral diseases* ni viango duni. Watu wa *TCU* wanasema waliopeleka kwenye vyuo hivyo ni wale wenye viwango duni. Sasa tunataka watuambie; kama *minimum qualification* ni 4.5 hawa inawezekanaje ni viwango duni? Kwa sababu nimechunguza, kuna wanafunzi wanaosoma Muhimbili, wanaosoma Bugando, ambao kimsingi wana *point* ndogo kuliko wanaosoma *Kampala University*, kwa hiyo hiyo siyo hoja.

Kwa hiyo, tunataka kujua ni kwa nini na kwa msingi gani wanafunzi wanasajiliwa katika Chuo cha St. Joseph na Chuo cha *Kampala University*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia suala la siasa vyuoni. Kumekuwa na hii migomo mbalimbali na mara zote kupitia hata Waziri mhusika anasema ni mambo ya kisiasa; lakini niseme, niliuliza swali hapa Bungeni kuhusiana na siasa vyuoni na mashuleni, Mheshimiwa Waziri Mkuu Pinda alijibu akasema; mtoto wa nyoka ni nyoka! Kwamba, hata chipukizi wao wanawafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili halikubaliki, lakini kubwa zaidi wanafunzi wanaosoma kwenye Vyuo Vikuu wakijulikana tu wana mlengo wa ki-UKAWA inakuwa ni tatizo, lakini haliishii hapo tu, hata sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano wangu binafsi; mimi ni Mfanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mheshimiwa Esther Matiko, *Lecturer* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Cha ajabu, nimeingia kwenye Bunge hili 2005 sikufanyiwa sherehe na Chuo Kikuu, 2010 wameingia Wabunge wawili; Mheshimiwa Mukangara na Huvisa, wanafanyiwa sherehe lakini naandikiwa mimi eti niende nikawapongeze! Nikawambia *over my dead body!* (Kicheko/Makofi)

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Chuo Kikuu kipo katika Jimbo la Ubungo na Ubungo inatawaliwa na CHADEMA, lakini Mnyika kama Mbunge wa Jimbo hakualikwa. Tunataka kujua hizo fedha zilikuwa za CCM au za Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalimu Susan Lyimo, Waziri Kivuli. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Sylvester Mabumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Hewa na Mheshimiwa Margareth Mkanga ajiandae!

**MHE. SYLVESTER MASELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupa nafasi ya kuongea katika mjadala huu unaoendelea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaongea ambayo nimepanga niyaongee, napenda niongelee jambo moja. Kama mnakumbuka, hivi karibuni Chama cha Walimu Tanzania kilifanya mkutano wake na Rais Dkt. Kikwete alialikwa na Rais wa Chama kile, Ndugu Mkoba, huku akijua Rais Kikwete ni Mwenyekiti wa CCM; lakini kwa imani ya Chama cha Walimu kwa Rais wetu, walimwalika na kama angelikuwa amesababisha Walimu kuza vitumbua, chama kile kisingemwalika. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, Walimu wana imani kubwa sana na Serikali hii ya CCM inayoongozwa na Dkt. Kikwete. Kwa hiyo, kusema Walimu wanauza maandazi, sijui nini, huku ni kuwakashifu Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema wazi kwamba, Walimu hawa ni wataalam sana, wanajua nani anaongea ukweli na nani ni mshabiki hapa. Wasitafute kura za urahisi urahisi hapa, Walimu hawako pamoja na waandamaji wa maandamano yasiyoisha kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpungeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa Hotuba yao nzuri, ambayo wamewasilisha hapa, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wanachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nataka niongelee mambo machache sana. Moja, Idara ya Ukaguzi wa Elimu. Tunapozungumzia ubora wa elimu na kuhakikisha elimu yetu inaendaa vijana ambao baadaye baada ya kumaliza masomo yao wanajijiri, inatokana pia na kukaguliwa mara kwa mara. Hivyo, napenda kuiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Elimu kwamba, isimamie ubora wa elimu ili vijana wetu wanapomaliza masomo yao, waweze kujijiri katika sekta binafsi. Haya yatawezekana tu iwapo Serikali, kwa mfano, sasa hivi niipungeze kwa kujenga maabara nyingi, lakini maabara hizi bila kuwa na vifaa hazitafanya kazi.

Niungane na msemaji aliyepita, aliyezungumzia habari ya kuwepo vitabu vya kutosha, kuwa maktaba, ambazo wanafunzi wetu katika *level* mbalimbali wataweza kufanya rejea na hivyo kujiandaa vizuri kwa masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu Sera nzima ya Elimu. Nataka kujua, katika Sera ya Elimu tumesema tunataka kusomesha vijana wetu kutoka elimu ya awali mpaka ya juu kwa Lugha ya Kiswahili. Nataka kujua ni lini hasa Serikali itatekeleza Sera hii kwa vitendo, kwa sababu siyo kweli kutokujua Kiingereza ndiyo utakuwa mbumbumbu wa elimu. Wengi tumetembea hapa, kuna Wachina, wengi wao kiingereza hiki hawakijui, lakini wamefanikiwa sana katika teknolojia na wengi tunajivunia China, tunaisifu China. Ukienda Korea ya Kusini, Kaskazini, ukienda pia India, Japani, ni Mataifa ambayo yameendelea sana. Sasa tuangalie kama Kiswahili kitawezesha vijana wetu kujifunza kwa uzuri na kuwaelewa Walimu wao, basi

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikali itamke, tusiweke katika maandishi tu; Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie Sera hii wanaanza kuitekeleza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunapenda sasa tuwe na vitabu ambavyo vitatosheleza kwa masomo yote, kwa maana ya masomo ya sayansi katika Lugha ya Kiswahili, lakini pia *Computer* ambazo zitakuwa zinaweza kuwasaidia kwa Lugha ya Kiswahili ili wanapofundishwa waweze kufahamu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili elimu yetu ifanikiwe, Serikali inahitaji kuwekeza sana katika elimu. Leo hii ni aibu bajeti yetu kubwa iko katika matumizi ya kawaida. Sasa unapokuwa na bajeti kubwa ya matumizi ya kawaida, maendeleo hayawezi kufikiwa. Tukumbuke tuna Dira ya 2025, leo ikiwa ni mwaka wa 2015, bado miaka kumi. Tujitathmini Dira yetu tunaifikia kama ambavyo tulitarajia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iangalie upya bajeti yake. Waziri wa Fedha alipozungumzia bajeti ya mwaka huu trilioni 23, trilioni tano tu kwenye maendeleo, kwa hiyo, haiwezi kutusaidia. Vyuu Vikuu vyetu vinahitaji fedha nyingi wa ajili ya utafiti. Mimi ni Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria, Chuo Kikuu Huria kinadai karibu shilingi bilioni moja katika fedha za maendeleo kwa muda mrefu hakijapewa. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri; ni lini madeni haya ambayo Vyuu Vikuu vyetu vinadai yataweza kulipwa na hivyo kuwawezesha watafiti, Maprofesa kufanya kazi yao ya kiutafiti?

Haiwezekani ukawa na wataalam lakini huwawezeshi, hawawezi kufanya utafiti ambao utachangia maendeleo ya nchi yetu. Naomba Serikali ikae chini itathmini na pia naiomba Kamati ya Bajeti iangalie na kuishauri Serikali ipasavyo kwamba, elimu lazima iwekewe bajeti ya kutosha na ndiyo maana utakuta Maprofesa wengi wameacha kazi ya ualimu na kuingia kwenye siasa. Tuna Maprofesa wengi humu ndani, tungewawezesha hawa katika Vyuu Vikuu kule, wangeji-engage katika kufanya utafiti na hivyo wasingekimbilia siasa hizi. Kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe inapeleka fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu ambao nimewasifu kwa mapenzi yao kwa Rais wetu na kwa Chama cha Mapinduzi, tuendeleo kulipa madeni yao. Walimu wanatakiwa wafanye kazi katika mazingira mazuri. Katika *process* ya kuanzisha Benki ya Walimu, naiomba Serikali ielekeze Halmashauri kutenga asilimia fulani ambayo itaenda katika Benki hii ya Walimu wapate mikopo kwa masharti nafuu na kuwaondolea shida zao.

Siku zote tunasema ualimu ni wito, kweli ni wito lakini wanatakiwa kuboreshewa mazingira ya kazi. Walimu ni nguvu kazi ambayo tunahitaji kwa kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu. Tusipofanya hivyo, itakuwa ni kazi bure, ambapo Walimu wakifundisha kwa manung'uniko haitasaidia.

Mwisho, nizungumzie habari ya madawati. Napenda kuiuliza Serikali ni lini hasa itaondosha kero hii kwa sababu kama wanafunzi wataendelea kujifunza wakiwa wameketi chini, uwezo wao kujifunza utakuwa umeathirika katika sehemu kubwa sana. Kwa hiyo, nashauri madawati yapelekwe katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu vitabu vya chenji ya rada. Ziko Halmashauri nyingi hapa nchini hazikunufaika sana. Napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atuambie ni Halmashauri zipi zilipata vitabu hivi na zipi bado hazijapata na atupe maelezo kwa nini vitabu hivi havikupelekwa wakati Bunge lako Tukufu lilielekeza vitabu hivi vipelekwe.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, ninakushuru sana. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ninamwita Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Margareth Mkanga ajiandae na Mheshimiwa Faki Makame!

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii finyu ambayo na mimi nimeibahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Nina imani na Shukuru Kawambwa na hasahasa nina imani na rafiki yangu Anna Kilango huyu, ni mtani wangu mkubwa, lakini hata Taifa linajua limepata jembe. Anna Kilango Malecela, hakuna asiyemfahamu na Watanzania wanaamini Wizara imepata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, napenda kusema yafuatayo:-

Mimi ni zao la wazazi Walimu. Kwa hiyo, siri za Walimu pamoja na kwamba mimi sikuwa Mwalimu, lakini kwa vile nilikuwa naishi na Walimu, wazazi wangu; Martha Ibeshi Mathias na Lukas Sengasenga, napenda kusema yafuatayo:-

Walichokuwa wananiambia na jinsi gani wenzetu wa Upinzani mnapobeza hatua tuliyofikia, kwa kweli nawashangaa sana; yaani *as though*, bado tuna elimu ya kikoloni, hapana, tulikotoka ni mbali na ni mbali sana. Mama yangu aliishia darasa la sita akawa Mwalimu kwa masharti ya wakoloni, baba yangu akaishia la nane kwa masharti ya wakoloni. Wale wa zamani, waliotuzaa sisi bado wapo na wanawasikia uongo mnaosema kana kwamba Tanzania haijatoka mahala ilipo, *is a shame to you jamani!* *(Makofi)*

Niombe kabisa jamani, tukosoeni tu mahala tulipofikia, upungufu unaojitokeza ndiyo muuseme jamani, lakini si kwamba eti Tanzania na elimu ni zero, eti ni sifuri, *no*, hapana nasema! *(Makofi)*

Tukosoeni tu mahala tulipofikia, lakini si kwamba hatujafanya kitu, tumefanya na tumefanya na Watanzania wanaelewa kwamba, tumefika mahala CCM iendelee kuaminika, CCM iendelee kuwa madarakani na CCM ndiyo chama pekee ambacho kinaweza kikaeleweka kwa Watanzania. *(Makofi)*

Nasema yafuatayo; kwa vile nilisema, tuendelee tu kuambizana kwamba, tulikotoka kulikuwa kugumu, kugumu na mpaka tumefikia hapa walau sasa ni palaini na Watanzania wanasoma wakiwa ndani ya uhuru ulioletwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo watu wanasema, ninyi mnasema hao wanaosema na kubeza Elimu ya Tanzania. Ninyi fikirieni jamani, hata Watanzania wanajua, walemavu kama walemavu, walikuwa wanafichwa ndani hawawezi hata kutoka. Walemavu wapo wa aina mbalimbali, lakini kwa juhudi za Watanzania na Uongozi, tena na ninyi mmo humu, tumefanya kila jitihada ndani ya Chama cha Mapinduzi, walemavu wametoka wanasoma, hawafichwi tena; unadhani ni kitu kidogo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu klikubwa sana, walikuwa hawawezi hata kutoka tu, lakini kwa Sera za Chama cha Mapinduzi, wameweza kutoka, wameweza kuelimishwa. Kwa hiyo, katika hali hii ongezeko la wanafunzi linakuwa wengi na kwa wale ambao walikuwa hawawezi kabisa kutoka na kusoma, leo wanatoka, leo wanasoma, wako maprofesa walemavu, wako



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

watu wenye *Ph.D* walemavu, wako wa kila aina. Leo mnasema sisi CCM tumetulia tu, *quite please!* (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, kuhusu masuala ya Walimu sasa, naleta maombi, kengele imeshagonga ya kwanza, jamani, Tanzania hii imeweka mahusiano mazuri hata na shule za *privates*, vikiwemo vyuo vya ualimu. Jamani kuna Walimu rundo waliofuzu kufundisha *kindergarten*. Tunalia hatuna Walimu wa kufundisha *kindergarten*, tafadhali, tafadhali, tafadhali, wako rundo, wanapomaliza wanadakwa na hizi *primary schools* za *private* na ndiyo maana tunasifu shule hizi, kwa sababu wenyewe wanawathamini, kwa nini sisi hatuwathamini? Wabebeni wako rundo, muwasambaze kwenye shule zetu za misingi. (Makofi)

Mimi nina uzoefu huo kwa sababu hata mimi nina mtoto wa mpiga kura wangu ambaye ametokea mikononi mwangu amemaliza hapo. Naomba hebu tangazeni, mtawapata wako wengi sana, wakatufundishie *kindergarten* kabla ya kuanza darasa la kwanza.

VETA, jamani viwanja watu wameshanunua, vipo kwenye Halmashauri zetu. Hivi mafungu yale mliyotenga kwenye bajeti iliyopita yameishia wapi? Simameni mliokuwepo humu ambao milioni hiyo bajeti halafu mambo yaka-cease, muwaseme hapa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni madawati. Kama Rais ameweza kuhamasisha maabara zikajengwa, sasa hivi anahamasisha madeni yote ya Walimu yalipwe na *so long as* amesema yeye, mtayalipa tu mtake msitake. Walimu jueni hilo, maana ametumia chombo chenu, kwa hiyo, muwe na amani na madeni yenu yatalipwa. Je, madawati yasimamiwe na nani mpaka tumsubiri tena yeye na yeye ndiyo animaliza muda wake? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, jamani ile *issue* ya watoto wanaochukua sayansi, wanaojitolea kuchukua sayansi hasa wasichana, jamani zoezi halijawa vizuri! Bado mnabeba rundo la watu wenye *arts*, mnawaacha wanatulilia wanasema, Mama Hewa, mbona mmesema tuchukue sayansi, matokeo yangu ya sayansi haya hapa! *I am being left behind*, wanabebwa wasio wanasayansi, mnaanza tena kukatisha tamaa. Hapana, naomba hili na liwe kweli *in practical*. (Makofi)

*Last*, mazingira magumu ya Walimu, lipeni, tafuteni mafungu, hivi hayapo? Hakuna kweli mafungu ya kulipa Walimu wanaofundisha katika mazingira magumu? Tulilahidi hilo humu, hebu leo Shukuru Kawambwa, tena nakusema sasa kwa jina, mtani wangu, uniambie mazingira magumu maana yake nini na Walimu wako huko waa hali ngumu, hawajalipwa kabisa sijui niite nini, *bonus* au niite posho eti ya mazingira magumu, kama ni kindengereko uniambie leo? Kwa nini hamtaki kuliweka sawa hili suala la walimu wanaofundisha kwenye mazingira magumu?

Mbunge mwingine amesema hapa, wanalala kwenye tembe, hawana usafiri, hawana barabara, hawana maji, hata pikipiki hawana. Nini maana ya mazingira magumu Mwalimu anapokuwa nje ya mambo hayo ya kum-*harmonies* na yeye akaonekana ni sawa na Mwalimu wa Mwanza Mjini?

Naomba mtuambie leo na wao wasikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, wapandisheni Walimu vyeo wakati vyeo vyao vinapostahili. (Kicheko)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maria Hewa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishia hapo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Sijaunga mkono hoja nimeunga mwanzoni!

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Margareth Mkanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Faki Makame!

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja muhimu ya elimu, mimi mwenyewe nikiwa Mwalimu, tena Mwalimu mzoefu kabisa na matunda mnayaona humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa wanaoendesha gurudumu hili la elimu nchini hapa, wawili, wanajitahidi sana pamoja na kwamba, wanafanya kazi katika mazingira magumu, fedha ndogo na mengineyo yote na mzigo ni mzito, vyo vyote, sijui nini, kwa kweli wana kazi na bila fedha matatizo matupu.

Nikiwa kama Mwalimu naanza na umuhimu kweli wa kumaliza suala la Tume ya Utumishi ya Walimu. Mimi ni wa enzi hizo, tulikuwa chini ya Tume kama hizi hizi; vyeo vilikuwa vinaenda vizuri tu, ukikosa unaadhibiwa na nini, hebu rudisheni tena haraka. Kwa hiyo, hiyo ile Sheria tuliyoisoma mara ya kwanza hapa, mimi naamini kabla hatujamaliza uwanja huu hapa, ile sheria itapita na hiki chombo itarudi tena, tena kwa uzuri zaidi, kwa sababu kitu kipya mtakuwa mmeshaki-*modify* sawasawa kuliko hata sisi wengine tulikokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BTP*, ni muhimu sana Walimu Tarajali waende kujifunza, sisi tulikuwa tunaenda miezi mitatu, unatetemeka siku za kwanza, baadaye unakuwa Mwalimu mlemle kwa *practical* ukitoka hapo Mwalimu umeiva. Sasa hivi hayapo, anatememeka darasani, watoto wanamcheka, wanamwona ni kituko. Kwa nini fedha za *BTP* hazitolewi zikahifadhika ili muda ukitimia watoto hawa waende? Vinginevyo, mnawatoa hawajaiva na mkiwatoa hawajaiva, hawafundishi kikamilifu.

Sitalaumu kwamba mtu anaenda kuuza maandazi, kwa sababu ualimu wenyewe ni nusunusu, haujamwingia, hamjamkolezea. *Teaching practice* ni muhimu mno kwa Mwalimu, *failure to do that* kwa kweli hakuna tunachokifanya. *BTP*, na fedha wapewe waende mazoezi miezi mitatu, mmeshindwa sana basi miwili. Mimi nilipita mitatu na nikawa mwalimu mzuri tu nimesema, matunda mnayaona humu, bila *BTP* ningewezea wapi mambo hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ningependa kuishukuru Wizara, imesema katika ukurasa wa 61, inaandaa mwongozo wa miundombinu na vifaa kwa watoto wenye mahitaji maalumu; ni vyema, naomba yasiwe kwenye maandishi haya, yatekelezeni. Mpaka sasa hivi pamoja na maneno mazuri haya, hawa watoto wenye mahitaji maalumu mashuleni, ruzuku ni kidogo na hiyo hiyo kidogo inachelewa kuja, kiasi kwamba, hata walimu jamani inasikitisha eti huwa wanajitolea kujichangisha changisha, kusudi watoto hawa wawanunulie unga wawapikie uji jamani!

Mwalimu huyu hana tunajua, lakini anajitoa kwa upendo wa watoto hawa kuchangishana fedha wakapika uji kwa ajili ya wale watoto. Kwa sababu kuna aina ya ulemavu, usipompa uji, yaani njaa ikiingia hawaelewi lolote wanageukia kushoto, kulia, inategemea aina ya ulemavu. Tafadhali, pamoja na kwamba ni fedha ndogo, haya

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

mliyoyasema mnaandaa sijui miundombinu na vitu gani, timizeni. Ruzuku zifike kwa wakati katika vitengo hivi ambavyo vingi tumeshavisambaza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia waliyoyasema wenzangu, kisiasa ukiona kitu kinasemwa sana, hebu kitafute kina ukweli wake hiki. Umuhimu wa Kitengo cha Elimu Maalumu kule Wizarani, sijui kipo Wizarani sasa, sijui kipo TAMISEMI, Mungu wangu hata sielewi, mtanisaidia hapo baadaye. Kitengo hiki kisiwe kitengo, watoto hawa sasa wengi wameshatolewa na wazazi, kama mzungumzaji alivyosema, wanakwenda shuleni na Serikali mmehimiza kwamba, kila shule pawe na kitengo cha watoto kama hawa angalau wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Wanatoka hawa wako wengi, kitengo tu hakisaidii, wekeni iwe idara maalumu, itakayoweza kuchanganua na kuchambua yote yanayohusu watoto hawa. Vinginevyo, hapa tunaongopa na huenda ndiyo hiyo idara ingehimiza hata hayo mambo ya ruzuku yafike mahali, ili watoto hawa waweze kupata haki zao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko chini ya Wizara, Serikali ni hiyo hiyo moja. Nasisitiza umuhimu wa ujenzi wa mabweni na hosteli jamani. Watoto wa kike hawa tunajua, mwanzo huku wanaanza vizuri wote, jinsi wanavyoendelea wanakwapuliwa kwapuliwa hapo katikati. Moja ni haya haya matatizo, umbali wa shuleni na nini na nini, jengeni, yaani hii nayo iwe ni operesheni, kama ya maabara nadhani nayo hii tuifanye operesheni kabisa. Kila shule iliyochaguliwa angalau iwe na bweni na hosteli, iwe ni muhimu hasa kwa watoto wa kike, kwa sababu tunajua wanayopambana nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kufahamu, hivi karakana inayotengeneza karatasi maalumu za *brail* pale Shule ya Uhuru Mchanganyiko ipo imekufa? Maana *brail papers* ni tatizo katika shule zote ambazo wenzetu wasioona wanasoma, hii karakana imekufa kabisa; tunashindwa kuifufua?

Mimi naomba nipatiwe *status* yake ndipo niweze kulaumu au kushauri, lakini ilikuwa ni kitu muhimu sana, kilikuwa kinasaidia hata ku-save fedha, karatasi zinatoka pale kwa urahisi rahisi, mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho naomba kufahamu ni mfumo wa elimu jumuishi. Mwenzangu alieleza vizuri tu mchana, lakini nataka tujipe kazi kidogo, hebu tujaribu kufanya utafiti kidogo, mfumo huu umefanikiwa vipi tangu tuanze hapa nchini Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni ilikuwa *experiment*, yaani jaribio, je, mfumo huu umeshaenezwa katika shule zote nchini hapa au mambo yanakwendaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa hilo la utafiti tuone, kama tunaenda vizuri au kuna matatizo. Pamoja na kwamba, mengi yanaweza yakawa mazuri, lakini hebu tucheki pia yale matatizo yake tuweze kuyafanya vipi. Kwa sababu elimu jumuishi, bila Walimu wa kutosha, wa taaluma ya elimu maalumu, mbona inakuwa tatizo, maana haki yake darasani pawe na *sign language* ya *teacher*, pawe sijui na akina nani; hivi hao tunao wa kutosheleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niendeleo kuwapa pongezi pamoja na matatizo, haya ambayo yamesemwa katika pande zote mbili, Kamati kubwa iliyojadili wameeleza vitu vizuri na huku wenzetu. Yale mazuri okoteni, ili mya-*combine* hayo, ni kwa manufaa ya nchi yetu, tuweze kufika vizuri katika maendeleo ya elimu.

Miundombinu iwe sahihi ngazi zote, tangu msingi mpaka Vyuo Vikuu, vitabu vyao, madaraja yao. Vyuo Vikuu huwa kuna kitengo kabisa kinawashughulikia watu wenye ulemavu

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

na nini, nacho mkifadhili muweze kukiona kinakaa sawasawa, kusudi wanavyuo nao waweze kusoma vizuri, kwa *challenges* chache kuliko.

Nikushukuru Mheshimiwa Kawambwa, ulinisaidia sana wanafunzi wangu wawili wa UDOM, ambao waliingia kwenye matatizo, eti hawapewi mitihani ada. Sasa na wale wenzangu mimi mbendembende, ndiyo haya haya ya mikopo haya, ada rahisi hivyo wanapata wapi, lakini ulilifanyia kazi, wamekushukuru sana na mimi mwenyewe nakushukuru, kwa sababu sasa wanaendelea vizuri kusoma wale kwa amani kabisa, mitihani wameshaletewa matokeo yao, wanaendela vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nawashukuruni sana kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalimu Margareth Mkanga. Sasa namwita Mheshimiwa Faki Makame, atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda!

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie chochote kuhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Nachukua nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, halafu nilishukuru Baraza langu Kuu la Taifa la Chama cha CUF kwa kunitewa kuwa mgombea katika mwaka 2010. Nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Mtoni wakanipokea wakanichagua kwa kura nyingi sana. Nawashukuru kwa sababu tumeshirikiana vizuri mpaka hii leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, labda niseme kidogo kuhusu elimu. Sote tunafahamu ndani ya hili jengo kwamba, elimu ndiyo kila kitu. Kila anayesimama anasema bila elimu hakuna afya, bila elimu hakuna *engineers*, bila elimu hakuna masuala mengine yoyote. Hata vitabu vya dini vinasisitiza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Muislam, lakini katika Kitabu changu cha Dini cha Quran kinasema, amri ya kwanza aliyopewa Mtume wetu Muhammad *Swalallahu Alayhi Wasalaam* ilisema; "*Iqra bismirabbika ladhi khalaqa.*" Sasa kwa tafsiri nyepesi yangu mimi ya juu juu anaambiwa wewe Muhammad wewe soma na usome kwa jina la Mola wako ambaye amekuumba. Maana yake kila unachokitenda umuweke mbele Mungu. Sasa na Wizara hapo ulipopewa kila unachokifanya ujue kwamba, unaelimisha kwa ajili ya Mungu, Mungu aridhike, hiyo ndiyo maana yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka tuchukuane twende zetu hapo UDOM, UDOM pana Miradi mingi lakini mimi ningesema miwili tu. Kuna Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Sayansi Asilia na Hisabati; na ujenzi wa Chuo cha Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, allocation ya bajeti inasema mahitaji ni bilioni 104 ili Mradi huu uweze kwenda, lakini allocation inaonekana kwa mwaka huu ni bilioni 1.5. Kwa kweli hawana miujiza ya kufanya wakaweza kujenga hata kidogo na itawachukua zaidi ya miaka sitini kuweza kukamilisha Miradi hii miwili. Tunachoshauri, tunaomba basi angalau kila mwaka zipelekwe bilioni sita ili angalau wazigawe tatu kila Mradi na ichukue japo miaka ishirini lakini kimalizike. Huo ndiyo ushauri wangu. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na wazabuni; wazabuni sehemu nyingi wanalalamika na imekuwa tatizo. Moja ya kuviza elimu ni suala la wazabuni. Kwa mfano, watu wa Tabora wanalielewa vizuri hili, walishawahi ku-experience namna yalivyowatesa madeni ya wazabuni. Kagera kule kuna mifano; kwa mfano, Rugambwa Secondary School, haya majina magumu kidogo na Kahororo Secondary School, zimewahi kufungwa kwa tatizo la madeni ya



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sita. Huyu ni Mwalimu ambaye alipitia mafunzo ya ualimu kamili kama alivyowaambia ya miezi mitatu, leo mimi niko hapa, kama ninafanya vizuri mimi ni matunda yake. Nakushukuru sana Mama Mkanga kwa kunifikisha hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba niunge mkono Hotuba ya Kamati ya Huduma za Jamii, mimi nikiwa ni Mjumbe. Naiunga mkono pia Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, ameongea mambo mazuri sana, hakuweka siasa, Wizara mkiyaangalia kwa umakini, kwa kweli mwaka ujao tutakuwa hatuzungumzi haya tunayozungumza, itakuwa ni makofi na vigelegele kwenye Wizara hiyo. Naomba myachukue myafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye ukaguzi. Tumezungumza kama Kamati, wamezungumza wachangiaji na Kambi Rasmi ya Upinzani pia imezungumza. Kamati tumekuwa tukishauri kila wakati kwamba, Ukaguzi wa Shule uwe Wakala unaojitegemea ili tuondokane na mporomoko wa ubora wa elimu. Mkituangalia hapa wote ni Watanzania, tuna nia njema kabisa na elimu yetu ya Tanzania, hakuna siasa kwenye elimu. Mtoto wa Kitanzania anayekwenda shule haangaliwi ni wa Chama gani ila ni mtoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ya Elimu na ninasema leo hapa nitanyofoa shilingi kama hamjaniambia mtaleta lini Muswada wa kufanya Idara ya Ukaguzi iwe wakala inayojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ninayasema kwa sababu Msemaji wa Kambi amezungumza hapa, hii imeleta mgogoro kwa wachangiaji wengine, katika page yake namba 28 akizungumzia jinsi ambavyo Shirika la Twaweza limefanya utafiti wake na kuja na matokeo kwamba, kabla ya BRN, asilimia 53 ya Walimu walikuwa hawapo darasani. Baada ya BRN asilimia 34 tu. Wanasema inaonekana kuwa hivi sasa ni asilimia 34 tu ya Walimu ndiyo wanaoingia na kufundisha darasani. Hakusema Walimu hawafanyi kazi, amesema utafiti wa Twaweza, baada ya Serikali kutowapa motisha Walimu kutokana na Matokeo Makubwa Sasa, imewavunja moyo Walimu sasa hawataki kufanya kazi yao sawa sawa. Walimu wana mgomo baridi kama hamfahamu. Sisi akina Mama Margareth Mkanga walikuwa hawana mgomo baridi kwa sababu walikuwa wanafahamu kazi zao, ndiyo maana sisi tuko hapa. (Makofi)

Nimetoka Msalato shule nzuri, mmesema *giant school*, nimetoka Msalato nimwekwenda Kilakala, zote ni *giant school*, mtaniangalia hapa. Walimu wale walikuwa wanapata angalau motisha kidogo walikuwa wanathaminiwa, sasa hivi mmesahau. Kwa hiyo, Walimu kote nchini msikilize pia Kambi ya Upinzani tunasema nini, msitugombanisha na Walimu, hapana; Walimu tunawapigia kelele sana. Wapeni motisha Walimu, lipeni madeni yao, wajengeeni mazingira mazuri ya kufundishia, hapo wataingia darasani, lakini tuiseme tunawabeza Walimu, haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwa na Wakala imara wa Ukaguzi na hapa tuseme wazi, mimi natoka Jimbo la Singida Magharibi, Jimbo lile Walimu Wakuu sasa wamewageuza watoto wa shule kuwa manamba wa kufanya vibarua kwenye mashamba ya watu kwa ujira wao. Hili liko dhahiri na linajulikana, Mkurugenzi analifahamu na wote wanalifahamu. Kutokuwa na Kitengo imara cha Ukaguzi, shule hazikaguliwi, Walimu wanawatumia, narudia; wanawatumia wanafunzi wadogo kufanya vibarua kwenye mashamba ya watu wanachukua ujira. Maana yake wanafunzi hawaendi shule, wana-*drop out*, hasa watoto wa kike; hii maana yake nini hapa? Tunaporomoshia elimu, mlisikie hili na mlifanyie kazi.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Bodi ya Mikopo. Tulikwenda kuitembelea Bodi hii, tuliangalia jinsi wanavyofanya kazi na changamoto wanazozipata. Cha kusikitisha, Waziri katika hotuba yake amesema, sijui ni ukurasa wa ngapi kuhusu Vyuo vya Ualimu lakini umesema kwamba, mafunzo ya ualimu, umetaja vyuo kadhaa ambavyo mmeanzisha *special program* ya *diploma* kwa Walimu wa Sayansi na *Mathematics*, pamoja na *certificate*. Umevitaja Vyuo vya Korogwe, Monduli, Kleruu pamoja na UDOM hapa. Bodi ya Mikopo msinipige danadana hapa tena, mniambie ni kwa nini wanafunzi wanaosoma Monduli, Korogwe na wanaosoma Kleruu, tena wa Kleruu ni 44 wasichana watupu, hamjawapa mikopo yao mpaka sasa hivi? Kwa nini mmewadanganya watoto hao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuisikie oooh hawakumaliza sijui usaili, oooh hawakujaza *form* mbalimbali! Tangu mwaka wa jana mwezi wa kumi mpaka leo hawa wanafunzi hawajui kujaza, basi wafukuzeni hawafai kuwa Walimu. Kama hawawezi kujaza *form* siyo Walimu hao, watoeni warudi nyumbani, lakini msitupige danadana. Tuliwauliza hivi, bajeti inatosheleza baada ya kuongezewa hawa wanafunzi wa *special program diploma* na *certificate*; mkasema ndiyo, pesa ipo lakini hawana pesa hawa, wanaishije? Wanawake ambao wako Kleruu wataathirika watarudi nyumbani, leo tutakuwa na upungufu wa wanawake kwenye vyombo vya maamuzi. Hiyo kazi hatuitaki, tunataka watoto wa kike wapate elimu sawa na wanaume, muwatendee haki wale wasichana 44. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hapa UDOM kuna wanafunzi 150 ambao pia mikopo yao haieleweki sawa sawa; wengine wanapata *semester* moja, wengine wanapata *semester* sijui wameshamaliza wenzao; hebu tuambieni ni kwa nini mnafanya mchezo? Huo ni mzaha hatuwezi kuvumilia, naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye malipo ya wazabuni. Malipo ya wazabuni katika vyuo vya ualimu, ninalo gazeti hapa msije mkasema mimi nimeandika, hili hapa la Mwananchi, tarehe 26, wanasema wazabuni TTC waidai Serikali, watishia kusitisha huduma. Hapa ni Chuo kimoja tu cha Ualimu Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wazabuni wanakidai chuo zaidi ya shilingi milioni 534. Chuo kimoja shilingi milioni 534; hiki chuo hakitafungwa hiki? Pale kuna wanawake wapo, mimi leo nina wanawake tu. Pale watoto wa kike wapo wanasoma, hizi pesa mtazilipa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitenga bajeti mwaka huu unaoishia Juni ya chakula shilingi bilioni 8.7. Mwaka huu sasa zinaombwa bilioni 8.9; hizo za mwaka wa jana zimekwenda wapi kama bado chuo kimoja kinadaiwa zaidi ya milioni mia tano? (Makofi)

Huu ni mzaha tunawaambia na mimi siko kwenye siasa hapa kabisa mnitoe, huu mzaha siko kwenye siasa, niko kwenye elimu hapa sitaki siasa hapa. Chuo kikifungwa mnaanza kumwambia Mkuu wa Chuo awajibike, haiwezekani. Hawa ni Walimu wenzetu na sisi tuko hapa kupigania masilahi ya Walimu na watoto wanaochukua ualimu. Lipeni hilo deni na mtuambie mtalimaliza lini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ya Miradi ya Maendeleo. Hiki nayo ni kichekesho kingine, Vyuo vikuu vyote ukiacha UDOM ambayo mwaka wa jana ilitengewa bajeti ya shilingi bilioni 2.3, imepata bilioni 1.2 tu kwenye Miradi ya Maendeleo, *the rest* hakuna senti tano iliyokwenda. Chuo changu cha Mkwawa, ni-*declare interest*, mimi ni *lecturer* wa Chuo Kikuu cha Mkwawa. Mkwawa wametimiza lengo, wameweza kuvuka lengo, wamedahili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalimu...

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mpeleke hela za Miradi. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu Christowaja, ahsante sana. Msemaji wetu atakuwa Assumpter Mshama! (Makofi)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi kubwa wanayoifanya, hata kwa namna yoyote ile ilivyo na kwa namna ambayo yote tunaongea, naamini hata wao mioyo yao inaonesha ni jinsi gani inawagusa. Kwa hiyo, niwape pole na niwapongeze kwa kazi kubwa.

Namshukuru Mheshimiwa Anne Malecela, ambaye aliamua kuja katika Jimbo letu la Nkenge na akakiona tunacho Chuo cha Gera. Chuo hiki nadhani Mheshimiwa ulijionea, kwa hiyo, nategemea utakuja na majibu au maelekezo tunakwenda kufanya nini ukizingatia Chuo hicho kipo chini ya Maendeleo ya Jamii na hakiwezi kuingia VETA, kimechakaa, kimechoka, lakini nahisi kama kitakuwa chini ya Wizara ya Elimu kinaweza kikafanya kazi. Ningetamani vyuo vingi hapa nchini ambavyo viko chini ya Maendeleo ya Jamii, Serikali ifikirie namna gani inaweza ikavitoa vikawa chini ya Wizara ya Elimu na hatimaye vikapata ile nafasi kama VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbele, ninataka nimuulize dada yangu Suzan, mimi ninaye mtoto wangu ambaye anaitwa Juliana Mshama, ame-graduate juzi, tena amemaliza *form six* na PCM na sasa hivi amemaliza *degree* yake ya pili ambayo ni ya *pharmacy*. Sasa nashangaa unaposema au labda kama sikusikia vizuri, kama sijasikia vizuri nitakuomba msamaha, lakini kama nimesikia vizuri, PCM ambayo ni *Physics, Chemistry* na *Mathematics*, hakuna sababu ya kusema unashangaa kuona huyo mtu hawezi kuchukua *pharmacy*. Kama nimekusikia vibaya utanisahihisha, lakini naamini waliosoma hiyo wanachukua *pharmacy* bila tatizo lolote na bado wanaweza kuwa madaktari wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye elimu. Naomba Watanzania tuwe wakweli na tuwe kwa kweli Wapinzani, kweli kabisa! Utakapokuwa unasimama unasema hii nchi ya Tanzania iwekwe kwenye maajabu ya duniani, hao watu unaowaambia watakuona wewe ni wa ajabu duniani, ambaye huwezi ku-*appreciate* hata kazi ambayo angalau tumeifanya. Yaani wewe ndiyo unaonyesha Watanzania kwamba, wewe tena Mwalimu na umetaja chuo ambacho unakifundisha, labda wewe ndiyo utuambie, uwezo wa kufundisha unao au huna? Unapungukiwa au hujapungukiwa?

Nataka niulize umesoma hapahapa Tanzania...

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, naomba ukae, hatuna muda.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan naomba ukae, mwache aendelee aseme.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mimi nadhani uniachie. Kama unafanya kazi...



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa, ngoja tuweke mambo vizuri.

Kama unafanya kazi Chuo Kikuu na ulisomea katika elimu hii hii ya Tanzania tukupime kwamba hutoshi tukutoe maana unatuletea mazao mabovu? Kama umesomea Tanzania na tukakuajiri kwenye hicho chuo, ninaamini hata wale wanaofuata wana uwezo huo huo na wanapata mafunzo kutoka kwako yaliyo mazuri. Ukisema kwamba, hujadhilisha mimi ninashangaa, tunaweza kusema labda tuongeze *speed* kidogo ya kwenda, lakini ukisema inaweza kuwekwa kwenye maajabu, kwa taarifa yako kwa Shule za Kata, Rais wetu wa Tanzania katika Dunia nzima, Afrika nzima, ndiyo amepata nishani ya kuendeleza elimu katika Dunia nzima. (Makofi)

Ngoja tuwaambie Watanzania, kubeza ni lazima, Mpinzani ukimwambia nyekundu ili ajulikane ni Mpinzani atasema ni nyeusi, hapo ndiyo ana-*qualify* kuwa Mpinzani, lakini ukimwambia nyeupe akasema nyeupe *then* huyo siyo Mpinzani. Kwa hiyo, Watanzania waelewe, *we are moving*, tunatembea hatujasimama. Kama kuna vitu vya kurekebisha Watanzania mtasema na tunavisikia katika Majimbo, mimi kila mahali ninapokwenda wanasema Mheshimiwa Mbunge tunapungukiwa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Wape vidonge hao!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Juzi waliniambia wamepungukiwa Walimu 300, jana wameniambia wanapungukiwa Walimu 155 na bado juzi waliniambia wamepokea Walimu 64.

Jamani, kama kitu kinafanyika tuseme ongeza nguvu, lakini kusema kweli eti mtatuondoa, ngoja niulize nilikuwa najiuliza; niwape staili niliyofanya nilipotaka kugombea Ubunge, nilianzisha VICOBA na sikuwa Mbunge, lakini nikawawezesha wanawake, vijana na wanaume. Baadaye wakasema huyu kwa nini tusimpe Ubunge?

Hivi ninyi Wapinzani tuwape Urais wa nchi hii kwa kipi mlichonyesha au mmefanya hata tuwaamini kuwapa nchi hii? Hivi ni lazima uwe Rais ndiyo utafanya maendeleo? Lazima muongoze nchi? Hebu tuonyesheni hata mchango wenu kwenye Hospitali ya *Ocean Road* ambayo mmeweka ninyi. Tunachangia watu, tuonyesheni michango ambayo mmefanya hata tuwaamini, tuonyesheni uwekaji wa fedha na kudhibiti fedha ili tuwaamini kuwapa hii nchi. Hiyo imetoshia.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kugombania posho tu hapa! (*Kicheko*)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipofika hebu tuongeze bidii, mmesema mmeanza kulipa madeni ...

**MJUMBE FULANI:** Wee Keissy nyamaza!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mmesema mmeanza kulipa madeni, naomba mlipe yote na sasa tuanze hatua nyingine kwamba, tulikuwa hatulipi *allowance* ya mazingira magumu, hebu tuweke katika kipindi tunachokiendea kwamba, tumejenga mashule, tumeweka utaratibu, sasa tuwawezeshe Walimu wanaofundisha vijijini wapate *incentives* za kuwafanya watamani kwenda vijijini.

Ukienda Uganda wameweka 30% kwa mshahara juu ya nyongeza ya mshahara wa Mwalimu ili aweze kukaa vijijini. Ukienda Zambia wamehakikisha vijijini wanaweka nyumba za

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Walimu ili ku-motivate Walimu waende vijijini. Tuweke mazingira fulani kuwatofautisha Walimu wa vijijini na wa mjini ili wapate moyo wa kwenda kufanya kazi vijijini huko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda niseme ni maabara tulizosema tumewawekea mzigo mkubwa. Nashauri badala ya kusema wajenge *labs* zote tatu kwa nini tusiseme mwaka huu tujenge chumba kimoja, mwaka wa pili tujenge chumba cha pili, mwaka wa tatu tujenge chumba cha tatu ili wachangie kwa unafuu namna hiyo na baada ya miaka mitatu shule zote zitakuwa na *laboratory* kwa mzigo mdogo lakini staili ileile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachoomba, hivi kusema kweli ubongo wa mtoto unatengenezwa kuanzia sifuri mpaka miaka sita ndiyo unaweza ukatengeneza kitu kipya kwenye *computer* ya mtoto. Sasa naomba kuuliza, unamuanza mtoto na Kiswahili mpaka darasa la saba na Kiingereza unakaweka kidogo kwenye darasa la tatu, wakati unasahau kutengeneza ubongo wa mtoto na ku-*catch up* haraka ni pale sifuri mpaka miaka sita.

Sasa naomba kama tunatamani watoto wetu wawe *international* na waweze ku-*compete* na Kenya na Uganda na ukiamini *interview* zinapotokea zinasema Kiingereza, kwa nini tusiseme hivi; kuanzia *nursery* tuwe na lugha zote mbili na zaidi Kiswahili kikawa kama somo lakini Kiingereza kitawale kwenye kufundisha lakini Kiswahili kiwe somo kujikinga wakati tunafanya *interview* na Mataifa mengine ili waone na sisi tunaweza?

Mtanzania anafikiri kwenye Kiswahili, ukimwambia aongee kwenye Kiingereza kwanza ana-*translate* Kiswahili kwenda Kiingereza dakika tatu, ambapo yule aliyeanza la kwanza anaongeza Kiingereza anakwenda *straight*. Kwa hiyo, inamfanya Mtanzania aonekane hana uwezo wakati tukienda kwenye utendaji au katika kuelezea mambo, Mtanzania ana uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tufanye vyote viwili, lakini ukafika siku moja ameanza kidudu, darasa kwanza, hajui kuandika hizo herufi mlizosema KKK wala hajui kuandika hicho Kiingereza, anafika Darasa la Saba anaambiwa vipindi vyote ulivyokuwa unasoma kwa Kiswahili sasa utasoma kwa Kiingereza! Matokeo yake kuja kujifunza mwaka wa kwanza, yule aliyeeondoka huku nyuma akiwa ameanza Kiingereza lazima atamshinda.

Nafikiri tubadilike kidogo na mnasema tunakienzi Kiswahili, ni sawa, kiwe somo, kiwe ni lugha ya kutumia nyumbani, lakini ya kufundishia, ya kuinua tutumie Kiingereza. Kama siyo hivyo, Mheshimiwa Waziri uruhusu watu watakapokuwa wanakwenda kwenye mambo ya Kimataifa muwapatie watu wa kutafsiri, kwa nini waonekane hawana uwezo wa kuongea wakati hawa wengine wanaweza kuongea na Tanzania ni moja? Matokeo yake watu wanakosa kupata nafasi kwenye nafasi kubwa, kwa sababu ya lugha, kwa sababu wakati anakomaa hakitumia hiyo lugha.

Nadhani tumeshaongea vya kutosha, tumeshasema mara nyingi katika Bunge hili kwamba, hizi lugha zinasumbua, hebu jaribu kuona namna gani tutafanya. Hakuna anayekataa Kiswahili, lakini kinatushinda tunapokwenda kuongea na wenzetu katika Mataifa mengine. Mtu anaweza kuwa *capable*, lakini akisimama na mtu aliyesimama Kenya au aliyesoma *International School* hapa, anaonekana yeye ni *useless*; kwa nini tuwafanye hivyo watu wakati wamekosa *opportunity* ya kusoma hizo shule ambazo zinalipiwa?

Ukienda kwenye vidudu vya *International* anasoma Kiingereza, lakini mtihani wanafanya wote kwa Kiswahili, matokeo yake hatuwatendei haki Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza jambo la mwisho, kwa nini mnarundika Vyuvo vya Maendeleo kwenye Maendeleo ya Jamii wakati hamuwapi pesa za kupeleka huko?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa nini tusichukue vile vyuo vyote tuviweke chini ya Wizara ya Elimu ili mnapoongea habari za VETA na kile chuo changu cha Gera kipate?

Mheshimiwa Waziri Mama Anna Malecela umekiona, hebu nisaidie, walianza watoto 400 leo kuna watoto 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mshama. Sasa naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mheshimiwa Majaliwa; dakika kumi na tano!

### TAARIFA

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mambo yanaharibiwa Bungeni ni lazima tutoe taarifa. Umekataa tusitoe taarifa matokeo yake mtu anaongea kwanza hata hiyo *Bachelor Degree* hana, nimeangalia nikakuta amesoma *Bible* mwaka mmoja. Kwa hiyo, kama hujapita Vyuo Vikuu ndiyo sababu unauliza habari ya maendeleo ya jamii kwenye Wizara ambayo haihusiki. Kwa hiyo, hii inaonyesha *level* yako ya kufikiri ni ndogo sana.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mshama, naomba ukae!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *degree* anayosema niko nayo na wala siyo ya mwaka mmoja.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Wee hizo ni *ma-face book* yako hayo, tena naitwa Dokta kwa taarifa yako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe na uvumilivu. Sisi ni viongozi lazima tuwe na uvumilivu.

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi mingi ya Maendeleo ya Elimu ambayo ni ya muhimu sana kwa Taifa letu, ipo chini ya ufadhili wa wageni, kwa mfano, *UNICEF*, Benki ya Dunia, Serikali ya Sweden, Ufaransa, Canada na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi inaweza kuwa msaada mkubwa katika kuwasaidia vijana wetu kupata ajira kwa kujijiri wenyewe. Hata hivyo, fedha iliyotengwa katika mwaka 2015/2016 ili kuboresha na kuendeleza elimu ya ufundi ni fedha za ndani Tshs. 1,000,000,000/= tu na fedha za nje ni Tshs. 5,382,362,000/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ya kuimarisha vijana kiuchumi ambao wengi wao hawana ajira ni kuboresha na kuendeleza elimu ya ufundi kwa kutenga fedha za ndani za

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

kutosha kuliko kuendelea kutegemea wafadhili ambao hata wao huko kwao wana matatizo yao ya kuwatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke kipaumbele katika elimu ya ufundi ili kupunguza tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu ambao wengi wao wapo njiapanda, hawajui la kufanya. Fedha ya ndani itengwe ya kutosha kwani iliyotengwa ni kidogo sana kulingana na uhitaji uliopo kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetelekeza Elimu ya Ualimu kwa kutoitengea fedha ya kutosha katika mwaka huu wa fedha 2015/2016. Fedha iliyotengwa katika eneo hili kufuatana na randama ni fedha za ndani Tshs. 0 na fedha za nje Tshs. 3,000,000,000/= kutoka Serikali ya Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Serikali ya Canada itashindwa kutoa fedha hizo kwa wakati, basi ukarabati wa Vyuu vya Ualimu hapa nchini utaendelea kuwa na hali mbaya au duni kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo kwa maandishi.

Elimu ni ufunguo wa maisha na kwa kutambua hilo, naomba niseme wazi kuwa Serikali imeshindwa kutatua matatizo ya Sekta ya Elimu takribani miaka 53 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa bajeti hii ijielekeze kutatua matatizo ikiwemo:-

Mimba kwa wanafunzi. Hili limekuwa ni tatizo kubwa kwa wanafunzi na Serikali imeshindwa kulitua. Chanzo chake ni wanafunzi wa kike na wa kiume kusoma shule kwa umbali usiopungua km 7 – 10 wanatembea kwa miguu; hivyo, watoto wengi wa kike hudanganywa kwa bodaboda ili kurahisisha usafiri wa shuleni utandawazi pia kwa wanafunzi kutumia simu kuangalia picha za ngono; na mazingira magumu kwa watoto wa kike hasa kipindi cha masika wanapoachiwa kaya na wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika bajeti hii ni ufuatao:-

- Serikali ihakikishe kuwa inaandaa utaratibu wa watoto wa kike kukaa hosteli ili kunusuru maisha yao.
- Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya Serikali kukataza matumizi ya simu mashuleni ili kuwafanya watoto wawe makini na masomo na si kwa utandawazi.

Maji safi na salama mashuleni. Shule nyingi za Kata hazina maji safi na salama, wanafunzi hupoteza muda kwenda kutafuta maji badala ya kusoma. Tunajua maji ni uhai, lakini wanafunzi wanashindwa kutumia vyoo vyao kwa usafi kwa sababu ya kukosa maji na hivyo kuhatarisha afya zao. Nashauri Serikali katika bajeti hii kuhakikisha wanakaa na Waziri wa Maji ili watatue suala hili haraka na kuhakikisha visima virefu vinachimbwa katika mashule na wanafunzi wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwani imethubutu kusimamia chakula mashuleni, kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula shuleni, lakini mwamko wa wazazi ni mdogo. Nashauri Serikali itilie mkazo kuhakikisha chakula kinapatikana mashuleni kwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuwaelimisha wazazi iwe ni lazima kuokoa maisha na afya za watoto wanaozunguka mitaani kutafuta chakula wakati wa masomo. Pia, Serikali iweke utaratibu wa kila shule kuwa na mashamba darasa. Suala hili liwe kipaumbele ili kuepusha utoro kwa wanafunzi hasa kipindi cha mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maabara bado ni tatizo kwani shule nyingi za sekondari bado wanafunzi wanasoma nadharia. Hatuwezi kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira kwa sababu hatuwaandai wanafunzi wetu kuwa waelewa bali tunawaandaa kukariri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaidhalilisha Sekta ya Elimu. Kwa nini Mwalimu mwenye *degree* mshahara wake unalingana na Mwalimu wa Cheti cha *Nursing* tena mwenye *Division Four* au mwenye *D* mbili tu? Mwalimu huyu amefaulu *Form Four* ana *A*, *B* au *C* za kutosha na pia amesoma mpaka *Form Six* akafaulu akaenda mpaka chuo na kufaulu. Namwomba Mheshimiwa Waziri alifafanue hili kwa faida ya Walimu wanaolalamika na malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Walimu bado ni tatizo. Shule za Kata bado hazina nyumba za kuishi Walimu na chache zilizopo hazina kiwango kulingana na wakati. Mbaya zaidi Walimu waliosalia wanakaa mjini na kila siku ili wafikie shule zao wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 7 au 10 kwenda na kurudi; je, ni kilomita ngapi? Huyo Mwalimu akichoka mwili si anachoka na akili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwajengee Walimu nyumba bora za kuishi zinazoendana na wakati, pia wakopeshwe vyombo vya usafiri kwa sababu kila siku ni kama wanasafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukaguzi bado halipewi kipaumbele. Wakaguzi wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana; usafiri wa kuzungukia ukaguzi hakuna; rasilimali fedha hawana; miundombinu ya majengo ya ofisi za ukaguzi ni tete; na vitendea kazi ofisini ni vibovu. Kwa hali hii tutaitambuaje elimu bora bila ukaguzi?

Naiomba Serikali izingatie haya katika ukaguzi, iwezeshe sekta hii ya ukaguzi kwa kuwapatia usafiri (magari) kwa ajili ya kazi ya ukaguzi na siyo kunyang'anyana magari ya Wakurugenzi. Ipatiwé rasilimali fedha; Serikali ihakikishe kitengo hiki kinakuwa na fedha ili watumishi wasitumie nauli zao kwa kugharimia usafiri wanapotumwa kufanya kazi za ukaguzi. Huku ni kuwaumiza na kuwadhalilisha. Vilevile samani za ofisini ziboreshwe pamoja na majengo ya ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kufanya kazi katika mazingira magumu ya bajeti finyu.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kufuatilia kwa karibu sana ujenzi wa Kampasi ya MUHAS Mlongazila (Kwembe). Pongezi hizo nazitoa kama Mwenyekiti wa *Council* ya MUHAS kwa niaba ya Jumuiya ya MUHAS.

Naiomba Hazina ipeleke fedha za ruzuku moja kwa moja kwenye Vyuu Vikuu badala ya kupitia Bodi ya Mikopo. Ruzuku siyo mkopo. MUHAS haijapewa ruzuku ya shilingi 3,611,810,000 kwa miaka miwili mfululizo; 2013/2014 na 2014/2015. Kama Hazina haiwezi kupeleka fedha za ruzuku moja kwa moja kwenye vyuo, basi izipitishé Wizara ya Elimu badala ya Bodi ya Mikopo. Pili, nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na Watendaji kwa kusimamia na kutoa Sera ya Elimu, hata kama sera ina upungufu utasahihishwa. Chondechonde hata mara moja Lugha ya Kiingereza isipuuzwe kama *medium of instruction*, lugha ya kufundisha katika Shule za Sekondari

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

na Vyuo Vikuu. Tanzania haiwezi kuwa kisiwa katika Dunia ya utawandawazi (a globalized world). Wachina na Wajapani wanajifunza Kiingereza kwa nguvu sana. *English is the lingua franca* ya *European Union*.

Tatu, niwapongeze dada zangu; Prof. Barahusesa (*Chief Education Officer*) pamoja na *Chief Inspector of Schools*), kwa kuhakikisha Ngara tunapata *High School* ya tatu ya Muyenzi. Kwa mujibu wa Sera ya Serikali ya kuwa na *High School* kila Tarafa, Ngara ina Tarafa nne; hivyo, tunahitaji kuwa na *High School* ya nne ya Murusagamba. Nawashukuru sana.

Kwanza, naiomba Wizara na ombi langu ni la muda mrefu la kujengewa Chuo cha Ufundi Ngara.

Ombi la pili, naiomba Wizara iongeze bajeti ya Idara Ukaguzi. Ukaguzi ni *core function* ya Wizara. *Need for quality assurance of education provided in schools*. Shule chache sana zimekaguliwa katika Wilaya ya Ngara. Idara ina gari lakini haina mafuta inabidi imwombe Mkurugenzi. Niliwahi kushauri Wizara inunue pikipiki ambazo matumizi yake ni gharama ndogo.

Ombi la tatu, Serikali itoe asilimia moja ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya *research* katika Vyuo Vikuu. Bila *research* hakuna maendeleo; hii ilikuwa ni ahadi ya Serikali mwaka 2010.

Ombi la nne, Ngara imepata fedha kidogo sana kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu. Hii ilikuwa ni ahadi ya Rais mwaka 2010 kwamba, Serikali ingetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu. Ngara tumepata shilingi milioni 195 tu na tumejenga nyumba 10 tu katika miaka mitano wakati Wilaya ina Walimu 2,070, nyumba zilizopo ni 467, pungufu nyumba 1,303. Naiomba Serikali iikumbuke Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Idara karibu zote zimehamia TAMISEMI, Wizara ijishughulisha na tafiti za kuboresha elimu. Wizara iwe *think tank*.

Muundo wa sasa wa Wizara sijui lengo lake ni nini; siyo kuongeza ufanisi?

Nashauri Wizara ichukue jina la *Ministry of Innovation and Higher Education*.

Haukuwa uamuzi sahihi kuhamishia UDOM diploma za *half combination*. UDOM haina Walimu ambao ni *professional* katika fani ya elimu; hivyo, hawawezi kuzalisha Walimu kwa ajili ya *secondary schools*.

Haukuwa uamuzi mzuri kuhamishia TAMISEMI *demonstration schools* za vyuo vya ualimu. Shule hizi zilikuwa ni muhimu kwa vyuo vya ualimu kupeleka wanachuo wake kuona jinsi Walimu wazuri wanavyofundisha. Mkuu wa Chuo ndiyo alikuwa na *mandate* ya kupeleka wahitimu wazuri kufundisha pale.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa kike wanatembea umbali mrefu kufika shule. Hii inasababisha wakutane na vishawishi wanapokuwa wanaenda shule na kupata mimba zisizotarajiwa na kutokumaliza masomo yao au baadhi kupata maradhi ya kuambukiza. Je, ni lini Serikali itajenga mabweni ya wanafunzi wa kike ambao wanaishi pembezoni vijijini?

Je, ni lini Serikali itajenga shule kwa ajili ya wanafunzi waliopata mimba wakashindwa kuendelea na masomo yao?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Baadhi ya shule hasa za vijijini, vyoo vyake havina ubora hasa kwa wanafunzi wa kike, wanapata tabu sana wanapokuwa kwenye hedhi hawahudhuria shule na wengine kuamua kukatisha masomo yao na kuolewa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea mazingira mazuri wanafunzi wa kike kuanzia elimu ya awali hadi vyoo vikuu ili kupata Maprofesa wengi wa kike kwa sababu kwa sasa tuna Maprofesa wachache wa kike ambo ni asilimia sita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria (OUT) ni Chuo cha Serikali na wanafunzi wanaosoma Chuo hiki ni Wafanyakazi wa Serikali. Bajeti ya Maendeleo inayopangiwa Chuo hiki hazifiki kwa wakati na kusababisha baadhi ya majengo kuwa chakavu. Vilevile kwa upande wa Zanzibar ni lini Serikali itaipa kipaumbele *branch* ya Chuo Kikuu Huria na bajeti yake ifike kwa wakati mwafaka. Kwa mfano, kuna baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara imepatiwa vifaa kama maabara, mfumo wa intaneti isiyotumia waya na kadhalika. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri mbona hakuzungumzia *branch* ya Zanzibar ya Chuo Kikuu Huria nao watanufaika vipi katika mwaka huu wa fedha? Naomba maelezo ya kujitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Watanzania ambao wanaishi vijijini mpaka leo hawajui kusoma na kuandika. Hii inasababisha baadhi ya Watanzania kukosa haki zao muhimu. Naiomba Serikali itenge fungu maalum kwa ajili ya Watanzania ambao wanaishi pembezoni ambao hawajui kusoma na kuandika.

Je, ni lini Serikali itaipa kipaumbele elimu ya watu wazima kwa Tanzania Bara na Visiwani na kama haiwezekani basi watangaze kama Serikali haina pesa ili wananchi wajue au iwe kama zamani wananchi wasome madarasa ya usiku?

Nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mrudi tena mjengoni kwa kura za kishindo na muwe tena Mawaziri.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuhamasisha na kujenga maabara katika Shule za Sekondari. Ninashauri sasa ijielekeze kwa nguvu zote kusomesha Walimu wa Sayansi (*Physics, Chemistry and Biology*). Serikali iweke mipango madhubuti kuhakikisha *reagents* za kufanya *practical* katika shule hizo zinapatikana kwa urahisi na vya kutosha. *Reagents* zikiwa *diluted*, *results* za *practical* hazitakuwa sawa.

Nashauri fedha za *capitation* ziongezwe ili kila mwalimu mkuu awe ananunua *reagents* kwa ajili ya *practical* za shule yake, lakini kuwe na ukaguzi kabla mitihani yoyote haijaanza ili kuhakikisha madawa hayo yako sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi katika shule za msingi na sekondari bado haujafikia kiwango cha kutosha. Bado kuna Walimu wengi wanakacha vipindi na Wakurugenzi wa Wilaya hawawezi kuwachukulia hatua yoyote. Iko haja Serikali kuboresha Kitengo cha Ukaguzi na *strictness* iwepo hasa kwa Walimu wanaokacha vipindi.

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa madawati. Maeneo mengine yana misitu mizuri ambayo Serikali inaweza kupitia Wakuu wa Wilaya wachukue vibali, wavune misitu kwa ajili tu ya madawati yanayotakiwa katika eneo fulani. Hili linaweza kufanyika kwa ufanisi kwa kushirikishwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya. Vitabu vinavyotolewa mashuleni vibakizwe shuleni mara darasa moja unapohitimu, ili darasa unaloendelea livitumie. Wenzetu Amerika na Ulaya wanafanya hivyo na wanapata maendeleo.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ya Shule za Msingi na Sekondari ambayo wananchi wamevamia na wanafanya kilimo. Nashauri maeneo ya shule yapimwe na Walimu Wakuu watumie *workforce* ya wananchi walionayo kuotesha miti kwa ajili ya kivuli na pia uzio. Naipongeza Serikali kuweka mitaala ya elimu, itakayotumia vitabu vinavyofanana. Jambo hili litaondoa mkanganyiko uliokuwepo na malalamiko ya wazazi, wanafunzi na wananchi kwa julma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni afya, michezo ni ajira. Serikali kurudisha vipindi vya michezo mashuleni ni nzuri. Liko tatizo la Walimu wavivu kuwaweka wanafunzi nje ya darasa kwa zaidi ya saa sita kwa *pretext* ya michezo. Nashauri Serikali itoe maelekezo muda wa vipindi vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kilimanjaro Shule za Msingi ni nyingi kuliko Mikoa mingine. Hii ni kutokana na wazazi wa Mkoa huo kujua umuhimu wa elimu hasa kipindi cha Mwl. Nyerere alichowataka Watanzania kuchangia kujenga shule. Wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro walijenga Shule za Msingi. Mradi wa MEM ulirekebisha shule kadhaa, ninashauri Serikali iendelee kukarabati shule zilizobakia katika Wilaya zote za Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa matatizo ya nyumba za kuishi katika maeneo ya Shule za Kata, Sheria ya PPP inaweza kutumika kushauri wakazi wa maeneo husika, hasa wafanyabiashara, kupewa viwanja katika maeneo hayo ambayo yatakodishwa kwa bei nafuu kwa Walimu. Zinaweza kujengwa kwa maelekezo ya michezo iliyoandaliwa vizuri na Halmashauri ya Wilaya ili kukidhi mahitaji ya nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibiwa hoja yangu ya Chuo kinachoitwa *Kampala International University* kilichopo Gongo la Mboto, Dar es Salaam. Chuo hicho usajili wake umefanyika Uganda lakini *branch* ipo hapa Tanzania na kinahudumiwa na Serikali. Vijana wanaosoma huko pia wanapewa mkopo na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara yako.

Je, Chuo hicho ni cha binafsi au Serikali ndiyo msimamizi wa Chuo hicho? Naomba jibu lako.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. Pili, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wizara hii, kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuboresha elimu hapa nchini.

Pamoja na pongezi hizi, napenda kutoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manyoni haina Chuo cha VETA; hivyo, Wilaya ilileta ombi hapa Wizarani kwamba, majengo yaliyokuwa Kambi ya Kampuni ya Konoike ya ujenzi wa barabara yaliyopo Kata ya Chikuyu yatumike kutoa mafunzo ya ufundi VETA; badala ya kuyaacha yazidi kuchakaa bure, wakati maelfu ya vijana wanashindwa kujijajiri kwa kukosa elimu ya ufundi.

Tunamshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Anna Malecela, alifika kukagua majengo hayo na kabla ya hapo walikuja Maafisa wa VETA wa Kanda ya Kati kuja kukagua majengo hayo. Ukaguzi huo ulionyesha yanaweza kutumika kwa ukarabati mdogo na kwamba, zingeanza kozi za fani chache na zitaongezeka jinsi muda unavyoendelea.

Hoja ni kwamba, je, mafunzo hayo yalianza lini?



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1970's na 1980's Taifa lilipiga hatua kubwa ya kufuta ujinga wa kutojua kusoma na kuandika. Miaka ya sasa idadi ya Watanzania wasiojua kusoma na kuandika inaongezeka. Kwa hiyo, Wizara ina jukumu la kuweka mikakati ya kufufua juhudi za kuongeza kasi ya elimu ya watu wazima kwa maana ya Watanzania kuondokana na tatizo la kuondoa ujinga na kutojua kusoma na kuandika. Aidha, utaratibu wa watu wazima waliomaliza elimu ya msingi kujitendeleza masomo ya sekondari, huko nyuma Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilikuwa inasimamia vizuri, lakini kwa sasa juhudi hizo hazionekani. Hivi sasa Sekondari zimejengwa katika kila Kata ambazo zingesaikia kutoa elimu ya sekondari kwa watu wazima (waliojenga Sekondari hizo), lakini hilo halionekani likifanyika.

Vilevile huko vijijini na mitaani kuna Watanzania wengi wanaofanya shughuli za ujasiriamali, kilimo, ufugaji, kwa kubahatisha tu. Elimu ya Watu Wazima inahitajika itolewe kwa wananchi ili kuleta tija katika shughuli zao na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niunge mkono hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu ina changamoto nyingi ambazo zinatakiwa zitatuliwe kama ifuatavyo:-

Uhaba wa vyumba vya madarasa. Nanyumbu ina matatizo na uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa. Shule nyingi za msingi madarasa yake ni chakavu kwani yalijengwa siku nyingi na sasa yamechakaa. Hivyo, naiomba Serikali itusaidie kuleta fedha tuweze kujenga madarasa. Mfano, ni shule za msingi za Chihuve, Ulanga, Lukwika, Nangaramo, Chivirikiti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa matundu ya choo ni changamoto nyingine inayokabili Nanyumbu katika sekta hii. Shule nyingi katika Wilaya ya Nanyumbu hazina vyoo; hivyo, kuwapa wakati mgumu watoto wa shule hizi ambao wanajisaidia porini. Nimeomba Wizara kupitia vyanzo vyake mbalimbali itoe fedha kwa ajili ya Wilaya ya Nanyumbu iweze kuboresha shule zake.

Tatizo la ukosefu wa nyumba za walimu limeikumba pia Wilaya ya Nanyumbu. Walimu wengi wanaishi kwenye nyumba za kupanga mitaani ambazo hazina kiwango. Aidha, baadhi ya walimu huishi kwa kuchangia nyumba moja na hivyo kuwanyima uhuru wa kufanya mambo mengine. Kuna tatizo pia la uhaba wa madawati Wilayani Nanyumbu. Madawati hayatoshi na wanafunzi wanakaa chini katika baadhi ya shule.

Upungufu wa walimu ni tatizo pia katika Wilaya ya Nanyumbu. Sambamba na hili kuna upungufu pia wa walimu wa kike. Naomba Serikali ituletee walimu wa kike ili waweze kutoa elimu kwa wasichana wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu hatuna Shule ya Sekondari ya Kidato cha Tano na Sita. Hata hivyo, Wilaya ina mpango wa kuipandisha Shule ya Sekondari ya Mangaka kuwa ya *A level*. Kuna baadhi ya miundombinu kama bwalo la chakula, jiko na tatizo la maji ndizo zinakwamisha shule hii kupandishwa hadhi.

Ninaiomba Serikali itoe fedha tuweze kukamilisha ujenzi wa miundombinu hii ili shule hii iweze kupandishwa hadhi. Naomba Waziri atoe tamko kuhusu hili.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuwasilisha hotuba yao iweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana katika Ustawi wa Jamii, lakini inasikitika kuona bado Serikali haijaweza kutoa pesa ya kutosha. Pesa inayotengwa haitolewi kwa wakati na kusababisha kutokamilika kwa wakati Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuona umuhimu wa Kitengo cha Ukaguzi kuwa Wakala wa Kujitegemea, bado haijaweza kutenga pesa ya kutosha kwa ajili ya kuwezesha Vitengo vya Ukaguzi viweze kufanya kazi kwa ufanisi na uhakika.

Kitengo hiki karibu nchi nzima kimekuwa kikifanya kazi zao za ukaguzi katika mazingira magumu sana, hakuna magari, pamoja na jiografia ngumu zilizopo katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona tangu Sheria ya Bodi ya Mikopo kuanzishwa, bado zipo changamoto nyingi sana zinaendelea kujitokeza katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini na kusababisha kutokea kwa migomo na maandamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua mkakati wa Serikali ili kukabiliana na changamoto hiyo. Ninapenda pia kujua mikakati ya Serikali ya kuongeza vyanzo vya mapato kwa Bodi ya Mikopo ili kukabiliana na ongezeko kubwa la Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum hasa wenye ulemavu na hata watoto wenye uyatima ambao Serikali imekuwa ikiwalipia ada katika ngazi za shule za sekondari, wanapofaulu na kwenda kujiunga na elimu ya juu. Kwa kweli vijana hawa wamekuwa wakipata mateso makubwa kwa sababu hata uwezo wa kukopa hawana. Ningependa kujua mkakati wa hawa vijana kuendelea kusaidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule ambazo wapo watoto wenye ulemavu wa ngozi, yaani *albino*, kama Lugalo Sekondari iliyopo Iringa lakini hakuna uzio. Je, nini mkakati ili kulinda maisha na usalama wa watoto hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kati ya Wizara nyingi zinazokabiliwa na madeni makubwa kutoka kwa wazabuni na kusababisha matatizo makubwa sana; hao wazabuni wamekopa katika mabenki na wengine wametishiwa mpaka kuuziwa mali zao. Vilevile kutolipwa kwa malipo ya wazabuni kunasababisha mpaka baadhi ya shule kutishia kusitisha huduma na kusababisha kufungwa kwa shule hizo au vyuo. Naomba kujua mkakati wa Serikali kukabiliana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malalamiko ya wazazi wengi kulalamikia shule nyingi za binafsi na vyuo kwa ada kubwa sana zinazotowazwa katika masomo, bado kuna baadhi ya shule na vyuo vyetu nchini vinatoza ada zake kwa kutumia pesa za kigeni. Ningependa kujua mkakati wa Serikali kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua mkakati wa Serikali kuhusiana na ujenzi wa mabweni katika Shule za Kata. Vijana wetu waliofaulu kwenda katika Shule za Kata, wanatoka maeneo ya mbali sana na kusababisha kupanga vyumba vya kuishi katika mazingira magumu sana. Matokeo yake watoto wa kike kupata mimba za utotoni na kusababisha kusitisha masomo.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza TEA kwa juhudi kuhamasisha ujenzi wa mabweni. Sambamba na hilo; je, Serikali imewapa ushirikiano gani ili kukabiliana na hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wa kike wamekuwa wakipata mimba zisizokuwa tarajiwa, yaani zinasababishwa na mazingira magumu waliyonayo kama kutokuwa na mabweni, kubakwa, walimu kutaka rushwa ya ngono na kadhalika.

Naomba kujua kama Serikali ina mpango wowote wa kumsaidia huyu binti baada ya kujifungua ili aendelee na masomo yake kwa sababu kijana wa kiume akimpa binti mimba, kijana anaendelea lakini binti anafukuzwa shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutanguliza kusema kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuelezea upungufu wa taaluma kwenye maeneo ya vijijini. Kutokana na changamoto nyingi kwenye shule hizo imetokea wanafunzi kutokujua kusoma na kuandika. Mfano, kwenye baadhi ya shule kwenye Jimbo langu wanafunzi wengi hawajui chochote kutokana na walimu kutokwenda huko wa ajili ya ugumu wa maisha ulioko huko. Kwa hiyo, maeneo hayo yenye changamoto nyingi wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwenye bajeti zote kwenye Wizara hii nachangia kuhusu chuo cha VETA wilaya ya Longido. Wananchi wamekwishatenga eneo kwa ajili ya kujenga chuo hicho. Naomba leo hii Waziri atuambie ni lini chuo hicho kitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya walimu kwenye maeneo yenye mazingira magumu walipwe zaidi ili waweze kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira magumu kwenye maeneo ya wafugaji tunaomba kuongezewa shule za mabweni kutokana na makazi kuwa mbali na shule. Ombi langu kwenye eneo la wilaya ya Longido shule ya Gilay Merugoi iweze kuwa ya bwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni walimu wa mchepuo wa sayansi ambao hawapo kabisa katika shule kama Tingatinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, naunga mkono hotuba ya Kamati na hotuba ya Kambi ya Upinzani. Hotuba hizi zinakamilishana. Kwa kuwa msimamo wangu umeakisiwa vizuri katika hotuba hizo, nitachangia katika maeneo machache ili kuelekeza Serikali kwenye upungufu mahsusuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni kiini macho. Mwaka jana Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 453.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Machi mwishoni mwaka huu Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 319.8 yaani asilimia 70.5 ya tengeo la bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hiki ni kiini macho kwa sababu kiasi kikubwa cha fedha, shilingi bilioni 306 ni kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Ni kiasi kidogo tu kinachobaki kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ndiyo maana hadi Machi mwishoni taasisi nyingi zilizo chini ya Wizara zilikuwa hazijapokea hata senti za miradi ya maendeleo. Kwa mfano, shilingi bilioni 850 za miradi

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya maendeleo Chuo kikuu Mzumbe hadi sasa hazijapelekwa. Ipo mifano mingi kama hiyo. Kwa hiyo, tatizo kubwa linaloikabili Wizara ni ufunyu wa bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu imezinduliwa mwanzoni mwa mwaka huu. Ni sera inayoelezea maoteo zaidi, si sera inayoelezea hali inayoweza kurekebisha au kubadilishwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayoikabili Wizara ni uandaaji wa ramani ya utekelezaji (*road map*) wa sera hii. Katika kuandaa mkakati wa kutekeleza sera hii, Wizara lazima itafakari jinsi ya kubadilisha kila shule ya msingi kuwa na madarasa kuanzia madarasa ya awali hadi kidato cha nne. Mkakati huo utakuwa tayari lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la lugha ya kufundishia limewekwa kwa njia tata kidogo kwa kuruhusu lugha mbili. Hata hivyo, jambo kubwa zaidi ni Wizara kujipanga kwa yafuatayo:-

- (i) Vitabu sekondari na vyuo vikuu viandaliwe kwa Kiswahili.
- (ii) Lugha ya Kiingereza iandaliwe njia bora za kufundishwa.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule nyingi mkoa wa Dar es Salaam walimu wamekuwa na utaratibu wa kutoza wanafunzi fedha za maboresho, mitihani, uji na malipo ya ulinzi. Vilevile, wanafunzi wanalazimishwa kufika shuleni kila siku na fedha ya *tuition*, wanafunzi wasiokuwa na fedha hizi huchapwa na kurudishwa majumbani. Jambo hili linalalamikiwa sana na wazazi. Nitaomba majibu kwa maswali yafuatayo:-

- (i) Je, kuna waraka unaowapa walimu mamlaka ya kukusanya fedha hizi?
- (ii) Wizara itachukua hatua gani kudhibiti hali hii?

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwapa mikopo wanafunzi wa elimu ya juu ni jambo jema ambalo mimi binafsi nalipongeza. Hata hivyo, zipo changamoto ambazo zinapaswa kuangaliwa kwa umakini sana. Miongoni mwa kero hizo ni:-

(i) Kutoangalia kwa makini mchanganuo juu ya wahusika wanaopatiwa mikopo hiyo. Mara nyingi, kama siyo zote, watoto wa maskini, wanyonge na wasio na uwezo hawapati mikopo na wale ambao ni kinyume na sifa hizi ndiyo wanaopata mikopo hii. Kwa mfumo huu, nia njema ya Serikali haitafikiwa.

(ii) Kukosekana utaratibu mzuri wa kurejesha mikopo hii na kusababisha adha kubwa kwa wahitaji wengine ambao wangepaidika na mikopo hii kama ingerejeshwa kwa wakati, naomba Serikali iangalie vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kucheleweshwa na kutokupatikana fedha za maendeleo kwa wakati ni tatizo sugu linalodumaza maendeleo ya taasisi hii muhimu na kudumaza nguvu kubwa inayoenda na ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya kupatikana elimu bora. Inahitajika kuangalia kwa umakini mahitaji ya walimu kwanza ili waweze kufundisha vizuri kwa moyo na uzalendo. Mishahara yao iangaliwe kila wakati na malimbikizo pamoja na stahili zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Serikali inapaswa kuwaangalia vizuri walimu wa shule za msingi. Walimu hawa ni muhimu sana katika kukuza elimu. Kama walimu wa shule za msingi wakitengenezwa vizuri, basi tumejenga msingi mzuri wa elimu na ukiharibika matokeo yake tutazalisha wanafunzi wengi wa darasa la saba wasiojua kusoma na kuandika. Naomba wawezeshe wafanye kazi kwa manufaa ya nchi.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ni lini Serikali hii italipa madeni yote ya walimu hususani walimu wa mkoani Kigoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ina mkakati gani wa kujenga *library* za kisasa zenye *access* za *information* kwa ajili ya mafunzo kwa vijana wetu katika halmashauri mbalimbali na mikoa kwani uwepo wa *library* utasaidia sana vijana kujisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua Serikali imejipangaje kuhusu kuzuia mimba za utotoni kwa watoto wa kike ambao kutokana na vyakula vya siku hizi wanapata balehe mapema na hivyo kuwa katika hatari ya mimba za utotoni na magonjwa ya zinaa?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa kupandisha kiwango cha elimu kutoka asilimia 57.09 mwaka 2013 na kufika asilimia 69.76 mwaka 2013 mwaka 2014. Hii imeonyesha kweli kuna hatua japo hiyo asilimia 12.67 iliyoongezeka bado haijafanya sekta hii kuonyesha mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Missenyi mpaka sasa inapungukiwa walimu 155 na hali hii ni mbaya maana inawafanya walimu kutofanya vizuri kwa kuzidiwa mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi vijijini walimu wanaopangiwa hawaendi na wakati mwingine ni vigumu kuwalaumu maana mazingira hayavutii kwenda huko. Lini Serikali yetu itaandaa mazingira mazuri kama wanavyofanya majirani zetu? Kuna nchi zinatoa motisha kwa kuwaongezea asilimia 30 kwenye mishahara ya walimu wanaofundisha pembezoni, nchi nyingine hutoa *course* mbalimbali mara kwa mara kwa walimu wanaofundisha katika mazingira magumu, nchi nyingine hutoa nyumba kwa walimu hao na nchi nyingine huwafanya wapande vyeo haraka haraka kuliko wa mjini. Lini Serikali itatoa motisha kwa walimu hawa ili wajisikie kwenda huko badala ya kukimbia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mkanganyiko juu ya Vyuho vya Maendeleo ya Jamii, vina hali mbaya sana, viko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii lakini havipangiwi hela na vyote vimekufa mbaya zaidi VETA haivitambui. Kwa nini vyuo hivi visiwe chini ya VETA na hivyo vikawa chini Wizara ya Elimu moja kwa moja kuliko hivi vilivyo sasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii hawavipatii fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza suala la ujenzi wa maabara lakini kwa nini tusiweke utaratibu mzuri wa kutoa unafuu kwa wananchi kama vile kila mwaka kumaliza chumba kimoja ukizingatia wananchi wetu hasa huko vijijini uwezo wao ni mdogo?

**MHE. GRACE S. KIWELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu. Urithi pekee kwa watoto wetu ni elimu hivyo ni wajibu wa Serikali iliyoko madarakani kuhakikisha vijana na watoto wa Tanzania wanapata haki yao hiyo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo. Napenda kuzungumzia suala la mikopo ya wanafunzi wa vyuo kwani kumekuwa na tatizo kubwa sana la upatikanaji wa mikopo hiyo kwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanafunzi hao. Napenda kujua ni kwa nini mikopo hiyo haitoki kwa wakati ili kuondoa adha kubwa wanayoipata pale wanapocheleweshewa mikopo hiyo na kulazimika kugoma au kuandamana na matokeo yake wanapigwa mabomu na virungu vya polisi na kuumizwa vibaya? Serikali inatoa majibu gani katika suala hili ambalo limekuwa kero ya muda mrefu kwa wanafunzi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji wa madaraja. Napenda kujua ni nini hatma ya walimu waliopanda madaraja toka mwezi wa saba mwaka jana lakini mpaka leo hawajarekebishiwa mishahara. Nini kauli ya Serikali katika suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure. Serikali itaanza kutoa elimu bure, Napenda kujua ni lini itaanza na kama fungu hilo lipo kwenye hii bajeti tunayopitisha leo? Ikumbukwe suala hili lilikuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA ya mwaka 2010 na Serikali hii inayojiita sikivu iliibeza sana kwamba haiwezekani ila leo wanaipigia debe. Pia lipo suala la michango katika mashule ambayo ni zaidi ya ada, nini kauli ya Serikali katika mambo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya vyoo katika shule. Ni jambo la aibu sana kwa Serikali hii ya CCM shule kukosa vyoo na kufungwa. Je, Wizara imejipanga vipi kumaliza tatizo hili ili watoto wetu waweze kupata huduma hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya nyumba za walimu. Bado lipo tatizo kubwa sana la nyumba za walimu hasa maeneo ya vijijini na hii inawakatisha tamaa walimu wanaopangiwa maeneo hayo kwa sababu hakuna hata nyumba za kupanga tofauti na mijini. Je, Serikali imejipanga vipi kumaliza kero hii ya nyumba za walimu ili wale walimu watakaopangwa maeneo hayo waweze kwenda kwenye maeneo waliyopangiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho za walimu wapya. Yapo malalamiko toka kwa walimu wapya walioajiriwa hivi majuzi bado hawajalipwa posho zao na hivyo kupata wakati mgumu katika maisha yao ya kila siku. Napenda kupata kauli ya Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kusema msemu ufuaao "elimu ni ufunguo wa maisha lakini kama elimu bora ni ufunguo wa maisha bora na vilevile mbaya ni ufunguo wa maisha mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno hayo nimeyanukuu kutoka kwa Jackson Makwetta ambaye alikuwa Waziri katika Awamu ya Kwanza ya Serikali. Aliyesema maneno haya kupitia kongamano lililofanyika tarehe 26 Novemba, 2011 pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya tathmini ya elimu baada ya miaka 50 ya uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo mhimili wa maendeleo katika nchi. Kwa hiyo, mnapoichezea elimu jua kwamba na mambo mengine katika nchi hayataenda sawasawa kupitia maeneo mbalimbali mfano uchumi, siasa, kilimo na kadhalika. Leo Tanzania ni ya mwisho katika kutoa elimu bora baina ya nchi wanachama wa Afrika Mashariki zikiwemo Uganda, Kenya, Rwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kusemea elimu katika Mkoa wangu wa Arusha na haswa Jiji la Arusha ambapo nimekuwa nikiishi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kutokujua kusoma na kuandika kwa watahiniwa wa shule za awali au msingi. Mkoa wa Arusha mwaka jana baada ya matokeo ya

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

darasa la saba kuligundulika watoto 344 ambao walikuwa hawajui kusoma na kuandika na kati ya hao watoto 230 walitokea Jimbo la Ngorongoro. Hii ni aibu kwa Taifa letu yaani badala ya kupunguza wasiojua kusoma na kuandika ambao idadi yake inafikia milioni 14, Serikali imezidi kuumiza wananchi na hasa wazazi ambao wamekuwa wakilipa fedha za michango mbalimbali na matokeo au shukrani yake anarudishiwa mtoto mbumbumbu baada ya miaka saba. Naombeni tulisaidie Taifa kwa kutoa elimu bora na siyo bora elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia ufasadi katika Bodi za Shule. Kumekuwa na ufasadi wa ajabu hadi katika mkoa kupitia wilaya na kata zetu. Katika shule ya Ngarenaro kumetokea ubadhirifu au wizi wa hela shilingi milioni 49 na hili limefanywa na *signatories* ambao ni walimu na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Ngarenao na kibaya fedha hizi zimekuwa zikichangwa na wananchi ambao ni wazazi wa watoto hao sababu shule huwa haipokea ruzuku kutoka Serikalini. Mwenyekiti wa Bodi alivyoona hivyo akamwandikia Afisa Elimu Mkoa na RAS kuwapa taarifa na wachukue hatua. Cha kushangaza na kusikitisha Afisa Elimu alisimamisha Bodi isiendeleo na kazi na Mwalimu Mkuu na mwenzake wamebaki huru. Hapa kuna sintofahamu baina ya Mkuu wa Shule na Afisa Elimu Mkoa. Naomba Wizara ifuatilie hili na kutoa adhabu kali kwa Mwalimu Mkuu huyo na yeyote aliyehusika katika ufasadi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ya upungufu wa madarasa katika shule za msingi na sekondari. Katika Jiji la Arusha kuna upungufu wa madarasa 103 lakini yangepatikana hata 66 tu yangeweza kusaidia kwa kuanzia. Manispaa wamekiri kutokuwa na hiyo hela ya kujenga madarasa hayo kwa sasa. Mfano shule zenye tatizo hili ni Sombetini, Elerai, Sinoni, Ngarenaro, Olasiti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la miundombinu au mahitaji muhimu mashuleni. Shule nyingi hazina madawati ya kutosha, matundu ya vyoo, vifaa vya kufundishia, maji, viwanja vya michezo na kadhalika. Mfano katika shule ya msingi inayoitwa Maweni iliyopo Kata ya Terati ni tatizo kubwa. Shule haina choo, madawati, madarasa ya kutosha, maji na iko mbali na kupelekea wanafunzi kuchelewa kufika shuleni na kuanza masomo kwa wakati. Mfano kama mwalimu anatumia shilingi elfu nane kwa siku kwa ajili ya nauli tu. Wanafunzi na walimu kujisaidia vichakani hii siyo afya na inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kama kuhara na kipindupindu na hata kupelekea wanafunzi kubakwa au kuanza mapenzi katika umri mdogo huko kichakani wakati wa kujisaidia. Naomba hii shule isaidiwe au kama hakuna hela za kuwapatia miundombinu basi ifungwe.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napongeza Serikali kwa kufanikisha kwa kiasi kikubwa kuongeza idadi kubwa ya walimu wa shule za msingi na sekondari. Pamoja na mafanikio haya ya kuongeza walimu, Serikali sasa haina budi kuangalia mambo yafuatayo ili kuboresha elimu nchini.

(i) Kuboresha mazingira kwa walimu na vitendea kazi (vifaa vya kufundishia na mazingira). Ili walimu hawa watoe huduma yenye kiwango bora lazima mazingira yao ikiwemo nyumba na posho ya mazingira magumu itolewe ili kutoa motisha ambayo itashawishi kuinua kiwango cha utendaji kazi zao kila siku.

(ii) Kuongeza mafunzo ya ufundi stadi (VETA) kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la wahitimu wa shule za msingi na sekondari. Aidha, hata wale wa ngazi ya vyeti, diploma na shahada ambao soko la ajira linashindwa kuwahudumia wote. Hivyo basi Serikali sasa ipeleke kipaumbele katika mikakati na miradi ya elimu kujenga vyuo hivyo vya VETA kwa wingi hata nje ya wilaya hadi katika ngazi ya tarafa ili kuwawezesha vijana kupata ujuzi/ufundi stadi ambao utawawezesha kujijiriri wenyewe.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

(iii) Upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Miradi ya maendeleo haitekelezwi na Wizara kutokana na ukosefu wa fedha zilizotengwa katika bajeti zinazopitishwa na Bunge. Naiomba Serikali kurekebisha tatizo hili kwa kupeleka pesa zilizotengwa na Wizara kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni msingi wa maendeleo ya nchi. Kwa kuwa elimu ni msingi wa maendeleo, nchi/Serikali yetu inatakiwa kuboresha zaidi miundombinu ya elimu.

Mheshimiwa Spia, nyumba za walimu. Ili kuondokana na ukosefu wa nyumba za walimu, Serikali ishirikiane na wananchi kujenga nyumba za kutosha ili kuondokana na tatizo la nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kwa ujenzi wa maabara kwa sekondari zetu lakini changamoto kubwa ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia. Maabara ili ikamilike lazima vifaa viwepo katika vyumba vya sayansi, *chemistry*, *physics* na *biology* pamoja na kuwa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu kutopandishiwa madaraja yao. Wapo walimu bado madaraja hayajapandishwa kutoka mwaka 2011 hadi leo. Kwenye Wilaya ya Mufindi baadhi ya walimu hawajapandishwa madaraja yao. Naomba Serikali kuchukua hatua ya kupandisha madaraja kwa walimu ambao hawajapandishwa madaraja yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado katika shule za msingi kuna changamoto ya michango mingi bila kufuata utaratibu. Hii inasababisha walimu/wazazi kulalamika. Naiomba Serikali kutoa utaratibu wa kuchangia katika shule za msingi. Tunajua kuwa ada shule za msingi ilifutwa, je, ni lini Serikali itafuta ada kwa shule za sekondari?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja hii ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ina mpango gani kuhusu wanafunzi wanaofeli darasa la saba ambao ni wengi sana? Je, Serikali inatengeneza taifa la wajinga? Hali kadhalika wanafunzi wa kidato cha nne?

(ii) Kwa kuwa tatizo la walimu wa sayansi na hisabati limekuwa sugu, Serikali ina mpango gani wa kuajiri walimu wa kigeni?

(iii) Je, Serikali ya Tanzania imefanya utafiti kwani viwango vya elimu vimeshuka katika ngazi ya shule ya msingi hadi chuo kikuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja iliyoko mezani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo. Serikali imejitahidi sana kutoa mikopo na kuhakikisha wanafunzi/wazazi wasio na uwezo wanapata elimu kwa kupatiwa mikopo. Katika utaratibu wa kutoa mikopo bado kuna shida ya wanafunzi walio na



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

wazazi wenye uwezo mzuri wa kiuchumi kupatiwa mikopo hii wakati walengwa/wahitaji halisi - wakikosa mikopo hiyo. Nashauri Serikali iendelee kuboresha utoaji wa mikopo hasa kwa kuwashirikisha wazazi/walezi katika zoezi zima la kuomba mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro vyuoni. Kumekuwepo na migomo ya mara kwa mara katika baadhi ya vyo. Mfano mzuri ni *Kampala International University (KIU)* kilichopo Dar es Salaam (Jimbo la Ukonga). Chuo hiki kimekuwa na tatizo la wanafunzi wake kugoma kila mara. Mfano mzuri ni mgomo uliopo sasa uliosababishwa na wanafunzi waliosoma kozi za famasia na udaktari kukosa ajira kwa vyeti vyake kutotambulika. Wapo wanafunzi walifukuzwa chuoni kwa sababu ya mgomo uliotokea lakini hadi sasa bado hoja yao ya kutotambuliwa shahada zao halijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aje na jibu la tatizo la *Kampala International University* ili kuwapa uhakika wanafunzi wanaosoma katika chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Bodi hii iangalie utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wote hasa wale wanaostahili, hususan wanaotoka katika familia maskini kuliko utaratibu wa sasa wa kuangalia vipaumbele. Napendekeza Serikali ibuni vyanzo mbalimbali vya mapato ili kuiwezesha Bodi hii iweze kutoa mikopo kwa wanafunzi wote bila ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi iwezeshe kwa kadiri itakavyowezekana ili iweze kusimamia kazi yake iwezekanavyo. Idara ya Ukaguzi ifanye tathmini, ukaguzi, usimamizi, ubora na hata kubaini changamoto zinazowakabili wanafunzi, walimu na wadau wengine wa elimu ili kuboresha mazingira ya kujifunza kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Nashauri Serikali iangalie utaratibu huu uwe endelevu kwani kuna halmashauri nyingine katika nchi hii zina mazingira magumu mfano Tarime, walimu wengi wanakimbia wanapopangiwa shule za vijijini. Posho ya walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ni njia pekee ya kuwapa motisha walimu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima. Napendekeza Idara hii ipewe fedha ya kutosha na isaidie sana kufanya utafiti, ili kubaini ni watu wangapi wasiojua kusoma na kuandika. Utafiti ubaini ni namna gani ya kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wazabuni. Kwa nini Serikali imeshindwa kuwalipa wazabuni? Je, ina utaratibu gani wa kuwasaidia hao wazabuni kwa kuwalipa madeni yao? Ni jumla ya fedha kiasi gani kinadaiwa na wazabuni? Nahitaji majibu sahihi kuhusu suala hili la wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba za walimu. Serikali ina mpango gani mahsusi na wa haraka wa kujenga nyumba za walimu hasa maeneo ya pembezoni kama vile Tarime? Ni kwa nini Serikali isiingie ubia na mashirika ya kijamii kama vile *NSSF, PSPF, LAPF*, na kadhalika ili kujenga nyumba za walimu?

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Tarime. Ahadi nyingi zimetolewa katika Bunge hili kuhusu ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Tarime. Napendekeza Serikali itekeleze ahadi hiyo juu ya ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ya 2014. Je, utekelezaji wake utaanza lini? Je, kuna maandalizi yoyote? Je, inatekelezeka au iko katika maandishi tu? Je, itawashirikishaje wadau?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya kufundishia. Kama ni Kiswahili, ni lini itaanza rasmi? Kama ni Kiingereza, ni kwa nini kisianzie toka darasa la kwanza au elimu ya awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo. Napendekeza Serikali iangalie utaratibu wa kuifanya lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya kutolea elimu toka elimu ya awali, msingi, sekondari hadi vyuo vikuu. Masomo ya Kiingereza, Kifaransa na Kichina yafundishwe toka elimu ya awali hadi vyuo vikuu ili kuwafanya Watanzania kuwasiliana na mataifa mengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa Chuo cha Ualimu Tarime. Chuo hiki kimechakaa sana, je, Serikali ina mpango gani wa kukikarabati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matabaka katika elimu. Suala hili limezua sana tofauti kati ya wenye nacho na wasionacho. Napendekeza Serikali iangalie utaratibu wa kupunguza matabaka haya yaani hizi shule za Academy au za Kimataifa zitumie mitaala ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Elimu na Ufundi Stadi - Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge; na Naibu Waziri wa Elimu na Ufundi Stadi - Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge; Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela - Naibu Waziri wa Elimu na Ufundi Stadi, kwa muda mfupi aliokaa kwenye Wizara hii ameshatembelea maeneo mengi ikiwemo Wilaya ya Manyoni kuona majengo ambayo tunategemea kufungua Chuo cha VETA. Alipoyaona majengo hayo aliridhika sana kufungua Chuo hapo. Naomba kauli ya Waziri, ni lini Chuo cha VETA Wilaya ya Manyoni kitafunguliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasubiri majibu wakati wa majumuisho ya Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinatoa kozi na semina mbalimbali kwa wananchi, mfano ufundi umeme, ufundi uashi, upishi, ushonaji, ufundi vyuma, na kadhalika. Kwa kuwa, Vyuo hivi vinatoa elimu ya ufundi stadi, ni dhahiri kuwa Vyuo hivi ni mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itenge fedha kupitia Wizara ya Elimu kusaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili taaluma inayotolewa iweze kuwa na tija. Nasubiri majibu ya Waziri au Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kuwa Idara ya Elimu ya Watu Wazima haitengewi fedha za kuendeleza utoaji taaluma kwa wananchi ambao hawakupata elimu na kama inatengewa ni kiasi kidogo sana hutosha kwa kuendesha Ofisi tu. Napenda kujua Serikali

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

imejipanga vipi kuhakikisha kuwa utoaji wa elimu kwa wale ambao hawakupata elimu ya msingi kwa kutoa *honorarium* kwa Walimu. Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuboresha Idara ya Ukaguzi wa Shule za Msingi na kusogeza huduma hadi ngazi ya Kata. Ni matumaini yangu kuwa Walimu watafanya kazi kwa bidii na kwa kiwango kinachotakiwa, kwani ufuatiliaji wa Wakaguzi utakuwa wa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ihakikishe uboreshaji huu unaenda sambamba na vifaa vya usafiri ili kuwafikia Walimu kwa urahisi. Ni kweli wawe Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo anafanya kazi nzuri sana, anatoa mikopo kwa wakati, bali changamoto anayokutana nayo ni ufinyu wa bajeti. Hivyo basi, naiomba Serikali kuongeza bajeti ya mikopo ya Vyuo Vikuu ili wote wanaohitaji wapate tena kwa wakati. Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jitihada za kulipa madeni ya Walimu kwani kutoka Shilingi bilioni 50 sasa hivi zimebaki Shilingi bilioni tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii Shilingi bilioni tatu ilipwe ili tuombe migogoro na Walimu na Serikali yao. Serikali itamke ni lini deni litaisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Walimu. Ni ukweli usiopingika kuwa, Tume ya Walimu bado ina umuhimu wake, kwani ndiyo inayosaidia Walimu kushughulikiwa haki zao mbalimbali. Hivyo, ni vyema Tume hii ya Utumishi ya Walimu Tanzania iandaliwe vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kupiga kelele kwa ajili ya Serikali kuanza kutoa posho ya mazingira magumu kwa Walimu, kwa kuwa Walimu wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana. Ualimu ndiyo kada pekee inayotoa huduma hadi vijijini maeneo ambayo mengi hayana barabara, hayana nyumba za kuishi, hakuna umeme, hakuna maji, na kadhalika. Endapo Serikali itasikia kilio hiki cha Walimu, itawaongezea Walimu ari ya kazi. Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kurudia mfumo wa zamani katika kufundisha madarasa ya Kwanza na Pili kwa kuwa na masomo matatu KKK – Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Hii itasaidia kujenga msingi mzuri wa uelewa, kwani mtoto kufundishwa masomo saba ilikuwa shida sana watoto kuelewa. Kwa kuwa Serikali imeanza kutoa Semina kwa Walimu ni vema Walimu hao wote wapewe elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukupongeza kwa hotuba yako na kazi nzuri ambayo umekuwa ukifanya. Aidha, nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Anne Kilango ambaye naamini kwa umahiri wake anakupa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi wanazofanya. Lakini kwa umuhimu mkubwa, naomba nimpongeze Mkurugenzi wa Wilaya ya Kilindi, pamoja na Wakurugenzi wa Elimu ya Msingi na Sekondari na Wataalamu wote wa Idara hiyo katika Wilaya ya Kilindi pamoja na mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie kama ifuatavyo:-

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha uliopita Wilaya ya Kilindi pamoja na Chunya na Ukerewe zilitengewa fedha za ujenzi wa VETA. Jambo hili lilipokelewa kwa shangwe sana na wananchi wa Kilindi. Kwa kiasi kikubwa, eneo lilitengwa ambapo Wataalamu walifika na michoro ikaandaliwa. Baada ya hapo ilitangazwa kwenye gazeti kwa ajili ya zabuni, lakini hadi leo hawajarudi tena. Suala hili limewakatisha tamaa wananchi na kuwakosesha imani na Serikali yao. Nilipofuatilia mwezi Machi mwaka huu nilijibiwa kuwa fedha hizo zilibadilishiwa matumizi. Inakuwaje jambo linapitishwa ndani ya Bunge halafu linabadilishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa mara nyingine naona tena iko kwenye *speech* yako kwa mwaka huu. Naomba katika majibu yako ueleze kilichotokea na kusababisha VETA hiyo kutoanza kujengwa mwaka 2014 na uwahakikishie wananchi kuwa ujenzi unaanza mwaka huu. Wilaya zilizoanza baada ya Kilindi baadhi zimekwishajengwa Vyu vya VETA; hivyo kwa niaba ya wananchi naomba mtufikirie kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi ni umuhimu wa kuwepo maktaba katika shule zetu, hasa za Sekondari. Naomba hili liwekewe mkazo kwani litasaidia wanafunzi hao kujisomea na pia zikiwemo *computer*, naomba kama tulivyoweka kipaumbele masuala ya Maabara, basi na Maktaba zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilindi pamoja na mazingira magumu imekuwa ya kwanza katika BRN kwa Mkoa wa Tanga. Hii imetokana na jitihada za pamoja za Waalimu, Halmashauri, Madiwani, Mbunge wa wananchi kwa ujumla. Naomba Wizara kwamba maeneo kama haya iyaangalie kwa macho maalum na kuwaunga mkono ili waendeele kufanikisha mikakati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya VETA na ninaunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Mbunge, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri. Nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Busanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita Walimu wanadai madai mbalimbali ikiwemo fedha za likizo, malimbikizo ya fedha kwa kupandishwa vyeo. Mbaya zaidi, madai haya badala ya kupunguza madeni, yanazidi kuongezeka. Malalamiko yaliyopo kwa sasa, Walimu kwa sasa wanapewa fedha ya likizo nusu ya ile inayotakiwa kulipwa. Je, ni lini sasa Serikali itamaliza tatizo hili la Walimu la kupewa fedha nusu nusu, hasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba, nahitaji ufafanuzi juu ya utekelezaji wa ujenzi wa Vyu vya Ufundi katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa. Mipango imekuwa ni ya muda mrefu sana; ni lini sasa ujenzi utaanza rasmi katika Mkoa wa Geita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa huu hauna Chuo cha VETA, Mkoa mzima! Vijana wengi wanaohitimu masomo yao ya Darasa la Saba na Kidato cha Nne hawapati fursa za kujiendeleza kiujuzi. Hii inaathiri maisha na uchumi wa wananchi hawa. Hivyo, katika majumuisho, Serikali itamke ni lini sasa ujenzi utaanza rasmi katika Mkoa wa Geita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sera ya Taifa inazungumzia juu ya kila Wilaya kwamba iwe na Chuo cha VETA, napenda kujua pia ni lini Wilaya ya Geita tutajengewa Chuo cha VETA cha Wilaya?

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo machache, naomba Serikali katika majumuisho itoe maelezo ya kina ili wananchi waweze kusikia namna Serikali inavyofanyia kazi changamoto zao. Naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima wa afya katika kipindi chote cha miaka mitano 2010 - 2015 katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi leo kupata fursa hii ya kuchangia Bajeti ya Wizara hii kipindi cha mwisho. Namshukuru Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nitaanza kama ifuatavyo:-

(i) Nataka unieleze changamoto zinazoikabili elimu ya jamii kupatiwa fedha za kutosha ili kuweza kutekeleza majukumu yake, kama vile kuwapatia wanafunzi waliofaulu vizuri mikopo kwa wakati kwa kuwalipia fedha zinazostahili kupatiwa.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi ni eneo moja muhimu katika kuendeleza gurudumu la elimu. Eneo hili (Kitengo) limeachwa nyuma bila kufikiwa ni dhambi kubwa kuandaa mpango usio na usimamizi. Ni kweli bajeti zetu ni ndogo na dhaifu kutokana na uchumi dhaifu. Naomba kuishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itunishe fungu la kitengo cha Ukaguzi.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Madeni ya Malimbikizo ya stahili za Walimu. Naomba niishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu Walimu wapatiwe malimbikizi yao ya mishahara kwa wakati, wapandishwe vyeo na Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu waongezewe malipo ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri lakini katika mazingira magumu. Mchango wangu ni:-

(1) Umuhimu wa kuanzisha Tume ya Huduma kwa Walimu ni sasa ili Walimu wapate faraja na moyo zaidi wa kutenda kazi vizuri zaidi.

(2) Umuhimu wa Kitengo cha wenye ulemavu, Wizara chini ya Kamishna, kuwa Idara kamili.

(3) *BTP* ni lazima iwe ya muda stahiki ili kupata Walimu mahiri watakaofundisha vizuri ili kuweza kupata wataalam mahiri.

(4) Umuhimu wa kusisitiza ujenzi wa mabweni na hosteli ili kuwawezesha wanafunzi wa kike kuepukana na vishawishi vya kupata mimba za utotoni.

(5) Nataka kufahamu: Je, kiwanda cha kutengeneza karatasi za *Braille* kwa wasioona cha pale Shule ya Uhuru, kiko katika *status* gani? Kwa sababu yaelekea kuna upungufu mkubwa wa karatasi hizo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Walimu wa Halmashauri ya Kwimba kwa Walimu wapya wanaodai fedha za kujikimu, Walimu wa zamani wanadai fedha za uhamisho, mishahara na fedha za kujikimu kwa Sekondari na Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wengi wa Kwimba hawapandishwi madaraja tofauti na Walimu wa Wilaya na Mikoa mingine. Naomba majibu yenye uhakika, ni lini stahili zao ambazo siyo hisani watalipwa?

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja namba moja ni ujenzi wa Vyuo vya VETA. Mwaka 2012/2013 Waheshimiwa Wabunge tulipewa majedwali yaliyokuwa yanaonesha *plan* za Wizara ya Elimu kujenga Vyuo vya VETA Wilaya zote nchini. Wilaya ya Liwale, katika majedwali yale yalionesha kwamba Wizara ilipaswa kujenga Chuo hicho cha VETA cha Liwale katika mwaka wa fedha 2013/2014. Naomba kupata jibu la Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, ujenzi wa Chuo hicho cha VETA Wilaya ya Liwale umeyeyukia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ni kuzitenga *giant schools* kutoka TAMISEMI na badala yake utafutwe utaratibu wa kuzihudumia shule hizo. Unapozungumzia *giant schools* ninamaanisha shule zile kubwa za zamani ambazo zilizo nyingi kwa sasa zina 'A' Levels. Shule hizo ni kama *Mtwara Technical, Ndanda High School, Kilakala, Azania, Ilboru, Mzumbe Sekondari, Msalato* na nyingine zinazofanana na hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani sana Shule zile za zamani tunazozijua, zingeendelea ku-*maintain* heshima yake. Shule hizo hazitaweza ku-*maintain* heshima yake kama *budget* ama kiasi cha fedha zinazopelekwa kwenye shule hizo hazilingani na mahitaji. Ninashauri kwamba shule hizo ziondolewe kwenye kuhudumiwa na TAMISEMI na badala yake zirudishwe Wizarani ama itafutwe namna nyingine ya kuzihudumia shule hizo moja kwa moja badala ya kuhudumiwa na TAMISEMI kupitia Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tatu ni madeni makubwa ya Wazabuni wa vifaa vya Maabara na chakula. Shule zetu ziko hoi sana kutokana na kuwa na madeni makubwa ya Wazabuni wa vyakula na Wazabuni wa vifaa vya Maabara. Ombi langu ni kwamba hebu fanyeni utaratibu wa kuhakiki madeni ya wazabuni wa chakula na vifaa vya Maabara na vitabu. Angali utaratibu wa kuwalipa Wazabuni hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mnawapa *limit* ya matumizi, lakini kutokana na fedha mnazowapelekea kutowiana na uhitaji, wanalazimika ku-*accumulate* madeni. Kama mnavyoona, ndani ya Wizara ya Ujenzi kuna madeni makubwa ya Sazabuni wa ndani, ndivyo hivyo katika Shule zenu, kuna madeni makubwa ya vyakula, vifaa vya Maabara na vitabu. Mnafanyaje ninyi kama Wizara pamoja na TAMISEMI kumaliza madeni haya ya Wazabuni wa vyakula na vifaa vya Maabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SYLVESTER MASELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Katibu Mkuu na Watendaji wote pamoja na wataalamu wote kwa hotuba yao nzuri na uchapakazi wao uliotukuka kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa muundo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi uliopo kwa sasa unafaa kuangaliwa upya kwani ni dhahiri kuwa Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Sekondari husimamiwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI wakati Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi na Elimu ya Juu vyote husimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ufundi, hivyo utekelezaji na usimamizi wake huleta usumbufu, kwani utekelezaji unahitaji Wizara zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Serikali inapaswa kwa vyovyote vile kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya juu wanapata mikopo ili iwawezeshe kupata fursa ya kujifunza bila usumbufu. Nchi yetu inawahitaji sana wataalamu wa fani mbalimbali. Fedha za maendeleo ambazo pia zinapelekwa kwenye mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ni lazima zipelekwe kama Bunge linavyoidhinisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kulipa madeni yote inayodaiwa Wizara na Walimu ili kuwapa moyo, ari na motisha ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi wa Elimu ipewe kipaumbele ili kuboresha ubora wa elimu hapa nchini. Idara hii nashauri ipewe fedha za kutosha ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa ujenzi wa Maabara nyingi na hivyo kuleta matumaini ya kupata wanafunzi kwenye fani ya Sayansi. Ombi langu na ushauri wangu ni kwamba Maabara hizi haziwezi kufanya kazi kama hazitapelekwa vifaa. Vifaa ni muhimu sana, lazima Maabara hizi zipelekwe vifaa ili azma ya Serikali iweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu vilivyounuliwa kutokana na chenji ya Rada havikufikishwa kwenye Halmashauri zote. Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge ni Halmashauri ngapi zilizoufaika na vitabu hivyo vya chenji ya Rada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina sera ya kufundisha elimu kuanzia elimu ya Awali hadi Elimu ya Juu kwa lugha ya Kiswahili. Je, maandalizi ya utekelezaji wa sera hii yamefikia hatua gani? Ni lini hasa sera hii itanza kutumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu uhaba wa madawati katika shule mbalimbali za Umma hapa nchini. Naomba Serikali iliambie Bunge, ni madawati mangapi yanahitajika ili kuomba fedha hii? Ni mkakati gani umeandaliwa kuhakikisha shule zote za Umma zinapatiwa madawati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Serikali yetu imekuwa na mazoea ya kuwa na sehemu kubwa ya bajeti yake kwenda kwenye mahitaji ya kawaida: Je, Serikali haioni kwamba mfumo huu hausaidii katika kutekeleza Dira ya Taifa inayoelekeza na kulisitiza kuwa Tanzania ni lazima iwe ni nchi ya kipato cha kati (*middle income*) ifikapo mwaka 2025. Naomba Vyu vya Elimu ya Juu vipewe fedha za maendeleo ili Vyu hivyo viweze kutekeleza majukumu yake. Mfano Chuo Kikuu Huria kinadai fedha za maendeleo kwa muda mrefu sasa. Ni lini Serikali italipa madeni haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawajibika kuandika ama kuchangia hotuba za bajeti ya Wizara hii ukizingatia hali mbaya ya uchumi nchini kuanzia Elimu ya Awali hadi Elimu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kushuhudia kushuka kwa elimu nchini na Wizara yenye jukumu la kuhakikisha elimu yetu nchini inakuwa bora, ni Wizara hii na hata katika kitabu chake cha bajeti ya mwaka 2015/2016 ameanisha majukumu ya Wizara katika ukurasa wa nne na wa tano, vitu ambavyo vyote havitekelezeki wala kutimia.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri sera zote za elimu zinatungwa lakini hazitekelezeki kama kusudio halisia la elimu kwa sasa. Mfano, sera ya elimu ya Shule za Awali inatamka dhahiri kuwa Walimu wa kufundisha watoto wa awali lazima wawe na Diploma ya Ualimu wa awali, lakini ukweli ni kuwa sehemu nyingi hazina Walimu hawa hasa vijijini, ndiyo hamna kabisa. Je, uhalisia wa sera hii upo wapi? Pia inazungumzia kuwa Shule za Awali lazima ziwe kwenye shule husika ya msingi na mtoto akimaliza Elimu ya Awali anajiunga moja kwa moja kwenye hiyo Shule ya Msingi. Ukweli mchungu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Shule za Msingi hasa vijijini zipo mbali, kwingine ni kilomita tatu au zaidi. Sasa ujulize, huyu mtoto wa awali atawezaje kutembea kwenda shuleni ilhali hata gari ama usafiri wa kwenda huko hamna, hasa vijijini? Ni dhahiri hamna dhamira ya dhati kurobeshwa elimu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Elimu ya Msingi, kuna upungufu mwingi sana na mkubwa wenye athari kwa elimu na zao la elimu miaka ijayo. Leo hii bado tunaendelea kushuhudia uwiano wa Mwalimu kwa mwanafunzi ukiwa hata Mwalimu mmoja na wanafunzi zaidi ya mia mbili hasa vijijini ambapo unakuta Walimu watatu tu kwenye shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaendelea kushuhudia mazingira mabovu ya kufundishia na kujifunzia. Leo hii unakuta Walimu hawana ofisi, wanakaa kwenye miti tena shule za vijijini kabisa, mfano Shule ya Msingi Mapinduzi, Sabasaba za Mjini Tarime. Walimu wanakaa nje ndiyo ofisi zao. Shule ilikuwa ni Saba Saba tu, lakini leo hii kuna shule tatu pale tena zinaingia kwa *shift* kwa maana ya Azimio, Saba Saba na Mapinduzi. Mazingira ya hii shule yenyewe ni duni, ni ya zamani na ipo mjini na majengo ni hatarishi kupitia mfumo wa *shift*. Kiukweli, hawa wanafunzi wananyimwa muda wa kujifunza kama ilivyokusudiwa na ambavyo watoto na wenzao wanafaidika na muda mwingi wa kujipima na kujifunza darasani, huku hawa kwenye shule tatu zenye *shift* wakipunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo haki. Naomba Serikali ilianganalie hili na kulipa kipaumbele ili kila shule ipate muda wote. Vilevile katika Halmashauri ya Mji wa Tarime kuna Shule ya Msingi Nyamisangure ambayo inachangia madarasa na Shule ya Msingi Tarime. Hii inadhoofisha uelewa wa wanafunzi na inanyima muda wa wanafunzi kujifunza. Hii inatoa athari kubwa sana kwani Walimu wanalazimika kuondoka mara baada ya muda wao wa *shift* na hivyo kukosa muda wa kujiandaa na ukizingatia Walimu hawakai pale pale shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika Elimu ya Msingi ni ukosefu au uchakavu wa majengo ya Shule hizi za Msingi, miundombinu ya choo ni mibaya sana na hatarishi kwa afya ya watoto na Walimu kitu ambacho kinapelekea shule kufungwa. Mfano, Shule za Msingi zaidi ya sita Wilayani Tarime zimeshafungwa na nyingine zipo mbioni kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Shule hizi za Msingi hazina maktaba kabisa. Mfano, shule takribani zote za Mkoa wa Mara za Msingi, siyo za Vijijini wala Mijini, hazina maktaba kabisa. Ikumbukwe maktaba ni moja ya *inputs* au miundombinu hitajika katika shule zetu. Maktaba ni eneo tulivu ambalo linawapa fursa wanafunzi kujisomea na kupata vitabu ili kutunza uelewa baada ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule nyingi za Msingi siyo tu zina mejengo chakavu, bali hazina madawati, sakafu ni ya udongo/mchanga, hamna vitabu, hamna madarasa ya kutosha, hamna Walimu wa kutosha na hamna nyumba za Walimu. Kiukweli, inasikitisha sana na haionyeshi dhamira ya dhati ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu katika kuboresha miundombinu



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya Elimu ya Msingi nchini. Kinyume cha hapo, hamna elimu bora bali bora elimu. Ni aibu hadi sasa tuna shule zinakaa kwenye miti. Hivi karibuni tulishuhudia wanafunzi huko Peramiho Jimbo la Mheshimiwa Jenista ambaye ni Waziri, watoto wakifanya mitihani chini ya miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu ambayo yamekuwa ya muda mrefu sasa, ambayo ni pamoja na yale ya uhamisho na mengineyo, tunaomba Walimu hawa walipwe. Vilevile, kuwepo na motisha kwa Walimu wanaofundisha katika mazingira magumu ili kupunguza wimbi la Walimu kukimbia vijijini mara wanapo-report kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika suala zima la Elimu ya Msingi, ni vyema Serikali iwezeshe ujenzi wa nyumba bora na imara katika Shule za Msingi zote, maktaba, vyoo ni muhimu sana. Kinyume na hapo, itapelekea maambukizi ya magonjwa, rejea hali halisi ya choo kwenye tangazo la Haki Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Elimu ya Sekondari, ni matatizo yale yale kama ya msingi. Hizi sekondari hazina maktaba, hazina maabara ndiyo zimejengwa kwa agizo la Mheshimiwa Rais, lakini vifaa vya Maabara ni kiini macho. Uhaba wa Walimu hasa wa sayansi; kwenye ziara yangu mashuleni Mkoani Mara nimegundua uhaba wa Walimu wa masomo ya sayansi hamna kabisa! Sasa hata hizi Maabara nani atazifundishia? Hatua madhubuti zichukuliwe yashughulikiwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Walimu kutokuwepo kwenye sekondari hizi nalo ni tatizo sana na hatarishi kwa Walimu. Lakini pia linapunja muda wa Walimu kufika shuleni na kuondoka mapema ili wawahi uraiani ambapo wanaishi. Lakini pia kwa zile shule zenye nyumba shuleni, mfano Shule ya Sekondari ya Indufu iliyopo Tarime nyumba zake ni mbovu, zinavuja kitu ambacho ni hatarishi kwa maisha ya Walimu na familia zao. Hawana choo ndani ya uzio wa nyumba zao kitu kinachopelekea wajisaidie kwenye makopo na *plastic bags*. Hii siyo haki kwa rasilimali nyingi tulizonazo kwenye nchi hii. Hii ni fadheha sana tena sana kwa mustakabali wa nchi yetu.

Hivyo, naomba shule zetu za msingi ziwe na Maabara, Maktaba, vitabu na Walimu wa kutosha kwenye shule hizi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni juu ya Elimu ya Juu, imekuwa mwiba kwa watoto wa masikini ambao wameendelea kupigwa na mabomu kwa kudai fedha ambazo wapo *entitled* kulipwa kwa wakati lakini hatuoni Watendaji waliofanya uzembe wa kutopeleka fedha kwa wakati. Pia, kumekuwepo na uchakachujaji wa nani anastahili kupewa mkopo, kitu hiki kimewaacha wengi wenye uhitaji na masikini na kuwapa wasio na mahitaji, kwa maana ya wenye uwezo. Nawasilisha.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya maendeleo ya elimu ambayo ni ya muhimu sana kwa Taifa letu iko chini ya ufadhili wa wageni mfano, UNICEF, Benki ya Dunia, Serikali ya Sweeden, Ufaransa, Canada na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi inaweza kuwa msaada mkubwa katika kuwasaidia vijana wetu kupata ajira kwa kujijiri wenyewe. Hata hivyo, fedha iliyotengwa katika mwaka 2015/2016 ili kuboresha na kuendeleza elimu ya ufundi ni fedha za ndani Sh. 1,000,000,000/= tu na fedha za nje ni Sh. 5,382,362,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ya kuimarisha vijana kiuchumi ambao wengi wao hawana ajira ni kuboresha na kuendeleza elimu ya ufundi kwa kutenga fedha za ndani za kutosha kuliko kuendelea kutegemea wafadhili ambao hata wao huko kwao wana matatizo yao ya kuwatosha.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke kipaumbele katika elimu ya ufundi ili kupunguza tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu ambao wengi wao wapo njapanda, hawajui la kufanya. Fedha ya ndani zitengwe za kutosha kama zilizotengwa ni kidogo sana kulingana na uhitaji uliopo kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetelekeza elimu ya Walimu kwa kutoitengea fedha ya kutosha katika mwaka huu wa fedha 2015/2016. Fedha iliyotengwa katika eneo hili kufuatana na randama ni fedha za ndani Shilingi sifuri na fedha za nje Sh. 3,000,000,000/= kutoka Serikali ya Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Serikali ya Canada itashindwa kutoa fedha hizo kwa wakati, basi ukarabati wa Vyuo vya Walimu hapa nchini vitaendelea kuwa na hali mbaya/duni kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mchango wangu hapa.

Upungufu wa vifaa vya kufundishia; kuna upungufu mkubwa wa vitabu katika shule za msingi na sekondari hapa nchini umuhimu wa wanafunzi kuwa na vitabu unajulikana kwa kuwa inamjenga katika uelewa wa masomo anayojifunza. Nini mkakati wa kuhakikisha vitabu vipo vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo katika Vyuo Vikuu; kumekuwa na dhana ya Serikali kutopeleka fedha za maendeleo katika Vyuo Vikuu hasa Vyuo Vikuu vikongwe. Ni muhimu Serikali ikahakikisha fedha za maendeleo zinapelekwa kuliko kuviacha bila ya fedha. Serikali isipuuze na kuviacha Vyuo Vikuu bila ya fedha za maendeleo, huko ni kuviua vyuo hivyo. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa Vyuo hivyo vinapata fedha kwa wakati?

Usajili wa Vyuo Vikuu vipya na binafsi; kuna umuhimu wa TCU kutokuangalia namba ya Vyuo Vikuu wanavyosajili bali kuzingatia mambo ya msingi kuhusu vyuo hivyo kama vina mitaala na miundombinu inayokidhi kuitwa Vyuo Vikuu na siyo kusajili tu ili mradi kuongeza idadi na si ubora. Ni muhimu sana kwa TCU kuangalia ubora wa Vyuo hivyo vilivyosajiliwa tayari kwa kuvihakiki tena ili kuangalia elimu wanayoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Vyuo ambavyo vimeonesha udhaifu na kukosa sifa ya kuitwa Vyuo Vikuu kwa mfano, *Saint Joseph* na *Kampala University*, tunahitaji hatua za haraka zichukuliwe kwa Vyuo hivyo.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze suala la elimu ya msingi imeshuka kwani mwanzo wa msingi ulio bora ni bora na si bora elimu isiyokuwa na tija. Elimu iliyokuwa na nzuri ni kuachana na suala la udini na ukabila. Itagharimu Taifa hili kukosa watoto wasiojua kusoma na kuandika kutokana na Serikali kutaka watawala na si utawala wa kujijua na kujitambua, bali kukuza watoto tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao uchungu mkubwa wa suala la elimu ingerudisha elimu ya mwanzo kama ilivyokuwa kipimo darasa la nne, akishindwa kusoma na kuandika arudishwe darasa na kupimwa kiuwezo kwani si vema kuwapeleka tu huku tukisema watoto wetu wamemaliza elimu ya msingi na wameanza elimu ya sekondari wakati hawana uwezo hata wa elimu ya msingi, ni aibu kubwa.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukizwa na sera isiyotimilika, hatutendi haki kwa vijana wetu waingiapo vyuo vikuu, aibu nchi hii vijana mpaka waidai mikopo ndiyo muwape na wamalizapo hawana ajira. Je, Serikali inaposimamia elimu inatarajia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya ufundi, vijana hujitunga kwa pesa zao kwa maana ya kulipa ada ya mafunzo na kupata vyeti, lakini hamuwapi tenda za ajira wanahangaika, bila Serikali kujua wingi uliopo wa ajira kwa vijana ni ndoto nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumaliza changamoto zinazoikabili Sekta hii ya Elimu na Ufundi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna vitendea kazi kwenye baadhi ya Vyuo vya Ufundi kama kule kwenye Chuo cha Malia bado, VETA zilizopo Dodoma na Kondo hakuna vitendea kazi kwa vitendo, hii husababisha kuzorota kwa elimu nchini na kukosa ajira na kukosa elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya Walimu, kutopewa Walimu pesa zao za pensheni na uhamisho. Je, ni lini Serikali itatua migogoro hii ili iishe bila kuleta fujo? Tunashuhudia leo kero za vijana wa vyuo mkigogana nao kwa kupinga mabadiliko ya vyeti vya *diploma* chuo cha *LTI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madawati mashuleni hakuna, baadhi ya Mikoa imekuwa tatizo. Vyoo hakuna, baadhi ya mashule imekuwa tatizo kubwa kwa wanafunzi na Walimu hasa Kondo. Ukitembea baadhi ya mashule vyoo ni tatizo, mazingira yaliyopo hapo ni tatizo. Maji hakuna, afya ni lazima. Je, kwa mazingira haya ambayo haina mashiko ya bajeti ya kutengeneza miundombinu ya elimu watoto wetu wataishije?

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pia naipongeze Wizara kwa kazi nzuri inayofanya na kuongeza ufanisi wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; ipo haja ya kuangalia upya kwani kuna wanafunzi wengi wanaofaulu masomo ya *Arts* na wanatoka katika familia maskini, watu hao wanakosa mikopo na wanashindwa kuendelea ipi ni mipango ya baadaye kwa wanafunzi wa aina hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migomo ya wanafunzi mashuleni; ni mibaya inaleta madhara na uharibifu mkubwa. Baadhi ya nyakati hali hii isipodhibitiwa na kuachwa iendelee, inawakatisha tamaa wale wanafunzi wasiotaka kugoma, kwani hulazimishwa na wasipokubali hupigwa au kuzuiwa wasiendelee na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa kike kutoendelea na masomo mara baada ya kupata mimba; suala hili linarejeshwa nyuma maendeleo ya wanawake hasa ukizingatia kuwa mimba ni mashirikiano kati ya mwanamume na mwanamke, lakini adhabu hii inamkabili mwanamke tu jambo ambalo siyo sawa, kwani huu ni unyanyasaji wa kijinsia. Tunaiomba Wizara ilete Sheria Bungeni tuibadilishe ili kumnusuru mtoto wa kike na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango au ada mashuleni; Tunaipongeze Wizara kwa matamko ya mara kwa mara kuwa wanafunzi wasikose elimu kwa kukosa kulipa ada, lakini hadi sasa wapo wanafunzi toka familia maskini walikosa kuendelea na masomo kwa kukosa kulipa ada. Tunaiomba Wizara iweke msisitizo katika jambo hili tusije tukawa na matabaka katika nchi yetu utegemezi utaongezeka na nchi itakuwa na mzigo mkubwa wa wajinga.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule binafsi; Wizara ya Elimu isiwe mbali kufahamu utendaji kazi wa shule binafsi. Hali hiyo itasaidia kuwa na utawala bora katika Sekta ya Elimu na kupunguza changamoto mbalimbali kama ubaguzi, malipo ya ada kuwa makubwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi; ukaguzi wa elimu haiufanyiki maeneo yenye ukaguzi hakuna pesa wala magari na vifaa vingine, kwa nini hamjali elimu? Elimu ikikaguliwa ubora utaongezeka, hamuoni kutokukagua elimu ndiyo maana elimu inashuka? Wakaguzi wakifika watagundua mengi, shule nyingi vijijini hazina hadhi ya kuitwa shule hazina vyoo, madawati, sakafu na nyingine hazina paa na wengine madarasa hayatoshi wanasomea chini ya miti. Zingine hazina milango wala madirisha kwa kuwa hazikaguliwi ndiyo maana siyo rahisi kuzitambua na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya shule na baadhi ya vyuo, vyoo vibovu mabomba kwenye mabafu mengine yamepasuka na vyoo vingine vimeziba, kagueni muondoe upungufu huu hasa *University of Dar es Salaam*, majengo mengi ni ya zamani, yamechoka, hivyo upungufu ni mwingi na vyuo vingi vilivyochakaa vina upungufu huo nilioutaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile shule za sekondari hasa zile kongwe zina upungufu mwingi, unafanana na huo nilioutaja hapo juu, fuatilieni shule kama Tabora *Girls, Boys, Mazengo*, Msalato na nyingine nyingi kongwe, nyingi zinahitaji marekebisho makubwa ili ziendeleo kuwepo kwani ni shule za kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho hayo ya shule za kale yanakwenda sambamba na marekebisho ya shule ambazo siyo kongwe kwani nazo zina upungufu mbalimbali kwa upande wa shule za msingi zipo pia baadhi ya shule zenye matatizo niliyoyataja, nazo zinahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo ya TEHAMA; Vijiji vyetu vingi havina umeme, hivyo shule zetu pia hazina umeme, lakini pia zipo shule nyingi mjini hazijaunganishwa na umeme, hivyo ni ngumu kuwafundisha somo la TEHAMA, lakini pia shule hazina maabara yaani (*computer labs*), watoto wanachorewa ubaoni wataelewaje wakati wapo watoto wengine hata TV hawajawahi kuona. Kama Serikali imeamua somo la TEHAMA lifundishwe basi miundombinu inayotakiwa iwekwe. Tuache usanii katika elimu. Mazingira mabovu, elimu kutotolewa kivitendo inasababisha wanafunzi kufeli na elimu kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya Mitaala; Mitaala inabadilishwa lakini Walimu hawapewi mafunzo au semina. Serikali ikibadili mitaala iwape semina au mafunzo elekezi ili Walimu waweze kufundisha vizuri na waendane na wakati kulingana na mitaala mipya inayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matabaka katika elimu; Wazazi wenye uwezo hawapeleki watoto wao kwenye shule za Serikali kwa kuwa nyingi ni duni na hazina vifaa. Shule za *private* zina maabara za sayansi, maabara za kompyuta, Walimu wa kutosha, chakula shuleni madarasa na mazingira mazuri, viti, madawati na wafanya usafi. Mtoto anayesoma shule ya *Private* hawezi kufanana kiasya na uelewa wake na shule duni za Serikali, tunaona matokeo tofauti na hata kwenye matokeo ya mitihani.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye mkakati wa kuboresha shule zetu za msingi na sekondari ili elimu inayopatikana kwa mtoto wa Kitanzania maskini, Serikali iweke *standard* nzuri ya elimu ili kusiwe na tofauti kubwa kati ya mtoto wa shule ya Serikali na wa *private*.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara katika sekondari zetu; naipongeza Serikali kwa ujenzi wa maabara nchini, hii itaimarisha na kuboresha uelewa wa masomo ya sayansi kwa wanafunzi wetu wa vidato cha kwanza mpaka cha nne katika bailoija, fizikia na kemia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, somo la *ICT* (kompyuta) linahitaji pia kuwa na maabara yake kwa umuhimu wa somo hili ili vijana wapate uelewa wa kina na mapana na kuweza hata kujijiri mara wanapomaliza elimu ya vyuo vikuu. Ingefaa *ICT* ifundishwe tangu shule za msingi, hivyo tujenge maabara nne badala ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulaya (*EU*) asilimia 50% ya wanafunzi kutoka vyuo vikuu wenye uelewa wa *ICT* (*TEHAMA*) wanajijiri kwa kuanzisha kampuni zao. Marekani asilimia 70 ya wahitimu wanaanzisha Kampuni binafsi na kujijiri. Mitaala yetu ilenge kukuza sekta binafsi na siyo kuajiriwa Serikalini au katika sekta ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira katika kilimo itenge matumizi bora ya sayansi na teknolojia pia katika ufugaji na uvuvi pato litakua na uchumi utakuwa wa kati ifikapo 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitaala ya Sayansi, Teknolojia na Ujasiriamali; miaka ya 60 na mwanzoni mwa 70 elimu ya kilimo bora, uvuvi wa kisasa na matumizi ya uhifadhi wa chakula na nafaka ilikuwa ni sehemu ya mitaala tangu shule za msingi. Sayansi ya Kilimo na Uhandisi wa Kilimo kupitia Maafisa Ugani. Mafunzo ya matumizi ya mashine za ukamuaji mafuta ya alizeti, ufuta, karanga, yafundishwe shule za msingi kujenga uwezo mapema wa kuongeza thamani katika mazao hayo (*value-chain*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa na Mikongo ya Kimataifa – Chanzo cha Ajira kwa vijana; utakumbuka kati ya Wizara Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, *TAMISEMI*, ubuniwe ili Halmashauri kuwe na *hub* za kutumia mkongo wa Taifa na Kimataifa (*EASY, SECOM, TIS* na kadhalika) ili kuchakata biashara (huduma) *Business procesing* za Kimataifa kwa mikataba ya kibiashara na kuanzisha maeneo ya viwanda mbalimbali vya uunganishaji (*Assembly*) ya bidhaa mbalimbali za kielektroniki kwa kuingia mikataba na makampuni ya Kimataifa Ulaya, Marekani na Asia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maabara za shule za mfano sekondari Goweko na Tura kwa fedha za Benki ya Dunia zijengwe bajeti hii. Moja ya hizi shule iwe ni ya mfano kufundisha komputa kwani umeme tayari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika kumi na tano!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ambayo nitatumia kuchangia hoja za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nianze kwa kauli ya kwamba, naunga mkono hoja hii ya elimu, elimu ndiyo ambayo inatuletea tija nchini na tutaendelea kuimarisha kama Serikali ili Watanzania wapate elimu inayotarajiwa. (*Makofi*)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi kubwa niliyopewa hapa ni ya mambo matano ambayo nitajitahidi kutoa ufafanuzi na hasa katika kuwapa matumaini Waheshimiwa Wabunge na kuwaomba tushirikiane katika kufanya kazi za elimu ili tuboreshe wote kwa pamoja. Sisi TAMISEMI na Wizara ya Elimu kwa pamoja, tumeendelea kuratibu mambo yote ambayo mnashauri na malengo yetu kwa pamoja ni kufikia malengo mazuri kwa maana ya kuwa na mafanikio yaliyo sahihi.

Moja kati ya jambo ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni lile ambalo linawagusa sana Walimu wetu kwenye eneo la madeni. Eneo hili nimelieleza mara nyingi na hata nilipokuwa nachangia hoja za Wizara yetu kwenye Ofisi yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nililieleza pia vizuri. Ninaomba nitumie nafasi hii pia katika kurudia, lakini kujiridhisha na hili na kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, sisi Serikali kwenye Sekta ya Elimu, shughuli zetu sasa tunafanya kazi pamoja na Chama cha Walimu Tanzania, ambacho chenyewe kimechukua nafasi kubwa ya kufanya ufuatiliaji na kutushauri Serikali namna sahihi ya kuboresha elimu.

Nataka niwaambie kwamba, wiki moja iliyopita tulikuwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania kule Jijini Arusha na Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu yupo hapa. Ninafurahi kuwaambia kwamba, Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania, alipokuwa anatoa taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, moja ya eneo ambalo aliona na kulieleza kwa Rais ni kuridhishwa kwake kwa namna ambavyo Serikali sasa imeendelea kujitahidi kupunguza kwa kiasi kikubwa, kuwepo kwa madeni ya Walimu. Nataka niendeleo kumthibitishia Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu, lakini na Walimu wenyewe na Waheshimiwa Wabunge chukueni hii kama *position* yetu Serikali kwamba, tumeendelea kuratibu vizuri madeni ya Walimu na kuyawekea utaratibu wa namna ya kuyalipa na tumeendelea kuyapunguza vizuri zaidi na tunatafuta utaratibu mzuri zaidi wa kutokuwa na madeni ya Walimu kwa kiasi hiki ambacho tulikuwa nacho. (*Makofi*)

Utaratibu tuliokuwa tunautumia awali wa kuwa tunaacha madeni halafu tunakurupuka mara moja kuyahakiki na kuyalipa, tunataka tuimalize baada ya kuwa tumekusanya madeni ya mwisho yaliyofikia shilingi bilioni kama 54 hivi na tumeanza kuyalipa kwa kusaidiana na Ofisi ya CAG kuyahakiki kujua deni gani ni sahihi na lipi siyo sahihi; kwa sababu tumeona mara nyingi madeni yanazidi kuwa makubwa zaidi, hata tukilipa leo madeni tutakayoyapata kesho ni makubwa zaidi. Tumeendelea kuhakiki na kwa bahati nzuri kufikia mwezi Aprili mwaka huu, zaidi ya shilingi bilioni 25 tumeshalipa madeni hayo. Madeni ambayo yamehakikiwa na CAG, yenye thamani ya shilingi bilioni tano yapo na yatalipwa. Hazina wametuhidi kwamba, watalipa mpaka kufikia mwaka huu wa fedha na kwa bahati nzuri Naibu Waziri wa Fedha atasimama ataeleza utaratibu atakaoutumia katika kulipa hili. Kwa hiyo basi, madeni haya yataendelea kulipwa.

Bado hatuishi hapo, madeni haya yapo katika maeneo mawili makubwa. Moja ni yale ambayo yanatokana na kupanda kwa madaraja, kubadilika kwa daraja la mshahara wa zamani na kupata mshahara mpya. Eneo hili ndiyo la malimbikizo yenye malipo haya makubwa.

Eneo la pili kama ambavyo nilisema ni eneo ambalo linajumuisha likizo, matibabu, masomo na posho mbalimbali. Eneo hili linalipwa kupitia OC kwenye Halmashauri zao na tumeweka utaratibu mzuri sana wa ulipaji wa madeni haya. Likizo zinalipwa na TAMISEMI kwa kuwapelekea fedha kila inapokaribia muhula, kutokana na idadi kubwa ya Walimu hatujamudu. Niseme kabisa kwamba, hatujamudu kulipa fedha za likizo kwa 100% kwa Walimu wote wanaopaswa kwenda likizo. Tumeendelea kujitahidi kwa zaidi ya 50% kulipa fedha hizi za

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

likizo kwa Walimu ambao wanapaswa kwenda ili waende kwenye likizo zao. Tutajitahidi kuongeza bajeti yetu ili tumudu kulipa fedha ya kuwawezesha Walimu kwenda likizo.

Malipo yote ya uhamisho wa ndani, tumetoa maelekezo mazuri kwa Halmashauri na ninaomba nirudie; tumeleza kwamba, Afisa Elimu au Mkurugenzi si lazima ahamishe Mwalimu kama hana fedha za kumlipa Mwalimu. Ingawa uhamisho upo pale ambapo unatokea ni pale ambapo labda Mwalimu hana mahusiano mazuri kwenye eneo hilo ni lazima umbadilishie kituo. Ukitaka unataka kuweka vizuri ikama ya Walimu kwa masomo lakini pia kwa uongozi, huo uhamisho upo, uhamisho huo siyo mkubwa wa kuzalisha madeni kwa kiwango hiki.

Kwa hiyo basi, madeni haya yote tunayaratibu kwa pamoja, tunashirikiana na Halmashauri kupitia OC inayokwenda ingawa si kubwa sana, lakini inaweza kulipa maeneo haya. Posho za kazi za ndani hizi zinapopangwa kazi zile zinakuwa na malipo yake, kama sasa ambapo tunaleta Walimu zaidi ya 5,000 hapa Dodoma kusoma taaluma ya KKK, tunalipa kila kitu na hatuna madeni. Kwa hiyo, Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba, eneo hili hatuzalishi madeni.

Waheshimiwa Wabunge, nataka niwahakikishie kwamba, kazi tunayoifanya pamoja na Chama cha Walimu Tanzania ya kushauriana na kuona namna bora ya kuboresha sekta hii iendelee vizuri; na kwa kuwa wamekiri kwamba tunafanya kazi vizuri na sisi pamoja na pongezi hizo ni wajibu wetu kuendelea vizuri katika kuhakikisha eneo hili hatupati madeni makubwa.

Eneo la pili ni lile ambalo limezungumzwa na mama yangu Mama Al-shymaa na Mama Mkanga, juu ya huduma za wanafunzi wetu wa elimu maalum. Nataka niwahakikishie kwamba, sasa tumeendelea kuweka mazingira mazuri ya vijana hawa kupata elimu ya msingi na ngazi zote zinazofuata. Kwanza, tulichokifanya, tumehakikisha tumejenga msingi imara kwa jamii yetu, kila mwenye mtoto nchini mwenye ulemavu wa aina yoyote ile, ni lazima ampeleke shule pale anapofikia umri wa kwenda shule. Tumeitaka pia jamii, kama yupo mzazi anamficha mtoto wake mlemavu nyumbani, jamii itusaidie kuwaibua watoto hao, lazima waende shule. Utaratibu tuliouweka Wizarani na kwenye Halmashauri zetu ni kuhakikisha watoto hawa wanapata elimu sawa na watoto wengine na wacheze pamoja na watoto wengine ili kuondoa ile hali ya kujiona wako tofauti na wengine.

Takwimu tulizonazo mpaka Aprili 2015, tuna idadi ya watoto 11,794 wa Elimu ya Msingi wapo madarasani wanaendelea na tuna takwimu ya wanafunzi wa Sekondari 1,406 ambao wanapata elimu ambao wamefaulu Darasa la Saba. Hawa wote tumewataka wakae darasani kwa pamoja na watoto wengine wote walioimarika kwa viungo, lazima wasaidiane na watoto hawa katika kuwasaidia ili kuweza kupata elimu, watacheza pamoja, lakini pia watapata msada wao.

Pale Wizarani TAMISEMI, Kitengo hiki kimeimarika, tayari tumeshapata Afisa Elimu ngazi ya Wizarani ambaye pia anashughulikia elimu maalum. Afisa huyu pia ameshasimamia uimarishaji wa vitengo katika kila Halmashauri. Tunaye Afisa Elimu katika kila Halmashauri anayeshughulikia elimu maalum. Wakati tunaendelea na haya, tunaendelea kutenga bajeti kupitia bajeti ya Idara ya Elimu ya pale TAMISEMI, kwa kutenga fedha za mahitaji maalum. Kwa mfano, Mwaka wa Fedha 2014/2015 tulitenga jumla ya shilingi bilioni 7.5 ambazo zinakwenda kwenye shule za bweni za watoto wenye mahitaji maalum kwa ajili ya ununuzi wa chakula. Fedha hii tuliipeleka Shule ya Migongo kwa ajili ya kuimarisha Bwalo lao ili watoto hawa wakae mahali salama wanapopata chakula chao.

Kupitia mpango wetu wa kifedha Wizarani, kwenye Elimu Maalum tulitenga shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia kwenye maeneo hayo.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Vilevile kuna vifaa ambavyo kijana mmojammoja anavitumia; kwa mfano, fimbo kwa wale ambao wa uono hafifu, tumenunua *lotion* au mafuta kwa vijana ambao wana matatizo ya ngozi, kuna vitabu vya nukta na mashine zake pamoja na baiskeli kwa walemavu wa viungo pamoja na viongeza sauti kwenye masikio kwa watoto wetu ambao wana usikivu hafifu. Kwa hiyo, tumeendelea kutenga fedha kwa ajili ya hili.

Hatujaishia hapo, tumepeleka fedha kwenye Halmashauri, jumla ya shilingi bilioni tatu tumezipeleka Halmashauri na kila Halmashauri imepata shilingi milioni sita kwa ajili ya kununua vifaa kulingana na mahitaji ya mtoto aliyepo kwenye shule ya msingi au sekondari ili apate elimu yake. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba, eneo hili tunaendelea nalo. Nami namshukuru sana Mama Al-Shaymaa, mara nyingi amekuwa akilieleza jambo hili, lakini tumemwona akipita kwenye shule zetu na anapita kwa wananchi kusaidia kutoa elimu ya kuwaibua watoto hawa ili waende shule. *(Makofi)*

Mama Mkanga pia ameendelea kuwasemea. Wote kwa pamoja mmeendelea kulisemea eneo hili na Wizara kwa maana ya Serikali, imewasikia na tutaendelea kuimarisha eneo hili ili tupate manufaa makubwa. *(Makofi)*

Eneo lingine ambalo nitatumia muda huu kulizungumza ni suala la miundombinu. Tumeendelea kulitekeleza jambo hili na utekelezaji wetu ni uleule wa ushirikishaji Wananchi kwenye maeneo yetu. Tumepata mafanikio makubwa sana kwenye eneo hili, ambayo tumeanza kuyaona. Ukilinganisha hali tuliyokuwa nayo mwaka 2005 mpaka 2015 ni nzuri kwa kuwa na idadi kubwa ya shule, lakini pia tumeongeza Walimu. Hatujaishia hapo tu, mpaka vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vitabu, kule maabara tumeweza kutenga fedha na kuwapelekea kwenye Halmashauri waweze kuvinunua. Wajibu tulionao sisi ni kukagua kama vifaa hivyo vipo na vinatumika. Matokea ambayo tunayaona sasa ni jitihada za uwepo wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo pia Mheshimiwa Mrema alilizungumza ni la pale Moshi na alisema anataka maelezo sahihi. Kama ambavyo tulieleza na niliwahi kulijibu hilo swali lake kwenye maswali ya kawaida Bungeni kwamba, mgogoro uliokuwepo pale Moshi ni kati ya Walimu na Maafisa Elimu kwa Maafisa Elimu kutotoa huduma safi kwa Walimu, wanapouliza hawapati majibu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeendelea kuimarisha Halmashauri zote nchini kuwa na Maafisa Elimu ambao wako tayari kuwahudumia Walimu wetu. Tumetoa msisitizo, kila Afisa Elimu ni lazima ampokee Mwalimu, amsikilize na amhudumie, hata kama jambo atakalolisema hanalo wakati huo lakini ni lazima Mwalimu apate jibu sahihi. Wale wote ambao tumepata taarifa zao hawafanyi vizuri, tumewaondoa na tumewaweka watu wengine. Hicho ndiyo ambacho tumekifanya pale Moshi, wale Maafisa Elimu ambao hawakuwa na mahusiano mazuri na Walimu; na kwa kuwa tatizo lao lilikuwa si kula fedha au kuharibu mali, ispokuwa mahusiano; tuliwaondoa Halmashauri ya Moshi na kuwapeleka mahali pengine. Pale Moshi tumepeleka Maafisa Elimu ambao kwa kweli sasa wanafanya kazi vizuri na Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madeni tumeendelea kulipa kama ambavyo nimelieleza kwenye utaratibu huu, ni wa nchi nzima pamoja na Moshi. Malipo ya ndani tumeendelea kuyaboresha kwenye OC pamoja na Moshi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mrema usiwe na matatizo kabisa, ninaomba utupitishie bajeti yetu tuweze kuendelea na utekelezaji na tutakuhudumia. Tunatambua sana mchango wako pale Moshi kupitia hata Mfuko wa Jimbo, ingawa pia kidogo ulileta matatizo, lakini ninataka kukuhakikishia Mfuko wako kwa namna ambavyo unachangia, endelea kufanya hilo na kama ambavyo Serikali inaendesha elimu kwa ubia na wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wewe pia ukiwemo. Kwa hiyo, endelea na kazi hiyo. *(Makofi)*



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa sababu ya kengele nitoe, taarifa kwamba, ajira mpya ya Walimu imekamilika na sasa Walimu wanaenda kuripoti. Awamu ya pili wanaripoti kuanzia leo na *deadline* ni tarehe 5. Walimu hawa tunatarajia watakapofika vituoni, taratibu zao zote zitakuwa zimekamilika pamoja na zile stahili zao za siku mbili, tatu, za kuishi ili waweze kwenda vituoni kwao. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, atatoa taarifa nzuri ya namna ambavyo wameteteleza utumaji wa fedha hizi kwenye maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na kundi la vijana wetu ambao walikuwa na *supplementary* hatukuwaingiza kwenye ajira ya kwanza, lakini tulipopata taarifa wale wote ambao wanastahili kuajiriwa na wame-*clear supplementary* zao, tayari nao tumewaingiza kwenye kundi hili na wataendelea kushirikiana na wenzao. Kwa hiyo, tuwatake Walimu wetu hawa waliokwenda kuripoti waende wakafanye kazi yao, wawe na matumaini na Serikali yao na tutaendelea kushughulikia matatizo yao pale wanapokuwa vituoni. Halmashauri tumepata taarifa nzuri wanawapokea na wanawasindikiza kwenye vituo vyao vya kazi, jambo ambalo pia tumelitaka liendelee vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, wale ambao watakuwa hawapo katika awamu hii na kwa kuwa kibali chetu ambacho tulipata cha kuajiri Walimu 31,056 kitakuwa kimekamilika, bado tuna ajira nyingine ya Walimu, hapo itakapotangazwa wale wote waliokosa sasa tutawaajiri kwenye kipindi kijacho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza haya, ninajua mengi zaidi yataelezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu, Mama Malecela, lakini pia na Mheshimiwa Waziri wetu atakuja kuweka vizuri mambo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja tena, ahsante sana kwa kunisikiliza. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Majaliwa. Sasa ninaomba nimwite Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu, dakika kumi!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie mawili, matatu, katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja.

Jambo la kwanza ambalo limeongelewa kwa kirefu na Waheshimiwa Wabunge, lilikuwa linahusisha madeni, malimbikizo, pamoja na madeni ya watoa huduma. Tukianza na hili la malimbikizo kwa upande wa watoa huduma, Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla kwanza ilifanya uhakiki na baada ya uhakiki mwaka wa fedha ulipoanza, ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 180 kwa ajili ya madeni ya watoa huduma waliotoa katika Wizara mbalimbali ikiwemo na Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kwa upande wa watoa huduma, Wizara ya Fedha iliandaa zaidi ya shilingi bilioni 50 na sasa tayari tangu Wiki mbili zilizopita imeanza kulipa madeni ambayo tayari yalishahakikiwa. Kwa hiyo, kwa wale ambao walitoa huduma, wajue tayari mchakato huo wa kuwalipa unaendelea na watapewa fedha zao ili waendelee kutoa huduma hizo.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa watoa huduma na umuhimu wa kuwalipa watoa huduma. Tunatambua kwamba, watoa huduma wengine mitaji yao hiyo waliipata kwa kukopa. Kwa hiyo, asipopata malipo yake anaweza akaingia kwenye matatizo na benki na yeye mwenyewe kuyumba katika biashara yake. Kwa hiyo, Serikali inalitambua hilo na imechukua hatua hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme miongoni mwa vitu ambavyo Watanzania watamkumbuka Waziri wa Fedha, boshi wangu Mheshimiwa Saada, ni pamoja na kuyazingatia mahitaji haya ya watu ambao tayari yako Serikalini, kwa kufanya uhakiki na kuwalipa yale ambayo wanastahili kulipwa. Kama ambavyo tumeendelea kusema, katika deni lililokuwa zaidi ya shilingi trilioni moja mwaka jana, lilipohakikiwa fedha ambayo ilitakiwa kulipwa ikaonekana ni chini ya shilingi bilioni 500. Hata kwa upande wa madeni haya ya malimbikizo, ilipokuwa inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 29, uhakiki ulipofanyika ikaonekana zinazotakiwa kulipwa ni shilingi bilioni 5.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata sasa madeni yote yamehakikiwa yanayoishia mwaka wa fedha wa mwaka jana Juni na ndiyo yanayofanyiwa utaratibu wa kulipwa. Kwa sasa kwa watoa huduma kwa mwaka huu wa fedha ambao tunaendelea, tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 200 ambazo zitaenda kwa ajili ya kulipa watoa huduma ambao wametoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa malimbikizo ya Walimu, niwakumbushe tu kwamba, mpaka mwaka wa fedha wa mwaka jana tunaanza, zilikuwa zaidi ya shilingi bilioni 70 ambazo mtakumbuka miaka ya nyuma zilikuwa zikipigiwa kelele. Kwa sasa tunaongelea shilingi bilioni 2 au 3, kwa sababu mchakato unakuwa endelevu, hakuna siku ambayo kutakuwa hakuna kabisa kinachodaiwa kwa sababu likizo zinaendelea kuwepo. Utaona kwamba, hiyo ni dhamira ya dhati ya Serikali ya Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha kuhakikisha zile ambazo ni haki za watumishi wetu hawa zinapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kwenye hili la Walimu wapya, ni kweli Walimu wetu wanapopangiwa vituo vyao vipya wanapata shida. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha nitoe rai na niilekeze kwa Wataalam wa Wizara zetu zinazohusika, wanapoandaa mchakato wa kuwapangia Walimu wetu, waandae na mahitaji yao ili siku wanapowapa barua kwamba, unatakiwa ukaripoti mahali fulani utaratibu wa fedha zao uwe umeshakamilika. Huu utaratibu wa kuripoti kwanza, katika Halmashauri zingine kunakuwepo na michakato ambayo inawachelewesha kuwapatia fedha zao na Walimu wa aina hiyo wanapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ilikuwa Wilaya ya Igunga, mwaka jana ambapo ilibidi waende mpaka kwa Mkuu wa Wilaya kuelezea kwamba, fedha zao zimechelewa. Kwa hiyo, hili litarekebishwa kiutawala ili kuhakikisha Walimu wanapopangiwa hawapati shida wanaporipoti katika maeneo hayo, kwa sababu ni kweli wanakuwa katika mazingira mapya, mazingira ya ugenini na wanapocheleweshewa kupata hicho ambacho wanatakiwa wakitumie, linakuwa siyo jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya Elimu ya Juu. Niwakumbushe Watanzania kwamba, jambo linalotokea si kwamba, Serikali inachelewesha kulipa mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa makusudi. Lililotokea ni kwamba, katika utaratibu wa kulipa wa kutoka Wizara ya Fedha kwenda Bodi na kwenda vyo husika, kunakuwepo na taratibu za kibenki zinazofanyika. Katika kipindi kilichopita mpaka Wanafunzi wanagoma, tayari mchakato ule ulikuwa unaendelea na hilo tumeshaliongea kuhakikisha taarifa zile ambazo zinatakiwa kwa ajili ya kulipa madai hayo ya wanafunzi, zifanyike mapema ili inapofikia wakati wa kulipwa waweze kulipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushie tu kwamba, katika hii sekta ya elimu ninaona tumeliongelea sana. Mimi niseme tu kwamba, kwa mtu yeyote hapa Tanzania hii siyo ajenda ambayo tunaweza tukabishiana kwa sababu kila mmoja anatambua umuhimu wa elimu; lakini ni vyema Watanzania wote tukatambua kwamba, nchi yetu ni kama imepita kwenye kipindi cha mpito kuhusu suala la elimu kutokana na *expansion* kubwa iliyofanyika katika sekta hii ya elimu. Kutoka shule 1,700 kwenda shule 3,500, kwa mtu yeyote anayeweza akawaza anaweza akaona ilikuwa ni kazi kubwa kiasi gani. Ukisema ungeweza kuzifanya shule 3,500 zote zikawa za kiwango cha kama ilivyo Mzumbe, Iliboru, ama zilivyo hizo shule nyingine za binafsi, ni lazima sekta zingine zote shughuli zake zingekwama kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi ambavyo tumeweza kupiga hatua hii, niseme tu kaulimbiu aliyoisema Mheshimiwa Rais kwamba, baada ya kutoka katika ujenzi wa aina hii sasa tunakwenda kwenye ubora, ndiyo utaratibu ambao ni njia sahihi. Mimi niamini kwamba, tutakapokuwa tumekamilisha kwenye hatua hiyo ya ubora, kila mmoja ataona uamuzi iloufanya Serikali ulikuwa ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia kwenye upande wa Vyuo Vikuu, Awamu ya Nne ilipokuwa inaingia fedha zilizokuwa zinatumiwa kwa ajili ya mikopo ya Elimu ya Juu zilikuwa shilingi bilioni tisa na sasa tunavyoongea zinatumiwa zaidi ya shilingi bilioni 350. Kwa hiyo, ukiangalia miaka 10 kutoka 1994/95 mpaka 2004/2005, zilikuwa zinatumiwa shilingi bilioni 51. Mwaka mmoja tu wa 2005/2006 tayari zikatumiwa shilingi bilioni 56 na sasa tunaongelea zaidi ya shilingi bilioni 300 kwa mwaka. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni *expansion* kubwa ambayo imefanyika na hiyo ndiyo ambayo inaweza ikawa imesababisha taratibu zake ziwe katika namna ya kimpito.

Mimi niwahakikishie kwamba, kwa kuwa Serikali imeweza kumudu hatua hizi za kuweza kujenga majengo, maabara na kupata Walimu, hatua inayosalia ya kuzifanya shule hizi ziwe na ubora kwa huduma na watoa huduma wenye motisha ni jambo ambalo litawezekana na shule zetu zitakuwa bora na wanafunzi wetu watasoma katika mazingira mazuri.

Jana tu na mimi nilitoa kauli, kwa hiyo, hata hapa ninaendelea kuwahakikishia Walimu kwa sababu niliongelea hili kwamba, katika awamu zinazofuata kwa sababu misingi yote hii imeshajengwa, basi tutaifanya Sekta ya Elimu iwe moja ya sekta bora inayoheshimika na tutafanya kila mmoja atamani kuitwa Mwalimu na atamani kufundisha. Tunatambua kazi kubwa na ngumu ya Walimu na mazingira magumu wanayofanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi Walimu walinipokea nikiwa sijui Kiswahili, unanzia na kuambiwa hii ndiyo “a” iko kama kikombe. Hii ndiyo “e” iko kama bata. Kwa hiyo, wametutoa mbali tunawatambua, hakuna mtu anayeweza kumdharau Mwalimu. Unaweza ukacheza na mengine, lakini huwezi ukacheza na elimu kwa sababu ndiyo ina-*transform* jamii nzima. Huwezi ukawa na viwanda bila kuwa na wasomi wa kuendesha mitambo kwenye viwanda. Kwa hiyo, hili ambalo Serikali imechukua hatua hii ni jambo la msingi na wengine ambao walikuwa wanabeba utaratibu wa kila Kata kuwa na Sekondari, hawajui hii pia ni silaha ambayo itatusaidia kupunguza pengo kati ya walionacho na wasionacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa ambayo ilikuwa na shule mbili za sekondari, leo hii ina wataalam wachache katika sekta binafsi na katika Wizara, mmojawapo ukiwa Singida. Mikoa ambayo ilikuwa na shule nyingi wakati Singida ikiwa na shule mbili, yenyewe ikiwa na zaidi ya shule 100, leo hii ina wataalam wengi katika kila ofisi unakowakuta. Kwa hiyo, jambo hili alilolifanya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kwamba, kila Kata kuwe na Sekondari na kila kata kuwe na Wataalam waliofundishwa vizuri, maana yake tunakokwenda tutakuwa na

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

mgawanyo mzuri wa Wataalam katika sekta mbalimbali na hivyo kuwezesha kugawana vizuri Keki ya Taifa na hivyo kuondoa pengo kubwa la walionacho na wale wasionacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine limeongelewa sana na Mheshimiwa Esther Bulaya na pia Mheshimiwa Diana Chilolo. Hayo yote mliyoyasema ni mambo ya msingi na Serikali inayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutengewa fedha Mfuko wa TEA; ni kwamba, katika mwaka wa fedha kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnaelewa, Serikali ilikuwa na mambo mengi ya kuyatekeleza katika mwaka wa fedha na mtaona kulikuwepo na matatizo ya hapa na pale ya kibajeti. Msingi wa yote kwa sababu hiyo ni sheria, Sheria ya TEA ni sawasawa na sheria zingine zilizowekwa zikiwemo za *Road Fund* pamoja na REA. Kwa hiyo, Serikali itajitahidi kuhakikisha fedha zimekwenda kwenye Mfuko huo kama zilivyotengwa. Leo hii nimeulizia nikaambiwa tayari zipo ambazo zilikuwa ngazi ya *exchequer* ambazo tayari nazo ziko kwenye mchakato wa kuweza kulipwa ili kuhakikisha Serikali inatimiza azma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo aliyoyasema Mheshimiwa Chilolo kuhusu Walimu na mimi ninasisitiza hapo hapo; hata kama tutashindwa kuwalipa Walimu wa Tanzania, basi tutambue hata kazi yao na kuwatia moyo kwamba, kazi wanayoifanya ni njema na ni ya manufaa makubwa kwa Taifa letu ili waweze kutambua kwamba, Taifa linawathamini na tunatambua kazi yao kwamba, ina umuhimu mkubwa sana katika taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali hivi vingine vyote vilivyotajwa ametaja Mheshimiwa Mama Sitta kuhusu chombo kimoja cha Walimu, kuhusu mahitaji yao, hivyo vyote vilishatolewa kauli na vilishapita ngazi zote. Kwa hiyo, tunapokwenda yatapungua matatizo ambayo walikuwa wanayapata kutokana na kukosekana kwa chombo hiki.

Jambo moja la mwisho kabla sijagongewa kengele, imeelezwa kuhusu fedha za mikopo ya Elimu ya Juu kuwekwa sehemu moja pamoja na fedha za matumizi za Wizara na hivyo Wizara kuonekana ina fedha nyingi kumbe fedha hizo zinakwenda kwenye Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imeshapokea na tayari tulishapitisha uamuzi wa kuziweka fedha hizo kuwa sehemu ya maendeleo, kwa sababu katika maelezo ya uchumi wa kisasa, unapowekeza kwenye elimu hiyo si matumizi mengineyo, bali ni fedha ambazo zinakwenda kwenye maendeleo. Kwa hiyo, hatua inayofuata itakuwa ni kuzitenga pembeni katika Mfuko Maalum ili kuhakikisha fedha hizo haziondoi nafasi ya matumizi mengineyo katika Wizara husika ili Wizara husika iweze kupanga.

Nilisema miaka mitatu ijayo tutakuwa tunalipia Wanafunzi zaidi ya 169,000 wa Vyuvo vya Elimu ya Juu na tutahitaji zaidi ya shilingi bilioni 730 kwa ajili ya kuwalipia wanafunzi wa Elimu ya Juu. Fedha nyingi kama hiyo hauwezi ukaichanganya katika matumizi mengineyo ya Wizara na bado Wizara ikaweza kupangilia matumizi yake katika bajeti za matumizi mengineyo na ufanisi ukapatikana. Kwa hiyo, hilo nalo litakuwa limeshapatiwa majibu namna hiyo. Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wizara husika, waone sisi sote tunaliona hilo na tunakubaliana na hiyo ambayo wao wamekuwa wakiiona na kutoa hayo mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya wenzetu wa Halmashauri ya Moshi; hii ilikuwa ni shilingi milioni 509 na mpaka sasa shilingi milioni 436 tayari zilishalipwa. Kwa hiyo, hiyo nayo ni habari njema ambayo Serikali imefanya kwa ajili ya kuondoa tatizo hilo kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na hongera kwa kutangaza nia. Sasa ninaomba nimwite Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, dakika ishirini!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hata sijatoa shukrani, ninaomba niseme kwamba, mimi ni Mwalimu wa Sekondari wa Masomo ya Biashara (ECA), ninaupenda ualimu, ninauheshimu na ninawapenda Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nikaanza kwa shukrani. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa leo mbele ya Bunge lako Tukufu ili nami kwa mara ya kwanza niweze kujibu hoja za Wabunge waliochangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii kwa heshima na taadhima, kumshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunitewa kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Aidha, ninakupongeza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa busara na hekima kubwa, kwa muda wote wa majadiliano ya hotuba za bajeti kwa Mwaka huu wa Fedha wa 2015/2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru mume wangu mpendwa, Mheshimiwa John Samuel Malecela pamoja na watoto wangu watano kwa kunipa ushirikiano na kunivumilia kutokana na majukumu niliyonayo ya Serikali na ya Jimbo ambayo yanarifanya mara kwa mara nisiwe nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Same Mashariki kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu Jimboni na kwa kunivumilia pale niliposhindwa kuwa nao kwasababu ya majukumu mengine ya Kitaifa. Napenda kuwahakikishia kwamba tupo pamoja katika dhamira ya kuleta maendeleo ya uhakika katika Jimbo letu. Hii inajidhihirisha wazi kutokana na kazi ambazo tumezifanya ndani ya miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wabunge wote kwa kuchangia Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Katika hoja za Waheshimiwa Wabunge, wengi mmeeleza baadhi ya mafanikio na changamoto tulizonazo. Ni kweli kwamba changamoto ni nyingi, tunaahidi kuendelea kuzifanyia kazi katika mikakati yetu ya kuendelea kuboresha elimu yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti mambo mengi yanayohusu sera atazungumzia Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nami nitajikita katika maeneo maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kusahau baadaye lakini nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. Napenda tena kurudia kusema kwamba nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge na mliochangia kwa maandishi.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Suzan Lyimo kipekee kabisa. Naomba nikiri kwamba Mheshimiwa Susan Lyimo amekuwa ni Waziri Kivuli mfutiliaji mzuri sana, amekuwa anakwenda kwenye Vyuo Vikuu; na naomba nimwambie tu neno moja. Siyo kwamba Wizara, aidha Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu na sisi hatuendi kwenye hivyo Vyuo na kuziona hizo kasoro. Tunazona na tunazirekebisha. Lakini sisi ambao tuko Serikalini hatuwezi kusema, lakini wewe ni kazi yako kama Mbunge unayeisimamia Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba nimekuwa Mbunge kwa miaka 14 nikiwa naisimamia Serikali kama Mheshimiwa Suzan Lyimo. Sauti yangu ilikuwa ni kali kuliko yake, isipokuwa mimi nilikuwa naka pale, yeye anaka hapa. Mheshimiwa Suzan Lyimo nakuheshimu sana, endelea na kazi yako kwa mtindo wako, nami nilikuwa na mtindo wangu. Karibu sana! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kutoa picha kamili ya Sekondari za Kata. Kwanza napenda Watanzania wanisikilize vizuri na waelewe chimbuko la Sekondari za Kata. Chimbuko ni Serikali ya awamu ya tatu, ndiyo iliyotoa Azimio la kwamba sasa tuwe na Sekondari za Kata. Utekelezaji umeanza kwenye awamu ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kitaalamu kidogo. Kwa wale watu ambao mnapenda kusoma vitabu sana, aidha iwe ni vitabu vya vya biashara, uchumi na kadhalika; maisha ya binadamu na maisha ya kitu chochote ya *stage* nne. Unianza na *introduction stage*, unakuja kwenye *growth*, unakwenda kwenye *maturity* na mwishoni unafika kwenye *decline stage*. Sasa awamu hii ya nne ndiyo imeanza ku-*introduce* Sekondari za Kata, ni lazima tulikubali hilo. Ilipo-*introduce* Sekondari za Kata awamu ya nne, ndugu zangu msibeze, ilikuwa ni kwa nia nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesoma nimesoma Shule ya Msingi miaka ya sitini na kitu na mwaka wa 1970 naingia Sekondari. Shule niliyokuwa nasoma ilikuwa inaitwa Jitengeni *Primary School*. Kwa miaka 10 ilikuwa haijatoa mtoto kumpeleka Sekondari. Nikachaguliwa mimi nikaenda Weruweru Sekondari. Naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuazimia na kutekeleza Sekondari za Kata. Naomba sasa nami nizungumze kama Mheshimiwa Suzan Lyimo, kwamba kama hujafanya *research*, usiwe unasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumze kama Naibu Waziri ambaye nina wataalamu, wamenipa takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufaulu wa Shule za Sekondari za Kata katika *Form Four*, naomba wananchi mnisikilize vizuri kwasababu Shule za Kata ni Shule za *Community*, ni shule za wananchi. Kwa hiyo, kama kuna mafanikio, ni ya Watanzania maana yake shule hizi zinagharamikiwa na Halmashauri pamoja na wananchi. Kwa hiyo, naomba kuwapa picha Watanzania, Shule za Sekondari za Kata zinakwendaje sasa, japo wako kwenye *introduction stage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniwie radhi sana! Mwaka 2012, Sekondari za Kata kwa matokeo ya kwanza walipata *Division I* wanafunzi 482; mwaka 2013 wanafunzi wa *Form Four* waliopata *Division I* ni 1,323; mwaka 2014 wanafunzi waliopata *Division I* kutoka Sekondari za Kata ni 1,153. Hapa kuna utafiti, siyo kwamba nazungumza kama mtu tu, hapana! Mimi ni Naibu Waziri. Kuna utafiti! (Makofi)

Kwa hiyo, Watanzania naomba niwaambie, shule zenu mnazozijenga mkishirikiana na Halmashauri, zina mafanikio makubwa. Shule hizo hizo mwaka 2012 wanafunzi waliopata *Division II* walikuwa ni 3,388. (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo! *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Naomba mnyamaze kimya! Mwaka 2013 *Division II* ni 7,348; mwaka 2014 *Division II* ni 8,348.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukibeza hizi shule, hata nyie ndugu zenu wanasoma huko, msiwabeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 *Division III* ilikuwa ni wanafunzi 10,728; mwaka 2013 *Division III* ilikuwa 21,423; mwaka 2014 *Division III* ilikuwa ni 19,158; na hawa wote ni wanafunzi waliokuwa na hadhi ya kwenda kidato cha tano. Hii ni *Form Four* kwenda *Form Five*. Sasa... *(Kelele)*

Mimi siongei na nyie, naongea na Watanzania!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu! Hayo ndiyo tunayowaambia kuwa na uvumilivu wa Kisiasa. Mbona nyie mkizungumza wenzenu wananyamaza? Naomba mtulie atoe hoja yake. Tulieni.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mimi nazungumza na wananchi nawaambia mafanikio ya shule zao.

**WABUNGE FULANI:** Siooo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, zungumza na Kiti!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi sasa kwa *form five*.

**WABUNGE FULANI:** Sioo! *(Kelele)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ningependa watoto mnyamaze msikilize.

**MWENYEKITI:** Zungumza na kiti huku Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie shule 10 bora Kitaifa, Watanzania nisikilizeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule kumi bora kitaifa katika mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2014, Waheshimiwa Watanzania nisikilizeni mwone jitihada zenu zimezaa nini? Mwaka 2014 shule kumi bora Kitaifa katika mtihani wa Kidato cha Sita ya kwanza ilikuwa ni Igowole Iringa; ni Shule ya Serikali, ni Shule ya Kata, imekuwa ya kwanza hiyo. Ni Shule ya Sekondari ya Kata; Shule ya pili ilikuwa ni ya binafsi, shule ya tatu Kisimiri Shule ya Mkoa wa Arusha, ni Shule ya Sekondari ya Kata. Imeshika namba tatu kwenda *Form Five*. *(Makofi)*

Shule ya nne ni Iwawa ya Njombe, ni shule ya Sekondari ya Kata. Imeshika namba nne katika kumi bora. Shule inayofuata ni Kibaha, Mariane Girls. Shule ya saba ni ya Nangwa ya Mkoa wa Manyara, ni shule ya Sekondari ya Kata. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sawa sawa!

**WABUNGE FULANI:** Siyooo!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Waheshimiwa Watanzania, katika shule kumi bora... *(Kelele)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Nyamaza!

Katika shule kumi bora, shule nne ni Shule za Sekondari za Kata. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kuwaambia Watanzania wafurahie kazi yao, wamefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Shule za Sekondari za Kata Watanzania nawashukuru kwa jinsi ambavyo wamekuwa na moyo wa uthubutu, hawakusikiliza kelele za watu wasiotaka maendeleo na leo watoto katika shule kumi bora, shule nne ni shule za Kata.

**MWENYEKITI:** Shule ya Iwawa iko Makete!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni ada elekezi kwa shule binafsi. Naomba msikilize maana najibu hoja zako hapa Mheshimiwa Suzan Lyimo. Hata kama siyo ya kwako lakini iko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka ulinganifu wa ada inayotolewa baina ya Shule za Serikali na zile za binafsi na ili kudhibiti upandaji wa ada kiholela, Serikali imechukua hatua ya kumtafuta mtaalamu elekezi wa kuandaa gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi wa sekondari.

Mtaalamu ameshapatikana na mkataba umeshasainiwa na ameanza kazi kuanzia tarehe 1 Juni, 2015. Anatarajiwa kukamilisha kazi hii tarehe 31 Agosti, 2015. Kukamilika kwa kazi hii kutasaidia kudhibiti upandaji holela wa ada katika shule mbalimbali, pamoja na kutoa mwongozo wa upandaji wa ada kwa shule binafsi.

Aidha, shule zote zinalipisha ada kwa kutumia Shilingi ya Kitanzania isipokuwa kwa baadhi ya Shule za Kimataifa, kwa mfano, *Internatinal School of Tanganyika*. Endapo kuna shule isiyo ya Kimataifa na ina toza ada katika fedha za kigeni itakuwa imekiuka utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika awamu ya kwanza ilipanga kujenga Vyuo vya ufundi stadi VETA kwenye Wilaya ambazo hazikuwa na Chuo Chochote cha Ufundi Stadi. Ujenzi ulianza na Chuo cha Makete ambacho kimekamiliwa. Hatua inayofuata ni ujenzi wa Vyuo vya Ludewa, Namtumbo na Karagwe. Ipo katika hatua ya kumpata Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maandalizi ya awali kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo Vya Ukerewe, Kilindi, Chunya na Korogwe yanaendelea vizuri. Tuko kwenye hatua ya kupata washauri waelekezi. Gharama ya ujenzi wa Chuo kimoja, nirudie tena, ni kati ya Shilingi bilioni nne na kuendelea na hivyo kuwa ni matatizo upande wa kibajeti, ninaendelea kutoa rai kwamba kutuendeleee kutumia na wafadhili pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imejirudia. Aliizungumza Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Chiligati kuhusu ujenzi wa Chuo cha VETA cha Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba mimi mwenyewe nilifunga safari nikaenda Manyoni. Niliketi na Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Katika kikao hicho alikuwepo Mbunge wa Manyoni Mashariki nafikiri, Mheshimiwa Chiligati. *(Makofi)*



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia ya kujenga Chuo Manyoni. Pale Manyoni tuna tatizo kidogo. Tuna Majimbo mawili; Manyoni Magharibi na Manyoni Mashariki na haya Majimbo yote mawili yana majengo. Kwa hiyo, sisi tulipokuwa kwenye kikao kile tuuliambia Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwamba ni vyema wakakaa wakazungumza kabisa wakamaliza mvutano ambao ulikuwepo pale halafu watuletee taarifa kamili ili tujue wameamua chuo kile tukijenge Mashariki au Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo majengo yenyewe hayakukidhi haja, yanahitaji yapitiwe, yatengenezwe upya. Majengo ambayo tuliyaona ni ya Mashariki tu, ya Magharibi hatukuyaona. Lakini tuliomba Halmashauri ituletee mrejesho ili tujue imeamuaje katika katika maswali yote ambayo tuliwaachia na mpaka sasa bado tunangoja ripoti kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. (Makofi)

Tuna tatizo kubwa la Walimu wa sayansi, lakini katika tatizo hilo tumejitahidi kutafuta mikakati ya kwamba tutapunguzaje hili tatizo.

Katika juhudi za Serikali za kupunguza tatizo la upungufu wa Walimu wa masomo ya sayansi na hisabati, kuanzia mwaka 2014/2015, Serikali ilianza programu maalumu ya mafunzo ya Stashahada ya Walimu wa Sayansi na Hisabati katika Chuo Kikuu cha UDOM ambapo jumla ya Wanachuo 2,142 wamedahiliwa kwa mwaka wa masomo, aidha ya mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Walimu 365 wa sayansi na Hisabati wamedahiliwa katika Vyuo Vya Ualimu Korogwe, Kleruu na Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeandaa mkakati wa kuajiri walimu wastaafu wahitimu wenye sifa linganishi na Walimu kutoka ndani na nje na wale wa kutoka katika soko la pamoja la Afrika ya Mashariki. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ya Elimu ina mkakati wa kufanya ukarabati na upanuzi wa Vyuo Vya Ualimu kwa lengo la kupanua zaidi programu zilizoainishwa hapo juu.

Jumla ya Vyuo kumi vipo kwenye mpango huo ambao ni Tabora, Marangu, Mpwapwa, Dakawa, Kleruu na Butimba ambavyo vinakarabatiwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Vyuo vya Kitangali, Mpuguso, Ndala na Shinyanga vitafanyiwa upanuzi mkubwa kwa ushirikiano wa Serikali yetu na Serikali ya Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu utaiwezesha Serikali kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya Ualimu kwa masomo ya Sayansi na Hisabati kutoka idadi ya sasa ya 2,482 mwaka 2014, hadi 10,000 mwaka 2017 ili kutosheleza mahitaji ya Walimu wa masomo haya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukwambia kwamba Serikali iko imara na inasimamia hili tatizo kwasababu tunalielewa. Bila kuwa na Walimu wa masomo ya Sayansi tutakuwa tumeachwa nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC). Ni kweli Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ndio wamiliki wa Vyuo hivi. Uwezo wa kibajeti ni mdogo na hii inapelekea Vyuo hivi kuwa duni. Vyuo hivi ambavyo viko 55, Wizara yangu kupitia VETA, tumewapa mitaala ya VETA. Pia Walimu 100 wa FDC wamepata mafunzo ya elimu ya ufundi stadi.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mfano, sasa naomba niende kwenye Chuo cha Gera ambacho ni Chuo kilichoko Misenyi Jimboni kwa Mheshimiwa Assumpter Mshama. Naomba nikiri kwamba mimi mwenyewe nilikwenda kwenye Chuo hiki, ni kati ya Vyuo vya FDC na nikiri kabisa kwamba Vyuo Vya FDC vina hali mbaya kwasababu ya hali halisi ya Bajeti inayotoka kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali inajaribu kuangalia itawezaje kuviondoa hivi Vyuo katika hali ile kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naomba tu kwamba hivi Vyuo vya FDC viendeleo kusubiri wakati Serikali inatafuta utaratibu wa kuboresha Vyuo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Elimu ya mwaka 2014, hapa kidogo naomba nizungumze kidogo lakini Mheshimiwa Waziri atazungumza kwa kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamejitokeza sana kuibezwa Sera ya Elimu ya 2014, lakini niseme ukweli kabisa kwamba Sera mpya hii siyo kwamba mnasema Wizara ya Elimu, hapana! Sera mpya hii walitafutwa Maprofesa wenye taaluma yao, wakakaa kwa muda mrefu kushughulikia Sera hii mpya ya Elimu. Naomba tusiwe tunabeza kila kitu. Maprofesa hawa wanatoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam huko huko mlisosoma, wamekaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho tuzungumze, wadau wote pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge mlihusishwa kwa muda mrefu kuhusu Sera mpya ya Elimu. Kibinadamu, inawezekana kuna upungufu, lakini tunakwenda stage ya pili sasa. Ukishatoa Sera mpya kama hii ulimwengu mzima, ni lazima uende stage ya pili ya kwenye mikakati (*strategy*). Wakati tunaingia kwenye stage ya mikakati, upungufu ambao tutauona na ninyi mmeupigia kelele na wananchi wamelalamika, ni lazima tutauangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapopata taabu, nizungumze ukweli! Amezungumza Mheshimiwa Mbatia nikaingia baridi kidogo! Mheshimiwa Mbatia alipokuwa anainyanyapaa Sera mpya ya Elimu wakati anachangia, anasema hii Sera mpya ya Elimu ni Sera ya Elimu gani ambayo haina mitaala? Aah! Mimi nikahoji, jamani sijui labda taaluma yangu mbovu. Huwezi kuwa na Sera mpya leo ukawa na mitaala wakati huo huo! Huwezi!

Mitaala ni stage baada ya mikakati. Sasa mimi nikahoji, sijui, labda taaluma zetu zinatofautiana. Lakini naomba nimwombe Mheshimiwa Mbatia aangalie vizuri anapochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba niseme kwamba naunga mkono hoja na ninawashukuru wote mliochangia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalimu Anna Kilango Malecela, Naibu Waziri wa Elimu kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Dkt. Shukuru Kawambwa, dakika arobaini! (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa wakati wakijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Anna Kilango Malecela kwa ufafanuzi mzuri aliyotoa na kwa majibu aliyoyatoa kwa kina. Katika kipindi kifupi tu ameweza kunisaidia kufanya kazi kwa namna ya kipekee kabisa na kuiweka elimu katika taswira nzuri. (*Makofi*)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Wajumbe wake kwa kuchambua na kujadili kwa kina bajeti yangu.

Aidha, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwa kuwasilisha maoni ya Kamati hapa Bungeni. Nampongeza pia Mheshimiwa Susan Lyimo, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Sekta ya Elimu kwa kuwasilisha vema maoni ya Kambi ya Upinzani, ushauri na mapendekezo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bagamoyo kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu Jimboni na kwa kunivumilia pale niliposhindwa kuwa nao kwa sababu ya dharura za majukumu mengine ya Kitaifa. Kipekee kabisa, naishukuru familia yangu kwa kuwa karibu nami na kunitia moyo kila wakati na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majadiliano ya hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge 39 walitoa hoja zao kuhusiana na Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Aidha, baada ya kuwasilisha hotuba ya Wizara yangu, Waheshimiwa Wabunge 28 wamechangia hoja yangu kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge 35 kwa maandishi. Nawashukuru sana Waheshimiwa hao wote waliochangia kwa kuongea na waliochangia kwa maandishi, kwa michango yao mikubwa na mizuri ya kina ambayo bila wasiwasi wowote ni kwamba itachangia katika kuboresha Sekta ya Elimu na kuhakikisha kwamba watoto wa Kitanzania wanaelimika kwa kiwango kikubwa katika miaka ijayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nami napenda nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo yaliyojitokeza wakati wa majadiliano. Lakini kwa sababu ya ufinyu wa muda, ni dhahiri kwamba sitaweza kutolea majibu kila moja ya hoja ambazo zimezungumzwa hapa au tulizozipokea kwa maandishi. Naahidi kuwa hoja za kila Mbunge zitajibiwa na Wizara yangu kwa maandishi katika kabrasha ambalo tutalikabidhi katika Ofisi ya Spika ili kila Mbunge aone hoja yake tumeifafanua au tumeijibu kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao waliyoitoa kwa maandishi na kwa kuongea hapa Bungeni wakati wakijadili hoja ya Wizara yangu. Michango hii ni mizuri na iliyojaa busara na hekima, itatusaidia sana katika kusimamia utekelezaji wa bajeti hii na kuboresha Sekta ya Elimu na mafunzo ya Ufundi katika siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo. Nitaanza na hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Huduma za Jamii imetaja hoja kadhaa na sitaweza zote kuzitolea ufafanuzi na baadhi ya hizo Mheshimiwa Naibu Waziri amezigusia na kuzitolea ufafanuzi. Kwa hiyo, mimi nitasema baadhi ya hizi hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, inahusiana na Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa Wakala inayojitegemea, kwamba Idara hii sasa iwe Wakala inayojitegemea kwa mantiki ya kuboresha kazi ya Ukaguzi wa Shule. Pia bila shaka ni kwa mantiki ya kuongeza rasilimali katika kazi nzima hii ya ukaguzi; rasilimali watu, rasilimali fedha, vitendea kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezungumza hili lakini Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamechangia na pia kulizungumzia na kuliunga mkono jambo hili. Sisi Serikalini tulikuwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

tumesitisha kazi ya kuunda Wakala. Baada ya kuunda Wakala nyingi hapo nyuma na bado tukaingia katika kipindi ambacho baadhi ya Wakala hazikufanya kazi ambazo tulizitegemea. Tulidhani zitapata rasilimali nyingi zikiwa Wakala zenyewe, badala yake zikaendelea kuitegemea Serikali. Tulidhani ufanisi utapatikana mkubwa zaidi, lakini haikuwa hivyo. Kwa hiyo, uundaji wa Wakala ulisitishwa kwa barua maalumu ambayo ilitoka tarehe 13 mwezi wa Kumi, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli hii ya Kamati na kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kwamba jambo hili Wizara yangu imelipokea na Serikali imepokea. Mimi binafsi nimeshaanza taratibu husika kwa maana ya kumwandikia rasmi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba sisi kama Wizara tunaomba mchakato huu uruhusiwe kuanza, tuweze kufanya kwa umakini kwa sababu baada ya kuzuiliwa na Serikali siwezi tu kama Waziri moja kwa moja nikasema tunaanza, lakini tupate kibali cha Mheshimiwa Waziri Mkuu kufanya kazi hiyo. Nimeshamwandikia rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalotoa moyo zaidi ni kwamba yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anawasilisha hoja yake na kufanya majumuisho hapa, jambo hili amelitolea kauli ambayo Mwenyekiti wangu amlil-*quote* kwamba limempendeza na kwamba ametoa ahadi Serikali itaifanyia kazi.

Kwa hiyo, hili ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshalitolea ahadi kwamba litaangaliwa vizuri, mimi nitafuata hivyo hivyo kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotoa ahadi hapa Bungeni nami nimeshamwandikia rasmi. Kwa hivyo, jambo hili la ukaguzi kuwa wakala, naomba Bunge lako Tukufu liridhie kwamba limewasilisha Serikalini na Serikali ina nia thabiti ya kulifanyia kazi kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la Kamati katika Wakala lilihusiana na kwamba Idara hii ya Ukaguzi sasa hivi iko Wizarani ni kwamba iongezewe bajeti. Jambo hili kila siku tunaliangalia kwa macho mawili na tumeendelea kufanya kazi hiyo mwaka hadi mwaka.

Ukiangalia mtiririko wa bajeti mwaka hadi mwaka, kuanzia mwaka huu tuliokuwa nao kwenda miaka ya nyuma, utaona kwamba pesa kila mwaka katika Idara hii zinaongezeka. Nitatoa mfano, mwaka wa fedha 2013/2014 ukaguzi ulitengewa Sh. 18, 308,000,000/=, lakini mwaka wa fedha uliofuatia ulipangiwa Sh.18,792,000,000/= ambao ni mwaka 2014/2015. Mwaka huu wa fedha 2015/2016 Idara hiyo ya Ukaguzi ilikuwa imepangiwa Sh. 25,823,000,000/= . Katika mwaka wa fedha 2015/2016 mwaka ambao tunaujadili bajeti yake hivi sasa, tumetenga pesa nyingi zaidi ili Idara hii iweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni pesa za Serikali tu. Nje ya pesa za Serikali, Serikali imeendelea kuwaomba wahisani na wafadhili wengine waweze kuchangia katika kazi hii ya ukaguzi, ndiyo tuna mradi ule wa LANES, ambapo chini ya mradi wa LANES tuna rasilimali fedha na rasilimali vifaa chungu nzima ambavyo vitaenda kwenye ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza katika hotuba kwamba mwaka huu peke yake tutanunua jumla ya magari 51 ambayo yataenda kusaidia katika Halmashauri zile za Wakaguzi ambazo hazina gari katika Wilaya zao, lakini pia chini ya mpango huu wa LANES ambao pesa zake tumeziomba kutoka kwa Shirika la GPE, tutahakikisha kwamba kila Mratibu Kata ndani ya nchi yetu anapata pikipiki ya kumwezesha kusafiri katika shule ndani ya Kata yake bila wasiwasi mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pikipiki hizi kwenye LANES 2,800; lakini mradi wa USAID nao unanunua pikipiki na mradi wa DFID nao unanunua pikipiki, ndiyo maana nikasema kwamba

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

kila Mratibu Elimu Kata katika nchi yetu atakuwa na pikipiki mpya kwa ajili ya kazi ya ukaguzi katika shule yake. Kwa hiyo, rasilimali tunaendelea kuzifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba jambo hili la ukaguzi linaenda vizuri na linatuletea tija katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la Kamati ni kuhusu mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo ama *Block Teaching* ambayo imelalamikiwa kwamba katika mwaka uliopita yalifanywa kwa wiki mbili badala ya wiki nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tu kwamba hilo siyo la mtaala kwamba mtaala wa Ualimu umepangwa kwamba uwe na mafunzo ya kufundisha shuleni; na Walimu hawa hawa wapate mafunzo ya kufundisha wiki nane ama siku 56 siyo wiki mbili.

Sasa najua kwamba kwa sababu mwaka 2014 na mwaka huu wa fedha tumepata mtikisiko katika bajeti. Kwa hiyo, Walimu hawakufanya mafunzo ya kufundisha kwa ukamilifu, walifanya tu wiki tatu, lakini pia mwaka huu wamefanya wiki mbili. Kwa hiyo, imekuwa haba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kwa sababu ya matatizo ya kifedha ambayo yamejitokeza ndani ya Serikali. Siyo nia kwamba tuendelee na hali hiyo, au siyo nia kwamba sasa sisi tumejipanga kwamba Walimu watoke tu bila kufanya *module* moja muhimu sana katika mafunzo yao. Kwa hiyo, katika bajeti ya mwaka huu 2015, pesa ambazo zimetengwa ni pesa zile ambazo zitatoshwa mafunzo ya Walimu shuleni ya wiki nane kwa Walimu hawa.

Kwa hiyo, kazi ni juu yenu Waheshimiwa Wabunge katika bajeti hii. Bajeti hii msishike Shilingi na mpitishie bajeti kamili ya wiki nane ya mafunzo shuleni ili Walimu Wanafunzi wanapomaliza wawe wanatoka wameiva. Bila shaka Serikali tutajitahidi kwa uwezo wetu wote kuhakikisha kwamba pesa hizo zinatoka. Wale ambao walikosa watakuwa wamekosa, lakini hawa wanaokuja wasiendelee katika kadhia ile ile ya kukosa kufanya mafunzo ya kufundisha katika shule katika kipindi kile ambacho kinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Kamati ya Huduma za Jamii ilizungumzia ni kuhusu posho maalum ya Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Suala hili limekaziwa pia na Waheshimiwa kadhaa ambao walichangia katika bajeti hii.

Ni jambo ambalo tumelipokea na ni jambo jema, tumelifanyia kazi katika hatua mbalimbali. Lakini hili ni jambo ambalo pia linahusisha Mabaraza ya Wafanyakazi kwa fani ya Ualimu na Utumishi wa Umma. Majadiliano lazima yafanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano haya yatahusisha Watumishi wa Umma pamoja Walimu. Walimu pamoja na upweke wao na umuhimu wao, lakini kule kijijini na sehemu zisizofikika kwa urahisi, kwenye mazingira magumu, *Nurse* yupo, *Daktari* yupo, *Mkunga* yupo na wengine na kadhalika wapo. Wote ni Watumishi wa Umma ambao Serikali ingependa kwamba inapomjali Mwalimu isikose kumjali *Daktari*; isikose kumjali *Mkunga*; isikose kumjali *Nurse* kwa sababu Walimu hawataweza kufanyakazi kazi zao huko kwenye mazingira magumu kama hawa wengine watakuwa wamenyongea kusema kwamba mbona sisi hatukuweza kupata posho hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho hii tungependa ifanyiwe kazi kwa umakini, nasi tumeipokea vizuri na tuna nia nayo nzuri ili tuhakikishe kwamba Walimu wetu wanafanya kazi ya uhakika. Kwa sababu yule ambaye yupo katika mazingira magumu, anapokuwa na uwezesaji ambao unamfanya aone kwamba amefutwa jasho, basi bila shaka atakuwa anajisikia vizuri zaidi na kujituma vizuri zaidi. Lakini hivi sasa wakati hilo hatujafikia utekelezaji wake, kitu ambacho tumejikita zaidi ni kuhakikisha kwamba maeneo yale ya mazingira magumu yote

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

kwamba nyumba zinajengwa za Walimu, umeme, huduma za maji na kadhalika, zile huduma zote za kumwezesha Mwalimu aweze kufanya kazi vizuri, basi zinamfikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna Halmashauri 80 zimetimia ambazo tunazitengea Shilingi milioni 500 kila mwaka kwa ajili ya kujenga nyumba za Walimu. Tulianza na Halmashauri 40, tukaja mwaka 2014 tukaongeza 40 tena.

Kwa hiyo, sasa zipo 80 na mwaka huu wa fedha tutaongeza Halmashauri nyingine; zile ambazo zina maeneo ambayo ni magumu kufikika. Pesa hizi ni kwa ajili tu ya kuhakikisha kwamba Mwalimu anapata nafuu anapokuwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatua kadhaa tumeanza kuzifanya ili kuhakikisha kwamba tunapunguza mazito ambayo Walimu wetu wanayapata wanapokuwa katika maeneo hayo magumu. Kwa hiyo, hili naomba nilijibu katika hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Muswada wa uanzishwaji wa chombo kimoja cha kumhudumia Mwalimu na Kamati imeomba kwamba Muswada huu uwasilishwe Bungeni kwa ajili ya kupitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa kuanzisha chombo kimoja cha kumhudumia Mwalimu ambacho kinajulikana kama Tume ya Utumishi ya Walimu ama kwa lugha ya Kiingereza *Teachers Service Commission*, uliwasilishwa na kusomwa hapa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 1 Aprili, 2015. Kwa hiyo, hatua ya kwanza tayari imeshatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, imeshatekelezwa kabla kwa maana ya kutafakari umuhimu wa kuwa na chombo kimoja cha kumhudumia Mwalimu na Serikali kukubali kufanya hiyo na kukubali kwamba chombo hicho kiundwe na ndiyo maana Serikali ikaenda kwenye hatua ya pili kuandaa Muswada uliosomwa hapa Bungeni kwa mara ya kwanza.

Kwa hiyo, kazi ya kumhudumia Mwalimu ni kazi ambayo Serikali inasema haina mbadala. Hii haina msalie Mtume, haina mchezo, ukiitaka elimu, maana yake ni lazima umthamini Mwalimu. Serikali hii ya awamu ya nne ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete inaithamini elimu na kwa maana hiyo inamthamini Mwalimu kwa kila hali na kwa kila fani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa barua ya ombi la kuwasilisha Muswada huu kwenye Mkutano wa Ishirini wa Bunge la Bajeti iliwasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 29 mwezi wa Nne ili Muswada huu uingizwe kwenye ratiba ya Vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Serikali hii imekubali kwamba tutaongezewa muda, baada ya bajeti hii ndani ya mwezi wa Saba angalau siku kumi tuweze kuhangaika na Miswada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada umeshafika tayari Bungeni. Muswada huu muusome vizuri Waheshimiwa Wabunge, muuchambue vizuri ili itakapofika sasa kuchangia, basi muuchangie kwa kina ili kuhakikisha kwamba tunapata chombo kimoja cha kumhudumia Mwalimu, kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali ya awamu ya nne ya Chama cha Mapinduzi chini ya Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya Kamati ambayo imezungumzia kwamba Elimu ya Juu itenganishwe na Elimu ya Msingi na Sekondari ili kuongeza ufanisi wake. Niseme tu kwamba hili tunalipokea la Kamati na Wizara yangu na Serikali kwa ujumla itaifanyia kazi ya kina ili kuhakikisha kwamba tunapata ufanisi.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba kama ni kwa lengo la rasilimali fedha au vitendeakazi, nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba rasilimali fedha kwenye Elimu ya Juu imeendelea kuboreka mwaka hadi mwaka tangu Wizara hizi mbili zimeunganishwa, pamoja na kwamba Wizara moja inasimamia pia Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutenganishwa, wakati kulikuwa na Wizara ya Elimu ya Juu rasilimali fedha ambazo zilienda kwenye Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundi mwaka 2004/2005 ilikuwa Shilingi bilioni 84, mwaka 2005/2006 ilikuwa Shilingi bilioni 138, mwaka 2006/2007 ilikuwa Shilingi bilioni 209 na mwaka 2007/2008 ni Shilingi bilioni 287. Baada ya hapo, Wizara ikaunganishwa Elimu ya Juu ikawa katika Wizara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2008/2009 Elimu ya Juu na Ufundi zilitengewa Shilingi bilioni 305 ambazo ni juu ya mwaka uliopita; mwaka uliofuata ni Shilingi bilioni 376, mwaka uliofuata ni Shilingi bilioni 542, mwaka uliofuata ni Shilingi bilioni 681, mwaka uliofuata Shilingi bilioni 719 na mwaka 2013/2014 ni Shilingi bilioni 865.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukiangalia mtiririko huu, unaeleza kikamilifu kabisa kwamba wala Elimu ya Juu haijatetereka kwa maana ya rasilimali fedha iwe na tengeo dogo kushinda sekta nyingine au sekta ndogo nyingine katika Elimu kwa sababu ya muunganisho huu. Ni kwamba imeendelea kupata hela nyingi zaidi kuliko hata wakati ule elimu ya juu ilipokuwa peke yake. Lakini hata kwa maana ya udhibiti wa Elimu ya Juu wenyewe, kwa maana ya udhibiti wa Elimu ya Juu, miaka mpaka ya 2007/2008 Taasisi zetu zile ambazo ndizo za udhibiti, kabla ya hapo ilikuwa moja kwa moja na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadaye tumeunda taasisi za udhibiti kwa mfano Mamlaka ya Vyuo Vikuu ama TCU. Pia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Hivi vyombo kadiri miaka ilivyozidi kuendelea, tumezidi kuvipatia Wataalamu wengi zaidi, kuvipatia bajeti nzuri zaidi na vimejenga uwezo mkubwa zaidi wa kuweza kusimamia Taasisi zetu vyema zaidi kushinda ambavyo ilikuwa mwanzo. Ndiyo maana hivi sasa vijana wetu wanapokuwa wanamaliza masomo hapa, hawapati matatizo popote pale wanapoenda duniani kwa ajili ya kukubaliwa katika ama Vyuo Vikuu ama Vyuo Vikuu Vishiriki ama Vyuo vingine ambavyo wanataka kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimesema nilitaje hili angalizo ili tuelewe taswira ya kuwa na Wizara moja ambayo inasimamia pia Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Elimu ya Juu tu inayosimamiwa na Wizara moja; na hili siyo jambo la Tanzania peke yake! Tanzania ina Wizara moja ambayo pia inasimamia Elimu ya Juu; Kenya ina Wizara moja ambayo pia inasimamia Elimu ya Juu; Uganda Wizara moja ambayo inasimamia Elimu ya Juu pia; Rwanda Wizara moja, Zambia moja, Malawi moja, Mozambique moja, Angola mbili, Namibia moja, Botswana moja, Swaziland moja, Lesotho moja, Mauritius moja, Ethiopia moja, Nigeria moja, Singapore moja, Malaysia moja, Republic of Korea moja. *It is not just Tanzania* kwamba kwa sababu Wizara ni moja, basi Elimu ya Juu haisimamiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ya nchi zote hizi Afrika na nje ya Afrika na pamoja na zile nchi ambazo zinafanya vizuri duniani kushinda Vyuo vyote katika Elimu ya Juu na elimu nyingine, nao wanasimamia elimu yao ya juu chini ya Wizara moja ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Serikali hatukuona tatizo, lakini Kamati imezungumza; na kama nilivyosema ni kwamba tunalichukua ili tuweze kulitafakari kwa mapana zaidi ili tuweze kuleta ufanisi katika elimu yetu.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Tamko la Sera Mpya ya Elimu ya Ufundi kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu kuwa Kiswahili, kwamba liangaliwe upya kwa kuwa halina uhalisia katika mazingira ya utandawazi na mawasiliano ya kiuchumi; na kwamba sera hii itawagawa watoto wa Watanzania makundi makundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya lugha ya kufundishia yanaelezwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 chini ya Tamko Namba 3.219 na Tamko la 3.220. Tamko la 19 linazungumzia matumizi ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Sera mpya inaelekeza kwamba sasa tunaanza safari ya kukiwezesha Kiswahili, lugha yetu ya Taifa kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu. Siyo kama hivi sasa tunapoishia katika ngazi ya elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tamko la Na. 3, Ibara ya (3) Ibara Ndogo ya (2) Kifungu cha (20), inazungumzia matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Kwa maana Sera sasa imefungua milango kwa lugha hizi mbili; lugha ya Kiswahili iweze kusonga mbele na lugha ya Kiingereza iweze kusonga mbele. Serikali iweke mikakati ambayo itahakikisha kwamba kwa shule zile ambazo zitakuwa zimeweza kumudu sasa kutoa Elimu ya Sekondari kwa kutumia lugha ya Kiswahili, zisonge mbele. Lini lugha ya Kiswahili itakua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiisimamisha tukasema kwamba sio ruhusa kwamba Wataalamu wetu wa Kiswahili sasa wabuni mbinu na namna ya kuwezesha somo la Kiswahili, Baolojia, Fizikia, Hisabati, na kadhalika, lisomeshwe katika Sekondari ya Juu na Vyuo Vikuu katika lugha ya Kiswahili.

Wakati huo huo Kiingereza nacho kinaruhusiwa kama ambavyo kinaruhusiwa sasa hivi kuendelea katika kutumia lugha hiyo.

Kwa hiyo, uelekeo wa Serikali ni kwamba sasa tunaipeleka elimu ya watoto wetu waweze kumudu lugha zote mbili. Akimudu Kiingereza, sawasawa na anakimudu pia Kiswahili sawasawa na kwa maana hiyo Lugha ya Taifa inakuwa Lugha ya Taifa kweli, kwa maana unaweza ukaitumia pia kwa ajili ya kujifunza na kufundishia kwa ngazi zote, hazina mipaka yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iko kwa Wataalamu wetu kuhakikisha kwamba sasa *challenge* hii ya kuandika vitabu vya kuweza kusimama mbele ya *Lecture Hall* ya *Zoology* au *Botany* ama *Electronics Engineering* au *Mechanical Engineering* na ukafundisha kwa lugha ya Kiswahili.

Wataalamu wa Kiswahili ni kama Mheshimiwa Mbatia ambaye leo amekosoa Sera ile Kiswahili chake, yeye bila ya shaka atakuwa mtu wa kwanza kuandaa Kitabu kile cha Chuo Kikuu ambacho kitafundisha kwa Kiswahili katika somo la *Engineering*. Namwona anapiga makofi. Kwa hiyo, nategemea kwamba hili litafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwamba ni *challenge* na nia ya Serikali sasa kuhakikisha kwamba tunakuwa *Bi-lingual*. Hatunyanyasi mahali popote. Lugha yetu tunaisema vizuri, tunaelewa vizuri, tunaweza kujieleza mahali popote kwa ufasaha na kwa umakini bila matatizo na ndani ya fani zetu. Pia tena kwenye Kiingereza hatuwezi kuachwa kwenye mataa tukiwa Uingereza, tukiwa Marekani, *Scandinavian countries* au mahali popote pengine kama vile ambavyo wale wenzetu wa Mataifa mengine kama *Scandinavian countries* wanavyoweza kufanya. Hiyo ndiyo nia ya sera hii na ndiyo nia ya kutumia lugha zetu hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kufuta ada?



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Sera ya mwaka 2014, hii ambayo tumeizungumzia hapa; Elimu Msingi kwa mfumo wa Umma itatolewa bila ada (*Compulsory and Free Free*) kwamba, Elimu Msingi ya mwaka mmoja jumlisha kumi, kwa maana miaka 11; mwaka mmoja wa Elimu ya Awali, miaka 10 Elimu Msingi. Ndani ya miaka 10 ya Elimu Msingi, miaka sita ni ya Elimu ya Msingi na miaka minne ni ya elimu ya Sekondari. Mtoto akiingia Elimu ya Awali atakaa miaka 11 ya lazima na bila ya ada ili aweze kupikika vizuri na kukua katika kiwango kile ambacho anapomaliza miaka 11 ile ana umri wa kutosha kuweza kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeanza mkakati huo na tunasema kwamba kwa sababu sasa tulichokiandika ni sera, kilichofuatia ni kuandaa mkakati wa utekelezaji wa sera na ndani ya sera hakuwi na mikakati; sera ni matamko ya mwelekeo wa nini mnachotaka kukifanya.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wale waliosema mbona mkakati haumo mle? Ndani ya Sera hakuwi na mkakati. Ni maelekezo yale ya kiseru, halafu mkakati ndiyo huo tunaoukamilisha sasa. Baada ya mkakati, ndiyo utatuwezesha sasa kuweza kusema kihakika kwamba sasa ile *Free-Free* inaanza kuanzia tarehe ngapi? Leo hapa sitaweza kulisema jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo linahusu mkakati, Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu ya Msingi; ilitengewa Shilingi ngapi na Mamlaka ya Elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijibu hili kwamba katika mwaka wa fedha 2014/2015 Programu ya Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu Msingi ama *BRN*, ilitengewa jumla ya Sh. 284,845,931,765/= ambapo kati ya hizo, Sh. 233,831,239,900/= ni kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya *BRN* ambayo imesimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu *TAMISEMI*. Pesa zilizobaki zilitengewa Wizara ya Elimu ili kuweza kutekeleza mikakati hiyo hiyo na tumepata mafanikio makubwa sana katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata mafanikio makubwa sana, tungependa labda kupata hela nyingi zaidi ya hizi, lakini hata pamoja na hela hizi, mafanikio yameonekana na Mheshimiwa Naibu Waziri ameyataja mafanikio ambayo tumeyapata. Ameonesha kwamba, nami nitasema kwa kifupi sana kwamba shule zetu za Kata ambazo bahati mbaya sana wenzetu wa Upinzani wamezibeba, ni kwamba zimechangia mno. Ukichukua mwaka 2014, huu mwaka uliopita, wale waliofaulu na nitakuja kwenye zero kama Wapinzani walivyokuwa wakipiga kelele kwamba tuambie na zero! Nazo nitazisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 waliofaulu Shule za Kata ni 84,306; Shule za Serikali kongwe ni 26,078, Shule za *Private* ni 51,339 na Shule za Seminari ni 5,920. Sasa ukichukua Kata 84,000 na Shule za Serikali kongwe 86,000, maana yake ni laki 110 na ushee, halafu uzilinganisha na hizi 51 za Shule za *Private*. Kama zisingekuwepo shule hizi za Kata hawa watoto wangesoma wapi? Hawa watoto wangesoma wapi? Leo hawa watoto wangesoma wapi? 84,000 wangepata kufaulu? Halafu 84,000 kutoka Kata wangepata wapi hivi leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme kweli! Zero ambayo mnaitaka niiseme; katika shule za Kata tulipoanza, watoto katika Shule za Kata waliopata *Division Zero* mwaka 2010 laki na 51,000. Mwaka 2011, 143,000; mwaka 2013, 117,000; mwaka 2015 mwaka jana 48,000. Kila siku wameendelea kushuka. Wale ambao wameendelea... (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, utulivu! Utulivu! Hatuko sokoni hapa!

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeitaka *Division Zero!* Nimewaambia *Division Zero*; mwenye macho haambiwi tazama! Mmeona katika kuzindua Sera na katika hafla ambayo Mheshimiwa Rais amepokea vitabu, watoto wale walivyokuwa makini.

Mheshimiwa Matiko, katika shule zako nimetembelea Musoma Manispaa, nimetembelea Shule za Sekondari za Kata, huwezi kuniambia kitu chochote! Mimi na wewe twende katika shule zile siku moja tuzitembelee, uone namna ambavyo watoto walivyokuwa wazuri. Ufaulu umeongezeka! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishusha kiwango, watu wote wa *Private* pamoja wale wa Shule za Umma wote wanafanya mihani huo huo. Sasa angalia, mwaka 2013 ufaulu Shule za Sekondari za Serikali ilikuwa asilimia 50.4 wakati zisizokuwa za Sekondari asilimia 83.

Mwaka 2014 za Serikali ufaulu asilimia 63, zisizokuwa za Serikali, asilimia 85. Kwa maana kwamba, zile za Serikali zimepanda kwa ongezeko la *point* 13 na zile zisizokuwa za Serikali zimepanda kwa asilimia 1.2 *you see difference* hiyo hali ambayo inakua! Hali ambayo inakwenda! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ni kwamba, ni lazima tuwaamini Walimu wetu kule shuleni. Lazima tuwaamini kwamba wanafanya kazi kubwa ndiyo maana wanapata ufaulu huu. Ndiyo maana Mheshimiwa Naibu Waziri akasema kwamba mwaka 2014, Kidato cha Sita katika shule bora 10 Kidato cha Sita, nne ni shule za Kata na amezitaja; ya kwanza Igowelo Iringa, Kisimiri ya pili, lwawa ya tatu na ya nne Nangwa. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Nangwa ni ya tatu! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hizo...

**MBUNGE FULANI:** Nangwa ni ya tatu? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Nakuorodheshea! Igowelo ya Serikali; Feza ya *Private*, Kisimiyu ya Serikali, lwawa ya Serikali, Kibaya ya Serikali, Marian ya sita siyo ya Serikali, Nangwa ya Serikali, Uwata siyo ya Serikali, Kibondo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu utulivu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kibondo ya Serikali namba tisa, na kumi Kawawa ambayo siyo ya Serikali! Walimu hawa wanafanya kazi nzuri na kubwa. Kama matokeo mazuri haya, utaniambia leo eti Walimu baada ya *BRN* wanafanya kazi kwa asilimia 30! *Please! Please! Please! Let's be fair with our teachers!* Lazima tuwe *fair*. Eti Walimu walikuwa wanafanya kazi kabla ya *BRN* na baada ya *BRN*, wanauza vitumbua! *Excuse me! Excuse me!* Haiwezekani! Lazima tuwaheshimu Walimu hawa ambao wanafanya kazi nzuri kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni katika shule zetu mtazona sasa hivi watakavyojuliza wazazi kwamba kwa nini nipeleke mtoto katika shule zisizokuwa za Serikali? *Soon*. Mlikuwa mkisema kwamba shule hizi zina Mwalimu mmoja; nitafutie Shule ya Kata ambayo ina Walimu chini ya 20 sasa hivi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Hakuna Taarifa, Mheshimiwa Keissy naomba ukae! Naomba ukae! Endelea Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilikuwa na hoja nyingi na sidhani kwamba kwa muda huu uliobaki nitaweza kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani huwezi kuniongezesa muda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilikuwa na hoja nyingi na sidhani kama nitaweza kuzijibu zote katika muda niliobakiwanao. *I wish* ungeweza kuniongeza muda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya hoja ni kwamba, watoto waliotoka familia duni wapewe mikopo licha ya kuwepo utaratibu wa kutoa mikopo kwa kuzingatia masomo ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilijulisha Bunge lako Tukufu kwamba kufuatana na Sheria Namba (9) ya mwaka 2004 ambayo iliirekebishwa mwaka 2007, iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, inataka mikopo kutolewa kwa wanafunzi ambao ni wahitaji. Uhitaji ndiyo kigezo cha kuweza kupewa mikopo; uhitaji huu upimwe kwa kuzingatia uwezo wa mwanafunzi kuchangia gharama za elimu ya juu kama Sera ya Elimu ya Juu inavyoelekeza. Utaratibu huu hupelekea watoto wanaotoka familia duni kupewa mikopo hata kama hawasomi masomo ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndio la uhakika. Bahati mbaya tuliyokuwanayo ni kwamba hata katika fani za vipaumbele ambavyo Serikali imeweka kwamba tutaangalia pia fani za vipaumbele ili tuweze kufunguka katika maendeleo katika nchi hii; hakuna maendeleo yanaweza kupatikana bila ya fani za sayansi kuwekwa mbele. Mnazungumzia Singapore iko mbele, kwani imesonga mbele kwa *Political Science* ambayo inanizalisha mimi Mwanasiasa? Tuko wangapi tunapigana vikumbo kule kwenye Majimbo? Lazima tuwekeze katika Sayansi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna unapokuwa na rasilimali hizi chache ukasema kwamba usiweke vipaumbele katika fani zile ambazo zitakusukuma mbele katika maendeleo ya Taifa. Utafikaje mwaka 2025 kuwa na nchi ya uchumi wa kati kama hizi fani za vipaumbele utasema zisiwepo? Lakini ukweli wa mambo ni kwamba idadi kubwa ya wanafunzi wenye uhitaji ndio wanaopata mikopo na idadi kubwa ya wasiosoma fani za kipaumbele ndio wanapata mikopo kwa sababu wale wa fani za kipaumbele kama Udaktari, Ufamasia, Udaktari wa Meno, Manesi pamoja na Wahandisi, idadi yao ukilinganisha na wanafunzi wote 100,000 sasa hivi ambao wanapata mikopo, wao idadi yao ni ndogo zaidi. Ndiyo maana tunafanya juhudi kubwa sana kujenga maabara, na kadhalika ili tui pandishe hii idadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla, haya yanayozungumzwa na wenzetu Wapinzani, ni ile ambayo unasema tu ukiona nyekundu wewe sema nyeupe; na ukiona nyeusi sema ya bluu. Kwa sababu hayana ukweli wowote na hayana ukweli hata chembe! Someni *data* kwa sababu hizi ziko *freely open* hata kwenye *website*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nakiri ni kwamba mpaka hivi sasa hatujaweza kufikia asilimia mia kwa mia ya wanafunzi wote wahitaji, kuweza kupata mikopo. Lakini sisi ni nani Tanzania? Uganda ndio kwanza wameanza juji; Kenya hawampi kila mtu; nenda Bara lote

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

la Afrika, hakuna sehemu ambayo inatoa mikopo kama nchi ya Tanzania. Hata Afrika ya Kusini haitoi mikopo kwa watoto wake bila vigezo.

Kwa hiyo, sasa hivi juhudi ya Serikali ya Tanzania ni kwamba imejiweka katika hali ya kuhakikisha kwamba, basi tunaweza kuwafikia wote waliokuwa wahitaji ili waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya Kambi ya Upinzani ni kuwa kuwe na mkakati wa makusudi ambao utawawezesha wanufaika wa Bodi kutambulika na kuanza kurejesha mkopo. Hilo tumelipokea na pia tumeshaanza kulifanyia kazi na Bodi tumeilekeza kwamba kazi yao siyo tu kutoa mikopo, lakini kurejesha mikopo. Mikopo ambayo ilitakiwa mpaka hivi sasa iwe imerejeshwa ni Shilingi bilioni 165; lakini mikopo ambayo imeshapokelewa ni Shilingi bilioni 69.

Kwa hiyo, kuna kiwango kikubwa ambacho kinahitaji kukusanywa bado. Kwa maana hiyo ni kwamba juhudi inabidi iongezwe na hili tunalipokea. Mmelizungumza Kambi ya Upinzani, nasi tutalifanyia kazi kuhakikisha kwamba linakuwa bora zaidi kwa sababu hatua zile tumeshaanza kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni wanafunzi kutopata fedha zao kwa wakati. Nadhani hili Mheshimiwa Waziri Mwigulu amelizungumzia. Nami nasema ni *very unfortunate*, linaniuma sana. Wanafunzi lazima wajue kwamba siyo kweli kwamba Waziri wa Elimu halimuumi jambo hili; na siyo kweli kwamba ni nia yetu kuendelea nalo. Hili mwarobaini wake tunao na tutafikia mwisho. Haikuwa hivi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukeni kipindi ambacho Marehemu Mgimwa tulipokuwanae, kipindi kile chote kile hatukusikia mgomo, hatukusikia kucheleweshwa. Sasa hivi nimemwambia Mheshimiwa dada yangu Saada, kama Marehemu aliweza, nawe unaweza. Wanawake wanaweza na wanaweza zaidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Saada amenihakikishia, na wasaidizi wake wale ni Mawaziri vijana; Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Malima ni Waziri vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linaniuma na wanafunzi mahali popote mlipo na leo Susan amepata wanafunzi wa KIU, wamekuja kwa ukaribisho wake. Niwaambie KIU, hiyo kiu yenu wala haitapata hayo matatizo ya kumalizwa katika Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwenye awamu ya nne na awamu zinazokuja. Hakuna usuluhishi katika mikutano ile ambayo mnaifanya. Nimeifanya mingi sana lakini matokeo yake hayapo.

Kwa hiyo, sasa nadhani imefika muda wa kuhakikisha kwamba mnakaa vizuri kwa kushirikiana ninyi wenyewe na uongozi wenu na kuisindikiza Serikali iweze kufanya yale ambayo inataka kufanya. Mimi nataka kila mtoto ambaye yuko Chuo Kikuu asome na Mheshimiwa Saada amenihakikishia kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, muda! Malizia.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Muda umeisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengi ambayo bado ingebidi niyajibu, lakini baada ya kusema hayo, naomba sasa kusema kwamba mengine tutayatolea majibu ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*... ..Sh.14,348,271,000/=

**MWENYEKITI:** Majina yote tunayo. Kwa hiyo, wote mkae tu, nitamwita mmoja mmoja, yameshaletwa na vyama, hakuna sababu ya kusimama. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuendeleza hoja ambayo nilizungumzia kama Mbunge lakini pia kama Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni moja tu, Mheshimiwa Waziri atufafanulie; pamoja na majibu yote aliyotoa pale, kwa kweli nilitaka aeleze Serikali inasema nini? Nini msimamo wa Serikali katika kutimiza mawili ambayo niliyazungumzia yote kwa pamoja kutokana na *Hansard* niliyonukuu hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu chombo cha Walimu pamoja Ukaguzi. Vyote vilikwenda pamoja na nilinukuu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikumpata Mheshimiwa Waziri kama kweli hiki chombo kinaanza mwezi Julai, 2015/2016, yaani katika mwaka mpya wa fedha. Hiki chombo cha Walimu kinaanza mwaka mpya wa fedha au hakianzi? Nilitaka sentensi fupi ili Walimu wajue kwamba Serikali hii ni sikivu, inajua matatizo yao ya kucheleweshwa mishahara, posho, mapunjo na mengine mengi tu, lakini tukijua kwamba hiki chombo kitasaidia. Je, kinaanza mwaka mpya wa fedha au hakianzi? Tena kwenye sentensi fupi kabisa Mheshimiwa Waziri ili ikurahisishie na sitaki kushika mishahara lakini ikibidi, nikiona sentensi ndefu inakona kona hivi, nashika mishahara wako...

Pili,...

**MWENYEKITI:** Ni moja tu Mheshimiwa!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwenda pamoja. Nakuheshimu sana! Yalikuwenda pamoja, nilinukuu pamoja vyombo vyote viwili vilizungumziwa na Waziri Mkuu pamoja na ukaguzi. Amesema pale kwamba chombo cha Walimu ni cha maana sana lakini ukaguzi ni wa maana sana. Nilinukuu hapa na ulisikia; vyote viwili! Ukaguzi unakuwa Wakala au hauwi? Kama sivyo, nashika Shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu! Anataka kwa ufupi, hataki sentensi ndefu amesema. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo cha Tume ya Utumishi wa Walimu Muswada wake utajadiliwa hapa Bungeni mwezi wa Saba. Kwa hiyo,

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Bunge ndilo ambalo litasema kwamba chombo cha Walimu kitakuwa au haitakuwa. Siyo Serikali; Serikali wajibu wake ni kuwasilisha ndani ya Bunge na Bunge ndiyo litakaloamua kwamba Tume ya Utumishi wa Walimu itakuwa au haitokuwa mwezi wa Saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa sita-*jump the gun*, uwezo huu ni wa Bunge kusema kwamba Serikali ndiyo itaanzisha mwezi wa Saba, wakati kumbe Serikali imewasilisha Muswada tayari au tumepeleka barua ya maombi ya kwamba Muswada huu ujadiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika, atakapokuwa ameupanga na Bunge likajadili na kuupitisha, ndiyo tutakapoweza kupata Tume. Ama sivyo, hatuwezi kupata Tume ile. Lakini pia hili la pili, ingawa swali ni moja, hili la pili; ni moja eh!

**MWENYEKITI:** Wewe endelea kujibu usiwaulize hao!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la ukaguzi kama alivyosema, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema ni jambo zuri, Serikali itaifanyia kazi. Nami nasema ni jambo nzuri sana na tutalifanyia kazi na kwenye maelezo yangu nimefafanua hatua ambazo nimeshachukua mpaka hivi kama Waziri, pia nia njema ya Waziri Mkuu kwamba hili jambo tumelipokea na litafanyiwa kazi kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalihakikishia Bunge lako kwamba hili jambo litafanyiwa kazi kwa uhakika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ajibu kama Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa sababu anapojibu hivyo kwamba anategemea kwamba hawa Wabunge wanaweza kukataa, maana yake ni kwamba hata fedha basi. Kwa sababu kama Serikali ilikuwa na nia, lazima iwe *positive* ijue kwamba Wabunge; nani Mbunge hapa athubutu aseme kwamba yeye atakataa chombo cha Walimu kisiundwe hapa?

Kwa hiyo, kwa vyovyote tunajua, kama Serikali ilikuwa na nia kweli ya kuanzisha mwaka mpya wa fedha, maana yake ni kwamba imetenga. Sasa kama haikutengea, basi tunapoteza muda hapa. Hebu naomba Serikali ituambie, kama Mheshimiwa Rais amelizungumzia, Waziri Mkuu amelizungumzia, halafu tunaambiwa kwamba inategemea Wabunge wakikubali; *please* maana yake ni kwamba basi hata hela hazikutengwa. Naomba hivyo, ama sivyo, natoka na Shilingi yenu hapa! Natoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Hoja ijadiliwe, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa majibu mazuri ya msingi ambayo yametolewa. Nataka kujadili hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi... *(Kelele)*

**WABUNGE FULANI:** Jadili hoja!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Ndiyo najadili kwa kutoa majibu ya hoja hiyo.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza jambo la msingi sana wakati wa kuanza... *(Kelele)*

**MWENYEKITI:** Tulieni Waheshimiwa, tulieni! *(Kelele)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Waziri wa Elimu ametoa majibu mazuri alipoanza kutoa majibu ya hoja hii. Naomba niendelee pale alipoishia Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Katika hoja hii ya kuanzisha chombo kimoja cha Walimu, kuna mambo mawili yamesemwa hapa.

Jambo la kwanza ni suala la Muswada. Jambo la pili, ni suala la bajeti la kuanzishwa chombo hiki. Waziri wa Elimu amesema, Waheshimiwa Wabunge, barua imeshaandikwa na ni kweli sisi kama Serikali hatua za ndani ya Serikali za uanzishaji wa chombo hiki kwa maana ya kuanzisha Muswada tumeshazikamilisha. Tumemwandikia Mheshimiwa Spika. Baada ya kumwandikia Mheshimiwa Spika, lengo letu sasa ni kumwomba Mheshimiwa Spika, atupangie atupe utaratibu wa kupanga Muswada huo uingizwe ndani ya Bunge ili ujadiliwe na kupitishwa. Mara utakapopitishwa Muswada huo na hapa picha inavyoonekana Waheshimiwa Wabunge wote tunataka chombo hiki kiwepo kama Serikali tunavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hapa kinachozungumzwa, jambo la pili ni bajeti ya kuendesha chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Utumishi wa Umma aliulizwa jambo hili wakati anawasilisha hotuba yake na alisema; kwa mujibu wa utaratibu na vifungu tulivyonyavyo, fedha ya uanzishwaji wa chombo hiki imetengwa kupitia Wizara ya Utumishi. Kwa hiyo, kama Bunge litapitisha chombo hicho, fedha zilizotengwa katika mafungu ya Wizara ya Utumishi wa Umma ndizo zitakazotumika. Katika utumishi wa Umma, tuna Tume ya Utumishi wa Umma na tuna TSD. Sasa tukishaamua kutengeneza sheria hiyo mpya, basi suala la fedha halina tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu ukaguzi huu wa Wakala, naomba nim-*quote* Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anahitimisha hoja yake hapa alisema yafuatayo, naomba ninukuu...

*(Hapa Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu alisimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu naomba ukae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize na mambo mawili ambayo nimemsikiliza Mheshimiwa Mama Sitta hapa akizungumza. Kimsingi ninamwambia, bahati nzuri Serikali imepokea jambo la kuanzishwa kwa Wakala, kuifanya Ukaguzi kuwa Wakala. Inalipokea jambo hilo na inakwenda kulifanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwathibitishie, mambo haya yote mawili, yameshafanyiwa kazi na Serikali kwa kiasi cha kutosha. Jambo la Tume ya Utumishi wa Walimu, Muswada ukishapitishwa hapa Bungeni, Tume hiyo inaanzishwa. Serikali kazi yetu tumeshaimaliza. Ukaguzi kuwa Wakala...

**MWENYEKITI:** Malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kazi inaendelea na mara tu tutakapomaliza, haya mambo yote mawili yatakuwa yamefanyiwa kazi.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kulithibitishia Bunge na Walimu, maneno aliyosema Mheshimiwa Rais ni sahihi, Serikali tuko makini na ni lazima tuyatazame mambo haya yote kwa maslahi ya elimu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu tusikilizane. Mheshimiwa Margaret Sitta, alikuwa hoja yake inasema kwamba kama tukubaliana hapa kwamba inaanzishwa mwezi wa Saba, fedha zimetengwa? Ndiyo jibu alilokuwa anapewa kwamba fedha zimetengwa. *(Kelele)*

Tusikilizane! Ngoja tusikilizane kwanza! Tusikilizane basi, tumalizie. Kwamba ziko Wizara ya Utumishi.

*(Hapa Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu alisimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu naomba ukae. *(Kelele)*

Si usikilize kwanza! Nimekwambia kaa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** *(Aliongea nje ya microphone)*

**MWENYEKITI:** Kaa kwanza. Eeh, kwa sababu nikisema kaa Mheshimiwa, unaheshimu Kiti, unakaa. Sasa utapewa utaratibu wakati umesimama! Nami nilikuwa nakupa ufafanuzi, nilikuwa nafuatilia ile hoja iliyokuwa imetolewa. Tuendele. Mheshimiwa Mama Sitta, Mheshimiwa tuendele. *(Kelele)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu sio...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu sijakuruhusu kuzungumza, nitakuruhusu utazungumza. Kwa nini uzungumze sijakuruhusu? Naomba ukae kwanza. Kaa, nitakupa nafasi ya kuzungumza. Sasa ukizungumza kabla sijakupa ruhusa inakuwaje?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** *(Aliongea nje ya mic)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo nimesema kaa, nitakupa nafasi. siyo kujiongelea tu. Amesimama mwenye hoja yake, subiri nitakupa tu. tulia kwanza! Mheshimiwa mama Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa alichozungumza ni kile alichozungumza Mheshimiwa Mhagama kwamba yeye ametuhakikishia Bunge hili kwamba fedha zimetengwa. *(Kelele)*

**MWENYEKITI:** Tulieni Waheshimiwa huko! Sasa nyie mnambishia aliyetoa hoja? Si mumsikilize kwanza? Mbona mnabisha na hoja ni ya Yule? Mheshimiwa Margaret endelea.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nilikuwa nafikiria kwa maoni yangu, anayetokeleza ni Mheshimiwa Kawambwa; aliyelianzisha, ambaye pia anashughulika na uanzishwaji wa Tume ya Idara mbalimbali ni Utumishi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria, baada ya Mheshimiwa Mhagama kuongea, Waziri wa Elimu angesimama pale kwamba itaanzishwa mwezi wa Saba. Yeye aji-commit tu pale kwamba itaanzishwa mwaka mpya wa fedha.

Sasa sisi Wabunge tukishapitisha ile sheria, kwamba ninyi mmepitisha sheria na mmeliahidi Bunge kwamba itaanza kazi na fedha zimetengwa, tutawabana huko. Cha maana, aji-commit hapa. *(Kelele)*



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba tu kuzungumza juu ya utaratibu, sitaki kujadili hoja. Kuhusu utaratibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 103, imeweka utaratibu wa juu ya hoja ya kuondoa Shilingi makadirio. Kanuni ya 103(3) inasema, "madhumuni ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyetoa aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahususi ambalo dhahiri linahusika na kifungu hicho.

Sasa akishatoa Shilingi, kanuni 103(4) inasema, hoja hiyo itatolewa kwa muda usiozidi dakika tano. Baada ya hapo, Wabunge wanaweza kuchangia hoja hiyo, 103(5)(6) Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu, Waziri anayehusika ni Mheshimiwa Kawambwa, siyo huyu mama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu futa hiyo kauli ulisema "siyo huyu mama," usimsemel! Siyo huyo mama, futa hiyo!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Sawa sawa, naomba niifute. Waziri anayehusika ni Mheshimiwa Jumanne Shukuru Kawambwa siyo Mheshimiwa Jenista Mhagama. Yeye sio Waziri anayehusika na jambo hili.

(7) Mbunge aliyetoa hoja ya kuondoa Shilingi ndiye atakayefunga mjadala. Alitakiwa Mheshimiwa Mama Sitta akae kwanza, tujadili hoja, tukishamaliza, anafunga mjadala. Sasa inaelekea wewe unaendesha Bunge siyo kwa mujibu wa kanuni hizi, unaendesha Bunge kwa mujibu wa kanuni za nyumba kwako, haiwezekani! (*Kicheko/Makofi/Kelele*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Aah, haiwezekani futa hayo maneno kwanza! Mheshimiwa Lissu naomba kwanza ufute hayo maneno ya kuendesha Bunge kwa kanuni za nyumbani kwangu. Futa hayo maneno kwanza! Naomba ufute hayo maneno kwanza! (*Kicheko/Kelele*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,..

**MWENYEKITI:** Futa!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Sasa si unataka nifute?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, futa!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Nataka uniambie, haya ambayo yamefanyika, yamefanyika kwa mujibu wa kanuni gani?

**MWENYEKITI:** Futa hayo maneno ya kuendesha Bunge kwa kanuni za nyumbani kwangu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Siyafuti usiposema kama hakuna uvunjifu wa kanuni hapa!

**MWENYEKITI:** Ndiyo futa hayo maneno!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Nimesema wewe unatakiwa uendeshe Bunge kwa mujibu wa kanuni hizi. Unavyoendesha, ni nje ya kanuni hizi. Unayatoa wapi kama siyo nyumbani kwako?

**MWENYEKITI:** Nakwambia hivi, futa!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Siyafuti

**MWENYEKITI:** Kanuni unaijua.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Siyafuti nimesema, sifuti!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niendeleo tu kukupa pole kwa kazi nzito ya kuendesha Bunge hili kwa maana ya taratibu na miongozo ambayo sisi wote tunaijua.

Mheshimiwa Tundu Lissu amesema jambo la muhimu sana hapa; ni kweli kabisa anasema, hoja ya namna hiyo Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu ya hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikufahamisha yafuatayo:-

Mheshimiwa Tundu Lissu anafahamu Waziri huyu anayeongea sasa ndiye mratibu wa shughuli za Serikali. *(Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Kumbe anayehusika ni wewe? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Tundu Lissu subiri!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja hii inahusishwa na Mawaziri wawili...

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Aaa wapi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Yuko Mheshimiwa Waziri wa Elimu, lakini masuala ya Utumishi wa Umma yanashughulikiwa na Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri anayeshughulikia masuala ya Bunge, *Government Coordination*, nimesimama hapa kujibu...

**MBUNGE FULANI:** Huo uongo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Na kutoa maelezo ya Serikali...

**MBUNGE FULANI:** Waziri anayehusika ni Mheshimiwa Kawambwa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kwa upande wa Utumishi wa Umma...

**MBUNGE FULANI:** Waziri anayehusika ni Mheshimiwa Kawambwa!

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Shukuru Kawambwa atapata nafasi ya kufunga hoja yake kwa matakwa ya kikanuni. Atapata nafasi ya kueleza kwa matakwa ya kanuni...

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Kanuni za wapi? Kanuni za nyumbani kwake!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Ataeleza umuhimu wa hoja hiyo na namna halisi ilivyokuwa na sisi kama Serikali tutaendelea kusimama imara. Hoja hii ni ya kwetu na tunatambua umuhimu wa Walimu katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa taarifa hiyo, nimetoa maelezo hayo na Waziri wa Utumishi alishaweka maelezo haya wakati anawasilisha hotuba yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu! Mkuu wa Shughuli Bungeni. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia kwako Waheshimiwa Wabunge, tuvumiliane na tuheshimiane. Hiyo moja.

Pili, naomba nisaidia Bunge lako kwamba kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuonyesha umuhimu wa chombo cha Walimu. Namshukuru sana Mheshimiwa Margaret Sitta kwa sababu hajaanza leo kupigania chombo hiki. Mimi nilikuwa Waziri wa Utumishi, anakumbuka...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah! *(Kicheko/Kelele)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Shilingi imetolewa, mjadala uko wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAHUSIANO NA URATIBU):** Sikilizeni sasa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana tena Wabunge kuonyesha kwamba wanakithamini chombo cha Walimu. Sasa niwaambie kwamba, hapa Bungeni nilitaka nijibu suala linaloletwa sasa hivi kwamba Mheshimiwa Jenista sio Waziri mhusika. Nataka niliambie Bunge lako Tukufu kwamba hapa Bungeni Serikali inafanya kazi kama kitu kimoja. Hiyo moja. *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala hili linamhusu Waziri wa Elimu na Waziri wa Utumishi. *(Kicheko/Kilele)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAHUSIANO NA URATIBU):** Suala hili linahusu Waziri wa Elimu na Waziri wa Utumishi.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna! *(Kicheko/Kelele)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAHUSIANO NA URATIBU):** Ninaomba Mheshimiwa Margaret Sitta akumbuke kwamba wakati wanadai chombo cha Walimu... *(Kelele)*

**MWENYEKITI:** Tulieni! Tulieni basi! Ninyi ndio mnaomaliza muda kwa kupiga kelele!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MBUNGE FULANI:** Kanuni za wapi hizi? *(Kilele)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, malizia!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha Bunge lako Tukufu kwamba wakati Walimu kupitia mama Margaret Sitta wanadai chombo cha Walimu, mimi mwenyewe nikiwa Waziri wa Utumishi niliwaambia kwamba tunakuwa na TSD kwa kujitayarisha baadaye kuwa na chombo. Ndiyo maana sasa Waziri huyu akakipokea chombo hiki baada ya sheria kupitishwa. *(Kelele)*

Kwa hiyo, nawaombeni sana, naombeni sana Waheshimiwa Wabunge, chombo cha Walimu kinatokana na TSD, hatimaye kitahamia kwa Waziri wa Elimu kikiwa chombo cha Walimu na hiki tunakitaka wote. *(Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Kelele)*

**MWENYEKITI:** Haya, alisimama Mheshimiwa Mbatia wakati wa kuchangia. *(Kicheko)*

Ndiyo, niliwaona wote waliosimama. Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu tuendeleo na hoja nyingine kwa sababu mtoa hoja mwenyewe amesharidhika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kifungu hicho kinaafikiwa?

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaoooo!

**MWENYEKITI:** Si amesema tuendeleo na hoja, mkawapigia makofi?

**MBUNGE FULANI:** Wizara ilikuwa bado Mheshimiwa...

**MHE. SUSAN A. LYIMO** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado watu wengi sana kwenye hoja hiyo!

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa kuhusu utaratibu! Taarifa kuhusu utaratibu!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Zima *microphone!*

Mheshimiwa Sitta amesharidhika ndiyo maana nilikuwa namwita Mheshimiwa; hujaridhika? Mheshimiwa Mama Margaret Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Wachangie wengine!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umweleweshe kwamba, hii ni hoja nyingine. Kama bado... *(Kelele)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Aah, hiyo siyo nyingine. Bado tuna hiyo. Tuimalizie hiyo kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta! *(Kelele)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeshasema kwa uwazi kabisa... *(Kelele)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Sasa mimi ndio mtoa hoja mnaninyima nisiongee?

**MBUNGE FULANI:** Ulishamaliza! *(Kelele)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Sijamaliza! *(Kelele)*

**MWENYEKITI:** Nimeshakwambia nimekupa ruhusa, ongea!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua, Mheshimiwa Celina Kombani Waziri wa Ofisi ya Rais (Utumishi) ndiye anayepanga. Lakini kwa leo jinsi tulivyokwenda kama mnakumbuka, mwanzoni kabisa kauli aliitoa Mheshimiwa Waziri Kombani, baadaye ikaonekana kwamba atakayehakikisha inafanya kazi ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kauli yake nini? Yeye ndio aongee. Akishaongea yeye, mimi ndio nitasema nimeridhika au sijaridhika Mheshimiwa Waziri akinijibu.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri, jibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji wa Serikali Bungeni ni uwajibikaji wa pamoja. Fedha ambazo Mheshimiwa Margaret Sitta amezihaji kama zipo ili kuhakikisha kwamba kweli hicho chombo kitakuwa kimeanzishwa, sasa nimeonyeshwa na fedha hizi zipo kwenye Vote 94 na siyo Vote 46 ambayo ni Wizara yangu. Nami sisemei Wizara nyingine, nasemea Wizara yangu. Kwa hiyo, kwa sababu ipo kwenye Vote 94 na *Sub-vote* 2003, kwa hiyo, bajeti hiyo ipo kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016. Kwa hiyo, *Teachers Service Commission* ipo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja, Mheshimiwa Margaret Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri kwa sababu katamka mwenyewe na *Hansard* ipo kwamba, chombo hiki kinaanza kazi mwaka mpya wa fedha 2015/2016 na ametutajia kifungu cha fedha kitakachotumika. Kwa hiyo, kwa msingi huo, naishukuru Serikali kwa kuwa sikivu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Ester Bulaya achange nini?

**MBUNGE FULANI:** Katika mshahara wa Waziri!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nilichukua muda mrefu sana kuzungumzia ni jinsi gani Serikali tunatunga sheria halafu haizitekelezi sheria tunazozitunga hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema, unapozungumzia *TEA*, ndiyo *engine* katika Wizara ya Elimu, kama ambavyo tunazungumzia *REA* kwenye Nishati na Madini. Masikitiko yangu, leo hii tunazungumzia kuhusiana na miundombinu mibovu kwenye shule zetu kuhusiana na upungufu wa madawati kwenye shule zetu, kuhusiana na ucheleweshwaji wa fedha za mikopo kwa wanafunzi. Hizo fedha zote hazitolewi kwa mujibu wa taratibu. Sheria tumezipitisha kwamba Serikali ipeleke fedha, fedha haipelekwi.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku tunakuja kupewa majibu mepesi na kutopeleka fedha ni kuvunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea Serikali ndiyo isimamie sheria, lakini ndiyo inakuwa ya kwanza kuivunja na mwisho wa siku ndiyo matatizo ya mazingira magumu yanaendelea kwenye shule zetu na kwenye vyuo vyetu. Sasa nataka majibu ya Serikali, kwa nini fedha hizi hazijatengwa? Kwa nini imevunja sheria badala ya kutekeleza sheria? Nahitaji majibu na ninaweka wazi kabisa kwamba nitatoa Shilingi kama siridhiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Bulaya kama ifuatavyo:-

Bahati ni kwamba Naibu Waziri wa Fedha alikuwepo hapa na ametoa maelezo kuhusu jambo hili. Mimi nitajaribu kulisisitiza kwamba, kwanza ni kweli pesa hizo hazikutengwa kama ambavyo ilikuwa imetarajiwa kisheria. Kwa upande wa elimu, hilo ni pungufu kwa maana ya kwamba, tutashindwa kutekeleza malengo yetu kwa Sekta ya Elimu hasa kipindi hiki ambacho tumejikita katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa ikiwa resources zenyewe hatuwezi kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha katika maelezo yake ameahidi hapa kwamba, makosa yametendeka, lakini makosa yale hayatarudiwa tena. Ni kwamba hili liwe fundisho kwa Serikali na ndiyo tunakuja mwisho wa mwaka sasa hivi, tuko ndani ya mwezi wa Sita, tunafunga mwaka; amegundua hakuna namna ambayo pesa zile zitapatikana kwenda TEA. Kwa hivyo tutafanya marekebisho katika miaka inayofuata, mwaka ujao.

Mheshimiwa Naibu Waziri Ametamka pia kwamba kiasi cha fedha kitaenda TEA na TEA kweli katika mafungu mengine kwa mfano asilimia 2.5 ya Education Levy ambayo nayo ni fedha ambazo zinapatikana kutokana na Sheria ile ya Education Levy, hizo zinaenda TEA kama kawaida na zinatusaidia katika Sekta ya Elimu. Nina imani kuwa Mheshimiwa Bulaya kwa hili ambalo umelizungumza kwa msisitizo mkubwa na kwa hisia nzito, nikusihhi tu kwamba Shilingi hiyo usiishike Shilingi na Serikali itahakikisha kama Waziri wa Fedha alivyosema, kwamba jambo hili halitarudiwa tena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa Shilingi tuchangie na naanza kuchangia. Natoa Shilingi! Natoa hoja hapa ya kuondoa Shilingi ili Wabunge tuchangie, jambo hili ni nyeti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ya kutoa Shilingi. (Kelele)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina sababu za msingi za kufanya hivyo. Wakati nachangia nilisema, tangu mwaka 2001 sikuwepo humu Bungeni, ilitungwa sheria, tena ilikuwa inasema, kutengwe fedha isiyopungua asilimia mbili ya bajeti katika kipindi cha miaka kumi sheria hiyo haijatekelezwa! Fedha hazijaenda TEA. Ni mwaka mmoja tu walipeleka asilimia 0.05 hata asilimia moja haijafika. Miaka kumi! (Makofi)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, baada ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kutoa hoja hapa tukafanya *amendment*. Waheshimiwa Wabunge, kama mnakumbuka tulifanya *amendment*, tukasema Serikali itenge asilimia isiyopungua mbili; inaweza ikawa tatu au nne ya bajeti. Ile miaka kumi, haikutetelezwa; tumefanya *amendment* mwaka 200e haijatekelezwa! Haijatekelezwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa huo mwaka 2014 ilipaswa kupelekwa Shilingi bilioni mia 185, haijaenda hata senti. Nitakubaliye majibu mapesi hapa? Mwaka huu wa fedha, TEA wanatakiwa wapewe Shilingi bilioni 346, bado hazijapelekwa. Ndiyo maana nilianza kuuliza humu suala hili katika mshahara wa Waziri Mkuu nikijua Serikali itapeleka hata fedha kidogo. Leo naambiwa ahadi. Wiki iliyopita ilikuwa ahadi, haijaenda. Ahadi hii itatekelezwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia suala la elimu ni suala nyeti. Tukiwapa hawa TEA fedha, hata michango ya Maabara itapungua kwa watu wetu wa kawaida, kwa sababu ndiyo kazi yao. Hatuwapi fedha, hawafanyi; mwisho wa siku tunaenda kule kuwabana wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kukomesha tatizo la migomo, asilimia 64 kati ya asilimia mbili inatakiwa iende, haijaenda! Asilimia 30 ibaki TEA kwa ajili ya *infrastructure*, haijaenda! Asilimia tatu inatakiwa iende NACTE, haijaenda! Asilimia tatu inatakiwa iende TCU, haijaenda! Sasa nitakubaliye leo itaenda wakati miaka kumi haijaenda? Tumefanya *amendment* haijaenda! Leo hii inaendaje? Nilichangia katika mshahara wa Waziri Mkuu haikwenda, leo inaendaje? Wanaoteseka ni vijana! Wanaoteseka ni wananchi wetu kuchanga wakati kwa kiwango kikubwa wakati wangepunguziwa mzigo na Serikali. Sasa leo nakubaliye? Miaka kumi sheria haijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *trend* ya Bunge hili kuwa tunatunga sheria, Serikali hamtekelezi, ifike mwisho. Tulipitisha Azimio hapa la Mheshimiwa Kigwangalla, halijatekelezwa; hii ya Mheshimiwa Mwigulu haijatekelezwa. Kwa nini tunafanya hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa hoja ya kutoa Shilingi Waheshimiwa Wabunge tuchangie. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya. Sekta ya Elimu ni Sekta nyeti, ni sekta ambayo kwa kweli kwa uhai na mustakabali wa nchi yetu, ni sekta ambayo inahitaji kupewa kipaumbele kwa kiasi kikubwa sana. Sasa hii *trend* ambayo Mheshimiwa Ester Bulaya ameigusia, nasi inatupa mashaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea, sasa hivi michango mashuleni imekuwa kero kubwa sana. Kuna michango ya maboresho, michango ya Maabara, michango ya uji, michango ya Walinzi; kumekuwa na michango chungu mbovu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imetoka na Sera mpya ya Elimu ambayo inasema elimu itakuwa bure. Sasa kama tunaongelea kwamba tutakuwa na Sera ya Elimu ambayo itakuwa bure, lakini pili vyombo ambavyo vinatusaidia sasa kupata fedha kwa ajili ya kuendesha hizo shughuli, hazipewi fedha; sasa utekelezaji wa sera hii itakuwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na Serikali ije itupe majibu mazuri, kwa nini fedha hizi haziendi katika hiki chombo kukiwezesha kufanya majukumu yake ya msingi? Kama tunaona kwamba chombo hiki siyo cha msingi, tukiondoe. Watu hawa wanalipwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

mshahara, wanalipwa marupurupu; kama tunakiona hakina maana, tukivunje kuliko kukiacha chombo ambacho mwisho wa siku tunatunga sheria, tunapoteza muda wetu halafu hakipewi fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake, atuambie ni lini Serikali imetoa Waraka wa kuchangisha wananchi? Sasa hivi wananchi wanapata shida sana. Watoto wanatozwa fedha za *tuition* na wasipokwenda nazo asubuhi wanapigwa viboko, wanarudishwa majumbani kwa sababu kuna mambo mengi ambayo hayajafanyika. Nataka Serikali ilitoe tamko katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami naomba kuchangia hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anayehusika amesema kwa maneno yake kwamba Serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Fedha inakili kwamba haijapeleka hizi fedha na akasema kwamba hili jambo halitarudiwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijawahi kupeleka pesa isipokuwa kwa mwaka mmoja ambao Mheshimiwa Esther Bulaya amesema. Miaka mingine yote Serikali haijatekeleza sheria, haijapeleka fedha; wanafunzi wanagoma, mashule hayajengwi, maabara hakuna, halafu Waziri anasema kwamba hili halitarudiwa tena. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri namna ya kuhakikisha kwamba halitarudiwa tena, ni kwa hawa ambao wamekosa kwa miaka ziadi ya 10, kuwajibika au kuwajibishwa. Hawa ni watu ambao ni wazi kabisa, hawajui watendalo. Kama hawajui watendalo, tunawalipa mishahara ya Uwaziri kwa sababu gani? (Makofi)

Mheshimiwa Waziri kama umeshindwa kupeleka fedha TEA kwa kwa miaka 10, hufai kuwa Waziri wa Elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wa Hazina, Mheshimiwa Waziri kama umeshindwa kupeleka fedha TEA kwa kutekeleza sheria kwa miaka 10, hufai kuwa Waziri. *Simple!* Ili isirudiwe tena, hawa ambao wameshindwa kazi, waondoke, wewekwe watu wengine ambao wanaweza kufanya kazi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO-:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na mimi naunga mkono sana hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa sababu moja kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TEA (Mamlaka ya Elimu Tanzania), inafanya kazi katika mazingira magumu sana. Lakini tumepitisha sheria sisi wenyewe mwaka 2001. Leo ni mwaka wa 14; tunatambua jinsi gani; na nimeona, mawaziri wote wanakuwa wanakwenda pale kwenye ile Ofisi.



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni wazi kwamba TEA imekuwa ikisaidia vyuo mbalimbali, kwa mfano Chuo cha Ardhi, wamesaidia sana kutoa mikopo. Siyo hilo tu, wamesaidia sana kujenga *hostel* na ninakumbuka tulikwenda mpaka Kongo wakati wanazindua *hostel* za watoto wa kike, ili kupunguza watoto wetu wa kike wasipate mimba na kutoroka mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ya msingi na ninaungana vilevile na Mheshimiwa Lissu; kwa kuwa muda wote huu Serikali imeshindwa na leo hii Mheshimiwa Waziri anatuambia, tena kwa maringo kabisa, kwamba *this time* watafanya, miaka 14 walikuwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wawajibike ili shirika hili au mamlaka hii iweze kufanya kazi yake vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, limeshazungumzwa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, mtoa hoja! (Kelele)

Mheshimiwa Waziri, naomba majibu! Naibu Waziri wa Fedha, majibu!

**MHE. MWIGULU L. M. NCHEMBA - NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tunalolizungumzia na tumeweka wazi mwanzo na takwimu hivyo ndivyo zilivyo. Kwanza, ziko hatua mbili; kuna sheria iliyokuwepo mwanzo na sheria ambayo ilikuja kufanyiwa marekebisho. Lakini tangu yamefanyika marekebisho hayo ambayo lengo lake lilikuwa ni kuboresha, kumekuwepo na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tunapoongea, Wizara ya Fedha ilishatoa Shilingi bilioni 29 na hivi sasa tunavyoongea pia, imeshatoa *exchequer* ya Shilingi bilioni tatu ambazo zinatakiwa zifanyiwe utaratibu wa malipo kwenda kwenye mfuko. Hii ni asilimia 59.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huo, ukitaka kuwa-*hold on* Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa miaka 10, wakati tumekuwa tukipitisha bajeti zile, tutakuwa tumekwenda mbali sana. Hapa tufanye *assessment* ya bajeti ya mwaka wa fedha; na mwaka wa fedha huu ambao tunaongelea, zimekuwa zikitoka. Hizo Shilingi bilioni 29 hazijatoka siku moja; zinatoka kufuatana na mahitaji. Hivi tunavyoongea, kuna *exchequer* ya Shilingi bilioni tatu ambayo ndani ya wiki mbili kufuatana na ukamilishaji wa masuala ya kiutawala itakuwa imetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lenyewe kama lilivyo, ni la msingi na linaeleweka wala halihitaji chachandu nyingine ambazo zimeanza kukolezwa. Lenyewe linajitegemea na Serikali inaona uzito wake. Tulivyokuwa tunasema, mazingira haya hayatajirudia, tulikuwa tunamaanisha kwamba siyo kila mwaka utakuwa mwaka wa uchaguzi, na siyo kila mwaka utakuwa mwaka wa Serikali za Mitaa; na siyo kila mwaka utakuwa mwaka wa kutengeneza Katiba.

Kwa hiyo, majukumu yale mengine ambayo yali-*crowd resources* za Serikali hayatajirudia kila mwaka. Kwa hiyo, tunategemea fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya mifuko mbalimbali zitakwenda kwenye mifuko ambayo ilikuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natambua jitihaa na kusimamia mambo ambayo anayaamini Mheshimiwa Ester, akishalibeba, analibeba kwa namna hiyo. Lakini kwa jambo hili

la leo, namwomba kwamba Serikali imeshachukua hatua, baada ya kubadilisha mfumo huu wa mfuko huu na fedha ambazo imezitoa na hizi ambazo tunategemea kuzitoa ndani ya wiki mbili, hatuna haja ya kukwamisha Wizara. Sisi kama Wizara ya Fedha, tunatoa ahadi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tutasimamia kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya mfuko huu zinakwenda ili kuhakikisha kwamba mfuko huo unatekeleza majukumu yake kama ambavyo ulikuwa umekusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge aridhie bajeti ya Serikali kwa Wizara hii ipite. Sisi tunamwahidi kwamba haya tutayafanyia kazi. Mwaka 2014 tulimwahidi kwenye Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, tulimwahidi kwenye jambo lingine alilolisimamia na hili tunamwahidi kwamba hana haja ya kuchukua Shilingi, tunakwenda kulifanyia kazi na taasisi husika itafanya kazi zilizokusudiwa kama ilivyokuwa imetarajiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua utayari wa Mheshimiwa Mwigulu, najua kabisa. Lakini ninachotaka majibu sahihi hapa, hii asilimia tatu iliyotolewa, maana hapa tunachozungumzia ni kitu kilichowekwa kisheria na fedha zinazotakiwa kutolewa kisheria; sheria kuvunjwa. Sasa hii Shilingi bilioni tatu ni katika ile miaka 10 ambayo haijatengwa? Hii Shilingi bilioni 29 ni katika ile miaka 10 ambayo fedha zilitakiwa kutengwa, hazijatengwa; au hii Shilingi bilioni tatu na Shilingi bilioni 29 ni katika fedha ambazo ni Shilingi bilioni 185 ambazo hazijatolwea hata Shilingi tano? Au hii Shilingi bilioni 29 na Shilingi bilioni tatu, ni katika Shilingi bilioni 346 za mwaka huu ambazo zinatakiwa kutolewa? Sijapata majibu! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge makini hawezi kukubali jibu kwa sababu tu jibu limetolewa. Lazima jibu liendane na ufafanuzi wa kutosha. Sina shida na Shilingi, ninachotaka ni majibu sahihi na utaratibu wa haya madeni yaliyopo kisheria yatalipwaje? Ili TEA waweze kufanya kazi zao vizuri. *Is not about* Shilingi bilioni tatu; ni zipi? Kwenye ile miaka 10, kwenye huu mwaka ulipita wa Shilingi bilioni mia moja na kitu, au kwenye Shilingi bilioni 360 za mwaka huu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shilingi bilioni 29 ni kwa miaka ile 10 ambayo haijatengwa, au kwenye Shilingi bilioni mia moja themanini na kitu, au Shilingi bilioni 340 ambazo hazijatengwa?

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipewe majibu! Tunafanya kazi ya nchi, tuko kazini.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, Mheshimiwa Waziri ameshaelewa. Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bajeti ya Wizara husika na kuna bajeti ya taasisi husika; na kuna fedha tunayoiongelea ambayo ni asilimia kwa mujibu wa sheria. Hii tunayoiongelea ambayo ni sawasawa na mifuko mingine ambayo tumeiongelea kwenye mifuko mingine ambayo na yenyewe inatengewa asilimia, hii tunaongelea *education levy* ambayo ilikuwa inatarajiwa iwe Shilingi bilioni 49 kutokana na ile asilimia 2.5 na asilimia ile mbili ambayo yenyewe inatoka kwenye marekebisho yale tuliyoyafanya kwenye sheria ambayo ilihusisha kupanua wigo wa mfuko wa hoja ile ambayo ameisema huku akinihusisha na mimi.

Kwa hiyo, kwenye hii ambayo tunaongelea inayohusu makato yanayokwenda moja kwa moja kwenye mfuko, achilia mbali bajeti ya taasisi nzima ambazo na Wizara nyingine

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

hazikupaya bajeti kwa asilimia 100, hii sisi tunaiongelea ambayo iko kisheria kama ambavyo tumeahidi kwenye Mfuko wa Barabara na kwenye Mfuko wa Umeme. Hii tumesema, hizi maadamu ziko kisheria, zitakwenda na tutahakikisha kwamba tunakokwenda mbele pia zinakwenda; na hata Serikali imekwenda hatua zaidi. Imesema fedha zote ambazo zinatakiwa kwenda kwenye mifuko, hazitachanganywa na matumzi mengine baada ya kuwa zimekusanywa ili kuepuka malimbikizo.

Kwa hiyo, jambo kama hili ambalo tunalisema, tunaongea kitu ambacho tuna uhakika nacho. Zikishakushanywa zikaenda mfuko mkuu, kabla ya kugawa matumizi mengine ambayo yanaweza yakasababisha fedha nyingine zikakosekana kwenda kwenye mifuko ambayo ilikuwa imepangwa, Wizara ya Fedha pamoja na Benki Kuu zimesema zitakuwa na utaratibu maalumu wa kuziweka pembeni zikishaingia mfuko mkuu ili ziweze kwenda kwenye mifuko ile ambayo ilikuwa imekusudiwa, kuondoa uwezekano wa kwamba fedha zinaweza zikaisha na kukawepo na fedha ambazo hazikutoka katika mwezi husika baada ya kuwa makusanyo yale yamepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hili tunalolisema ni jambo ambalo tuna uhakika nalo, ambalo Wizara tumejipanga na ndiyo maana tunaongea kwa uhakika kwamba fedha ambazo zinatakiwa kwenda kwenye mifuko zitakwenda kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, mwaka 2014 wakati tunamaliza mwaka wa fedha uliopita, kuna fedha ambazo zilitakiwa ziende kwenye mifuko ambazo hazikuwa zimekwenda, lakini ndani ya robo ya kwanza ya mwaka, tulikuwa tumemaliza fedha hizo ambazo zilitakiwa ziende kwenye ile mifuko. Kwa hiyo, hili tunalolisema ni jambo ambalo tuna uhakika nalo, na namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie kwamba na sisi tunatambua umuhimu huo na tunatambua *concern* yake kwa ajili ya huu mfuko na tutafanya hivyo ili kuweza kuhakikisha kwamba tunalitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfuko wake ama kwa taasisi yake kwa ujumla kuhusu bajeti, hilo tumelisemea kama ambavyo tumesema kwenye Wizara nyingine na tutahakikisha kwamba linafanyika hivyo.

Mheshimiwa Ester, mambo mengine haya tunayoyaongea, mzizi wa jambo lote ni makusanyo na mzizi wa jambo lote ni fedha ambazo tulikuwa tunategemea kwa ajili ya matumizi mengine ambazo zilikuwa zinatoka nje.

Sasa kwa kuwa tumeweka utaratibu, mnatambua Bunge lilibadilisha baadhi ya sheria ambazo zinatuhakikishia Serikali kuongeza mapato. Hiyo nayo ndiyo inayotupa *confidence* kwamba tunakokwenda, haya hayatakuwa yanajirudia na siyo kwamba hatukupeleka kwa makusudi, bali ilikuwa ni hali iliyokuwepo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni ya 104(1), naongeza muda wa nusu saa. Kuanzia saa mbili, nitaongeza nusu saa.

Mheshimiwa Ester unaridhika na majibu hayo?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na...

**MWENYEKITI:** Kama unamrudishia Shilingi au unaendelea nayo!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naenda huko huko.

**MWENYEKITI:** Usichangie tena.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sichangii, nisikilize basi. Ninachosema, sina shida na Shilingi, Mheshimiwa Mwigulu amesema atatoa.

Kwa uzito wa jambo hili, tunahitaji *commitment*. Baada ya muda gani, hizi Shilingi bilioni 30 ambazo wamesema watazitunga, zitakwenda? Utaratibu wa haya madeni ya nyuma ya kulipa yatakuwaje ili Sekta hii ya Elimu iende? Sina tatizo na Shilingi, lakini ukisema tuko, tutalifanyia kazi, lini? Yes!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu nimesema, hivi ninavyoongea, kuna Shilingi bilioni tatu tayari zimeshawekwa kwenye utaratibu wa *exchequer*. Kwa hiyo, wao wataandaa hati ya malipo. Wataandaa utaratibu wa malipo kutoka taasisi husika. Huo huwa ni utaratibu, ukipewa *exchequer* na wewe unaandaa.

**MWENYEKITI:** Anachotaka umwambie, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):** Kwa hiyo, hilo ni ndani ya wiki mbili. Haya mengine ambayo ni ya kibajeti, kama tunavyotarajia, sasa hivi tumeshabakiza mwezi mmoja ambao ndiyo ulioanza kwa ajili ya kukamilisha bajeti ya mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, hayo ni matarajio yetu kwamba nyingine hizi tutalipa katika utaratibu huu wa malipo ya mwisho wa mwaka wa fedha huu ambao ndiyo mwezi huu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo Shilingi bilioni 30 kama ndani ya wiki mbili zitoke na madeni mengine yalipwe na mwisho kuendelea kuvunja sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haki na wajibu wa Serikali kuwapatia posho wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa ajili ya huduma za lazima. Kinyume chake ni kukiuka haki za wanafunzi na hili ni suala la sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa hoja yangu ni kuitaka Serikali itueleze ni lini itaondoa tatizo la posho za wanafunzi wa Vyuo Vikuu? Hivyo Serikali haioni kwamba kuwakoshesha posho wanafunzi wa Vyuo Vikuu, wanawafanya wanafunzi hawa hasa wale ambao ni masikini waweze kukumbatia mambo ambayo yanakwenda kinyume na masomo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ni lini wanafunzi waliosimamishwa masomo yao, ama kwa kugoma au kwa kuandamana, kwa sababu ya kukoseshwa haki zao za msingi, yaani posho, waterejeshwa mashuleni? Kama sikupata jibu ambalo ni la msingi, basi nami nitazua Shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Kombo kama ifuatavyo:-

Moja, ni kuhusu kutoa fedha kwa wakati kwa fedha za mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mwaka huu wa fedha tulipata changamoto kwamba fedha zile ambazo ni za mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu katika awamu ya tatu, hazikutoka kama ambavyo ilitegemewa. Walipata fedha chache kuliko zilivyotegemewa, na matokeo yake ni kwamba baadhi ya

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanafunzi walichelewa kupata fedha zao. Lakini sasa fedha zile zimetoka, jumla ya bajeti ya mwaka huu wa fedha ni Shilingi bilioni 341.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha mtikisiko mwezi uliopita tulikuwa tunaidai Hazina iweze kupeleka Shilingi bilioni 30 katika Bodi ya Mikopo. Mpaka hivi sasa fedha zimetolewa na kilichobaki, kumbukumbu zangu zinaniambia haizidi Shilingi bilioni tisa ambazo ziko katika muda muafaka kwa sababu hizi zitawawezesha wale wanafunzi watakaokwenda mafunzo ya vitendo mwezi huu wa Sita watakapokuwa wanamaliza, walipwe waweze kwenda kwenda kwenye mafunzo yao.

Kwa hiyo, zilichelewa, katika awamu hii ya tatu, lakini imesharekebishwa na fedha zile zimetoka na wanafunzi wamelipwa. Zilizobaki zitalipwa kwa wakati na kama nilivyozungumza awali, ni kwamba hatutegemei tena mtikisiko wa aina hi kwa sababu tumejipanga na Wizara ya fedha kwamba fedha hizi zina mtiririko wa tarehe, kwamba lazima zitoke kwa tarehe yake. Kama hazikutoka kwa tarehe yake, tunajenga hisia kwa wanafunzi kwamba mpaka wagome ndiyo wapate fedha ambayo haiwasaidii wao wala haiisaidii Serikali.

Kwa hiyo, tunasema kwamba jambo hili tumefikia ukomo wake. Nina imani tulivyojipanga na Wizara ya Fedha ni kwamba, mwaka ujao wa fedha, kwa vile Baraza litapeleka Hazina mtiririko ule; kalenda ya mihula ile mine; tarehe zipi fedha fulani iwe imeingia kwenye Bodi? Hazina itafuata hivyo na jambo hili hatutakuwa nalo.

Sasa hili la pili la maandamano na migomo iliyotokea na uharibifu wa vifaa katika colleges husika; Vyuo ni *self-governing*, vinajiendesha, vina taratibu zake za taaluma, taratibu za utawala na taratibu za nidhamu. Atakayekwenda nje ya taratibu za Chuo, kuna vyombo kamili ambavyo vimejengwa ndani ya *charters* za Vyuo husika ambavyo ni kwa ajili ya kusimamia nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao sasa hivi katika Vyuo mbalimbali ambavyo hilo limetokea, wamepelekwa kwenye taratibu hizo na habari ambazo ninazo mpaka hivi sasa, katika Chuo kwa mfano *KIU*, ni kwamba karibu wote wamesharudi na ambao hawajarudi wapo katika kuhangaikiwa katika taratibu zile za Vyuo kuweza kuwaonyesha kama wana makosa wachukuliwe hatua na wasiokuwa na makosa watarudi.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Waziri kakiri kwamba wanafunzi bado wako ambao hawajapata posho zao. Sasa tunataka kujua, ni lini matatizo haya ya posho za wanafunzi hawa ambao hawajapata posho zao watazipata? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kakiri kwamba bado kuna wanafunzi ambao hawajarejeshwa kwenye masomo kwa sababu ama ya kuandamana au kwa migomo. Kuandamana huku na migomo hii, wanaosababisha ni Serikali! (*Makofi*)

Sasa kosa la Serikali huwezi kuwabebesha wanafunzi. Kwa hiyo, tunataka wanafunzi warejeshwe, halafu bado naondoa Shilingi na nataka hoja hii ichangiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, hoja ichangiwe na ninaondoa Shilingi ya Waziri. Kama hatujapata majibu ya msingi, basi naondoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Majibu! Amesema kama hajapata majibu, anaondoa Shilingi. Namrudishia mwenye hoja yake. Mheshimiwa Waziri majibu!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**WABUNGE FULANI:** Aaah! Ichangiwe! (Kelele)

**MWENYEKITI:** Ndiyo! Mheshimiwa Kombo! Tulieni, taratibu.

Mheshimiwa Kombo ulisema halafu ukarudia, ukasema kama sitapata majibu ya uhakika nitatoa. Sasa hivi umesema, mimi nakusikiliza sana ndiyo maana Waziri anampa majibu halafu mtachangia...

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hansard ipo!

**MWENYEKITI:** Basi, Mheshimiwa Waziri waache wachangie. Haya, Mheshimiwa Mchungaji!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kombo kwa sababu ni jambo ambalo ni fedheha kwa Taifa letu. Nchi za wenzetu, wanafunzi wa Vyuu Vikuu wako kwenye *greenhouses*, wanabuni mbegu mbalimbali, wanatafiti, lakini Vyuu Vikuu wanafunzi wa Tanzania wanakimbizwa na Polisi na Mgambo wakidai haki zao. Miaka 54 ya Uhuru!

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa Iringa, Polisi wamekwenda kuwapiga mabomu wakiwa ndani ya Chuo, kwa mfano Ruko pale, wanadai hela zao, wanadai stahiki yao. Sasa hii ya kupigwapigwa na wengine saa hizi wako Mahakamani. Wameburuzwa, wamepigwa mateke, wamepigwa mabomu, wanadai haki zao. Wakati huo huo Mheshimiwa Mwigulu alikuwa ameshaomba radhi hapa kwamba ni kosa la Serikali. Sasa tutaendelea kuwanyanyasa watoto wamekosa nini?

Mheshimiwa Shukuru Kawambwa wewe hukusoma kwa *style* hiyo! Wengi, akina Mheshimiwa Mary Nagu hapa hamkusoma kwa *style* hiyo; AG hukusoma kwa *style* hiyo. Mwalimu Nyerere aliwasomesha vizuri. Leo watoto wetu wanapigwa, wananyanyaswa na kosa ni la Serikali; na wengine wako Mahakamani. Hivi ninavyozungumza, kule Iringa kuna wanafunzi zaidi ya 20 wako Polisi, wanakwenda Mahabusu, wameteswa. Tukienda sisi Waheshimiwa Wabunge kuwapa dhamana wanasema sisi ndio tunachochea wakati ninyi hamjawapa mikopo.

Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kombo, ni hoja ya msingi. Tuwasaidie watoto hawa kwa sababu ndiyo sera yenu wenyewe. Kama mmeshindwa kuitekeleza, muitangazie Tanzania kwamba hii sera ni ngumu, hatuwezi. Mtangaze kwamba hamwezi kuwasomesha watoto hawa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwamba Serikali itoe majibu ya kuridhisha na kwamba kesi hizo zifutwe mara moja watoto hao warudi. Watoto warudi shuleni waende kusoma kwa sababu ni kosa la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kombo. Tatizo ambalo Serikali yetu inalo, wanashindwa kupanga. Wakati tunaambiwa taasisi muhimu ambazo ni mihimili ya elimu ya nchi yetu hazipewi fedha. Ukisoma kwenye kabrasha hapa, unaona Ofisi ya Rais Ikulu kwa mwaka huu wa fedha yaani zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 275 mpaka Shilingi bilioni 322, Ikulu. Lakini linapokuja suala la Vyuu ama wanafunzi wetu wa Elimu ya Juu tunafanya vitu vya ajabu.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sasa, naomba Mheshimiwa Waziri atoe majibu, kwa sababu mmekiri kwa maneno yenu; Naibu Waziri wa Fedha amekiri, Waziri umekiri kwamba Serikali imekosea, ndiyo maana kumekuwa na migomo, kwa sababu mmechelewa kupeleka fedha. Lakini leo ikitokea migomo wahanga wakubwa wa kufukuzwa Vyuoni ni Viongozi wa Serikali za Wanafunzi.

Sasa nataka wakati anajibu hayo majibu, atuambie leo; kwa sababu mmekiri mbele ya Taifa kwamba chanzo cha migomo ni ninyi, utuambie leo kwamba viongozi wote wa wanafunzi na wanafunzi wote ambao walisimamishwa Chuo, ama kufukuzwa Chuo na hawajarejeshwa mpaka sasa kwa sababu ya kudai boom lao, wamesamehewa. Mvielekeze hivyo vyo viache kujipendekeza kwa Chama cha Mapinduzi kwa sababu ni uzembe wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi wanafunzi warudishwe Vyuoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ndio mnaofanya watoto wa kike wanajiuza huko. Leo wanafunzi wa Vyu Vikiu wa kike wanafanya shughuli za umalaya kwa sababu Serikali ya CCM hampeleki hela. Wakiandamana kudai haki, mnawafukuza. (Makofi)

Kwa hiyo, naungana na hoja ya Mheshimiwa Kombo. Mheshimiwa Waziri, mmekiri upungufu, mmekiri uzembe; jiokoeni katika hili jahazi. Ondoeni aibu, rudisheni watoto wa masikini mliowafukuza wakidai haki yao kwenye shule waendeleo kusoma. (Makofi)

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu sana, ni kweli kwamba kuna changamoto katika kupata fedha za wanafunzi wa Vyu Vikiu. Lakini ukisikiliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu anavyosema, tatizo linarudi Hazina. Pia ni kweli kwamba bajeti yetu katika Taifa ni bajeti ambayo iko *based* kwenye *projections* kwamba tunaweka bajeti halafu tunategemea tuje tukusanye ndipo tupeleke kwenye matumizi.

Sasa mimi nashauri, kwa nini isifikie wakati tuwe na uwezo wa kukopa fedha sehemu ili tupeleke pesa kwa wakati kwenye Vyu ili wanafunzi wasipate taabu? Ili tutakapokusanya, tutarudi huku ku-*replenish*, kurudisha kule tulikotoa. Inaweza ikasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kero na tatizo la wanafunzi kugoma na kupata shida katika Vyu. Kwa sababu ni kweli kwamba bajeti yetu iko *based* kwenye *projection*. Kwa hiyo, nafikiri kutoa tatizo, ifikie wakati tuwe na uwezo wa kukopa, pesa ziende kwenye Bodi ya Mikopo mapema, wapeleke huko, ninyi mtakapokusanya, tutarudisha huku tulikotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka tuelewane jambo moja na Waheshimiwa Wabunge. Naona wanajumuisha tatizo mpaka na kwenye historia. Lakini kwa utaratibu uliopo, tangu nikichukulia kipindi ambacho siyo cha muda mrefu zaidi; yaani ukianza tangu enzi yuko Mheshimiwa Mgimwa, hakukutokea mgomo hata siku moja. Vile vile tangu mwaka huu wa fedha ulipoanza hakukutokea Mgomo. Umekuja kutoka mgomo *last incidence*. Ni hii ya juzi ambayo wakati wanafunzi wakiendelea kulikuwepo na mchakato wa kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi hazitembezwi kwenye vikapu zinatembeswa kwa utaratibu wa kibenki. Kwa hiyo, ilikuwa tu kwenye mchakato na baada ya kuchelewa hivyo, ndiyo maana niliwaambia wanafunzi kwamba tunaomba radhi, ni mchakato umesababisha fedha hizo zikachelewa. Ukiangalia kwamba Serikali ilitenga Shilingi bilioni 341 kwa ajili ya mikopo ya Elimu ya Juu na katika mwaka wa fedha ambao umesalia mwezi mmoja, kiasi ambacho hakijapelekwa ni Shilingi bilioni tisa ambazo zinategemewa zipelekwe katika mwezi

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

huu; kwa hiyo, utaona kwamba Serikali kwenye jambo hili imezingatia. Ingekuwa zilitakiwa Shilingi billion 400 halafu zikawa zimepelekwa Shilingi bilioni 200 na tunamaliza mwaka wa fedha, ingekuwa ajenda kubwa.

Kwa hiyo, utaona kwamba siyo kwamba fedha haijatoka, ni katika mazingira ya mchakato wa namna ya kuzotoa; utaratibu wa kibenki tu, kwamba kati ya Shilingi bilioni 341 hazijatoka tisa tu; na tunatarajia tuzitoe kabla ya mwisho wa mwezi. Huu ni utaratibu wa kawaida haipaswi kuwa ajenda kubwa. Mchakato wa kuzitoe fedha, wote mnajua kwamba unapotoa kutoka benki kwenda benki nyingine na *distribution*, ni tatizo la aina hiyo.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, jambo hili limepewa uzito unaostahili na kadiri unavyokuwa na wigo mpana wa kusaidi katika Elimu ya Vyuo Vikuu ndivyo ambavyo changamoto za aina hii za *distribution* zinavyoongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi fikirieni tu kwamba katika kipindi hiki hiki, Serikali imeongeza kutoka Shilingi bilioni tisa, yaani ninyi wakati mko kwenye Bunge hili hili, imeongeza kutoka Shilingi bilioni tisa hadi zaidi ya Shilingi bilioni 300, utaona uzito umewekwa na Serikali kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira haya, sisi Wizara ya Fedha tulihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba hii Shilingi bilioni tisa iliyosalia inatoka kabla hatujamaliza mwaka huu wa fedha na wanafunzi watapeleka fedha yao waweze kuendelea nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunajitahidi Wizara ya Fedha pamoja na taasisi nyingine zinazohusika kupunguza urefu wa mchakato. Ndiyo maana siku ile nilisema nikawaambia wanafunzi, kaeni madarasani, tutapunguza mchakato wa fedha kuwafikia, fedha zitoke kwanza halafu ndipo watu waweze kukaa kupitisha taratibu hizo ili kuhakikisha kwamba zinawafikia wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii anayoisema Mheshimiwa Halima, msi-generalize hivyo. Katika Vyuo hivyo wanaweza wakatokea watu wenye tabia mbaya, lakini msi-generalize hivyo. Kuna watu wana wanafunzi wao kwako kwenye hivyo Vyuo. Mnavyo-generalize kwamba wanafunzi wanafanya matukio ya aina hiyo, mtakuwa mna-generalize sana. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Hata enzi zetu kuliwa kuna *prostitution* na bado tulikuwa tunapewa...

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Halima, watu wanapoongea ni vizuri sana tukaheshimiana kwa sababu kuna wengine wanaofanya matukio mabaya hapa hapa na hawajakosa boom. Unataka tuseme hilo? (Kicheko/Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo, Mheshimiwa kaa, kaa kwanza! Mheshimiwa Kombo.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini niseme kwamba mwaka 2014 UDOM waligoma; na ninachokitaka mimi hapa sasa ni Serikali itoe *commitment*, iji-commit yenyewe kwamba ni lini wanafunzi hawa ambao walifukuzwa watawarejesha? Ni lini wataondoa tatizo la posho la wanafunzi? Watote, ni lini watawarejesha shule? Ajibu Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri ni lini wanafunzi watawarejeshwa shule? (Kelele)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, taratibu! Taratibu! Mheshimiwa AG! (Kelele)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu hapa Bungeni Serikali inafanya kazi kama timu moja. Kanuni hii tunayoitumia...



## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tulieni! Muda wote tunaupoteza kwa kufanya vitu tu hivi hivi! Tulieni mpewe majibu!

**MWANASHERI MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizi zimetafsiri maana ya neno "Waziri." Kwa maana ile kanuni ya 123, Waziri anayehusika ni Waziri yule ambaye ana facts anaweza akajibu!

*(Hapa Mheshimiwa Halima J. Mdee, Alisimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hili mimi nimesimama kuzungumza juu ya hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na tamko kwamba Serikali itoe tamko ndani ya Bunge hili kwamba kesi zile zitafutwa lini? Zifutwe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushauri kwamba tunapofanya kazi hizi za uwakilishi wa watu, tutambue mipaka ya mamlaka hizi; mihimili mitatu ya dola. Mheshimiwa Waziri ameshajibu kwamba kuna sheria hapa inaitwa Sheria ya Vyuu vikuu ya mwaka 2005, inafafanua vizuri *organs* za hivi Vyuu Vikuu na kazi zake, halafu zinaanzishwa na *charter*. Hivi ni vitu vya kuamuliwa na mamlaka za Vyuu husika; na kila kesi itamuliwa *on its own merit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo shinikizo kwa Serikali, naomba msiligeuze Bunge hili kuwa sehemu nyingine ya kufanya maamuzi ambayo yako ndani ya Serikali na vyombo vya uchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri. Sisi Wabunge kazi yetu ni lazima tuzilinde. So *much jealousy* sheria tunazozitunga humu ndani, tusiwe watu wa kwanza kuhamasisha uvunjaji wa sheria. Hicho ndicho ambacho mimi ningeomba kushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge ile kauli...

*(Hapa Mheshimiwa Halima J. Mdee, Alisimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, naomba ukae.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Mbunge, ile kauli ya kusema kwamba Serikali itoe tamko humu ni lini sijui zile kesi sijui zitafutwa; hizo tunaziachia mamlaka zinazohusika. *(Makofi/Kelele)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah! *(Kelele)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taratibu! Pia kuna namna, kama hawaridhiki na maamuzi ya zile taasisi, wanaweza wakaenda Mahakamani. Eeh, Waheshimiwa Wabunge ni lazima tuheshimiane kwenye hili suala! Hatuwezi sisi tukageuka tukawa Mahakama, tukawa Serikali, tukawa Bunge! Eeeh, ndiyo nasema! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naweza kusema hapa, kwanza mimi ndiye ninayesimamia kesi zote hizo. Kama ni kesi za jinai, nazisimamia. Zitafutwa tu kama kuna sababu ya kuzifuta *on a merit*. Eeeh! *(Kelele)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo nasema, lakini sio kwa shinikizo!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG zungumza na Kiti, usizungumze na hao!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza na wewe, natoa tamko la Serikali, kwamba hizi kesi jinsi zilivyo zinaangukia mamlaka ya Vyuo Vikuu husika ambao ndiyo wanaosimamia nidhamu ya huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna kesi nyingine ambazo ziko Mahakamani, hatima yake itakujulikana pale ambapo vyombo husika vilivyopeleka kesi Mahakamani. Kama ni sisi, tutakapofanya maamuzi. Vinginevyo, Mahakama itakapofanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sasa nawahoji, Wanaokubali...

**MBUNGE FULANI:** Bado!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ameshamaliza, nawahoji!

**MBUNGE FULANI:** Bado!

**MWENYEKITI:** Ndiyo! Nawahoji, wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Kombo waseme Ndiyo! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Kombo hajahitimisha!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Unakubali hayo maelezo uliyopewa au unayakataa?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngojea kwanza, mimi ndiye mwenye hoja.

**MWENYEKITI:** Ndiyo nakuuliza unakubaliana na hayo aliyoyasema au unayakataa?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mawazo yangu.

**MWENYEKITI:** Haya, haya, endelea!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme kwamba Serikali imekiri kwamba kosa hili lilikuwa ni lao. Maadamu kosa hili ni kosa la Serikali, wanafunzi wale ambao wamefukuzwa hawana makosa.

Sasa Serikali kwa sababu kosa hili ni lao wana wajibu wa kubeba makosa yao wanafunzi wale warejeshwe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, maelezo anayoyotoa AG analipotisha Bunge, kwa sababu kosa ni la Serikali, na Serikali tayari imeshakubali kama makosa yale yalikuwa ni yake. Kwa vyovyote vile wanafunzi wale hawana makosa na wana haki ya kurejeshwa. *(Makofi)*

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwarejeshe wanafunzi wale, kama siyo hivyo, mnaendelea kuwanyanyasa na kuwatesa Watanzania ambao hawana hatia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sasa nawahoji. Wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Kombo wasema ndiyo, wasiokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Kombo waseme siyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 104 kifungu kidogo cha (2), sasa tumebakiza dakika kumi kumaliza muda wetu hivyo, sasa nafunga mjadala huu na tunakwenda kwenye guillotine. Waheshimiwa, utulivu!

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 – Administration & HR Mgt ... .. Sh. 14,348,271,000/=

Kif. 1002 – Finance and Accounts ... .. Sh. 1,167,316,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

Kif. 1003 – Policy and Planning... .. 2,464,385,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – Internal Audit Unit... .. Sh. 671,841,000/=

Kif. 1005 – Procurement Mgmt Unit... .. Sh. 610,179,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

Kif. 1006 – Govnt Communication Unit ... ..Sh. 506,223,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 – Legal Unit... ..Sh. 581,820,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

Kif. 1008 – Inform. Comm. Tec & E-Learning..Sh. 667,280,000/=

Kif. 2001 – Basic Educ. Devel. Office... .. Sh. 53,674,387,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – School Quality Assurance... .. Sh. 25,823,307,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

Kif. 2003 – Reg.&Inter. Edu Affair Coord Unit..Sh. 233,640,000/=

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Kif. 2004 – Edu.Sector Perform. Coord. Unit... Sh. 135,709,000/=  
Kif. 3001 – Basic Education... .. Sh. 604,829,000/=  
Kif. 3002 – Adult Educ.& Information Educ... Sh. 890,256,000/=  
Kif. 4001 – Secondary Education.....Sh. 466,697,000/=  
Kif. 5001 – Teacher Education ... .. Sh. 34,238,988,000/=  
Kif. 7001 – Higher Education... ..Sh. 302,351,039,000/=  
Kif. 7002 – Techn.& Vocat. Train. Div.... .. Sh. 71,441,216,000/=

*(Vifungu vilivyotawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila marekebisha yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 – Administration & HR Unit... .. Sh. 600,000,000/=  
Kif. 1003 – Policy Planning... .. Sh. 11,667,304,000/=  
Kif. 1008 – Inform. Comm.Tech & E-Learning..Sh.100,000,000/=  
Kif. 2001 – Basic Educ. Devel. Office ... .. Sh. 9,168,915,000/=  
Kif. 2002 – School Quality Assurance. ... .. Sh. 1,500,000,000/=  
Kif. 3001 – Basic Education... .. Sh. 0  
Kif. 4001 – Secondary Education... .. Sh. 9,920,640,000/=  
Kif. 5001 – Teacher Education ... .. Sh. 3,000,000,000/=  
Kif. 7001 – Higher Education... .. Sh. 439,618,000,000/=  
Kif. 7002 – Techn.& Vocational Train. Div... Sh. 3,100,000,000/=

*(Kifungu kilichotawa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtoa hoja, Waziri wa Elimu

#### **TAARIFA**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na taasisi zake kwa mwaka 2015/2016 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko yake. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwe na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2015/2016 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 2.20 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 2 Juni, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*

